**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 18 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita muuliza swali la kwanza nina matangazo kuhusu wageni, kwanza wale vijana wanafunzi kutoka shule ya sekondari, naona tangazo halisomeki vizuri, naomba tu wanafunzi na walimu msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Tunafurahi sana walimu na wanafunzi wa shule zetu za hapa nchini Tanzania mnapokuja hapa Bungeni kujionea wenyewe demokrasia ya nchi yetu inavyofanya kazi. Karibuni sana.

Wapo Makatibu 26 wa UWT, ambao wamekuja kwenye Semina ya Utetezi na Ushawishi kwa Harakati za Wanawake inayofanyika Dodoma *CCT* wale pale mkono wangu wakulia karibuni sana kina mama tunawatakia mema katika semina yenu, ili ilete mafanikio na ipige hatua mbele katika kumkomboa mwanamke wa Tanzania, ahsanteni sana. Hawa ni wageni ambao tumetaarifiwa na Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga, Naibu Waziri wa Maji.

Wageni wengine nitawatamka kadri nitakavyopata taarifa, kwa sababu wamechelewa kuleta taarifa.

Na. 223

**Barabara Toka KIA – Mererani**

**MHE. DORA H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mererani ni *Controlled Area* na ipo kwenye mpango wa *Special Economic Zone* na kwa kuwa *Tanzanite* ni madini pekee duniani yanayochimbwa huko Mererani na inajulikana kote ulimwenguni kutokana na madini hayo, lakini barabara inayotoka *KIA* kwenda Mererani ni mbaya sana na kwa kuwa, Waheshimiwa Marais wa

Awamu ya Tatu na Nne waliwaahidi wananchi wa Mererani kuwa barabara ya kutoka *KIA* kwenda mererani itatengenezwa kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwago cha lami ili kurahisisha mawasiliano na usafirishaji?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya suala hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dora Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba *Tanzanite* ni madini pekee duniani yanayochimbwa huko Mererani kama ambavyo taarifa nyingi zimekuwa zikieleza. Aidha ni kweli kuwa Serikali imeingiza eneo la Mererani kwenye mpango wa *Specila Economic Zone. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana pia na Mheshimiwa Mbunge kuwa iko barabara ya kutoka *KIA* hadi Mererani yenye urefu wa Km. 18. Barabara hiyo inaunganisha Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha Km. 13, na Wilaya Simanjiro Mkoani Manyara km. 5. Sehemu ya barabara hiyo kuanzia *KIA* hadi machimbo ya madini ya *Tanzanite* ya Kampuni ya *Tanzanite One* (Km.13) iko katika Wilaya ya Arumeru na imekuwa ikihudumiwa na kutengenezwa na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya *Tanzanite One* kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru na hivyo kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Halmashauri ya Arumeru itatoa kipaumbele kutengeneza barabara hiyo ili ipitike kwa kutumia fedha za ruzuku isiyokuwa na masharti kutoka Serikali Kuu. Suala la kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami hivi sasa halipo kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti uliopo.

Mheshimiwa Spika, Km 5 katika barabara hii ziko upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro. Barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida ili iweze kupitika wakati wote na Kampuni ya *Tanzania One.* Kwa mwaka 2006/2007 Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 5 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida. Hata hivyo Kampuni ya Madini ya *Tanzanite One* imeahidi kuendelea kutengeneza barabara hiyo ili iweze kupitika kwa mwaka mzima.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako mazuri swali langu la nyongeza ni kwamba, tangu Mererani ipewe baraka ya kuwa mji mdogo, sioni ni kwanini Serikali isichukue jukumu la kuweka miundombinu mizuri kwa mafuaa ya wananchi wa Mererani na wachimbaji kwa ujumla?

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu namkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba unaongea na Spika, huongei moja kwa moja na Naibu Waziri. Usiseme Mheshimiwa Naibu Waziri, yeye anajibu tu, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kutengeneza mji mdogo wa Simanjiro kwa miundombinu yote na hasa barabara ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba barabara hiyo ilikuwa na inaendelea kutengenezwa kwa kiwango cha kupitika kwa mwaka mzima. Ni nia ya Serikali kwamba miundombinu yote ikiwa ni pamoja na maji, barabara zahanati na kadhalika. Hii ni katika azma ya kuidumisha miji hiyo ya Simanjiro na miji mingine ambayo inachimbwa madini. *(Makofi)*

Na. 224

**Tume za Kufuatilia Madai ya Watumishi**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. PAUL P. KIMITI )** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka mingi kumekuwepo na Kamati ya Tume za kufuatilia madai ya baadhi ya watumishi kama walimu, waganga na kadhalika:-

(a) Je, kwa nini Serikali badala ya kila wakati kuunda Kamati kama hizo kwa ajili ya dharura kusiwe na utaratibu wa Kamati ya Kudumu ya Wabunge kufuatilia malalamiko ya aina zote?

(b) Je, malalamiko ya watumishi wa Wizara nyeti kama Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama yanashughulikiwa kwa njia ipi nyepesi kutokana na unyeti wa shughuli zao?

(c) Je, madai ya watumishi waliostaafu kuhusiana na kuongezewa *pension* kwa kila mwezi yamefikia wapi na maombi hayo yanagharimu kiasi gani cha Bajeti ikiwa watapewa angalau kima cha chini cha mshahara wa mtumishi wa Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaongozwa kwa mujibu wa Katiba inayotambua mgawanyo wa majukumu baina ya nguzo tatu za dola yaani – Bunge, Mahakama na Serikali. Jukumu la Serikali ni kutawala. Kutokana na msingi huo wa Katiba na kwa madhumuni ya kupata ushauri kwa matatizo ya dharura au maalum Serikali imekuwa ikiunda Tume mbalimbali kuishauri kuhusu masuala ya kiutawala na kuhusisha baadhi ya Wabunge wenye taaluma husika pale inapoonekana busara kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo huo wa mgawanyo wa madaraka, Bunge lako Tukufu ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linao utaratibu wake wa kushughulikia matatizo mbalimbali nchini kwa kupitia Kamati zake mbalimbali za kudumu. Bunge pia linao uwezo kwa mujibu wa Kanuni zake, wa kutoa hoja/azimio Bungeni na kuamua kuhusu kuundwa kwa Tume kwa ajili ya kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, ili kuheshimu mgawanyo huu wa madarka, ni vizuri utaratibu unaotumika sasa ukaendelea. Aidha, ni vyema ikazingatiwa kuwa kuundwa kwa Kamati hizo hutokana na mahitaji maalum ya muda mfupi na haitarajiwi Kamati hizo kuchukua nafasi ya sehemu ya utawala Serikalini.

(b) Mheshimiwa Spika, malalamiko ya watumishi wa Wizara nyeti kama Majeshi, hushughulikiwa kwa taratibu zilizowekwa ndani ya Majeshi husika.

(c) Mheshimiwa Spika, takwimu za mwezi Mei 2006 zinaonyesha kuwa Serikali ina wastaafu 58,502 wanaolipwa pensheni ya wastani wa shilingi 29,177,490,930.66 kwa mwaka.

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa wastaafu wanaolipwa pensheni iliyo chini ya kima cha chini cha mshahara wa mtumishi wa Serikali ni wastaafu 41,629 ambao wanalipwa pensheni ya wastani shilingi 13,728,170,327.20 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali itaamua kupandisha pensheni za wastaafu sawa sawa na kima cha chini cha mshahara wa mtumishi wa Serikali, italazimka kulipa kiasi cha shilingi 32,470,620,000 ambacho ni sawa na ongezeko la wastani wa shilingi 18,742,449,672.80 ambayo ni asilimia 136.5 kwa mwaka kwa kundi hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanyia kazi madai yanayohusu kupandisha kima cha chini cha pensheni. Aidha kutokana na gharama kubwa za kupandisha viwango vya pensheni, Serikali pale uchumi unaporuhusu imekuwa ikihuisha kiwango cha chini cha pensheni hatua kwa hatua kwa lengo la hatimaye kulipa pensheni zinazozingatia angalau mshahara wa kiwango cha chini Serikalini.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia swali la msingi ningependa kuuliza swali lifuatalo, kwamba ni kweli na ni jambo zuri kila wakati kuweka Tume za kuchunguza, lakini kama watumishi wanaoutaratibu na kwa upande wa watumishi wanao utaratibu; na kwa upande wa watumishi tunafahamu pia kwamba kuna Tume yao inayoshughulikia maslahi yao. Je, isingekuwa jambo la busara kuliko kila wakati kuweka Tume hizi zinazoshughulikia mishahara na maslahi ya watumishi zikawa ndiyo wajibu wao kufanya kazi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, pensheni ya watumishi wa umma hutolewa kwa mujibu wa sheria zifuatazo:-

Kwanza ni *Finance Bill*, ambayo ipo chini ya Waziri wa Fedha na mara nyingi wao ndiyo wanaopanga kima cha chini cha pensheni, na pia inashughulikiwa na sheria ya hitimisho la kazi kwa watumishi wa umma.

Na. 225

**Gharama za Baraza la Mawaziri**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa ni kweli kwamba ukumbwa wa Serikali haupimwi kwa gharama bali hupimwa kwa ufanisi, lakini ni vema Watanzania ambao ndio walipa kodi wa nchi hii wakajua gharama halisi ambazo Baraza la Mawaziri linatumia.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kinachotumika katika Baraza la Mawaziri katika mishahara na magari?

(b) Je, ni kiasi gani kilichoongezeka ukilinganisha na Baraza lililopita?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali namba 50 la Mheshimiwa Kiwelu tarehe 13/2/2006, ni sahihi kabisa kwamba ukubwa wa Serikali yoyote duniani haupimwi kwa gharama bali hupimwa kwa ufanisi wa utendaji kazi ambayo ndiyo azma ya Serikali ya Awamu ya Nne. Muundo wa Serikali ya awamu ya nne umezingatia agenda na matakwa ya wananchi ya wakati tulionao hivi sasa. Agenda na matakwa ya kipindi hiki yameleta makujumu mapya na pia kuweka umuhimu wa juu katika baadhi ya majukumu yaliyopo ambayo muundo wa siku za nyuma usingeweza kuyatekeleza kwa ufanisi na tija, kama ambavyo imeanza kujionyesha katika hatua za awali za utendaji wa awamu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Mawaziri la sasa lenye Mawaziri 30 watalipwa mshahara wa shilingi 533,628,000/= na Naibu Waziri 31 ambao watalipwa shilingi 479,136,000/= kwa mwaka ukilinganisha na Baraza lililopita lilikuwa na Mawaziri 28 waliolipwa shilingi 499,284,000/= na Naibu Mawaziri 18 waliolipwa shilingi 278,208,000/= kwa mwaka.

Aidha gharama za ununuzi wa magari ya Mawaziri 30 wa Awamu ya Nne ni shilingi 3,150,000,000/= na Naibu Mawaziri 31 ni shilingi 3,255,000,000/=, wakati wa Barala lililopita lilokuwa na Mawaziri 28 gharama ilikuwa shilingi 2,940,000,000/= na kwa Naibu Mawaziri gharama ya ununuzi wa magari hayo ilikuwa shilingi 1,890,000,000/=.

(b) Gharama za mishahara katika Baraza la Mawaziri la sasa ukilinganisha na Baraza lililopita zimepanda kutoka shilingi 777,492,000/= hadi shs. 1,012,764,000/= ambapo ongezeko ni sawa na asilimia 30%.

Gharama za ununuzi wa magari zimepanda kutoka shs. 4,830,000,000/= hadi shs. 6,405,000,000/= ambapo ongezeko ni sawa na asilimia 32.6%.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika utangulizi hapa juu, naomba nisisitize kwamba kutokana na malengo ya Serikali ya awamu ya nne inahitaji timu ya usimamizi na utekelezaji ambapo kila mmoja wao bila ya kugubikwa na majukumu mengi na mazito anatekeleza wajibu wake kwa uadilifu, kwa wakati, kwa makini, kwa ufanisi na kwa tija.(*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali mmoja la nyongeza wakati Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, akijibu swali langu la nyongeza tarehe 13/6/2006, juu ya kuongezeka gharama kwa ukubwa wa Serikali alisema kwamba ni gharama ndogo sana na haina tatizo lolote. Leo Mheshimiwa Waziri wa Nchi hapa anatueleza kwamba ni asilimia 30.2 kwa mshahara na asilimia 32.6 kwa magari.

Hiyo ni Waziri peke yake mbali na Wizara nyingine, je Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anaweza kufuta ile kauli yake ya uongo aliyoisema siku ile?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU(MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli jibu langu siku hiyo lilikuwa hivyo na bado jibu ni lile lile. Asilimia hiyo iliyotajwa kwa mazingira ya kazi ya sasa hivi inastahili kabisa. Nchi yetu kugharamia kiasi hiki, na Watanzania wote kwanza Waheshimiwa Wabunge mlipo hapa, na Watanzania wanaosikiliza wanaona jinsi Serikali hii ya awamu hii inavyofanya kazi. Inafanya kazi kwa speed kwa umakini na kwa uhakika, kuhakikisha kwamba tunamhudumia Mtanzania vilivyo. Kwa hiyo, gharama hii bado nasisitiza kwamba inastahili kabisa kabisa. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri wakati anatoa majibu yake alielezea ununuzi tu wa magari hajatuambia uendeshaji wa magari yote yana-*cost* kiasi gani. Naomba atuambie magari uendeshaji wake ni shilingi ngapi? Kwa sababu swali la msingi lilitaka gharama za uendeshaji wa Serikali kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Nadhani swali linadai takwimu za ziada, tutafaidika ikiwa litaulizwa peke yake siku nyingine. Tunaendelea na *Order Paper*. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Na. 226.

**Uwekezaji wa Mnara wa *Celtel* Nkungi – Iramba Mashariki**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Je, ile ahadi ya Serikali iliyoitoa kwenye Mikutano ya Bunge mwezi Aprili na Juni, 2005 ya kujenga mnara wa *Celtel* Nkungi – Iramba Mashariki imefikia wapi na kwanini utekelezaji wake unacheleweshwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa kujenga mnara wa *Celtel* Nkungi –Iramba Mashariki ulichelewa kutokana na ufinyu wa bajeti ya *Celtel* iliyosababishwa na zoezi la kutenganishwa kwa shughuli za kibiashara, menejimenti na mali zilizokuwa zikiendeshwa kwa pamoja na kampuni ya Simu Tanzania. Kwa msingi huo *Celtel* ilibidi ianishe vyanzo vyake vya fedha kwa ajili ya mradi ikiwemo ya ndani ya nje ya nchi. Zoezi hili lilikuwa muhimu ili kampuni ya *Celtel* iweze kujitegemea na kuwa na uwezo wa kutekeleza mipango yake iliyojiwekea awali na inayotegemea kuifanya baadaye. Kampuni ya simu ya *Celtel* inatarajia kujenga minara katika miji ya *Old Kiomboi* na Iambi. Minara hiyo ndiyo itakayotoa huduma sehemu mbalimbali ikiwemo ya Nkungi – Iramba Mashariki. Kazi inatarajiwa kukamilika kabla ya Mwisho wa mwaka huu wa 2006.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa wiki mbili zilizopita nilikwenda *Celtel* nikakutana na wahusika wakaniambia sasa wanampango wa kujenga mapema iwezekanavyo minara ya simu sehemu ya Nduguti na Mwangeza. Je, sasa Waziri atasaidia kuwahimiza watekeleze ahadi yao?

Swali la pili, kwa kuwa nimeongea na watu wa *TIGO* na wao wapo tayari kujenga minara iyo Serikali itakuwa tayari kusaidia kuwahimiza wafanye hiyo kazi mapema?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgana Msindai, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali iko tayari kuwasukuma wenzetu waweze kufikisha huduma hizo na napenda nichukue nafasi hii nimpe pongezi zangu za dhati Mheshimiwa Mgana Msindai kwa ufuataliaji wa karibu wa shida zake za mawasiliano ambazo wananchi wake wa Iramba Mashariki zinawakuta. Lakini pia nimwambie kwamba si kampuni hizo mbili tu, lakini kampuni ya simu Tanzania itapeleka huduma zake za simu kwa mitandao hii mipya ya *SMDA*, Itigi, Kinampanda, Kilimatinde, Makiungi, Singida Mjini na Kiomboi. (*Makofi*)

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa minara ya *Vodacom* imewekwa

katika mji mdogo wa Loliondo na mji mdogo wa Waso tangu mwaka jana 2005 lakini hakuna mawasiliano yoyote. Ila mawasiliano tunapata wakati viongozi wanapokwenda kule, kama Mkuu wa Mkoa na wengine. Je, sio wakati muafaka sasa minara hiyo iondolewe kwa sababu haisaidii wananchi wa kawaida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya minara iliyobubu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie kwamba tutauliza kwa kampuni inayohusika ni kitu gani kilichosababisha mawasiliano yasiwepo kwa sababu sisi tunaamini, wanapojenga mirana ya simu huwa wamefanya *study* ya kutosha na wao wasingependa kupoteza fedha za kuacha mnara wa milioni 300, kukaa bure bila kufanya kazi.

Na. 227

**Ujenzi wa Barabara Kutoka Mwanza – Shinyanga**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (k.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA)** Aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya lami kutoka Mwanza hadi mpakani mwa Shinyanga imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na kwa kuwa, ubora wa barabara hiyo na thamani ya fedha inayotumika kutengeneza barabara hiyo, havifanani, na ndiyo maana inaendeleea kuharibika na huku ikiendelea kutengenezwa lakini haipitiki kwa urahisi:-

(a) Je, barabara hiyo ambayo wamepewa Wakandarasi wawili wa nje, imegharimu fedha kiasi gani?

(b) Je, tangu barabara hiyo imalizike kujengwa hadi leo ni miaka mingapi, na imegharimu kiasi gani cha fedha za matengenezo yakiwemo madaraja?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuitengea fedha maalum ili ijengwe upya ifanane na ile iliyojengwa kutoka Shinyanga - Mwanza kuliko kuendelea kuijaza viraka kama inavyofanyiwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya Mwanza – Shinyanga ilitengenezwa na Makandarasi wawili wa nje. Mkandaqrasi wa Kwanza ni *Zakhem International Construction Ltd* mwenye ofisi Dar es Salaam na Nairobi, aliyejenga

kilometa 54, Mwanza - Magogo *River* kwa gharama ya shilingi bilioni 12.2. Mkandarasi wa pili ni *SIETCO* ya China aliyejenga sehemu ya *Magogo River* - Ilula yenye urefu wa kilometa 47, mpkani na Mkoa wa Shinyanga kwa gharama ya shilingi bilioni 11.40. Makandarasi wote wawili walilipwa kwa Mkopo wa Benki ya Dunia.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Mwanza hadi kijiji cha Ilula mpakani na Mkoa wa Shinyanga ulikamilika mwaka 1998. yaani jumla ya mika saba imepita tangu ujenzi wa barabara hii kukamilika na kugharimu jumla ya shilingi 477,850,000/= za matengenezo ya kawaida. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, barabara huweza kudumu kwa muda maalum kutegemeana na aina ya ujenzi uliotumika. Barabara ya Mwanza hadi mpakani na Shinyanga ilijengwa kwa kutumia lami nyepesi *Surface Dressing* ambayo muda wake wa kuishi kabla ya kuhitaji kufanyiwa matengenezo makubwa ni kati ya miaka sita hadi saba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, umuhimu uliojitokeza wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara hii kuanzaia mwaka wa Fedha 2004/2005, na Serikali ikaanza kutenga fedha maalum kila mwaka kuanzia mwaka huo kwa ajili ya kufanyia matengenezo makubwa barabara hii kwa kuanzia na maeneo yaliyokuwa yameharibika zaidi. Kazi hii ya matengenezo inatekelezwa na Mkandarasi wa hapa nchini *Nyanza Road Works Ltd.* wa Mwanza chini ya usimamizi wa Kampuni ya Ushauri ya *Crown – Tech Consult Ltd.* ya Dar es salaam. Matengenezo yanayofanyika ni ya aina mbili:

Aina ya kwanza inahusisha kuchimba na kutoa tabaka lote bovu la barabara kuanzia tabaka la juu *(wearing course)* hadi tabaka la chini kabisa *(sub grade*) na kuimarisha tabaka la chini kwa kuweka udongo mpya *(capping layer),* kuweka tabaka jipya la changarawe *(sub base)* lenye unene wa sentimeta 20, kuweka tabaka jipya la kokoto, *base* lenye unene wa sentimeta 15, kuweka tabaka jipya la lami ngumu *(Asphalt Concrete)* lenye unene wa sentimeta 5. Aina hii ya lami haitofautiani na ile inayowekwa katika barabara ya kutoka Ilula – Shinyanga.

Aina ya pili ni kuziba viraka katika maeneo ambako barabara bado ina nafuu na kuweka tabaka jipya la lami ngumu *(Asphalt Concrete)* lenye unene wa sentimeta 5. Hadi sasa awamu ya kwanza ya matengenezo ya jumla ya kilometa 7.85 iliyogharimu shilingi bilioni 2.27 tayari imekamilika. Matengenezo ya awamu ya pili yenye jumla ya urefu wa kilometa 8.762 itakayogharimu shilingi bilioni 2.08 yalianza Januari mwaka 2006 na yamekamilika Juni 2006. Matayarisho ya zabuni kwa ajili ya awamu ya tatu itakayohusisha kilometa 8.75 yanaendelewa kushughulikiwa kwa ajili ya matengenezo makubwa ya aina hii yatakayogharimiwa na Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, barabara hii saa hivi inapitika bila matatizo yoyote majira yote ya mwaka. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kukamilisha matengenezo katika sehemu zilizobaki.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara kutoka

Ilula kwenda Mwanza hata akienda leo mchana, hata akienda kesho asubuhi, barabara ile sasa imekuwa ni majaribio ya kuweka viraka viraka mpaka Mwanza na Mkandarasi aliyekuwa ametengeneza Ilula mpaka Mwanza, alikuwa ni yule yule. Inakuwaje sasa Ilula mpaka Misungwi hali ya barabara ni mbaya na kutoka Misungwi kwenda mjini na fedha za Watanzania zimetumika?

Mheshimiwa Spika, la pili, ninataka Mheshimiwa Waziri anithibitishie. Hii barabara sasa kuanzia Ilula mpaka Mwanza itakuwa kwa Mkandarasi ambaye anatoka Tinde mpaka Mwanza mjini au itaishia mpakani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema barabara hii, kuna eneo ambalo lilijengwa kwa aina ya *surface dressing* peke yake na kama nilivyosema, utengenezaji wa barabara kwa kiwango hicho cha *surface dressing*, hakidumu kwa miaka mingi kama lami kamili na kwa hiyo ndiyo maana barabara hiyo kuna sehemu ilianza kuharibika mapema. Lakini kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, barabara hiyo sasa inatengenezwa kwa kulingana na uwezo wa Bajeti ya Serikali. Ndio maana kuna maeneo tunatoa tabaka zima la lami na kuweka upya na kuna maeneo tunajaribu kuziba viraka. Ukweli ni kwamba uwezo wa fedha ndio umefanya tufanye kwa awamu na kwa kiwango ambacho nimekitaja. Lakini nia ya Serikali ni kuendelea kuhakikisha kwamba barabara hii inaendelea kuwa nzuri na inapitika wakati wote. Nina hakika baada ya matengenezo haya kwisha, barabara hiyo itapitika vizuri.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Barabara hii ya kutoka Ilula kwenda Mwanza, imepita katika maeneo ya Mbuga ambayo yana udongo ule mweusi *(cotton black soil)* na matengenezo yanayofanyika yanafanyika kana kwamba hii barabara ni ya kawaida tu. Je, Serikali ipo tayari sasa kutengeneza ile *base*, kwa sababu wanachotengeneza ni kuziba na kupaka lami, lakini tatizo kubwa ni ile *base* yaani msingi wa barabara yenyewe. Je, Serikali ipo tayari kutengeneza *base* ili barabara hiyo iweze kudumu kwa kiwango kizuri cha lami ili kiweze kuhudumia wananchi wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, alivyosema ni kweli kwamba barabara hiyo imepita maeneo yenye udongo huo mweusi na kwa kweli kama unataka barabara hii iweze kuwa katika kiwango kizuri, ni lazima kuchimba *base* kama alivyosema na kujenga barabara upya. Ukweli ni kwamba kwa sasa ambapo bado tunatumia Bajeti yetu kwa fedha ambazo tunazipata bilioni mbili, tatu, kila mwaka kwa ajili ya barabara hiyo, huwezi ukatengeneza barabara hiyo katika kiwango hicho anachokizungumzia. Lakini, katika Bajeti zijazo na kama tukiweza kupata fedha za uhakika, barabara hii ingefaa kwa kweli ibomolewe na kutengenezwa katika kiasi hicho. Kwa sasa kutokana na Bajeti kuwa finyu kama nilivyosema, tutaendelea kutengeneza katika viwango hivyo ambavyo tunavitengeneza sasa ili barabara iendelee kupitika wakati wote. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara inapitika wakati wote na hiyo tumeahidi.

Na. 228

**Ubora wa Kiwanda cha Magodoro ya Dodoma**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, muda mrefu Kiwanda cha Magodoro Dodoma kilikuwa na sifa nzuri ya kutengeneza magodoro yaliyopendwa na wananchi kwa ubora wake:-

(a) Je, Serikali ina taarifa kwamba hivi sasa Kiwanda hicho kinatengeneza magodoro ambayo hayana ubora?

(b) Kwa kuwa, *TBS* inao uwezo wa kutembelea kiwanda, maghala, na maduka. Je, Serikali inaweza ikawaagiza wakachunguze magodoro ya kiwanda hicho hasa yale ya futi 5 x 6 na futi 6 x 6 ambayo yamebainika kupungua inchi mbili, jambo ambalo ni kero kwa wanunuzi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kujali ubora wa bidhaa zinazotumiwa na Watanzania. Pia ningependa kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kiwanda hicho cha magodoro kilichokuwa Dodoma kiliungua moto mwaka 1999 na kikahamishiwa Dar es salaam Mikocheni mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kwamba sasa hivi kiwanda hicho kinatengeneza magodoro ambayo hayana ubora. Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) baada ya kutoa leseni ya ubora huwa linafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye kiwanda husika na kwenye soko. Baada ya ukaguzi huo, sampuli huchukuliwa ili zikapimwe kuhakiki kwamba ubora wa bidhaa husika unafuatwa wakati wa uzalishaji. Ukaguzi wa mara kwa mara uliofanyika katika kiwanda hiki cha *Quality Foam Ltd.* tangu kipewe leseni ya ubora, haujaonyesha matatizo ya ukiukaji wa masharti ya ubora.

(b) Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Juni, 2006, Shirika lilifanya ukaguzi wa kushitukiza *(surveillance inspection)* katika kiwanda cha magodoro kama Mheshimiwa Mbunge alivyopendekeza. Matokeo ya vipimo vya maabara yalibainisha kwamba sampuli inakidhi viwango vya urefu, upana na kina.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili aweze kunipa taarifa ya sehemu yanapouzwa magodoro yasiyo na ubora ili niweze kuwagiza *TBS* waende huko kufanya uchunguzi wa kina ili hatimaye hatua za kisheria zichukuliwe dhidi wa wauzaji hao.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba yuko tayari ili niyadumbe maduka ambayo yana magodoro

amabayo hayana ubora na ubora wenyewe niliokusudia ni kwamba yamepungua inchi 1 na mengine inchi 2.

Kwa hiyo, Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba wiki yoyote kuanzia wiki hii, nimpeleke katika maduka au atoe watu wake waende wakayapime magodoro ambayo mimi mwenyewe na watu wangu na wauzaji wamethibitisha kwamba yana upungufu wa wa inchi 1, jambo ambalo Mr. X ambaye alilala yeye na mwenzake na mtoto mdogo, mtoto mdogo mguu ukaganda chini kabisa pembeni kwa sababu ilikuwa na uwazi. *(Kicheko)*

Swali la pili, baada ya kuthibitishwa hayo, Je, wale watu ambao wamenunua magodoro yale, Serikali itatoa tamko gani ili yarejeshwe na wapewe hela zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, vipimo vya godoro siyo inchi peke yake, lakini vipimo au ubora wa magodoro ni pamoja na *compression* na *maximum compression* ni asilimia 10. Lakini vile vile katika godoro tunaangalia *density*, kiwango cha chini kabisa ni kilogramu 22 kwa mita *cube* moja.

Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Haroub Said Masoud kwamba kama atakuwa na nafasi, nitamwunganishia ili tuweze kwenda kuangalia hayo maduka kusudi hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya watu hao ambao wanauza magodoro kama hayo. Lakini pia, hao walionunua, nadhani wameishanunua. Kwa hiyo, nadhani tunaweza kuanzia hapo tulipoanzia sasa hivi. Hatuwezi kujua wamenunulia wapi. *(Makofi)*

Na. 229

**Upatikanaji wa Soko la Mazao – Ludewa**

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA (k.n.y. MHE. PINDI CHANA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Ludewa ni miongoni mwa Wilaya chache sana nchini zinazozalisha mahindi na viazi kwa wingi sana na kuuzwa hata nje ya nchi kama vile Malawi na kwa kuwa Serikali imeahidi kuweka mikakati itakayoliwezesha taifa kuhimili ushindani wa biashara kimataifa katika mazingira ya utandawazi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea wananchi wa Ludewa Soko litakalokidhi uzalishaji wa mazao wanayozalisha katika Wilaya ya Ludewa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya barabara za Wialaya hiyo ili wakulima waweze kusafirisha na kuuza mazao yao kwa bei nzuri?

(c) Je, Mkoa wa Iringa upo kwenye Programu ya *AMSDP*?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:-**

Mheshimiwa Spika, Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Pindi Chana, kwa jitihada zake za kuwatafutia soko wananchi wake wa Iringa hususan Wilaya ya Ludewa. Pili, ningependa kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika kutambua mchango wa Wilaya ya Ludewa kwa uzalishaji wa mazao mbali mbali na katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha miundombinu ya masoko na ya mazao nchini, Serikali kupitia Programu ya *AMSDP* itaanza ujenzi wa soko la kisasa katika eneo la Malangali mwezi huu wa Julai.2006. Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ilifungua zabuni ya ujenzi wa soko hili tarehe 27 Juni 2006 na hivi sasa tathmini inafanyika ili kumpata Makandarasi anayefaa.

(b) Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi wa Soko hilo la kisasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, jumla ya kilometa 35 za barabara zitajengwa ili ziweze kusafirisha mazao kutoka maeneo ya uzalishaji kwa kipindi chote cha mwaka. Ujenzi wa barabara hizi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2006.

(c) Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa ni moja kati ya Mikoa inayotekeleza Programu ya *AMSDP*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa sehemu zote zenye mazao mengi na hasa kulingana na hali ya njaa iliyoko nchini kwetu hivi sasa, kuna baadhi ya sehemu ambazo zimekuwa zikizalisha sana mazao lakini hazina masoko na barabara zake pia zimekuwa siyo nzuri na tukumbuke kwamba ikitokea njaa, waathirika wakubwa siyo wakulima tu wa maeneo hayo, bali ni Watanzania ama wananchi wote kwa ujumla, yaani taifa zima.

Je, Serikali haioni kwamba wingi wa mazao ya ziada ndiyo kigezo kikuu muhimu cha kuwapatia wananchi hawa masoko na sio vinginevyo? Mfano ni mikoa inayozalisha sana kama Iringa, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Mwanza na kadhalika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wingi wa mazao ndio vigezo ambavyo vinaashiria kujengwa soko sehemu fulani. Lakini vile vile tunaangalia wingi wa watu na miundombinu ya masoko iliyopo maeneo hayo na maeneo ambayo yatahudumiwa na soko hilo kama litajengwa.

Mheshimiwa Spika, kama alivyotaja ile Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa, mikoa hiyo iko katika Programu ya *AMSDP*. Vile vile ipo mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Manyara ambayo inahudumiwa na hiyo *AMSDP*. Jumla ya masoko 20 yatajengwa katika mikoa hiyo 8. Masoko 6 tayari yameishajengwa katika awamu ya kwanza na sasa hivi tunategemea kwamba masoko 9 yatajengwa katika awamu ya pili. Lakini, sambamba na ujenzi wa masoko hayo, zitajengwa kilometa 1,136 za barabara pamoja na madaraja 115 pamoja na makalvati 575 mpaka mwaka 2009. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Mimi nataka nisaidiwe. Nini vigezo hasa vinavyotumika kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo chini ya Programu hii ya *AMSDP*? Ahsante sana!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo vinatumika, kwanza, ni kwamba kuwe na mazao ya kutosha ambapo yatakuwa yanauzwa katika soko hilo, pili, lazima hilo soko lijengwe sehemu ambayo barabara inapitika mwaka mzima, kwa mfano Soko la Kikatiti, liko barabarani, Soko la Kwa Saadala, liko barabarani, Soko la Mtindilo, liko barabarani, Soko la Soni, linajengwa barabarani, Soko la Matai, liko barabarani, Soko la Inyala, liko barabarani, Soko la Mbinga, linajengwa barabarani. Kwa hiyo, barabara ni muhimu sana katika kujenga soko la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wakumbuke kwamba masoko haya siyo ya masoko ya Kata wala Kijiji. Ni masoko ya kimataifa. Kwa hiyo, lazima yajengwe sehemu ambayo inapitika. Hatuwezi kujenga masoko ambayo lazima utembee kilometa 200 kufuata soko.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba sehemu hiyo lazima iwe na mitandao ya simu kusudi mtu kutoka nje ya nchi ama kutoka kwenye mkoa jirani anaweza kupiga simu na kusema kwamba aandaliwe kiasi fulani cha shehena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba lazima soko lijengwe sehemu yenye watu wa kutosha kwa sababu masoko haya siyo magulio ya Alhamisi wala Jumatano. Masoko haya ni ya kila siku. Ili masoko hayo yaweze kujiendeleza, lazima kuwe na *population* ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, masoko ya kimataifa yanatakiwa yajengwe maeneo ambayo ni ya kutosha. Hatuwezi kuanza ku-*compasate* watu kwa sababu tumejenga kwenye maeneo ya shule. Lazima, eneo liwe ni la kutosha kwa ajili ya *further expansion*. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kwa kuwa mwaka huu tulipata njaa, naona hili lazima liendelee kuulizwa tu. Mheshimiwa William M. Ngeleja, halafu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Jenista J. Mhagama.

**MHE: WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda kujua Serikali ina mpango gani kujenga masoko kwa maeneo mengine ambayo hayamo katika mango huu wa *AMSDP*, lakini yana sifa zile ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezisema ikiwemo Wilaya ya Sengerema na Wilaya ya Geita ambazo kwanza zipo katika barabara kuu ambayo inaunganisha nchi ya Tanzania na nchi nyingine za jirani. Lakini pia zina mazao ya kutosha ambayo yanaweza kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa letu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO**: Mheshimiwa Spika, Halmashauri yake ya Sengerema wangeweza kukaa na kuainisha vigezo kama ina kidhi vigezo vya kujenga soko la kimataifa. Lakini, siyo katika programu hii ya *AMSDP*, tutatafuta vyanzo vya fedha vingine na tutaunganisha Halmshauri na Wafadhili mbali mbali kusudi waweze kujengewa soko kama yalivyojengwa masoko ya Kibaigwa, Kilole na Tawa Morogoro Vijijini, yaliyojengwa na Ufaransa. *AMSDP* inatokana na *African Development Bank, IFAD*, Serikali ya Tanzania na serikali ya Ireland.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mpango huu wa ujenzi wa masoko uko katika mikoa na Ruvuma ni mkoa miongoni mwa mikoa hiyo aliyoisema na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zinazalisha sana mahindi katika nchi hii ya Tanzania na imekuwa kwa muda mrefu sana ikiomba kujengewa soko la kimataifa kwa ajili ya bidhaa za mahindi na nyinginezo na ukizingatia kwamba sasa Wizara ya Miundombinu imefungua mawasiliano kupitia Halmashauri hiyo na nchi ya Msumbiji. Je, katika masoko hayo 9 yanayotarajiwa kujengwa kwa awamu inayokuja. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kutoa ushirikiano katika Halmashauri hiyo ili soko hilo sasa liweze kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, Masoko hayo 9 tayari *tender* zimeishafunguliwa na sasa tunatafuta mjenzi. Katika masoko hayo, soko la Songea halipo, lakini soko la Mbinga litajengwa. Sasa, katika kufanya tathmini ya Halmashauri hiyo, wakiishafanya tathmini tutaangalia umbali wa kutoka Mbinga hadi Songea ili tuweze kujua kwamba hakutakuwa na *conflict of interest* ya kuchukua mazao yale ambayo yalitakiwa yaende Mbinga, kwa sababu haya masoko ni 20 na Wilaya ziko 37. Kwa hiyo, hatuwezi tukaweka masoko matatu au manne kwenye mkoa mmoja wakati mikoa mingine pia inazalisha.

Na. 230

**Usajili wa Wadhamini wa Klabu za Michezo**

**MHE. IDD M. AZZAN** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni Utamaduni wa kisheria kuwa Mdhamini wa Chama au Klabu ya Michezo anatambulika kisheria iwapo tu amesajiliwa Serikalini:-

(a) Je, ni nani Mdhamini/Wadhamini *(Trustees)* halali wa *Simba Sports Club*?

(b) Je, *Young African Sports Club Limited* imesajiliwa na Vyama vya Michezo au Msajili wa Makampuni na wamesajiliwa chini ya sheria gani na lini?

(c) Je, ni nani Wadhamini wa *Young African Sports Club*?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ofisini ya Kabidhi Wasii, Wadhamini wa Klabu ya Simba waliowahi kusajiliwa na Ofisi ya Kabidhi Wasii walikuwa ni Bwana Alli Mwinyi Tambwe, Bwana Saleh Mohamed Ghulum na Bwana Abdul Wahab Abbas, ambao walisajiliwa mwaka 1975. Kuanzia wakati huo Klabu ya Simba haijawahi kusajili wadhamini wengine au kupeleka taarifa nyingine ile kwa Kabidhi Wasii hadi sasa.

*(b) Young African Sports Club Limited* imesajiliwa mwaka 2000 chini ya Sheria ya makampuni *(Cap.212)*.

(c) Waliowahi kuwa Wadhamini wa *Young African Sports Club Limited* walikuwa Bwana Mangara Tabu Mangara na Bwana Ramadhan Maulid Mwinyikambi, ambao walisajiliwa na Kabidhi Wasii mwaka 1973. Kuanzia wakati huo Klabu hiyo haijawahi kuwa na wadhamini na kupeleka wadhamini wengine kwa Kabidhi Wasii.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa amekiri kwamba *Young African Sports Club Limited* imesajiliwa na Msajili wa Makampuni. Je, anaweza akatoa tamko rasmi hapa Bungeni kwamba Serikali inaitambua Yanga ipi kati ya Yanga hizi mbili, *Young African Sports Club Ltd.* na *Young African Sports Club* ambayo imesajiliwa na Msajili wa Vyama vya Michezo. Ni ipi ambayo inatambulika na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, Timu ya Yanga imesajiliwa kisheria kwa kutumia sheria ya Baraza la Michezo mwaka 1971 tarehe 23 Septemba. Kukatokea matatizo katika uongozi wa Rais wa wakati huo, Ndugu Abbas Tarimba, mwaka 2000. Wakakubaliana kwamba wabadilishe Timu ya Yanga kuwa *Club* ya kawaida ya michezo, sasa ijiendeshe ki-kampuni. Kwa hiyo, ikasajiliwa sasa Yanga kama kampuni, siyo tena kama *Club* ya michezo. Utata huo umeendelea kati ya Yanga Asili na Yanga Kampuni hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kuutatua mgogoro huo na kukawa na muafaka kati ya Yanga Asili na Yanga Kampuni hadi leo na wakakubaliana Yanga Asili na Yanga Kampuni watafute Mwenyekiti wa kuweza kumaliza Mgogoro huo, na kama mna kumbuka Ndugu Mengi alichaguliwa.

Mgogoro huo ukawa unaendelea na Serikali ikawa inasaidia hadi sasa ambapo Yanga inaendelea kama Yanga Kampuni kwa ajili ya kukubaliana muafaka na muafaka

huo bado haujakamilika. Utakapomalizika, basi suala hilo litatambuliwa. Lakini sasa hivi hatuwezi kwa sisi Serikali kusema tunatambua Yanga Asili ama Yanga Kampuni.

**SPIKA:** Hakuna anayeuliza kuhusu Simba, ni Yanga tu! *(Kicheko)*

**MHE. ZUBERI ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muafaka hauvunji sheria, Serikali inatuambia nini hizi Taasisi, *Young African Sports Club Ltd.* Pamoja na *Young African Sports Club*, ni kitu kimoja? Au ni Taasisi mbili, ni *entity* mbili tofauti?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye suala la nyongeza ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Idd M. Azzan, ni kwamba Yanga kama Yanga imejigeuza kuwa Kampuni na ni utaratibu wa kidunia kwamba sasa hivi vilabu vyote vya michezo vinajigeuza viendeshwe ki-kampuni.

Sasa, huu ni utaratibu wa kawaida na ndio maana nikasema sisi hapa, hii ni katiba ya *Club* na kila *Club* inajiendesha yenyewe. Sas hatuwezi sisi kama Serikali tuingilie kwenye mgogoro ambao ni wa *Club* yenyewe na wana katiba yao.

Mheshimiwa Spika, labda ningependa nitoe wito kwamba matatizo na migogoro katika Villabu vyetu, ndio inayofifisha michezo katika nchi yetu. Kwa hiyo naomba migogoro hii sasa ife ili tuendeleze michezo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Na. 231

**Lugha isiyofaa kwenye Sanaa na Muziki**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** Aliuliza:-

Kwa kuwa maendeleo ya sanaa ya muziki na michezo ya kuigiza imetokea kupendwa sana hasa kwa kizazi kipya, watu wazima na watoto katika nchi yetu na imetoa ajira kubwa kwa vijana na kwa kuwa, baadhi ya miziki hiyo hutumia lugha zisizo na heshima kushindwa kusikilizana kwa pamoja.

(a) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo ni kinyume na Utamaduni wa Kitanzania na kwa kiasi kikubwa inaathiri nidhamu na maadili ya kitaifa?

(b) Je, ni chombo gani ambacho Serikali imekipa jukumu la kuhariri kazi hizo kabla hazijapata kibali cha kurushwa hewani?

(c) Je, Serikali inatoa msimamo gani juu ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMMANUEL JOHN NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba matumizi ya lugha zisizo na heshima katika sanaa ya muziki na michezo ya kuigiza ni kinyume na utamaduni wa Mtanzania na inaathiri nidhamu na maadili ya Taifa.

(b) Vyombo ambavyo Serikali imevipa jukumu la kuhariri kazi hizo ni Bodi ya Filamu na sanaa za Jukwaani iliyoundwa chini ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 na Baraza la Sanaa la Tanzania (BASATA).

(c) Wito wa Serikali kwa wasanii wa aina zote ni kwamba wanapotunga nyimbo zao, watumie lugha yenye heshima na staha ili kujenga maadili mema ya kitaifa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sambamba na lugha isiyo ya heshima ambayo inatumiwa katika nyimbo ambzao zinaimbwa na baadhi ya wanamuziki, lakini vile vile kuna tabia ya uvaaji wa nguo nusu uchi kwa wanenguaji wa kike. Je, kwa nini wanenguaji wa kiume wanavaa nguo kamili na wanenguaji wa kike wanvaa nguo nusu uchi? Serikali inasema nini kuhusiana na hili?

**SPIKA:** Nadhani ni vizuri tu lijibiwe! Mheshimiwa Waziri wa Habari, majibu! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kila mmoja na uhuru wa kuvaa nguo atakayo na acheze atakavyo. Wanawake hawalazimishwi kufanya vile, bali wenyewe wanaona kama njia moja ya kuvutia watu ni kucheza wamevua nguo. Na wale wanaovaa nguo pia hawakatazwi, wanaweza wakavaa nguo wakacheza na mambo yasiharibike hata kidogo. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ningependa kuuliza swali moja dogo tu. Kwa kuwa Serikali inao uwezo mkubwa wa kutoa tamko, juu ya hao watu wanaocheza wakiwa nusu uchi. Je, Waziri analiambia nini Bunge na wananchi kwamba watachukua hatua gani juu ya hawa watu wanaocheza wakiwa nusu uchi?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuongezea majibu ya Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kila mtu ana hiari ya kuvaa nguo anazozitaka. Hiari hiyo basi iende kwenye kujenga maadili mazuri ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli vile vile jamii inaweza ikajenga maadili mazuri au ikaendekeza maadili mabaya. Ninatoa wito kwa jamii ya Watanzania wakatae kuona wale ambao wanavaa au wanatumia uhuru wao kujenga maadili ambayo ni mabaya.

Ningependa kutoa wito kwa akina mama Watanzania kwamba pale inapowezekana basi, tukinengua, tuvae nguo ambazo zinajenga maadili mazuri ya Watanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla swali la mwisho halijaulizwa, natoa tu ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba na ninyi msiwe mnakwenda kuangalia kwa sababu kama... *(Kicheko)*

Na. 232

**Mradi wa Kupeleka Umeme Njombe Magharibi**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (k.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)** Aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) lilikuwa na mradi wa kupeleka umeme katika Tarafa za Wanging'ombe, Mdandu, Imalinyi, Kidugala na Igosi:-

Je, ni lini mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme kwa ajili ya Misheni ya Kidugala unajengwa chini ya kandarasi ya kituo cha umeme cha Makambako wakati vijiji vingineni vimejumuishwa kwenye mipango mingine ya Serikali kwa kushirikiana na Washirika wake.

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi wa Makambako, Misheni ya Kidugala itapatiwa umeme katika awamu hii chini ya mradi unaoendelea wa kujenga kituo kikubwa cha kupunguzia nguvu za umeme Kilivoti 220/132/33 cha Makambako. Kazi za ujenzi wa mradi huu zinaendelea na mradi unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme wa Wanging'ombe ambao umesimama kutokana na ukosefu wa vifaa kwa ajili ya kuukamilisha, unategemewa kukamilika baada ya Desemba 2006. Vifaa vinavyotakiwa ni *transfoma* ya *Kva 50,* vifaa vya njia ya

umeme ya msongo wa Voti 400 yenye urefu wa kilometa moja pamoja na uunganishaji watejea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme Mdandu unahusu ufungaji wa *transfoma* ya uwezo wa *Kva50* na ujenzi wa njia za umeme mdogo wa msongo wa Voti 400 zenye urefu wa kilometa moja. Gharama za utekelezaji wa mradi zinakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 12. Mradi huu unategemewa kutekelezwa katika Bajeti ya Serikali ya 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Imalinyi kipo umbali wa karibu kilometa 20 kutoka Kidugala ambapo ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 utaishia. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 400. Vilevile, mradi huu unategemewa kutekelezwa mara fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Tarafa ya Igosi yapo umbali wa kilometa 70 toka Njombe mjini kuelekea Makete. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 1.2. Utekelezaji wake utafanyika mara fedha za utekelezaji zitakapopatikana. *(Makofi)*

Na. 232

**Mradi wa Kupeleka Umeme Njombe Magharibi**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) lilikuwa na mradi wa kupeleka umeme katika tarafa za Wanging'ombe, Mdandu, Imahinyi, Kidugala na Igosi:-

Je, ni lini mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme kwa ajili ya Misheni ya Kidugala unajengwa chini ya kandarasi ya kituo cha umeme cha Makambako wakati vijiji vingine vimejumuishwa kwenye mipango mingine ya Serikali kwa kushirikiana na Washirika wake.

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi wa Makambako, Misheni ya Kidugala itapatiwa umeme katika awamu hii chini ya mradi unaoendelea wa kujenga kituo kikubwa cha kupunguzia nguvu za umeme ya *KV 220/132/33* cha Makambako. Kazi za ujenzi wa mradi huu zinaendelea na mradi unategemewa kukamilika mwishoni mwa Septemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme wa Wanging'ombe ambao umesimama kutokana na ukosefu vifaa kwa ajili ya kuukamilisha, unategemewa kukamilika baada ya mwezi Desemba 2006. Vifaa vinavyotakiwa ni *transfoma* ya *KVA 50,* vifaa vya njia ya umeme ya msongo wa Volti 400 yenye urefu wa kilometa moja pamoja na uunganishaji watejea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme Mdandu unahusu ufungaji wa *transfoma* ya uwezo wa *KVA 50* na ujenzi wa njia za umeme mdogo wa msongo wa Volti 400 zenye urefu wa kilometa moja. Gharama za utekelezaji wa mradi zinakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 12. Mradi huu unategemewa kutekelezwa katika Bajeti ya Serikali ya 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Imalinyi kipo umbali wa karibu kilometa 20 toka Kidugala ambapo ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 utaishia. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 400. Vilevile, mradi huu unategemewa kutekelezwa mara fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Tarafa ya Igosi, yapo umbali wa kilometa 70 toka Njombe mjini kuelekea Makete. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 1.2. Utekelezaji wake utafanyika mara fedha za utekelezaji zitakapopatikana.

**MHE. JAKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na kushushwa kwa umeme wa gridi pale Makambako na kutokana na program ya *ERP* iliyoko ukurasa wa 12 ibara ya 26. Je, lile lisingekuwa jibu la swali hili? Pili, kama siyo jibu au ni jibu kwa nini basi chini ya mpango wa *ERPT* tusianzie na maeneo haya ambayo tayari nguzo na nyaya za umeme zimekwishapita juu yake?

Mheshimiwa Spika, naomba nisahihishe siyo Kidugara ni Kidugala.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tungependa kumthibitishia na kumhakikishia kwamba maeneo yote ambayo nguzo zilikuwa zimeshafika na kazi ilikuwa imeshaanza hayo ndiyo maeneo ambayo kazi itafanyika kwanza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kuna matangazo. Wakati nawatambulisha wageni wa mkono wa kushoto ambao ni walimu na wanafunzi sikutaja jina la Sekondari. Nimepewa sasa ni Sekondari ya Hijla Dodoma. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi Mheshimiwa Gideon Cheyo, anawatangazia wajumbe wake kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati yake ya Kilimo na Ardhi leo tarehe 18 Julai, 2006 saa saba mchana. Chumba Namba 432 ghorofa ya nne

saa saba mchana. Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila, anawatangazia wajumbe wake kikao saa tano asubuhi ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anatangaza kuwa kutakuwa na Kikao leo cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii, saa saba mchana chumba Namba 231.

Lakini nadhani vikao hivyo ambavyo ni vya saa saba itabidi wajumbe ambao ni wa Chama cha Mapinduzi, wazingatie kuwa saa saba hiyo hiyo, kutakuwa na kikao cha Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwenye ukumbi wa zamani. Saa saba kamili Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kutakuwa na kikao kifupi kuna taarifa moja muhimu saa saba kamili leo.

Wajumbe wote ambao ni wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *Amani Forum* wanaombwa kukutana saa tano asubuhi ghorofa ya kwanza Ukumbi Na. 133. Wajumbe wote wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kuna semina fupi ya *Jane Good all Institute Gombe* saa tano asubuhi ghorofa ya nne chumba Na. 428.

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao walihudhuria mafunzo ya kompyuta, mafunzo sasa yanaanza leo kwa madarasa mawili. Darasa moja litakuwa ukumbi Na. 131 ghorofa ya kwanza jengo la utawala na darasa jingine ukumbi wa zamani Namba 37 kote masomo hayo yataanza saa 8.30 hadi saa 10.30 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea hivi punde na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wasemaji ambao inawezekana wakachangia kwa hesabu zangu hawatazidi 12. Kwa hiyo, orodha niliyonayo hii ambayo ni ya ziada kabisa ya hivyo hatuwezi kufikia.

Kwa hiyo, watakaoweza kuchangia ni Mheshimiwa Mporogomyi, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Salum Hemed Hamis, Mheshimiwa Chacha Wangwe, nadhani Mheshimiwa Hamis amejitoa. Basi Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir.

Nimeamua tumalize mchango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa hoja hii saa 7.00 ili saa 11.00 Mheshimiwa Waziri ukianzia na Naibu Waziri, aanze kujibu hoja. Hii itatuwezesha kuingia kwenye Kamati ya Matumizi saa 12.00. Nimepokea malalamiko yenu kwamba tunakuwa hatufiki hata kwenye kitabu cha nne ambacho ndicho kitabu cha Maendeleo. Tunavutana tu kwenye kitabu cha pili ambacho ni Matumizi ya Kawaida bila kufika kwenye miradi. Sasa Wizara hii miradi yake ni mikubwa. Ni vizuri tukapata ufafanuzi ili tuweze kumaliza vizuri. Sasa basi kwa mpangilio namwita sasa Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Nishati na Madini

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niongee machache kuhusu Wizara hii. Kwanza kabisa ninaomba niunge mkono hoja ya Wizara hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, umekatiza baina ya Spika na Msemaji lakini bado tunaendelea kuelewa hizi taratibu. Endelea tu.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi walioko katika Wizara hii kwa kazi wanayoifanya. Nawapongeza kwa sababu kazi ya Wizara hii ni kubwa na ni kazi inayohitaji utekelezaji mkubwa kutokana watendaji na viongozi Wakuu wa Wizara hii kama Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu. Naomba niseme hivi, Serikali yetu ni Serikali ambayo sasa imeamua kwamba inataka kutekeleza na kufanya yale mambo yaliyoko mbele yetu kwa uhakika zaidi. Ndiyo maana ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Iwe kasi ya kufanya maamuzi ndani ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni moja ya Wizara ambazo zina matatizo makubwa ya urasimu, matatizo makubwa ya dhuluma zinazowakabili wawekezaji wa aina mbalimbali katika nchi hii. Watanzania wanayo haki ya kuuliza yale wanayoyataka na Watanzania wanawakilishwa na sisi Wabunge. Sisi Wabunge ndiyo wenye nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu sentensi moja ambayo iko katika kitabu kiitwacho *Beyond 2005*, inasema: "*The Role of the Parliamentarians. As Parliamentarians we now have a responsibility to the citizens we represent, to ensure that these commitments are implemented that money and policy changes are delivered and translated into making a real difference to the lives of Ordinary people across the country"*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mabilioni yaliyokuwa *allocated* kwenye Wizara hii mengi sana, bado tunalia umaskini lakini bado Wizara haifanyi yale ambayo watu wanategemea yafanywe. Yako mambo ambayo tungewategemea wawe wameyafanya yapunguze malalamiko kwa watu lakini mambo yameendelea kuzidi.

Nilimsikia Waziri mmoja siku moja ananung'unika anasema hata watalaam wetu wanatukwamisha. Mimi siamini mtaalam ambaye wewe uko juu yake anaweza

akakukwamisha wewe Waziri uliyejaa madaraka tele. Siamini kama mtaalam anaweza kukukwamisha. Lazima maamuzi yafanyike pale panapotokea kasoro.

Baada ya mambo yanayotendeka katika Wizara hii yanasikitisha. Mwaka jana Kamati ya Fedha na Uchumi, ilikaaa kuzungumzia habari ya bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Wizara ikasema imepata *RDC* tukaja na *due diligence* tukawaambia *RDC* hana rekodi ya kuweza kujenga hilo bomba kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza tukaonyesha kila kitu. Bomba hilo halikujengwa miezi ile aliyopewa sijui 18 imekwisha hakuna kitu leo naona amepewa *power generators* hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mtu aliyeanza ku-*develop* bomba hili miaka iliyopita ametumia fedha yake mpaka amekwisha ni mzalendo wa nchi hii hii, anaambiwa fedha hana hatuwezi kumpa hivi lazima uwe na fedha mfukoni ili kupata mradi? Tuliandika mpaka kwa Rais, Rais akaelekeza Wizara, Waziri Mkuu akafanya hivyo hivyo. Ninaomba yule aliyepewa bomba hili ambaye alikuwa anaambiwa kwamba kama *RDC* atashindwa yeye aendelee ku-*promote* hili bomba apewe bomba hili na lifanye kazi. (*Makofi*)

Wawekezaji nina uhakika anao na alituonyesha nakala za barua alizonazo za watu wenye *commitment* ambao wanaweza kuja hapa wakati wowote. *Africommerce International* wanaweza kufanya hiyo kazi wakishirikiana na kampuni moja iitwayo *Enegem* ya Canada wako tayari kuingia nchini kuanza kazi hiyo ya mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie habari ya umeme. Namshukuru Waziri ametenga shilingi bilioni kumi kuunganisha gridi ya umeme Tabora na Kigoma. Hii ni hatua moja nzuri sana inayofurahisha. Nampongeza Waziri kwa hilo. (*Makofi*)

Lakini hakuna kinachosemwa katika mipango lazima uonyeshe kwamba unatoka wapi na unakwenda wapi. Umeme wa Kasulu na Kibondo hauzungumziwi na sisi tumekuwa tunalia 1995 Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Mkapa alikwenda Kigoma akafika Kasulu akasema mtakaposikia umeme umewaka Masasi na hapa Kasulu utawaka. Tunaingia kipindi cha tatu hakuna mpango wa umeme Kasulu na ni Wilaya ya miaka mingi Kibondo halikadhalika.

Tunafurahi umeme unakwenda Kigoma sasa lakini wakitueleza lini umeme utafika Kasulu itakuwa vizuri watueleze hilo! Pale Kasulu ziko min hydro tatu, *min hydro* ya Mwoga, *min hydro* ya Kabanga na *min hydr*o ya Nyasogu kule *Heru Mission Hospital*. Zina uwezo wa kutoa umeme kwa vijiji vinavyozunguka sehemu hizo.

Tumeshazungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri, nina imani watakapozungumza watatueleza kwamba ni namna gani watatusaidia hasa ile ya *Heru Mission* ambayo tayari mazungumzo yamekwishaanza na hii nyingine ya Kabanga na hii ya Mwoga kupeleka umeme Heru Juu nazo zizungumziwe watueleze watatupatia umeme namna gani maana kinachotakiwa hapa si kuzungumza na hawa hawana *capacity* ya kutupa umeme. Tunataka umeme uende vijijini na wao waanze kuona haya matunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia habari ya matatizo ya Wizara hii yako mengi. Miaka iliyopita Rais wa Awamu ya Tatu alikuwa anakwenda Ulaya anaita wawekezaji waje hapa nchini na watu wetu wakaelewa *there is seriousness* katika kuita wawekezaji kuja nchini. Waziri Mkuu, aliyekuwepo naye akafanya hivyo hivyo. Wamekwenda Uswiss, wamekwenda Ujerumani, wamezungumza haya na watu wamevutika, watu wetu wameandika barua wakapeleka nje kutumia *chamber of mines* wakapeleka huko Ulaya. Kuna kampuni moja inayoitwa *Madinga and Madinga Company Limited*. (*Makofi*)

Wiki tatu zilizopita mimi nilienda *Vienna*, kule *Vienna* kuna wazungu waliosikia mimi niko pale, walikuja kuniona, wakaniamba bwana sisi tumekuja kukuona kwa sababu kule kwenu mnapenda sana *investors* waje. Lakini tuna masikitiko yetu. Sisi tumemsikiliza Rais wenu wa Awamu ya Tatu, tumesikiliza Waziri Mkuu wenu, tumevutika. *Madinga and Madinga Company* waliandika barua ikaja hapa, ikafikia kwenye *chamber*.

Kuna *chamber* pale Vienna ambayo bahati mbaya au nzuri mimi niliwahi kufanya kazi pale Austria taasisi iitwayo Autrian *Federal economic chamber*. Sisi tulipoiona tukafanya *due diligence* ya kwetu tukamchunguza huyu Madinga tukakuta *he is genuine* Tukaanza mawasiliano nayo mwaka 2001. Mwaka 2002 mwezi Februari wakaja hapa nchini, walipokuja hapa wakaamua sasa tunaanzisha kampuni wakaanzisha kampuni inayoitwa (*NMM) Madinga and Madinga Company Join Venture Limited*. (*Makofi*)

Kampuni hii ilipoanzisha hawa jamaa nao wakaingia kwenye *field, field* yenyewe iko Simbangulu Dodoma Vijijini hata hapo tulipo Waheshimiwa Wabunge, Dodoma Vijijini wakaja Dodoma Vijijini, wamekwenda pale wakaanza kazi yao ya *exploration*. Leseni zote zikiwa sawa kila kitu kikiwa sahihi. Mwezi Septemba wamepata madini wakagundua kwamba kuna kati ya aunzi 280,000 mpaka 300,000 katika kilomita 80 mpaka 90 walizokuwa wamefanyia *exploration*.

Walipogundua wakaandika *a pre-feasibility rerport*. Ile ripoti wakaipeleka Wizarani, wakaipeleka *TIC*, wakaipeleka kwa *Regional Commissioner Dodoma*, wakaipeleka Madini Dodoma na wakaisambaza mpaka kile chuo chetu kilichopo Kunduchi Dar es Salaam. Ilipopatikana pale Wizarani wakaomba sasa wafanye kazi. Bahati mbaya sana walipoandika habari ya kugundua dhahabu mwaka 2003 mwezi Machi, zikaanza hoja za kuwafukuza hawa wawekezaji.

Hizi hoja zilipokuja wakasema tunafanyaje tunaiona Wizara? Hawa wakamuona Naibu Waziri, ambaye ndiyo Waziri wa Wizara hii, Waziri akawaambia tunalishughulikia mwaka 2003/2004 limekwenda mpaka leo, wamemwona Naibu Waziri aliyopo, Naibu Waziri naye anasema tunalishughulikia miaka mingapi unalishughulikia jambo jamani bila uamuzi? (*Makofi*)

Afisa wa Madini aliyeko Dodoma alikwenda kwenye ofisi ya hawa jamaa akiwa na watu 4 watatu wenye asili ya Kiasia na mmoja mzungu wa Afrika Kusini, akawaambia

hawa kwenye ofisi yenu nataka m-*pack* muondoke hapa maana hili eneo limeshagawiwa kwa mtu mwingine. Kuna *serious double allocation* inayofanyika. Hawa wazungu walinieleza mimi nikachanganyikiwa nikasema hivi nchi yetu tunafanya nini? *We are saying tuna encourage investors* leo tunawa-*frustrate* kiasi hiki.

Fedha waliyokwishatumia ni zaidi ya shilingi 8 billion na wameleta *investment* pale na walikuwa wamezungumza na kampuni nyingi ya Sweden ya kufanya kazi hii ili ije nayo wasaidiane nayo. Tumewa-*frustrate* leo hawajui la kufanya, Wizara inawaambia tunashughulikia wapo tu wanakula fedha, fedha zao na wala hawajui la kufanya. Sasa wale wakasema sisi tungekuwa watu wabaya kuna mambo mengi tungukuwa tumefanya, *sky news* wanayo hii habari, hawa jamaa walipopata hizi habari wamechukua habari zetu wakazipelekea *London Stock exchange* wakapewa na fedha, lakini walizopeleka kule ni habari zetu, *how could it be possible* kwamba wanakwenda kufanya *due diligence* kwenye sehemu ambayo tayari ilikuwa na *dispute* kama Waziri alivyowaambia 2004? *It is very disappointing*. Tunataka *investors*. Hivi hii ndiyo *style* itakayotufanya tuendelee? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo mengi muda wa dakika 15 hautoshi ungenipa dakika 30 ningeeleza mambo ya ajabu kuna *horror stories* ninazo *evidence* hapa na *horror stories* za *Liganga and Mchuchuma* hapa ninazo. *Horror stories about* hiki ninachozungumza hapa, zote hizi ni *evidence* za haya majambo sizungumzii hisia. *I have never done that, I am a researcher. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Taifa hili kama tunataka kuendelea ninaomba hoja hii ya Simbangulu ijibiwe kwa uhakika tunapata aibu. *Imagine* wewe ulikuwa ni Mtanzania ndio unaulizwa maswali haya ya jinsi ambavyo Serikali yetu haifanyikazi vizuri, *it is a shame*. Tufanye kazi tuonyeshe kwamba *we have an interest in this nation* hizi hela ndogo ndogo zitatufukisha wapi? Hapa kuna mazingira ya rushwa na hatuwezi kukwepa hapa mazingira ya rushwa yapo. Tufanye kazi. *We need a commitment to the development of this country*. Nchi hii inakosa viongozi ambao wana *commitment*. Hata sisi humu sidhani kama tuna *commitment* inayotakiwa, *South East Asia transformed their economies in ten years, ten years was enough to change landscape of development* kule Asia. (*Makofi*)

Leo haiwezekani tuingie madarakani na kasi mpya na nguvu mpya na ari mpya kisha mambo yawe hivyo hivyo *ten years.* Watu wetu wana haki ya kutaka kuongozwa na viongozi wanaoweza kutoa maamuzi. Tufanye maamuzi ndani ya Wizara zetu na tusiogopa watu wanaoweza kuisaida nchi hii. Nchi zote zilizoendelea zilisaidiwa na watu wenye nguvu na wenye uwezo mkubwa wa kutenda mambo: *Make decisions*. Ofisa anakwenda kunyanyasa watu na wewe upo leo hivyo hivyo, *commission* anaandika watu hao Wafukuzwe waondolewe hapo wapewe wengine zote ninazo hapa. Mwingine ananiambia na yeye ameniambia na yeye ameipata hiyo habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba katika uchunguzi tuliosema ufanywe ambao Mheshimiwa Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji, ameeleza jambo hili

liingizwe humu ndani uchunguzi ufanywe juu ya kiwanja hiki na uamuzi utekelezwe na watu waruhusiwe kufanya kazi nchi hii ipate kwenda mbele yako mengi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ombi tu, ningeomba Mheshimiwa Mporogomyi unifikishie hapa mezani hayo ili na mimi niyafikishe rasmi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu najua Waziri Mkuu tuliyenaye siyo mtu wa aina hiyo. Kwa hiyo, najua hatua zitachukuliwa. (*Makofi*)

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Kabla sijaanza kuchangia hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba nichukue nafasi hii, kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo wamefanya katika mchakato mzima wa kumtafuta na kumpata Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, pamoja na safu nzima ya uongozi wake. Nadhani Bunge lako Tukufu, litakubaliana na mimi kwamba niwapongeze wale wote waliopata nyadhifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wawili Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake kwa kazi nzuri waliyofanya na kuwasilisha Bajeti yao mbele ya Bunge lako tukufu. Nianze na Sekta ya Nishati na Madini. Sekta ya Nishati ingeweza ikachangia sana uchumi wetu kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyo sasa hivi. Ukizingatia kwamba mchango wa taifa katika sekta hii ni asilimia 3.2 mwaka 2004 pia mwaka 2005 ikapanda kidogo kwa asilimia 3.5 kiwango hiki ni kidogo sana ukilinganisha na madini yanayotoka katika nchi yetu ya Tanzania. Tuna madini aina nyingi, tuna *diamond*, tuna *Tanzanite* tuna *Safire*, tuna *rub* tuna madini mengi katika nchi yetu ya Tanzania ambayo hata mengine majina yao hatuyajui. Yanaweza kuingizia taifa hili fedha nyingi. Lakini unasema kwamba pato la taifa katika sekta hii ni asilimia 3.5 inashangaza kwamba eti kila mwaka inaongezeka tu kidogo *point* 3 mwaka mwingine tena kidogo *point* 3. hii haieleweki kabisa kutokana na uvunaji wa madini tunayoyapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nachukua rai hii na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kauli yake aliyoitoa kwamba mikataba hii irudiwe upya na pia uundwe utaratibu mwingine mpya siyo ule wa zamani ili tuone kwamba mwananchi wa kawaida na Serikali pia inaweza ikafaidika kutokana na rasilimali hii. Mimi nimwunga mkono kabisa na naamini kabisa Bunge lako tukufu, litaunga mkono kupitia ile mikataba na Waheshimiwa Wabunge, wahusishwe na huo Muswada uletwe hapa Bungeni ili tuweze na sisi kuujadili na kuuweka mbele yetu tuone ni jinsi gani na sisi tutaweza kufaidika na rasilimali hii ambayo Mungu ametupa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikizungumza habari ya mikataba eti kwa upande wa Mererani *Tanzanite Mine* utakuta mwekezaji amepewa mkataba wa miaka 25. Haya madini ya *Tanzanite* ni madini ya vito ambayo yanakwisha. Yaliwahi kuchimbwa kule Marekani zamani na hata leo utaona kwamba hayajulikani tena wala Marekani

hawakumbuki tena kwamba waliwahi kuwa na madini kama yale. Sasa katika nchi yetu ya Tanzania yale madini tunawapa wawekezaji wao wanakwenda kujenga kwao sisi tunabaki na nini? Ukiangalia Mererani hakuna maji hakuna barabara, hakuna maendeleo yoyote, tunapata nini. Wao wanachukua madini wanakwenda kujenga kwao. Sisi tunabaki kusema nini hivi haya madini yatakapokwisha tutathubutu kusema kwamba haya madini ya *Tanzanite* yalichimbwa Tanzania kweli? (*Makofi*)

Haya tukizingatia tena miaka iliyopita Serikali yetu tunataka iwe makini sasa iamke kwa sababu zamani majangili waliwahi kuchimba madini haya ya *Tanzanite* wakiyapitisha kinyemela wakaenda wakauza Kenya. Baada ya muda mrefu sana Serikali haina habari tumesikia kwamba Kenya imepata zawadi ya ndege. Sielewi kama Tanzania ilikuwa wapi wakati huo, Serikali yetu ilikuwa wapi mpaka nchi nyingine jirani inapata zawadi ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kusafiri kwenda nchi za nje wakati ule Sweden na Marekani wakati wa Rais wa Awamu ya Tatu, wafanya bishara tulipata nafasi hiyo. Kwa kweli maswali Watanzania waliokuwa wanamwuliza Rais wetu ilikuwa ni aibu kwa sababu yalijitokeza pale, kwamba iweje Kenya ipewe zawadi ya ndege Mheshimiwa Rais. Kwa kweli naomba sasa tuamke tuangalie tusije tukalia baadaye tukasema kwamba hatukujua wakati madini haya yatakuwa yamekwisha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu na Serikali yako iangalie sana na kufuatilia jinsi ya kuweka hii mikataba vizuri, pamoja na kwamba hawa wawekezaji nasema wanalipa kodi. Lakini kiasi hiki cha kodi kinacholipwa hakitoshelezi hata kidogo. Hii asilimia 100.5 mimi nafikiri hiki kingetolewa tu na *Tanzanite. Tanzanite* ni madini pekee duniani yana thamani kubwa. Mimi nakumbuka miaka 20 iliyopita *Tanzanite* kidogo kama ukucha wangu ilikuwa shilingi 2,500/=, lakini sasa hivi *Tanzanite* kadogo hivi kama punje ya mbegu ya njegere ni shilingi milioni moja.

Na haya madini hayapatikani moja moja ardhini, yanapatikana kwa *pockets* wanasema kila mara unavyokwenda mbele unapata zaidi. Kwa hiyo, tuangalie sana eneo hili kwamba kweli tumeachwa mbali, bila kujua kwamba watu wengine wanavuna wanakwenda kujenga kwao na sisi tuachwe hapa hatuna mbele wala nyuma. Nikirudi kwa upande wa wachimbaji wadogo wadogo, hawa wachimbaji wadogo wadogo tena ni watafutaji wazuri. Ni watafutaji wazuri wa kujua miamba, miamba ya kuchimba madini. Wao wenyewe wanaweza tukawaajiri wao, tukachimba, Serikali kwamba kodi ni kubwa, hawa wachimbaji wakawa wananufaika pia na nchi yetu na nchi yetu ikanufaika na madini hayo.

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali kwa kuwa sasa imeshajua faida ya madini haya, imeshajua namna ya kuwatoza kodi, imeshajua namna pia ya gharama ya kuanzisha migodi mikubwa mimi ningeiomba Serikali isimamie hapo, ianzishe migodi mikubwa kama hiyo ya *Tanzanite* kuliko au kuwaleta wawekezaji kila mara wanakuja kutuchimbia wakati hawaleti utaalam wowote, utaalam tunao hapa, vyombo tunavyo hapa na wale watu wanaochimba ni wale wale wanawachimbia ndiyo hao hao watakaotuchimbia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tungeangalia eneo hilo kwamba tusikubali tena kuwaachia wawekezaji. Tuchimbe madini hayo wenyewe na tuweze kufaidika na hii rasilimali pekee. Ninarudi upande wa migogoro. Imetokea migogoro mara nyingi kuhusu wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, hii migogoro haitaisha kwa sababu kila mmoja anataka kuvuta upande wake, hasa yule mwenye nguvu zaidi anataka avutie upande wake. Kwa kweli hapa tunataka Serikali iangalie sana ione ni jinsi gani tutakavyoweza kuwapatanisha hawa watu wachimbe kwa amani, kwa sababu sasa kila mara migogoro, haina maana. Ukiangalia upande wa wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji waodgo wadogo nao wana akili sana, pamoja na vile vitalu wanavyopewa 50 kwa 50 wao wenyewe wanatobozana mara kwa mara. Lakini wanaitisha Kamati wanakubaliana, wanawekeana mipango mizuri, na wanaendelea na uchimbaji wao. Lakini inapotokea kwamba wametobozana na Kampuni kubwa hapo tayari ni marisasi, ni hapa na pale, ni maneno, ni kuwekwa ndani na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yako iangalie jambo hili na iweze kuangalia wachimbaji wadogo wadogo waweze nao kupewa haki wasiwe wananyanyaswa katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka tena kuna jambo ambalo linazungumzwa mara kwa mara kwamba huu mgogoro wa wachimbaji wakubwa na wadogo. Iliundwa Tume ya Generali Mbona na tukiangalia Tume inapoundwa, watu wanatumia fedha za Serikali na fedha nyingi zinatumika. Kwa hiyo, tuangalie ile Tume ilifanya nini? Kwa nini basi baada ya ile Tume hakuna majibu yoyote waliyoyaleta ili tujue kuwa kulikuwa na nini, kulikuwa na tatizo gani. Wachimbaji wadogo wa Mererani wanauliza hilo, kila mara tunapokwenda kule tunaulizwa je, ile ripoti ya Mboma vipi, mbona mmeinyamazia? Kwa hiyo, sisi Wabunge tunaonekana kwamba tumeinyamazia. Naomba kwa kweli tupate jibu ya hiyo ripoti ya Generali Mboma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi labda niendelee tena kwa upande mwingine kwamba Serikali iwe na mipango mizuri ya kuweza kuweka, kusimamia haya madini, kwa sababu gani, hawa wanaochimba na kusema kwamba wanalipa kodi, je, kuna udhibiti kweli wa wewe kujua kwamba wale watu wanapata kiasi gani na wanalipa kodi kiasi gani? Ningeomba Wizara iangalie hilo. Iangalie namna ya kuwadhibiti wale wawekezaji kwa sababu madini yanapotoka ni sawa na vile umempa mtu shamba, wewe ukaondoka ukaenda zako mbali, wakati unarudi anakuambia mimi bwana niliotesha mahindi pale nikapata mahindi magunia 100, kumbe alipata 10,000. Kwa hiyo, hata akikupa gunia mbili hapo wewe unakubaliana naye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba haya mambo yaangaliwe, Serikali ijaribu kuweka mikakati mizuri katika uchimbaji huu ikiwa ni wachimbaji wadogo wadogo, ikiwa pia ni wachimbaji pia wakubwa, Serikali isimamie kikamilifu. Ijulikane kwamba haya madini yanayotoka ni kiasi ili basi yaweze kutusaidia na kusaidia Taifa letu hili. Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi naunga mkono moja kwa moja kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nami kwa kupewa nafasi hii ili niweze kuchangia kidogo katika Bajeti hii ya wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini. Naomba nianze moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kama kuna bajeti ya Wizara au Serikali iliyokonga nyoyo za wananchi wa Kusini basi ni bajeti hii ya Wizara ya Nishati hususan upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Kusini. Yaani kila tukijiuliza wenyewe umeme toka Liwale kwenda Nachingwea, kwenda Masasi, kwenda Newala, kwenda Tandahimba, kwenda Mtwara, kwenda Lindi mpaka Ruangwa, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Na sisi watu wa Mtwara na Lindi tuna neno letu la kabila tunasema KUCHELE, kuchele maana yake kumekucha. Na maana hiyo ya kumekucha ni kwamba giza sasa imeondoka na mwanga umeingia na ndivyo tunavyoupokea mradi huu wa nishati ya umeme itakayotokana na gesi toka *Mnazi Bay.* Tunasema kuchele. Kwa namna ya pekee nataka kumpongeza sana sana Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ameonyesha ujasiri wa ajabu wa kuiokoa mikoa ya Kusini katika maamuzi yake. Ni juzi tu tulipokwenda na Waziri Mkuu, kwenda huko Mnazi Bay. Kule tulikwenda kuona kazi gani imefanyika. Naamini Waziri Mkuu mwenyewe alishikwa na butwaa kuona maendeleo na kazi kubwa iliyofanyika na wale ndugu zetu wa *ARTMAS* sasa naona hata kabla Rais hajaondoka kwenda Nigeria, Waziri Mkuu bila shaka alimwona na katika kumwona Rais mara moja, kwa kasi ya ajabu amesema mradi huu utekelezwe. Kwa hiyo, sisi tunashukuru sana sana. Kwa sababu maamuzi ya namna hii ndiyo yanayoleta mabadiliko mengi kwa wananchi au kwa maisha ya watu kwa baadaye. Kwa hiyo, kwa mfano huu tuliouona katika mradi huu sisi watu wa Kusini tunashukuru sana. Pili nataka kumshukuru Waziri Mkuu mwenyewe ameonyesha ni mtu wa mwendo wa kasi ya ajabu. Si rahisi kwa watu wote kufuata kasi yake. Lakini yeye aliona baada ya kuona akaamini, akakubali akaamua kwamba ni lazima Serikali ijitahidi kwa kila njia kukamilisha mradi huu uwe ukombozi kwa watu wa Kusini. Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Wabunge, suala la gesi ya Mnazibay msione linaelea tu. Huko zamani, ilikuwa imegubigwa na urasimu mkubwa kiasi kwamba hatungefikia hatua hii ya leo. Katika kuliona hili Waziri wa Nishati aliamua kutushirikisha sisi Wabunge wote wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na nasema haijapata kutokea. Sisi tulishirikishwa, viongozi wa Mikoa wa Chama na Serikali nao walishirikishwa pamoja na Kampuni inayowekeza *Mnazi Bay.* Pamoja na Serikali katika kuzungumza tukaja na mkakati ambao ulipelekea kwamba mradi huu uende upesi na si hivyo tu Waziri alikuwa ameamua kwamba Wenyeviti wa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara ambaye ni mimi mwenyewe pamoja na Mkoa wa Lindi, Ndugu Mudhihir, sisi kwa pamoja tuingie katika yale majadiliano rasmi ya Serikali. Kwa pamojas tukafanikiwa kuunda mkakati uliopelekea mafanikio haya. Hatimaye Waziri aliamua Wenyeviti wa Wabunge wa Mtwara na Lindi washiriki moja kwa moja katika majadiliano.*(Makofi)*

Na sisi tulikwenda kule. Nashukuru kwamba tumeona wenyewe, ni kitu gani kilichokuwa kinakwamisha na tukasaidia sana katika kutanzua matatizo yaliyokuwa yanajitokeza hata kama ni ya kitaalam, lakini sisi tuliingiza siasa yetu, wataalam wakatuelewa, kampuni ile ya *ARTUMAS* ikatuelewa, Serikali ikatuelewa, hatimaye tukaja kufikia makubaliano mazuri tu. Sasa mimi nasema huu ni mfano wa kuigwa. Ni mfano wa kuigwa katika sehemu zile zenye miradi mikubwa mikubwa. Mathalani wenzetu wa upande wa Magharibi tumesikia jinsi walivyochangia katika Bunge hili na inaonekana dhahiri kwamba kule kwa wenzetu kuna matatizo makubwa katika uchimbaji wa madini. Sasa mimi nimeona kwamba wale pia kama wangeshirikishwa kama sisi tulivyoshirikishwa katika mradi wa Mnazi Bay nadhani matatizo haya na malumbano yangepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuishauri Serikali kwamba ifanye utaratibu wa kuwahusisha pia hawa wawakilishi wa wananchi katika ile migodi mikubwa. Hili linawezekana, sisi tulishirikishwa mambo yetu yamekwenda vizuri. Ninachosema, sisi tulishirikishwa katika majadiliano yale kama watazamaji *Obsevers* si kama Wakurugenzi. Lakini kama watazamaji, kwa hiyo nilikuwa nafikiri pia katika hii miradi mikubwa mikubwa ya uchimbaji madini katika Bodi zile kwa sababu kama ukiwaambia wale wawekezaji kwamba muwaingize katika Bodi zetu Wabunge inawezekana watakataa. Lakini kama tuna kanuni inayosema kwamba mnapokuja kuchimba madini basi kuwe na utaratibu wa hao wawakilishi wa wananchi wawe watazamaji. Nafikiri hilo linawezekana na mambo yanaweza kabisa kabisa yakaji-*solve* yenyewe. Tukiacha kama hivi ilivyo, kwa vyovyote kutakuwa na kutokuelewana, kutakuwa na kulaumiana, na kutakuwa na kutupiana matope.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri sana Serikali iliangalie jambo hili. Lakini wakati wa kuchagua labda watazamaji au waangalizi, tuhakikishe kwamba wanatoka katika maeneo yale. Kwa sababu itakuwa siyo vizuri mgodi wa Geita, halafu anachaguliwa tuseme Mbunge wa Mafia aende kule akaangalie. Kwa vyote vyote vile haitakuwa sawa. Au kunichagua mimi Mrope nikaangalie au nikazungumzie mambo ya kahawa, mimi kahawa siifahamu. Au hivyo hivyo mtu wa bandari kwa mfano, kwenye maji ya bahari, umlete Mmasai pale. Kwanza Mmasai anaogopa maji ya bahari. Sasa najaribu kutoa mifano ambayo haitafaa katika uwakilishi, ikiwa tutawachagua wawakilishi hasa hasa wa maeneo yale naamini naamini haya matatizo yatakuwa yametoweka. Naomba sana Mheshimiwa Waziri vile tulivyofanya sisi wa Mtwara na Lindi hebu jaribu ufanye hivyo kwa wenzetu hawa. (*Makofi*)

Lakini hii ya leo wala hakuna sababu ya kutoana na shilingi, maana lugha ya kule shilingi moja haieleweki. Sasa wanaweza tu kuona mfano wetu sisi washiriki kikamilifu. Hata katika hii mikataba ambayo tunasema ipitiwe. Mimi ningeshauri sana Waheshimiwa Wabunge wa maeneo yale, washirikishwe kwa sababu ukiwaachia wataalam, wataalam hao ndiyo kwa namna moja au nyingine waliotuingiza hata katika migogoro yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa utawachukuaje hawa peke yao? Ni lazima tuwachague au tuwachukue wawakilishi wananchi ili waweze kuangalia mle namna gani wanavyoweza kuisaidia Serikali.Nilitaka pia upesi upesi kuzungumzia suala la umeme vijijini suala hili ni muhimu sana na tunaiomba Serikali ifanye utaratibu wa makusudi wa upendeleo kuhakikisha nguzo na nyaya zinapelekwa vijijini. Hili suala la kwamba huko vijijini kama mtu anataka umeme alipe sijui laki moja, laki mbili, laki tatu, aunganishiwe. Haya jamani haifai, nani ataweza? Wananchi vijijini hawana uwezo wa kiulipia njia za umemne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbona tunajenga barabara. Je, tunawatoza wanavijiji kwa ajili ya kupita katika barabara zile? Sasa kwa nini tusitengeneze barabara hizi za angani, yaani nyaya ili wananchi wawe wanalipia tu kodi ya kawaida ya kutumia ule umeme badala ya sasa hivi. Kwa kweli inakuwa vigumu kweli kweli kwa wanavijiji kutumia umeme kwa sababu ya gharama kubwa. Na utakuta katika sehemu nyingi katika vijiji ambapo wamepata umeme nyumba ya mzee labda anaweza kuwa na taa moja au glopu kwenye paa, hiyo moja inaangalia kwenye vyumba kama sita na wa kuwasha ni Mzee mwenyewe peke yake. Ukifika saa 3 saa 4 ameshazima, huna ruksa kuwasha. Hii yote wazee hawa wanaogopa gharama kubwa za umeme. Kwa hiyo, tukitaka *rural electrification* ya sawasawa ni lazima Serikali iamue kwamba tutapeleka barabara za umeme. Naziita barabara za umeme makusudi, tutapeleka barabara za umeme kwa ruzuku ili wananchi walipie tu bei ya kukodi mita au kitu kingine yaani kodi tu ya kawaida. Namna nyingine hatutaendelea katika nchi hii. Na hiyo iwe kabisa kabisa ni kwa makusudi, makusudi kwamba Tanzania tunataka kupeleka umeme vijijini. Kwa hiyo, hakuna cha kulipia mabarabara haya. Walipe tu moja kwa moja kutokana na zile t*ariffs*.

Sasa mwisho kabisa ninaomba katika Jimbo langu ni kwamba mradi huu wa Mnazi Bay tafadhali sana naomba wakati tunatoa kipaumbele, umeme huu toka Nyangao upite Mkwera, Chipite, Nanganga, Nangoo, Liputu, Ndanda, Chikundi, Mbaju, Liloya, Marambo mpaka Masasi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, umepitiliza kidogo, nilivumilia kwa sababu ulikuwa unataja vijiji vya jimboni kwako. Namwita sasa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Kwa faida ya wageni tu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ni Mbunge wa Wawi, Pemba, Chama Cha CUF na ndiye kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge kwa faida ya wageni wetu. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Kwanza naomba kunukuu Katiba ibara ya 63(2) inayosema hivi. Sehemu ya pili ya Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na

vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. Nataka kuzungumzia sana suala la kusimamia.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili Tukufu pia tumepitisha Sheria ya Maadili na Haki za Bunge Na. 3 ya mwaka 1998 kifungu cha 10 ambacho kinaipa madaraka Bunge kudai nyaraka mbalimbali na taarifa mbalimbali na kuwalazimisha watu hao kutoa taarifa kwa Bunge. Kwa hiyo, kwa kuangalia misingi hii miwili ya Katiba na Sheria ni haki ya Bunge kwa niaba ya wananchi wa Tanzania kudai mikataba na nyaraka mbalimbali zitakazowasaidia Wabunge kwa niaba ya wananchi wa Tanzania kusimamia kikamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kuweka wazi kwamba hili ni jambo la kikatiba na la kisheria. Lakini si suala la kubembelezana. Lakini Bunge lako Tukufu tu ni kwamba wakati wote lilikuwa linashauri shauri bila kuangalia kifungu hiki cha kusimamia. Kwa hiyo, nasema hii ni haki ya Katiba na tunaomba Serikali itufahamu hivyo. Kwa sababu wao na sisi pamoja kama alivyosema Rais Kikwete, mdau wetu ni mmoja tu, ni Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama wenzetu wana wadau wengine ndiyo maana hawataki kutupa hizi nyaraka na vielelezo vingine basi ni suala lingine. Lakini nasema mdau wetu ni mmoja, ni Mtanzania na tuna haja ya kujua kwa undani yale yanayotokea Tanzania. Natangulia kusema haya kwa sababu kwanza naungana kabisa na Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji kwamba kutokana na mazingira yanayojitokeza katika nchi yetu ya uwekezaji na hasa rasilimali ya nchi hii ambazo haziwafaidii Watanzania. Tuna ushahidi wa kutosha kabisa mwaka 2004 katika Bunge lako hili tukufu, tuliwasilisha Taarifa ya *Public Accounts Coomittee* yaani Kamati ya Hesabu za Serikali, ndani yake kulikuwa na nyaraka za siri za Kampuni ya *Williamson Diamonds* na Kampuni inayonunua almasi zetu. Mkataba wa siri unaowapa Kampuni hiyo ya London umiliki wa kununua almasi zetu za Tanzania bila kupewa mtu mwingine yeyote.

Kama hatukuunda Kamati sisi kuchunguza hilo mkataba ule tusingeuona ni baada ya kuandika barua mzito kwa wahusika kwamba lazima mtupe huo mkataba vinginevyo tutawapeleka Mahakamani. Ndiyo tukaupata, ninao hapa. Huu hapa. Huu ni mmoja tu, kuna mifano mingi sana. Serikali imejitoa katika kuwapa ruzuku Mashirika ya umma. Leo soma kitabu cha Mapato ya Matumizi ya Wizara, kifungu 28714 Ruzuku ambayo Wabunge hii hawana wamepewa Kamati tu. Serikali inaipa ruzuku *IPTL* bilioni 18. Tunauliza kwanza *IPTL* ni ya nani, ni ya Serikali?

Serikali inatoa ruzuku nyingine kwa ajili ya kupanda kwa bei ya mafuta ya bilioni 3 kwa *IPTL* wakati huo huo *IPTL* ambayo ndiyo *owners* wa mitambo ile *TANESCO* ndiyo wanaorepea mitambo hiyo, *TANESCO* ndiyo inayolipia mafuta hayo. Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya kufidia gharama za umeme, mbona bei ya umeme haipungui? Serikali hii ilisema katika sera zake inajiondoa katika kuyahudumia Mashirika yetu ya umma kwamba haiwezi tena kuwalipia ruzuku. Leo inatoa ruzuku ya nini? Sasa haya ni maswali ya msingi Wabunge kwa niaba ya wananchi ya kuisimamia Serikali wanataka kuelewa.

Kwa hiyo, tunapodai Kamati ya Bunge tunadai katika misingi ya Katiba na Sheria. Na mimi nasema kwamba nitashangaa sana, nitashangaa sana sisi wawakilishi wa wananchi kama tutakataa kuunda Tume ambayo itaisaidia Serikali yenye nia ya kuwaendeleza wananchi isiipitishe Tume hiyo kuisaidia Serikali katika kusimamia mikataba hii ambayo ina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ndiyo lilikuwa la kwanza. Lakini la pili, ukitizama kitabu cha mapato katika ukurasa wa mapato katika kitabu hiki hiki cha Wizara tulikuwa na shirika linaitwa *TANSOLT* ambalo Waziri katika hotuba yake amesema sasa wanaliondosha London kulileta hapa. Katika kitabu hiki tulitegemea tutaona sehemu ambayo *TANSOLT* inaleta mapato. Ukiacha pale ambapo sisi tulimalizia sisi kufanya *Performance Auditing* hailezei tena Serikali inapata mapato kiasi gani kutoka *TANSOLT* kwa mujibu wa kitabu hiki hapa. Je, Wabunge tunaposema tunataka kuunda Tume chunguza haya kuna dhambi gani? *(Makofi)*

Serikali inatoa ruzuku nyingine kwa ajili ya kupanda kwa bei ya mafuta kwa *IPTL*. Wakati huo huo, *IPTL* ambao ndio *owners* wa mitambo ile, *TANESCO* ndio wanao-*repair* mitambo hiyo na ndio inayolipia mafuta haya. *(Makofi)*

Sasa kama Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya kufidia gharama za umeme, mbona bei ya umeme haipungui? Serikali hii ilisema katika Sera zake, inajiondoa katika kuyahudumia Mashirika yetu ya Umma, kwamba haiwezi tena kuwalipia ruzuku, leo inatoa ruzuku ya nini? Sasa haya ni maswali ya msingi, Wabunge kwa niaba ya wananchi, kwa kuisimamia Serikali, wanataka kuyaelewa. Kwa hiyo, tunapodai Kamati ya Bunge, tunadai katika misingi ya Katiba na Sheria. Mimi nasema nitashangaa sana sisi wawakilishi wa watumishi, kama tutakataa kuunda Tume, ambayo itaisaidia Serikali, yenye nia ya kuwaendeleza wananchi, katika kusimamia mikataba hii ambayo ina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ukitazama kitabu cha mapato hiki hiki cha Wizara, tulikuwa na shirika linaitwa *TANSORT,* ambalo Waziri katika hotuba yake amesema, sasa wanaliondoa London kulileta hapa. Katika hili tulitegemea kuona sehemu inayoonesha *TANSORT* inaleta mapato. Ukiacha pale ambapo tulimalizia sisi kufanya *performance auditing,* haielezei tena Serikali inapata mapato kiasi gani kutoka *TANSORT,* kwa mujibu wa kitabu hiki hapa. Je, Wabunge tunaposema tunataka kuunda Tume, kuchunguza haya kuna dhambi gani? Tunakataa kwa manufaa ya nani?

Mimi nasema tuzungumze kama Watanzania, kama wawakilishi wote wa Tanzania, kama mdau wetu ni mmoja Mtanzania, kama alivyosema Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tunauliza haya si kwa sababu ya kuiandama Serikali, ni kwa sababu ya kutetea maslahi ya nchi hii. Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alipokataa huko awali, tusiingie kwenye miradi hii mikubwa ya madini, alielewa uwezo wetu wa kuweza kudhibiti haya mambo kwamba, nchi itabaki jangwa tu, rasilimali zote zitachukuliwa. Kwa hiyo, akaona na rasilimali zetu ni ndogo, tuache kwanza Watanzania waelimike ili waweze kuhodhi mali zao. Leo tumeshaelimika, bado Watanzania tunaendelea kusema

kwamba, rasilimali hazitutoshi, nchi hii haina tatizo la rasilimali, ina tatizo la menejimenti ya rasilimali zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio tatizo letu la msingi, hatuhitaji msaada wa mtu yeyote, leo asubuhi kabla sijaondoka nyumbani, alikuja mzee mmoja, alikuwa *STAMICO* zamani, akasema sisi hatuwafuatilii hata watu wanaojenga barabara zetu. Wanaojenga barabara anasema wakifika mahali ambapo kuna madini, ndio maana wanachelewesha *contract* za kujenga barabara, kwa sababu wakikuta madini, wanasema hapa kwanza tuvune. Sisi tunachelewa kujenga *contract* ya barabara, ni mzee kabisa alikuwa *STAMICO* zamani. *Do you know that*, kuna mtu anafuatilia?

Mheshimiwa Spika, hivi ndio rasilimali zetu zinavyokwenda. Kwa hiyo, hatuna tatizo la rasilimali, tuna tatizo la menejimenti ya *resource* zetu. Tunahitaji kushirikiana pamoja Wabunge wote, Serikali na wananchi wote, kuhakikisha hii rasilimali iliyopo inavunwa kwa maslahi ya Watanzania. Hili ndilo jambo la msingi, ambalo nataka kulizungumzia. Kwa hiyo, nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri, atueleze hizi shilingi bilioni tatu tunazowapa *IPTL;* kwanza *IPTL* ni ya nani na ni za nini hizi fedha? Kwa nini Serikali ilikataa kutoa ruzuku kwa mashirika ya umma, leo inatoa ruzuku kwa kampuni binafsi?

Tunataka maelezo kwa nini *TANSORT,* mapato yake hayajulikani hivi sasa hayamo katika kitabu chao, tunaona tu *TANSORT* itapewa shilingi 1.2 bilioni za kutumia; je, wanacholeta ni nini na sisi tunajua wanapata asilimia 4.5 kwa kila kareti ya almasi inayopelekwa nje. Iko wapi hii, haimo katika vitabu vyao! *These are basic questions,* tunaomba kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala la gesi na mafuta. Hivi karibuni kulikuwa na kikao cha Waziri Mkuu, Waziri Kiongozi na timu zao, Watanzania tukafikia mahali tukaamini kwamba, sasa ufumbuzi wa matatizo ya mafuta ya Zanzibar utapatikana. Lakini bado tumerudi pale pale kwenye *square one*, tulionana na jamaa wa *TPDC* jana hapo, bado wanasema tatizo liko palepale, mafuta ya Zanzibar hayawezi kwenda kuchunguzwa kwa sababu bado hatujakubalina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingeshangaa kama ingekuwa kule kuna chama kingine na huku kuna chama kingine, kula kuna Serikali nyingine na huku kuna Serikali nyingine. Miaka 40 tunashindwa kupata ufumbuzi wa tatizo dogo kama hili, Kenya wanatafuta mafuta, Uganda wanatafuta mafuta, ikiwa mgogoro wa ndani wa Zanzibar na Bara umeshindwa kufumbuliwa, utaweza kufumbuliwa wenzetu wa Kenya na Uganda watakapopata mafuta yao? Kutakuwa na *community* tena hapo, leo mgogoro wa ndani wa Serikali moja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mfumo mmoja. Wenzetu Waganda wanatafuta *uranium* na mafuta, wenzetu wa Kenya wanatafuta mafuta, leo kweli tunaweza kuja kukaa meza moja tena, kuzungumzia Muungano wa Shirikisho la Afrika Mashiriki, ikiwa sisi wenyewe ndani tumeshindwa kutatua? Tunaiomba Serikali, itupe kauli, baada ya Mkutano wa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ni nini msimamo wa Serikali juu ya utafutaji wa mafuta ya Zanzibar, tuelezwe kwa undani na tuelewe hasa

tatizo ni nini. Ni kwa nini hii inakuwa hadithi ya kila siku, hatuoni aibu kama Watanzania? *(Makofi)*

Kama tatizo ni mgawano wa mapato ielezwe, kama tatizo ni mfumo uelezwe, lakini tulimalize hili tatizo, hatuwezi kuendelea nalo kila siku. Kwa hiyo, tunaiomba kabisa Serikali na itote kauli ambayo ni kauli. Maana Malelo alitoa kauli, mwenzao mmoja kule akasema hiyo kauli ni tofauti. Sasa tungependa katika Bunge hili Tukufu, tupate hasa kauli ya Serikali, juu ya tatizo hili, limekwamia wapi ili tulitatue. Hatuwezi kuendelea hivyo, Bunge lishirikishwe kama kuna lazima ya kufanya hivyo, ili tatizo hili limalizike, hatuwezi kuacha rasilimali hizi zikae bure.

Mheshimiwa Spika, ukiwapa watu *block,* kila kilomita moja wanalipa dola nne za Kimarekani. Kwa hiyo, katika kipindi cha miaka kumi, wanapofanya uchunguzi ukikusanya dola nne, kama umewapa kilomita 10,000, maana yake ni fedha nyingi sana hizo. Hayo ni mapato bure yamekaa, kwa nini tusipate mapato hayo na huu ni wakati wa uchuguzi tu, yamepotea bure. Ndio maana nasema tatizo ni *management of resource* na *decisions* zetu ambazo haziangalii hasa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri sasa Serikali ije na kauli, tatizo liko wapi ili sote humu ndani tulielewe na wananchi wa Watanzania waelewe. Tukielewa kwamba, tunazungumzia Umoja wa Afrika ya Mashariki na wenzetu wana tatizo wanatafuta mafuta na vitu vingine; je, kama sisi tumeshindwa kuutatua mgogoro mdogo huu wa ndani, tutaweza kweli kuingia kwenye umoja huo, kwa sababu hii ya kugawana mapato? Nafikiri hili nalo linatakiwa litolewe majibu kwa wananchi na kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawaomba tena sana na ninaiomba Serikali tuna haja ya kuangalia matumizi yetu, haiwezekani sisi kila mwaka tunaipa *TANESCO* ruzuku. Tuliliomba sisi Bunge hili, tuletewe *Business Plan* ya *TANESCO*, tumetoa shilingi bilioni 60, tukatoa shilingi bilioni 30, tukatoa shilingi bilioni kumi, tukatoa shilingi bilioni 18 na sasa tunatoa shilingi bilioni tatu, yaani tunatoa tu na sasa hivi katika bajeti kuna *another 200 dollars!*

Waziri wa Fedha, alipokuwa ana-*present* bajeti yake hapa, tuliomba *Business Plan*, ili Watanzania wafike mahali waseme sasa *TANESCO* inaweza kusimama. Hatuwezi tuka-*dish money* kila siku, sasa imekuwa kama ni mchezo wa kitoto tu, leo tuna shida leteni pesa, hawa Watanzania watabeba mpaka lini mzigo huu? Kwa hiyo, tunaiomba *Business Plan* ya *TANESCO*, tuelewe *TANESCO* hasa *ultimately,* itafanya nini na kama kweli kuna maeneo tunayoweza kuwaachia watu binafsi wakawekeza, waruhusiwe watu binafsi wafanye hivyo. Lakini hatuwezi kwenda na utaratibu huu tunaokwenda nao sasa. Sisi hatuna nia yoyote ya kuiona maana ya Serikali, nia yetu ni kuisaidia Serikali, ifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, asante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Nishati na Madini. Awali ya yote, napenda kutoa pongezi sana, kwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha, kwa hotuba yao nzuri, ambayo imeweza kuletwa hapa Bungeni na vilevile nawapongeza kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, umeme ni muhimu kwa ajili ya maendeleo, bila kuwa na umeme hatuwezi kuendelea. Lakini vilevile ili tuweze kuendelea na tuweze kuwa na umeme ambao una uhakika tunahitaji mipango mizuri katika shughuli za umeme. Tunahitaji utekelezaji makini na madhubuti, lakini vilevile tunahitaji ufuatiliaji mzuri katika utendaji kazi. Nina imani kwamba, Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa wakati huu wameweza kuonesha mfano mzuri katika kufuatilia mambo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba, shughuli za umeme na shughuli za madini, zinakwenda sawasawa, nawapongeza katika hilo. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo, bado kuna matatizo mengi, labda kwa kuanza ningeanza na matatizo ya jimboni kwangu na kisha nitakwenda kwenye mambo ya Taifa. Mpango wa umeme wa Mbeya Vijijini, ulianza mwaka 1999, nguzo zimesimamishwa katika vijiji mbalimbali vya Iwiji, Ilembo, Santilia, Isuto, Igale, Horongo, Mshewe, Itimba, Haporoto, Idimi, Imezu na Ifupa. Sehemu zote hizi, zimesimamishwa nguzo za umeme toka mwaka 1999, mpaka leo umeme haujaunganishwa. Wananchi wamekata tamaa, tunajua kabisa kwamba, wangeweza kuendelea na kupiga hatua kubwa kabisa katika maendeleo yao, endapo wangekuwa wamepewa umeme mpaka sasa. Naomba Wizara, ifanye juhudi ili kuweza kuwapelekea umeme watu hawa, kwa sababu kwa hakika, wamengoja kwa muda mrefu na tumechelewesha maendeleo yao kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, nguzo hizo zikiendelea bila kuungwa umeme, zitaendelea kuoza. Kila nilipoangalia katika jedwali ambalo lilikuwa limepongezwa pamoja na hotuba, sioni utekelezaji wa Mradi huu katika kipindi kilichopita, wala haioneshi kwamba, utatekelezwa katika kipindi kinachokuja. Bajeti ya *REA* na *REF* ni shilingi bilioni 22.172. Kiasi hiki ni kidogo, ingawa tumepata mahali ambapo tunaweza kuwa tunaanzia. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, tunasema tutapeleka umeme vijijini ili kuongeza kasi ya maendeleo. Hiki ni kiasi kidogo kama tunataka kuleta maendeleo huko vijijini, kwa kupeleka umeme. Kwa hiyo, naweza kuelewa kwamba, ndio tunaanza na labda kiasi cha shilingi bilioni 16, zitatumika katika kuhakikisha kwamba, umeme unakwenda katika miji midogo ambayo imeanzishwa. Natumaini katika bajeti zijazo, tutaongeza kiasi hicho ili tuweze kuhakikisha umeme unakwenda vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, hicho kiasi ni kidogo, bado ningependekeza kwamba, Mbeya Vijijini ambayo tayari ina nguzo ambazo zimekwisha simamishwa, ipewe kipaumbele katika kupata umeme, kwa sababu ni kazi ya kuunga nyaya tu, hakuna kazi nyingine. Wakiweza kuunga nyaya na hawa wananchi walishajitayarisha muda mrefu katika kusuka nyaya katika nyumba zao. Nina uhakika kwamba, namba ya wateja kwa upande wa *TANESCO*, itakuwa imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, hizi ni hela za kufanyia chapuchapu tu, ni kuunga nyaya na

kuanza kupata mapato. Natumaini hiyo inawezekana na tunasema tatizo kubwa la *TANESCO* ni ukwasi, hawana pesa za kutosha, lakini itaendelea kupata matatizo hayo, endapo wateja hawataongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Hawa wateja tulionao hapo Mbeya Vijijini wanaweza kuongeza pato kubwa sana kwa upande wa *TANESCO.* Kwa hiyo, naomba waanze kuvuna mapato kwa kuhakikisha kwamba, umeme unapelekwa katika vijiji hivi ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Spika, huduma za umeme ni kero kubwa sana, kwa maana ya ughali. Wafanyabiashara wamepiga kelele kwa muda mrefu sana. Umeme ni ya ghali kwa sababu uongozi wa *TANESCO* ni hafifu. Uongozi ukiwa hafifu, mahali popote, huo uongozi gharama zake ni kubwa sana. Umeme ni ghali kwa sababu miundombinu ya maji imeshachakaa na kitu chochote ambacho ni chakavu, kinakuwa ni ghali katika kukiendesha.

Mheshimiwa Spika, kama kuna nguzo nyingi zimesambazwa sehemu mbalimbali katika nchi, ambazo bado hazijaungwa, zimekaa zaidi ya miaka mitano, sita, bado ni fedha nyingi zilizotumika na hiyo ni gharama, ambayo haivuni kipato chochote. Kwa hiyo, inaongeza gharama na kufanya umeme uwe ghali.

Mheshimiwa Spika, kuna dalili kubwa sana ya rushwa, pale ambapo wateja wanataka kuunganishiwa umeme na kunakuwa na matatizo ya kumpata mteja huyo, hiyo ni gharama. Kuna gharama kubwa katika mikataba ambayo imeingiwa na Serikali na mashirika mbalimbali au na taasisi mbalimbali. *IPTL*, kama wanapata ruzuku ya shilingi bilioni 21, ni pesa nyingi sana ambazo ni gharama kwa mteja. *NetGroup* walikuwepo hapa, tukifikiria kwamba, wanakuja kuleta mambo ya maana, lakini kwa kweli wametuletea matatizo makubwa, umeme haukuweza kuendelea kwa muda mrefu. Hiyo ni gharama. Naishukuru Serikali kwamba, wameweza kuisimamisha, lakini tutegemee kwamba, tunastahili kupata uongozi mpya ambao ni makini. Gharama za kukusanya pesa kutoka kwa wateja ni kubwa sana na gharama hizo zingeweza kuwa nafuu sana kama *TANESCO,* wangeweza kuchangamkia kwa hali ya juu kabisa, matumizi ya LUKU. Kwa sababu kama kuna matumizi ya LUKU, maana yake ni kwamba, watu wote wanaohusika katika kukusanya pesa au kusoma zile bili wasingekuwepo, ni mteja amewekewa LUKU na yeye mwenyewe umeme ukikatika anakwenda kulipa.

Vilevile kwa kuwa na LUKU maana yake ni kwamba, wangekuwa wanapata fedha *in advance*, kabla ya kutoa huduma, sasa hiki kigugumizi cha kununua LUKU kinatoka wapi? Yote hayo ni matatizo ya uongozi, ambayo yanakuwa ni gharama sana kwa wafanyabiashara. Ningeomba mambo hayo yaweze kuangaliwa kwa undani zaidi, ili uongozi mpya utakapokuwa unapatikana, kufikia mwezi Desemba, 2006, ambao unaweza kuwa ni wa Watanzania, basi mambo haya waweze kuyachukua ili gharama za umeme ziweze kuwa nafuu ili wafanyabiashara, waweze kupata nafuu ya umeme na kisha waingie katika soko la ushindani. Gharama za umeme zinakuwa chini tu pale ambapo gharama za kuendesha makampuni zinakuwa chini na wateja wanaongeza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara na watu mbalimbali, wamekuwa wakilalamika sana kuhusu uharibifu wa vyombo vyao vya nyumbani, pamoja na mashine

kwa sababu umeme unapokatika na kurudi, unarudi kwa kasi kubwa sana, hauwi *stable,* kwa hiyo, unaharibu vyombo vingi sana. Lakini vyombo hivi vinavyoharibika, basi *TANESCO* hailipi, na kunakuwa na matatizo makubwa sana ya kuweza kuwalipa wafanyabiashara na watu mbalimbali, kwa vyombo vyao ambavyo vimeharibika kwa sababu ya upatikanaji mbovu wa umeme. Natumaini hili linasthili kuwa ni suala la kisheria, ambalo tunastahili kuliangalia. Naomba suala la kutunga sheria liletwe hapa Bungeni, ili tuweze kuangalia, kuongeza tija ya watu wa umeme wahakikishe kwamba, huduma zao zinakuwa nzuri. Kwa kuhakikisha umeme unapatikana bila matatizo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu, vifaa vya ujenzi vya umeme vinavyoagizwa kutoka nchi za nje, ni duni sana. Ukichukua hizi soketi na vitu vingine ni vya chini sana na hata ukiweza kuweka katika nyumba yako, baada ya wiki moja, mbili, vinakuwa vimeshaharibika. Nina imani kwamba, kwa sababu vyombo hivi ni duni, basi bila shaka hata matumizi ya umeme yanakuwa ni ya hali ya juu sana. Ningeomba hivi vifaa vya umeme ambavyo vinaagizwa kutoka nje basi, Taasisi ya Viwango iweze kuviangalia ili tuweze kupata vitu bora, ambavyo vinaweza kutusaidia kutunza umeme wetu.

Mheshimiwa Spika, labda sasa niende kwenye upande wa migodi. Migodi ya madini ingekuwa ni vizuri kama ingemilikiwa na Watanzania wenyewe. Sisi wananchi tunastahili kumiliki migodi hiyo, tunajua kwamba, tatizo letu ni tatizo la mtaji, lakini mtaji unaweza kupatikana hapa hapa nchini. Natoa mfano, niliowahi kuutoa huko nyuma kwamba, tukiweza kuwahamasisha wananchi, kama ambavyo imekuwa ikifanyika mwaka 2005, wakati tunaanzisha *Unity Trust Fund*, ambayo iliweza kukusanya shilingi bilioni 97. Hizo fedha kama zingekuwa zimewekwa kwenye madini. Nina uhakika kwamba, wananchi wangekuwa wanamiliki madini hayo. Kinachohitajika ni kuwa na mkakati na utaratibu wa kuweza kuhamasisha wananchi kuweza kuchangia ili tuweze kukusanya pesa hizo. Tukamilika madini hayo na tutaendesha kwa manufaa ya Watanzania wenyewe. *NICO* waliweza kufanya hivyo na kukusanya shilingi bilioni 16 na sasa wanaweza ku-*invest* katika viwanda mbalimbali. Nina imani tukiweza kushirikiana Serikali, pamoja na wafanyabiashara mbalimbali, tunaweza kuhamasisha na kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilitaka kuzungumzia ni kuhusu madini ya *Panda Hill*, madini ya *Niobium*, ambayo yako pale, utafiti ulishafanyika, kuna madini mengi ambayo yanaweza kukaa kwa muda wa miaka 45 na uchimbaji ukianza, unaweza kuajiri watu zaidi ya 500. Nashukuru kwamba, nimeweza kushirikiana na Waziri katika kufuatilia hili suala hili na mwezi Februari, wawekezaji walipata ofa na waliweza kulipia. Hao hao waliweza kuilipia, lakini *mining licence* imekuwa inakwama mpaka sasa. Hao watu walianza kufuatilia kuhusu mradi huu miaka sita iliyopita, lakini mpaka leo *mining licence* ya *Panda Hill* haijapatikana. Nimezungumza na Waziri, alikuwa ameniahidi kwamba, itapatikana katika wiki moja au mbili.

Nina amini kwamba, itapatikana ili angalau watu wa Mbeya waweze kuwa na matumiani ya kuanza kuchimba madini *Panda Hill.* Ajira ziweze kupatikana na wafanyabishara waweze kushiriki katika kutoa *tender* mbalimbali katika madini hayo ili maisha yao yawe bora zaidi. Ili tuweze kuhakikisha kwamba, madini hayo yanaweza

kutumika, itakuwa ni vizuri kama kukiwa na mikataba mizuri, ambayo itahakikisha kwamba, vyakula mbalimbali na matunda, vyote vinaweza kununuliwa kutoka katika maeneo ya palepale Mbeya, ili wafanyabiashara na wakulima, waweze kunufaika kwa njia moja au nyingine, kwa kuwepo mgodi huo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nataka kumalizia kwa kusema kwamba, katika bajeti nzima, hatujaona suala la umeme wa Liganga kipewa kipaumbele katika bajeti, limezungumziwa kwa muda mrefu, ingawa watu wa Kusini Nyanda za Juu, tumewasahau. Mbeya ukiangalia katika bajeti haipo kabisa, mkoa mzima wa Mbeya na Iringa haionekani, Liganga haijazungumzwa kwa kina licha ya kuzungumzwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba bajeti ioneshe bayana mpango wa Liganga, ili tuweze kujua kitu gani kinastahili kutokea. Hapo tutajua kwamba, umeme unaweza kupatikana na ajira ikawa kubwa sana katika maeneo hayo. Lakini vilevile kama mikataba itakuwa ni mizuri, tuna imani kwamba, inaweza kuwanufaisha Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchukua nafasi kuunga hoja hii mkono na ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa hii nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wa Manyoni Magharibi, kutoa pongezi zangu tena kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa CCM. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza, Makamu wetu wa Rais, ambaye bila kuchoka, hupita huku na huko kuhimiza maendeleo na kwa kweli wananchi wa Singida, Makamu wa Rais kwa katika kipindi kifupi tu ametutembelea karibu mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa juhudi zake, nina amini katika kipindi kifupi kijacho atatua Manyoni, atatua Itigi na hiyo *corridor* ya Ruangwa, Mitundu mpaka Rungwe. Siwezi kukusahau kukushukuru wewe mwenye Mheshimiwa Spika, kwa jinsi unavyoliendesha Bunge hili, kwa haki na bila upendeleo kabisa. Kwa kweli tumeiona jinsi dhana ya *separation of powers,* inavyofanya kazi hapa ndani ya Bunge. Wengi tumefarijika na tunajisikia tuko nyumbani kabisa hatuna hofu na tunachangia bila wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija katika hoja, sisi watu wa Itigi tunaishukuru Serikali kwa kutuwekea umeme, lakini tumekuwa na matatizo na ndiyo maana nimesimama hapa niweze kuyaainisha na hii Wizara iweze kuyatilia maanani itutatulie. Ni kweli katika kipindi kifupi, Mheshimiwa Waziri, ametusaidia katika kutanzua kelele zetu pale ambapo tuliona kwamba, shughuli haziendi. Umeme tulikuwa tunao pale Itigi, lakini watu walingoja kwa muda mrefu sana kusambaziwa umeme huo. Mita zikawa hakuna, sasa mtu amejenga nyumba, amelima msimu mmoja, miwili, kwa ajili ya kupata pesa za kupata LUKU, aweze kujiwekea umeme, mita zikawa hazipatikani. Lakini Waziri alifanya juu chini na sasa hivi inavyoonekana, tatizo hili limepungua. Kwa hiyo, napenda

nimpongeze kwa hilo, lakini matatizo yapo na hili mimi ningeliomba nipate maelezo kutoka kwa Waziri. Kwa sababu watu waliungoja umeme kwa miaka mingi na wakaliwa pesa zao. Watu walilipa fedha nyingi sana, kwa ajili ya kulipia mita hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini wakaja kuwekewa mita ambazo hazikufuata utaratibu, sasa wakawa wamekuja kutupa mita mara mbili, kwa sababu ilikuja kuoneka kwamba, Mameneja walikuwa wanauza chini ya meza. Hili nilizunguma na Mheshimiwa Waziri, nilimpa dokezo katika Mkutano wa Tatu, nadhani kwenye Semina kule Dar es Salaam, akaahdi kufuatilia. Sasa kilichofuata ni kwamba, Meneja wa Manyoni alihamishwa bila kupata ufumbuzi hawa watu wengine wameshindwa kupata pesa za kupata LUKU mpya kwa sababu walishalipia lakini wameshindwa kwa sababu ni wakulima. Wanasubili msimu mwingine wavune, ndiyo waweze kununua. Lakini sasa hivi wanakaa gizani wengi, Manyoni, Itigi na kilio hiki tumekizungumza sana. Sasa huyu mtu badala ya kuwajibika, habari tulizonazo ni kwamba, kahamishiwa Biharamulo. Sasa sijui tena biashara hiyo inaendelea kule Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, lakini ninavyofahamu, wenzangu kule wakali, kuna Mheshimiwa John P. Magufuli na Phares K. Kabuye, sijui kama watakubali hii biashara iendelee kule. Lakini ni kweli kabisa kwamba, mita karibu 90,000 ziliibwa sehemu zikatua sehemu ya Manyoni kule, zikawa zinauzwa chini ya meza na orodha ya watu tunayo. Sasa hili tulilizungumza kwenye *RCC*, tukaambiwa kwamba, huyu mtu angerudishwa Itigi na Manyoni kuja kujibu matatizo ya hawa watu, lakini huyu mtu hajarudi mpaka leo. *Regional Manager*, naye katika orodha ya Mameneja wa *TANESCO,* waliofanyiwa uhamisho simwoni katika orodha. Sasa sijui kawekwa pembeni, amekuwa *desk officer,* sielewi lakini matatizo hayo yapo na wananchi wanatusumbua.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo la *conflict of interest*, watu wanaanza kufanya biashara ya Mwajiri wao huyo huyo, kwa kweli linaendelea kuleta matatizo hapa nchini. Ni sawasawa kabisa na Sekta ya Afya na kwingine, watu wanafanya kazi hiyo hiyo pembeni, sambamba na kazi za mwajiri. Sasa ningeomba nipate maelezo juu ya hawa watu, wamechukuliwa hatua gani, Mamlaka zao za nidhamu zimezungumza nini? *(Makofi)*

Maana kuna matatizo kwamba, Mamlaka hizi za nidhamu huwa zinawekwa mifukoni, bila shaka hawa watu wako kwenye chini ya Bodi. Sasa tuna tatizo bado katika nchi hii, kwamba Mamlaka zinazohusika, huwa zinapata kigugumizi kuchukua hatua. Hawa watu kwa nini wahamishwe wasichukuliwe hatua na vitu viko wazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nipate maelezo ya kina, kuhusu hilo suala ili wananchi wangu waweze kujua hawa watu hawa ni wengi waliouziwa mita kwa utaratibu huu. Kwa hiyo, Wizara inayohusika, nadhani ningependa ili tuachane na ile hofu ya kwamba, pengine kuna watu wanaowalinda, ndiyo tatizo tulilonalo sasa hivi. Mimi ningeliomba pia *PCB,* ingejaribu sana kuweka katika orodha yake, vitu hivi vinavyoitwa zawadi. Hizi za wafanyakazi wa chini au Mameneja kuwapelekea Wakurugenzi wao zawadi, halafu inakuwa tabu, maana sasa wanawa-*compromise*. Watu wahawezi kutoa maamuzi, Mkurugenzi unakuta mara gari likuja lina mahindi magunia 20, lina mbuzi.

Sasa unauliza imetoka wapi, imetoka Manyoni, Singida au Mtwara. Sasa kweli Mkurugenzi, anaweza kuchukua hatua hiyo. Sisemi Waziri, lakini ninachosema Mamlaka zinazohusika zinaweza zikachukua hatua kwa watu kama hawa na imekuwa ni kama tabia, mtu anapokea zawadi haulizi imetoka wapi na ni kwa sababu gani. Umefanya kazi gani mpaka upewe zawadi.

Mheshimiwa Spika, sasa hii imekuwa ni *culture* yetu, nafikiri ingelikuwa vizuri kabisa kama hawa watu wanaopeleka zawadi au mizigo hii wakarudishiwa. Gari la Serikali linatoka Mikoani kule, kama ni gari la *TANESCO* na kadhalika limebeba mizigo kedekede inakwenda sijui Dar es Salaam kwa wakubwa, hivi kwa nini asirudishiwe hiyo mizigo. Kwa nini asiitwe akaulizwa? Lakini sasa kama Mameneja watafanya hivyo na viongozi watende, *then* utakuta hakuna kinachofanyika. Ndiyo maana utakuta watu wanakataa uhamisho, atakwenda pale anapotaka, kwa sababu maamuzi yanakuwa magumu kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nafikiri *TANESCO* hawana sababu ya kuingia kwenye masuala ya rushwa, kweli kabisa kwa sababu ni kati ya Mashirika ambayo wanalipwa vizuri tu, ukilinganisha na mashirika mengine hapa nchini. Lakini tatizo hili la rushwa limekithiri na mimi nafikiri limekithiri kwa sababu ni tabia sasa watu hawa wasihamishwe. Naomba kwa kweli nipate maelezo ya kina, kuhusu hatua zilizochukuliwa juu ya hawa watu ili tuwaeleze wananchi, kuwahamisha tu sidhani kama inatosha kwa sababu tunahamisha tatizo.

Mheshimiwa Spika, nikiingia upande wa madini, ninashukuru kwamba, Wizara imetambua kwamba, kuna *Gypsum* Itigi na imeainishwa kwenye kitabu na wachimbaji wameanza ni siku nyingi tu, lakini tunashindwa kuelewa Serikali inasema nini juu ya hawa watu, wachimbaji hawa. Wataendelea kuwa vibarua kwa watu binafsi mpaka lini? Kwa sababu hivi hapa ninavyozungumza, tuna wafanyabiashara kutoka Uganda, Rwanda na Burundi, wamewaweka Manamba wanafanya kazi kule usiku na mchana, *Gypsum* inapelekwa nchi za nje. Tatizo kubwa unakuta hawa hawalipwi moja kwa moja, wanakopwa nguvu yao.

Mheshimiwa Spika, sasa katika hali hii na *Gypsum* kama mnavyofahamu ni sumu, mtu anahitaji lishe bora na maziwa, sasa tuna-*create* tatizo lingine tena la maradhi *(Occupational Health)*, watu wanaugua vibaya, *TB* imekithiri.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba pia kupata maelezo kutoka Wizara hii, inasema nini juu ya suala hili na hii *Gypsum;* inafikiria kui-*exploit* vipi? Iko katikati ya nchi, *infrastructure* ni nzuri kama reli na barabara, lakini sasa utakuta inachukuliwa kwenda nchi za nje, inachukuliwa nyingine inakwenda Tanga, nyingine inakwenda Mbeya. Kwa nini wasije na utaratibu wa kutafuta mwekezaji, akajenga kiwanda hapa ili tuweze kupata ajira na iweze kusambazwa vizuri?

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, hii *Gypsum* inatengeneza saruji, *POP,* Chaki, Chokaa na hata Mbolea na umuhimu wake unaeleweka, tungeweza kuwa soko zuri sana kwa hizi nchi za nje za Rwanda, Burundi na *DRC* inaelekea kutulia, pia

tungeweza kuwa na soko zuri sana na wao wenyewe wanakuja. Lakini hawa watu wamegeuka kuwa ndiyo matatizo, nchi zetu za Kiafrika watu wake wanateseka, kwa sababu ya rasilimali walizonazo wao wenyewe, ndiyo zinazowatesa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba nipate maelezo ya kina kuhusu suala hili, tuweze kujua tunaelekea wapi na hii *Gypsum* iliyopo Itigi. Mfuko wa kilo 50, kiloba sasa hivi wale watu wanafanya shilingi 350 mpaka 600, inategemea wapo wangapi, lakini sasa hivi wapo watatu, mwingine anatoka Jinja ananunua pale, lakini anajaza malori pale yanakwenda Jinja, hajawalipa hawa watu wameingia mkataba tu. Sasa lori lile likipinduka njiani kule au akipata matatizo, nani atawalipa hawa watu?

Mheshimiwa Spika, naomba sana sana nipate maelezo, Wizara ina mwelekeo gani kuhusu suala hili la *Gypsum* hiyo iliyopo Itigi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nina muda bado, labda nirudi tena kwenye Sekta hiyo ya Umeme kwamba, hii *Corridor* ya Mgandu mpaka Rungwa, yaani Itagata, Mgandu, Mitundu, Bakale, Mtakuja na Kalangali yote hiyo *Corridor* mpaka Rungwa ni *Game Reserve*. Sisi tulipewa ahadi na ilikuja *delegation* kabisa pale Manyoni kwa Mkuu wa Wilaya, tukaambiwa kwamba, safari hii ni zamu yenu ya kupata umeme watu wa Mgandu itakuwa 2007.

Mheshimiwa Spika, hilo la tatu ningeliomba kupata kauli kamili ya Wizara, kuhusu *Corridor* hiyo, kila mtu anajua umuhimu wa hiyo sehemu, watu wanahitaji umeme kwa ajili ya kupasua mbao, wanahitaji umeme kwa ajili ya kusindika mazao yao kama alizeti na vitu vingine kama nta.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tunapopanga mipango yetu, tuweze kuangalia sehemu ambazo zinaweza zikatukomboa kiuchumi. Kwa hiyo, napenda nipate maelezo kamili kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu mpango huo, sijauona vizuri humo kwenye kabrasha, lakini ahadi ilitolewa na barua sisi tukampongeza *Regional Manager,* pamoja na *delegation* yake. Watu wa Mgandu wako tayari na hiyo *corridor* wanasubiri kabisa mwaka 2007, maana si mbali ni miezi michache. Kwa hiyo, tuone hiyo mipango inaanza kuandaliwa sasa, mwingine alisema itaanza Desemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana, kama nitapata maelezo katika maeneo haya matatu, niliyoyaainisha ili niweze kukaa vizuri na niweze kuelewa ni nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo kwa kweli ninatamka juhudi zinazofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mbunge wa Tarime, kisha ajiandae Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala. Kwa taarifa wale wasioifahamu Msalala, iko Mkoa wa Shinyanga.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Nishati na Madini.

Napenda kumpongeza Waziri, Waziri wake mdogo na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa juhudi kubwa wanazofanya za kujaribu kubadilisha mkondo wa historia ya uchimbaji katika nchi. Kwa misingi hiyo, naipongeza Serikali iliyopo madarakani, kwa sababu kwa mara ya kwanza, Serikali imeonesha nia ya kutaka kuwasaidia wachimbaji na wananchi wa nchi hii, katika kero zao walizonazo. Hilo ni jambo ambalo linaingia katika vitabu vya historia ingawa bado ubishi unaendelea, lakini tunaamini ya kwamba, Serikali hii ina nia njema na wananchi wa nchi hii katika suala la madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Tarime na hasa Jimbo langu la Tarime, suala la uchimbaji wa madini na athari zake limekuwa ni tatizo nyeti kwa wananchi wa Tarime, kwa sababu kile ambacho wao walikiona kama ni neema, sasa kimegeuka kuwa ni balaa kubwa kwao, inayosababisha maafa na umaskini mkubwa. Kwa misingi ya haki, nadhani ingekuwa vema tungetambua kwamba, tatizo kubwa katika uchimbaji wa madini katika nchi hii ni ardhi, kwa sababu yale madini yako ndani ya ardhi na ninaona kama kuna hitilafu kubwa katika Sera yetu ya Ardhi, ambayo inahitaji irekebishwe na Serikali hii iliyopo madarakani. Kwa sababu chanzo cha mwananchi kuitwa mwananchi ni kwa sababu anamiliki nchi, yaani anamiliki ardhi, vinginevyo basi angeitwa mwanainzi. Kwa hiyo, *qualification* yake inayomfanya aonekane kwamba, yeye ni Mtanzania ni pale ambapo anamiliki kipande cha ardhi katika nchi hii. Hata nchi yetu yenyewe katika mapambano ya kupigana na wavamizi, tulikuwa na msemo tunaosema ya kwamba, hatutakubali hata ncha moja ya nchi ichukuliwe na mvamizi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hilo linaonesha ya kwamba, ardhi ni kitu ambacho ni kitu muhimu sana duniani na ndiyo maana kuna mipaka, nchi mbalimbali na ndiyo maana kuna uzalendo. Wananchi wa Tanzania, wana uzalendo mkubwa na nchi yao na hata iweje wanaamini ya kwamba, wao ndio wanaomiliki ardhi ya nchi hii, ingawa pia wako tayari kuwakaribisha wageni ambao wanataka kuitumia kwa kuleta mtaji na utaalamu walionao. Lakini kile kitakachopatikana kwa mantiki ile ya *natural justice,* basi tugawane nusu kwa nusu, yaani nusu wapeleke kwao na nusu watuachie. Lakini kama wanataka kubeba chote, yaani asilimia mia moja, halafu na kufanya uharibifu wa maisha, mali za wananchi na mazingira, hilo halitakubalika.

Kwa hiyo, naamini ya kwamba, Serikali yetu inaangalia hilo na imeshajua kwamba, athari zake zinaweza zikawa kubwa, kwa sababu tunaweza tukaangalia historia. Ndiyo maana ya kusoma historia. Tukaangalia *experience* kama zile za *South Africa,* wananchi wanyeji waligundua madini wao wenyewe na Waingereza walipokuja, wakawaonesha kwamba, haya madini yapo hapa, baadaye Waingereza wakataka kuyamiliki yote. Vita iliyopiganwa kwa miaka mine, ndiyo iliyosababisha Afrika Kusuni ya leo, iwe vile ilivyo. Inaitwa, *The Boer War 1898* mpaka 1902 wakakubali kwamba, waunde *The Republic of South Africa* na kilichopatikana nusu kilienda kwao na nusu kikabaki Afrika Kusini, ndiyo maana leo hii Afika Kusini inalinganishwa na nchi za Ulaya.

Kwa hiyo, hakuna wananchi wanaoweza kukubali kuporwa mali yao na hilo limetokea pia Sierra Leone. Migogoro ya pale inatokana na ardhi yenye madini. Tukiangalia Kongo vilevile, Mobutu aliharibikiwa kwa sababu ya kuamini ya kwamba, wale Wazungu wangeweza kumlinda na akawapa kila kitu. Matokeo yake mpaka sasa unaona, hali haijatulia, maisha ya watu milioni nne yamepotea. Kwa hiyo, hili suala Serikali iliangalie sana na sisi hatupendi yetu ifikie hapo, ndiyo maana tunaonya, lakini siyo kwamba sisi tunachochea, hapana. Tunawaambia ukweli wa hali halisi jinsi ilivyo ili wachukue hatua. *(Makofi)*

Umiliki wa ardhi katika Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria Namba 4 na 5, imezungumzia bayana kwamba, ardhi ina thamani. Kwa hiyo, wakati makampuni yanapokuja kutafiti basi ni vema, waweze kumfidia yule mwananchi wanayemkuta pale kutokana na kile kipande cha ardhi anachomiliki. Ambacho madini yameonekana yapo pale, kuliko kuingia kwenye mashamba ya watu na kuyavuruga na kuyaangusha na kusema sisi tumepewa barua kutoka Dodoma. Hii imeleta migongano mikubwa katika Jimbo langu.

Kuna watumishi wa Kampuni hata wamewahi kukatwa mapanga, kwa sababu mtu anaona kwamba hii ni *trespass,* ananiingilia. Lakini nadhani Serikali ingekuwa wazi kwamba, ardhi kulingana na Sheria ya Mwaka 1999, ina thamani. Kile watakacholipwa wananchi kitokane na ardhi, siyo mihogo iliyopo pale au migomba. Basi hiyo fidia ingeweza kuwasaidia wananchi vilevile kujikomboa.

Suala lingine ni katika utafiti. Tumekuwa na kampuni ya Afrika Mashariki *Gold Mine,* ambayo imetafiti kwa muda wa miaka kumi mpaka wananchi wameshindwa kuelewa ukomo wa utafiti huo. Katika kutafiti huko ni madini yanasombwa yanapelekwa nje, wananchi wakiona wanashangaa, ni utafiti gani wanafanya kwa sababu wananchi walikwishafanya utafiti pale na hili ndilo ambalo ningependa pia Serikali ilitambue kwamba, si Wazungu ndio waojua kutafiti dhahabu.

Migodi mingi ambayo sasa hivi imemilikiwa au imepewa wawekezaji, iligunduliwa na wenyeji, ambao wametumia gharama kubwa na muda mwingi na ubunifu mkubwa mpaka wakaigundua ile migodi na wakaanza kuifanyia kazi. Badala yake basi Serikali ikawapa wawekezaji, lakini hilo halina ubishi kwa sababu ni uamuzi wa Serikali, ila sasa mgao na haki za wale wananchi pale. Kwa mfano, si vema wananchi wakawa wanafukuzwa fukuzwa na Polisi kutoka katika maeneo ambayo wameyagundua wao wenyewe. Hata katika Sheria za Kimataifa, kuna kitu kinaitwa *Royalties* au tuseme haki. Hata haki za kufikiri siku hizi zinalipwa, zinaitwa *Intellectual Rights.* Mtu amefikiri kitu, amekigundua, basi anapewa haki zake vilevile, lakini siyo kwamba, waonekane wao si watafiti halisi.

Kingine ni kwamba, katika suala hilo vilevile tuangalie mrabaha. Wananchi wataendelea kuomba Serikali itoze kodi, lakini katika ile ardhi kitakachopatikana wananchi wagawane na hawa wafanyabiashara wengine, kwa sababu ni suala la kibiashara. Kimsingi, Serikali ilishajitoa kwenye biashara. Itoze kodi basi, tugawane na

wale kwa kusikilizana, lakini siyo wao wanaandika mikataba wanaileta Serikalini na inaidhinishwa halafu wanakuja kuwaondoa wananchi.

Suala lingine ambalo napenda kuongelea vilevile ni suala la kuangalia ukuaji wa Sekta ya Madini. Wenyeji, yaani wale Watanzania ambao wameshakuwa na uwezo wa kuchimba dhahabu au madini mengine. Serikali iwape ruzuku ili tuweze kukuza, yaani kuwapa *empowerment,* kuwawezesha. Kama vile nchi nyingine kama Afrika Kusini zinavyofanya, kitu kinachoitwa *Black Empowerment,* maana tumezuiliwa kuendelea kwa muda mrefu, siyo kwa sababu hatuna akili, ila makusudi. Kwa hiyo, wawe na uwezo wa kuendelea kuchimba ili tuweze kushindana na hao wawekezaji, maana wawekezaji wao wanasema hawawezi kuwasaidia, kwa sababu wale ni washindani wao. Kwa hiyo, Serikali ifanye mbinu za makusudi, kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wa ndani ili waweze kukua na hata ikiwezekana kwa baadaye, tuweze kumiliki migodi yetu basi na kuwaajiri hao Wazungu kama wana utaalam.

Suala lingine ambalo pia tutaliangalia ni katika ukuaji wa Sekta hiyo ya Madini, tuone ya kwamba, kuna nchi nyingine ambazo tayari zimeshaonesha ya kwamba, zinaweza kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Tunaweza kujifunza kutoka kwao. Ila suala la uchafuzi wa mazingira liangaliwe, suala la matumizi ya sumu kama *cyanide,* ambayo inatumiwa ku-*extract* ile dhahabu.

Haya matumizi tayari yameshaonesha athari kubwa, wananchi wanalia kwamba, sumu inatupwa katika mito na hiyo mito inatiririka hadi Ziwa Victoria na mle kuna samaki na watu wengi wanaweza kuathirika hata mpaka humu Bungeni na nchi za nje na tukaharibu hata soko la samaki wetu. Kwa hiyo, suala la *Environmental Impact Assessment,* ni la muhimu zaidi. Hili halina mjadala kwa sababu ni maisha ya wananchi ambayo yanaweza yakaathirika.

Suala la ajira, wananchi wanasema kwamba, hawaajiriwi katika migodi lakini ni kweli nitakupa mfano wa Tarime. Pale wanaolinda Mgodi ni watu wa Nepal. Sasa hata ukiangalia historia, tangu Mjerumani na Mwingereza, hakuna mtu ambaye ni *Professional* Askari kuliko Mkurya hapa. Sasa wale Wanepal, wana umuhimu gani pale na zile ni nafasi ambazo zingeweza kutumiwa na wananchi nao pia wakapata ajira. Hilo Serikali iliangalie, kwa sababu unaweza kukuta ni Jeshi la Kigeni limeingia humu kututafiti, halafu baadaye likaiIetea Serikali matatizo. Kwa sababu wale ni wageni. Wanakujaje kufanya kazi ya uaskari hapa? Hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la umeme *(Rural Electrification).* Serikali iliangalie kwa sababu ni muhimu sana. Nchi zote ambazo ziliweza kufanya *industrialization* kama Urusi na China, waliandaa kwanza kuweka umeme katika vijiji na hiyo haina ubishi kwamba, tukitaka kufanya *industrialization* ni lazima tuwe na umeme hadi vijijini. Nishati ya mafuta ile ambayo kwa mfano, Kampuni ya Machimbo inavyotumia hadi lita milioni mbili kwa mwezi, zile lita za mafuta tunanunua kwa pesa za kigeni.

Kwa nini tusipeleke umeme pale wa *TANESCO* ili waweze kulipa hizo fedha, kukuza shirika letu la umeme, badala ya hizo fedha kupotelea nje na malori mengi

yanaingia kuharibu barabara wakati ambapo umeme wetu ungeweza kufanya hiyo kazi ya kusukuma mitambo ya migodi.

Tunaishukuru Serikali, kwa jinsi ambavyo imeyafanya makampuni yatulipe dola 200,000 kama kodi. Sisi tumekubali. Wananchi walitaka kusema ya kwamba, mnapokea za nini, lakini tukawaambia hizi ni muhimu tupokee kwa sababu ni ushahidi ya kwamba, kumbe tuna haki ya kulipwa. Sasa baadaye tuulizie kuhusu *arrears* na tuone ya kwamba, hiyo *figure* ya dola 200,000 ilifikiwaje, kama pengine uzalishaji ule haujulikani.

La mwisho, wachimbaji wadogo wadogo wa Tarime katika maeneo ya Komarera na Kerende, wanaomba wapewe maeneo ya kuchimba.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Labda tu kwa taarifa, kama ambavyo ulidokeza mwanzoni kwamba, Jimbo la Msalala ndilo pia linaloaminika kwamba, lina madini mengi sana ya dhahabu na ndilo ambalo Mgodi wa Bulyanhulu upo, ambao ni mgodi mkubwa sana wa dhahabu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa jitihada ambazo zimeonekana kwenye hizi siku za mwanzo kabisa za uongozi wao katika hiyo Wizara. Ninasema hivyo kwa kuzingatia jitihada ambazo Mheshimiwa Waziri mwenyewe amezionesha, katika kukabiliana na matatizo mbalimbali. Lakini pia kwa kutambua matatizo makubwa yaliyopo kwenye Wizara hii, yaani matatizo ya umeme na migogoro mikubwa iliyopo kwenye madini, ambayo inatokana na sheria zetu hafifu na pengine si wawekezaji, bali inaweza ikatokana na sheria zetu ambazo zina matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza vilevile Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa majadiliano ambayo wameyafanya bila kubadilisha Sheria wala mkataba, lakini kwa kutafsiri tu vipengele vilivyopo kwenye mkataba ule, ikaonekana kwamba, kuna *justification* walau kwa makampuni haya kuanza kutulipa hizo dola 200,000, ambazo Wilaya yangu ya Kahama pia imenufaika. Kwa hiyo, nashukuru sana na ninawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nagependa nianze kuchangia bajeti kwa kuanzia eneo la umeme. Nimekuwa na *concern* sana na *performance* ya *TANESCO*, hasa kwenye suala la *management*. Kazi ambayo *NetGroup Solutions* wamefanya toka wamekuwa pale. Wabunge wengi wamezungumzia eneo hilo, lakini mimi nataka tu kuonesha ni kwa namna gani Serikali inapoteza pesa na inalazimika kutoa ruzuku kwenye shirika ambalo kwa kweli lingeweza kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kahama ni Wilaya ambayo inakua sana kibiashara, kuna mahitaji makubwa sana ya umeme, kuna wateja wengi sana ambao wanahitaji umeme, lakini matatizo yamekuwepo makubwa sana katika kupatiwa umeme. Katika *record* ambazo tunazo, taarifa ambazo zimefika katika ofisi yangu kama Mbunge ni kwamba, kuna wateja ambao wamepeleka maombi yao waunganishiwe umeme toka mwaka 2000, ambao tayari wameshalipia. Mpaka sasa hivi hawajapata umeme na majibu yanayojitokeza ni sababu ambazo hazina msingi kwa mfanyabiashara, hakuna mita, fungu la kufanya *extension lines,* vikombe na kadhalika. Sasa nashangaa, wateja 1,000 kama hata walau kila mmoja atakuwa analipa bili ya shilingi 10,000 kwa mwezi, maana yake ni shilingi milioni kumi, kwa mwaka maana yake ni shilingi milioni 120. Kwa miaka mitano ambayo hawajalipa kwa sababu tu hawajapewa huduma hii, Serikali imepoteza shilingi milioni 600, ambazo tunalazimika kutoa sehemu nyingine tuweke ruzuku *TANESCO.*

Kwa hiyo, naomba na niliwahi kuuliza siku moja katika mlengo huo huo kwamba, vifaa ambavyo Waziri alisema kwamba, *NetGroup Solutions* imenunua viko wapi? Msingi wa swali ulikuwa ni huo kwamba, *performance* ya *NetGroup Solutions* ni *poor,* hakuna vifaa ambavyo vimenunuliwa na kama vingenunuliwa wale wateja 1,000 wangekuwa na umeme na Serikali ingekuwa inapata pesa.

Kwa hiyo, naomba kuitahadharisha Serikali, nashukuru na kuupongeza sana msimamo wa Serikali kwamba, sasa hatuna mpango tena wa kuendelea na mkataba na wale watu, kwa sababu kwa kweli kuna matatizo makubwa yaliyotokana na hilo. Mfano mwingine ni pamoja na *procurement,* kuna viwanda ambavyo vilikuwa vinazalisha vifaa vya umeme, *TANALEC* sasa hivi almost imekufa. Ilikuwa ina-*supply* vifaa vyake vingi kwa *TANESCO, condition* ambazo zimejitokeza ni kwamba, vifaa vingi wanavyo-*supply* au kutengeneza *TANALEC* havina ubora. Kwa hiyo, vifaa vingi vya umeme vimekuwa vikiagizwa kutoka Afrika Kusini. *Tanzania Cables*, ambao walikuwa wanatengeneza *cables* nyingi na kuuza *TANESCO*, kumekuwepo mizengwe katika kuuziana au katika kuuza bidhaa zao. Lengo lao ni kuhakikisha kwamba, wana-*import* vitu ambavyo vingeweza kupatikana hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba kuiunga mkono kabisa Serikali kwa msimamo wake wa kuhakikisha kwamba, mkataba huu utakapokwisha, basi *management* ya *TANESCO* irudi kwa wazawa. Wapo wazawa wenye uwezo wa kufanya *business plan*, wenye uwezo wa kuhakikisha kwamba, shirika linaendeshwa vizuri na linapata faida na kupunguza mzigo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningependa vilevile nitoe tu ombi mahsusi kabisa kwa Mheshimiwa Waziri, kumekuwepo na majadiliano ya *route* ya kupeleka umeme Bukombe. Kuna mapendekezo ambayo yamekuwepo toka muda mrefu na Mheshimiwa Mbunge aliyenitangulia, amenieleza katika *handover notes* kwamba, tayari mazungumzo yalifanyika na yalikuwa kwenye hatua kubwa tu kwamba, umeme utoke pale Ilogi, ambayo ni Kata ya Bugalama Wilaya ya Kahama, upite Kata ya Lunguya, Segese, Ntobo, halafu uende uunganishe Bukombe Kusini kupitia lilipo Gereza la Kanegere, halafu ndiyo uende Ushirombo na haya ndiyo matakwa ya Wilaya zote mbili.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu kumkumbushia Mheshimiwa Waziri kwamba, tafadhali tunaomba umeme upite *route* hiyo, kwani tuna uhakika unakwenda Bukombe, lakini unapita njia ipi. Tunaomba tafadhali, usipite porini, upite kwa watu ili hawa watu nao angalau waweze kuzalisha na hao ni wajeta wengine. Nakuletea Mheshimiwa Waziri. Nakuhakikishia kwa kupitisha umeme *route* hiyo, utajipatia pesa nyingi sana na mzigo wa kuipa ruzuku *TANESCO* utazidi kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nihamie sasa kwenye upande wa madini. Kwa upande wa madini, tumekuwa na matatizo makubwa na matatizo makubwa, yanaanzia hasa kwenye Sheria ya Ardhi, Wabunge wengine pia wamechangia eneo hili na mimi nataka kusisitiza tu kwamba, kumekuwepo na migongano ya Kisheria. Mtu anapewa kwa mfano, *Prospecting Licence (PL),* inamruhusu kufanya utafiti wa madini kwenye eneo Fulani. Vile vile kuna Sheria ya Ardhi Namba 4 na 5 ya mwaka 1998/99 kwamba, kwenye lile eneo kuna watu wanaishi na ardhi ile ina thamani, sasa kunakuwepo na mgongano wa *Surface Rights* na *Mineral Rights,* ambazo zinakuwepo katika Sheria za Madini na Sheria ya Ardhi na mwisho wa siku katika migongano ya Sheria hizi mbili, anayeathirika sana ni mwananchi. Kwa sababu yeye katika *compensation* ambayo imekuwa ikifanyika kimakosa, kwa kweli naweza kusema inaangaliwa ni *development* gani aliyoifanya kwa eneo hilo, wakati mimi naamini kabisa kwamba, siyo sahihi *compensation* katika misingi hiyo.

Nimekuwa nikilisema hili kwa kufanya *reference* kwa *effects* ambazo zinatokea kwa wananchi, kwa mfano, wananchi wengi wanatumia maeneo hayo kwa shughuli zao za kawaida, achilia mbali kujenga nyumba kwa sababu maendeleo wengi tumekuwa tukiangalia katika shughuli za kulima kwamba, kuna mazao kiasi gani. Wafugaji wanachunga mifugo yao sehemu ambayo haijalimwa, ukimpa mtu eneo lile akalimiki, maana yake ni kwamba, wafugaji hawatapata tena haki ya kuchungia mifugo yao katika eneo hilo, itabidi waende huko ambako bado kuna nafasi na wakienda huko ndiyo inaanza ooh! sisi huku wafugaji hatuwataki.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba, Mheshimiwa Waziri awasiliane kwa karibu sana na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, waweze kuangalia eneo hili na kufanya marekebisho. Ninaamini marekebisho hapa yanawezekana na wala hapatakuwepo na matatizo yoyote ili na wananchi wenyewe waweze kunufaika, hasa inapofika wakati kwamba, wanafanyiwa *compensation* baada ya maeneo yao kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka kuzungumzia suala la michago au usaidizi ambao unatokana na Makampuni ya Madini kwenye maeneo ambayo yanazunguka migodi hii. Kumekuwepo na matatizo makubwa au *dispute* za mara kwa mara, ni kiasi gani wananchi hawa wapate kutokana na kuwepo kwa migodi kwenye maeneo yao. Ukiangalia takwimu zinaonesha kwamba, ni kweli wanachangia lakini suala limekuwa likijitokeza, ni kiasi gani na kiasi gani cha madhara yanatokana na kuwepo mgodi kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa Mgodi wa Bulyanhulu kwenye eneo la Kakola. Ule mgodi uendeshwaji wake unahusisha pia kusomba mchanga, yaani kifusi kupeleka nje ya nchi. Kifusi kile kina wastani wa tani 40 kwa lori moja na zaidi ya tani 400 zinachukuliwa kwa siku, yaani malori 10 yanasomba kifusi kile, yanapita kwenye barabara yenye urefu wa kilomita 56 kutoka Kakola kwenda Kahama Mjini, ili baadaye yaunganishe kwenye barabara ya lami kwenda Isaka na kupakua kwenye treni. Sasa barabara hii inakarabatiwa na Halmashauri, Halmashauri fungu lake inapata wastani wa shilingi 136,000 kwa kilomita kwa mwaka. Shilingi 136,000 kwa kilomita kwa mwaka, zinatosha tripu mbili za isuzu za kifusi na kinamwagwa bila kusambazwa.

Sasa kifusi kile halafu yanapita malori ya uzito ule, kwa uhakika kabisa, Halmashauri haiwezi ika-*maintain* barabara hiyo. Kule nyuma wenzetu wa mgodi huo wamekuwa waki-*maintain*, lakini sijui baadaye ni kitu gani kilitokea hapo katikati, toka mwaka 2002 wakawa wameacha na barabara iko kwenye hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, ombi langu naamini kabisa, kwa *spirit* ambayo Mheshimiwa Waziri ameionesha na Naibu Waziri, hili nalo linazungumzika. Kaeni na wale watu, waombeni tushirikiane kurekebisha barabara hii. Tunaitumia wote na ukiangalia watumiaji wakubwa ni wao, wala siyo sisi. Sisi tunapitisha mikokoteni inayovutwa na ng'ombe, sidhani kama tunahitaji sana barabara iwe katika hali nzuri kama ambavyo wao wanaihitaji.

Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri, awaombe tushirikiane kwa hilo. *Of course* tunahitaji kupitisha magari yetu madogo madogo pia tunapokuwa tunakwenda huko na kuna watu wanapata matatizo, wanahitaji kwenda hospitali. Kwa hiyo, tunahitaji barabara iwe katika ubora, lakini Halmashauri haina uwezo wa ku-*maintain.*

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kuzungumzia suala la Sheria ya Madini ya mwaka 1998, kuhusu leseni za kutafiti madini. Wengi wamezungumza kwamba, leseni hizi zinachukua muda mrefu. Kuna kipengele cha Sheria, nafikiri kuna tatizo katika usimamizi. Kifungu namba 29(3)(b) kinasema kwamba, mmiliki wa eneo katika ku-*prospect,* anapokuwa ana-r*enew,* anatakiwa ku-*surrender fifty percent* ya eneo lile. Sasa ukifika Kahama karibu asilimia 60 ya Jimbo langu la Msalala, watu wana leseni na leseni zinatolewa huku huku mjini mnatumia *grid reference* kwenye *computer,* mnasema hili eneo halina mtu anayelimiliki, anapewa mmiliki mwingine, lakini hawayaachi hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, tusaidiane kusimamia hiyo Sheria ili watu wengine wapewe nafasi hiyo. Bahati mbaya sana, wanaomiliki hayo maeneo wengi wao ni watu wa nje. Anachukua leseni ya ku-*prospect,* hafanyiki chochote kama alivyokuwa anasema mwenzangu, Mbunge wa Bukombe hapa, anakaa nayo miaka minane, anafanya *prospecting* ya ajabu ajabu, halafu kutakapokuja kutokea madini, anauza kwa bei kubwa. Kwa hiyo, tunaita ni kutengeshea faida kubwa kwa kumiliki eneo kusiko na sababu, na ndiyo maana nafikiri kipengele hicho cha sheria kikawepo kwamba, awe ana-*surrender* eneo fulani. Naomba Mheshimiwa Waziri azingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali izingatie Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika umiliki wa migodi. Kuna kipengele kinazungumzia kuwawezesha wananchi kumiliki migodi kwa njia ya hisa *(Equity Participation)*. Naomba kwa sababu iko kwenye Ilani, hili ni agizo. Kwa hiyo, naomba Serikali ilisimamie hili na kwa kuanzia kwa sababu tayari kuna nia hiyo, Mgodi wa Buzwagi, ambao uko katika hali nzuri kabisa, unamilikiwa kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamesema na tayari kuna wawakilishi walikuja hapa jana, nafikiri Mheshimiwa Waziri alionana nao, wanazungumzia waingie ubia wa kumiliki mgodi ule, kwa namna yoyote ile itakayowezekana, ili kwamba na wao wawe *shareholders.* Badala ya kusubiri kodi, wawe wanapata *dividend,* kwa sababu *the more you increase the taxes, the more you reduce the profitability* na wao wanalielewa hili. Ndiyo maana tunasema kwamba, tusisubiri kodi. Kwa sababu tukijikita kwenye kodi ambazo ni gharama za uzalishaji, maana yake ni kwamba, *profit* ya haya Makampuni haitapatikana na kwa maana hiyo, hatutapata ile asilimia 30 ya *income tax*. Kwa kulikwepa hilo, ndiyo maana nikasema vilevile tuwe na kipengele ambacho kinatupa nafasi ya kupata gawio kama wanahisa, yaani kupata *dividend.*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nimalizie kwa kuwashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa jitihada wanazozifanya na nawaomba tushirikiane kwa kuzingatia mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kusema ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwanza ya kuchangia katika hoja hii muhimu. Lakini pili, kwa kuweza kuwawakilisha wananchi wa Ludewa katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamezungumzia sana masuala ya Kitaifa na kwa kweli wamechangia vizuri sana na ninaafiki mambo mengi sana ambayo wenzangu wameyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii, napenda nitumie muda huu kuzungumzia masuala ya Ludewa na hasa suala la Mchuchuma na Liganga. Kwanza, naanza kwa kuishukuru Wizara na Mheshimiwa Waziri kwa upande wa nishati. Tunaambiwa umeme wa gridi utakapokwenda Ruvuma, basi pale Madaba, umeme vilevile utakwenda Ludewa na utapita katika Kata kubwa za Lugalawa, Mlingali na Ludewa yenyewe. Nataka kushukuru kwa sababu katika muda mfupi kinajengwa Kituo cha umeme wa dizeli pale Ludewa wakati tunasubiri umeme wa gridi.

Tunashukuru sana kwa hili. Lakini vilevile, nataka kutambua kwamba, umeme wa gridi utapita kwenye vijiji vikubwa. Kuna vijiji vingi vilivyo kando kando ya njia, ambavyo havitapata umeme huo na Ludewa inajulikana kwa kuwa na vyanzo vingi sana vya *mini-hydro* na Mheshimiwa Waziri, alipotembelea kule alijionea mwenyewe na

alizungumza hata na wananchi ambao wanataka miradi ya *mini-hydro*. Napendekeza kwamba, suala hili ambalo nimewahi kuliwasilisha kwenye Wizara yake vilevile, waliangalie ili wananchi ambao hawatafikiwa na umeme wa gridi waweze kupata umeme wa *mini-hydro*.

Sasa nizungumzie suala la makaa ya Mchuchuma. Nianze kwa kusema, ninasikitika sana kuona jinsi kulivyo na mkanganyiko mkubwa kwenye Serikali, hasa kuhusiana na suala la Mchuchuma. Watu wa *NDC,* walipewa kazi ya kufanya utafiti, nahisi walipendekeza kwenye Wizara, Wizara ilifanya maamuzi ikapendekeza kwenye *Cabinet.* Baraza la Mawaziri, wakatoa msimamo wao na maelekezo ya nini kifanyike kwenye Mradi ule. Lakini badala yake, *TANESCO* nao kwa sababu wana madaraka, wakakataa na wao wakapendekeza mambo wanayotaka wao. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, akafunga safari akaenda kuona mgodi labda mwezi mmoja na nusu hivi uliopita, alitembelea Mchuchuma, akafanya maamuzi yake na yeye katangaza mbele ya wananchi, kawaambia Mradi ule utaanza sasa na Ilani ya Uchaguzi ndivyo ilivyosema.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ile miwili ya Mchuchuma na Liganga, *priority* kubwa imewekwa kwenye Mchuchuma na Mheshimiwa Waziri, kasaidia sana kuleta suluhu kati ya wananchi na *NDC.* Wananchi walikuwa wamekata tamaa, hawataki kusikia habari ya *NDC,* kwa sababu wameuchelewesha ule Mradi na inaelekea wana-*hidden agenda*. Kwa hiyo, walikuwa wamekata tamaa. Mheshimiwa Waziri, alifanya kazi nzuri sana ya kupunguza jazba ya wananchi wale wa Ludewa ili waikubali Serikali kwamba, itakuja na mikakati mizuri. Mheshimiwa Waziri, alisema Mradi huu utaanza sasa.

Lakini kwenye kitabu hiki, sikuona mikakati ya wazi inayoonesha kwamba, Mradi wa Mchuchuma sasa unaanza. Ninachoambiwa ni kwamba, imeundwa Kamati ya Kutathmini Mapendekezo na ninanukuu: “Yaliyowasilishwa na wawekezaji, kutoa ushauri kuhusu njia bora za kuendeleza Miradi ya Mchuchuma na Liganga na kuzingatia Mkakati wa Utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005.” Sasa mtu unashangaa kwa nini kunakuwa na danadana na Kamati hiyo ajabu yake ni kwamba, Mbunge wa Ludewa, mwenye rasilimali hizo hahusishwi kwenye hiyo Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Raynald A. Mrope hapa amezungumzia kuwahusisha wananchi, kwani inaweza ikasaidia sana kutatua matatizo kwa kuwahusisha wananchi, kwa kutumia *top bottom and bottom up approach*. Tuunganishe *top bottom and bottom up approach,* tukutane katikati, wananchi washirikishwe katika masuala haya hata kama ni kwa kuwa wasikilizaji. Kwa nini kwenye Kamati hii, inayozungumzia masuala ya Madini ya Ludewa, wananchi hawawakilishwi na wala Mbunge wao hashirikishwi?

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa tisa wa kitabu hiki, tunaingiza sasa Mradi wa Ruhudji na ukisoma kwenye ukurasa ule wa nane na wa tisa, kichwa chake cha habari kinazungumzia ongezeko la uzalishaji wa umeme usiotegemea maji. Wametaja mikakati kadhaa pale, miradi ya muda mfupi na ya Kati na muda mrefu. Lakini katika Miradi ya muda wa Kati na muda mrefu, umeingizwa Mradi wa Ruhudji, ambao ni Mradi

wa Maji. Mimi nilitegemea hapa wangezungumzia masuala ya makaa, ambayo ni mbadala wa miradi ya maji. Kichwa kilikuwa ni suala la uzalishaji wa umeme usiotegemea maji, lakini katika kifungu kidogo cha (22), kinazungumzia tena Mto Ruhudji, ambapo bado tunaingiza Mradi wa Maji, badala ya kuzungumzia Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, hii inakatisha tamaa sana, hata wananchi wale wa Ludewa wanashangaa kwamba, baada ya maneno mazuri ya Mheshimiwa Waziri, leo hawaoni kitu kinachojitokeza waziwazi, kuhusiana na Mradi wa Mchuchuma kama utaanza. Hii inapingana vilevile na Sera ya CCM. Kwa utaratibu huo, haitawezekana ifikapo mwaka 2009, chochote kiwe kimeanza kwenye Mradi ule wa Mchuchuma, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18, Mheshimiwa Waziri, anazungumzia nishati mbadala, anazungumzia *solar* na *biofuel*. Lakini suala la makaa ambayo nayo ni mbadala, halizungumzwi. Haya yote yanaonesha kwamba, bado suala la Mchuchuma liko mbali sana katika *agenda* ya Serikali. Bado liko mbali sana, ndiyo maana inakuja Ruhudji na sitashangaa itakuja *Stiegler's Gorge.* Wanaona kwamba, Mradi huu hapana, bado wanauchelewesha uendelee kubaki.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaokaa na kuzunguka makaa ya mawe yale wana haki na ardhi. Kulikuwa na Mkataba kati ya wananchi na *NDC,* wa kutotumia ile ardhi, wasiendeleze, wasijenge nyumba za kudumu wala kuleta maendeleo. Mkataba ule ulitakiwa uishe mwaka 2003 na kwa kweli ume-*expire*. Wananchi wale wameshindwa kujiletea maendeleo yao, wakitegemea Mradi huu utaanza, mpaka leo hakuna kitu. Wananchi wale kwa kweli wamechoka, wanataka basi waruhusiwe waanze kuyatumia maeneo yao, kama Serikali haina utaratibu wa kuyachimba yale madini, wapewe ruhusa wanataka waendelee kutumia ardhi yao kama wanavyotaka wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuma cha Liganga. Kwanza, nataka kusema, Chuma cha Liganga kiko Ludewa. Ukisoma kwenye hiki kitabu ukurasa 29, chuma kile kimeonekana kiko Njombe, unaona tumeanza kuporwa, sasa siyo kwamba, kiko Ludewa. Hapa kumetokea mazungumzo kwamba, wananchi wa Ludewa labda wanaona ile mali ya chuma na mkaa ni mali ya wana-Ludewa pekee yao, si hivyo. Sisi hatujasema, wananchi wa Ludewa hawajasema hivyo na mimi Mbunge wao sijasema hivyo. Lakini tunasema mbuzi anapofungwa kamba, hula kufuatana na urefu wa kamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mategemeo ya maendeleo ya watu wa Ludewa, yanategemea rasilimali zilizopo Ludewa, kama vile madini yaliyoko Chunya ni kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Chunya, madini yaliyoko Mererani kwanza, wanategemea watu wa Mererani wa-*benefit* kutokana na madini hayo. Lakini tunajua wote kwamba, faida kubwa lazima itakuja kwenye Wilaya nzima, itakuja kwenye Mikoa inayozunguka na itakuja kwa Taifa zima, ndivyo tunavyoelewa. Hakuna mtu anayesema ni mali ya watu wa Ludewa peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siamini kwamba madini ya chuma hayawezi kuchimbwa mpaka Mradi wa Umeme ukamilike. Hili lingekuwa kama Serikali ingefanya uamuzi wa kutafuta wawekezaji wakubwa, ambao wanaweza kuwekeza katika Mradi wa Chuma ili kuoanisha Mradi wa Chuma na Mradi wa Liganga. Lakini inaelekea imeshindikana, miaka 40 hakuna kinachofanyika. Ndiyo maana wananchi wa Ludewa, wamependekeza kupitia Mbunge wao, tumesema jamani kama imeshindikana ku-*develop* Miradi hii Kitaifa, basi muigawe Milima ile ya Liganga katika vitalu, tuwape wawekezaji mbalimbali washindane.

Mheshimiwa Spika, tuseme wanaotaka kuchimba chuma kwa ajili ya kusafirisha nje, hao wangoje Mradi wa Mchuchuma utakapokamilika ndipo wachimbe chuma, hata ikiwa ni miaka 50 watakuja kuuza na kusafirisha wakati huo. Wale wanaotaka kukitumia chuma kwa kuzalisha vitu vinginevyo, wapewe fursa na maeneo madogo, waweze kuzalisha mazao mengine yanayotokana na chuma yaweze kusaidia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna wizi mkubwa wa nyaya za simu, juzi Mbeya ilitokea. Hii mifuniko ya *chamber* za majitaka Mijini, kila siku inaibiwa kwa ajili ya chuma chakavu. Afrika Mashariki nzima, hakuna. *Demand* ya chuma chakavu ni kubwa, ndiyo maana wanaiba vitu hivi hata kwenye madaraja. Njia moja ni kuzalisha *sponge iron,* ambayo ni mbadala wa chuma chakavu na sisi tuna chuma Liganga kimezubaa. Hivi kweli Milima yote, kumega kipande kidogo tukawapa wawekezaji wazalishe *sponge iron* kwa kusaidia nchi hii kuondokana na wizi wa nyaya, inakuwa ni nongwa. Lakini ni uamuzi, tunataka kukitumia chuma chetu kwa ajili gani, tunataka kuuza chuma au tunataka kuuza *products* za chuma. Ni uamuzi tu, tukiamua tunafanya tunachotaka.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa vile Serikali imeshindwa kuonesha kwamba, ina nia ya kuchimba kile chuma, kwa kweli wananchi wana haki ya kutafuta mbadala kwamba, labda kuna njia nyingine za kuchimba hiki chuma, kikatusaidia sisi na Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa habari ya kuchenjua chuma kile kupata, *vanadium* ya *titanium*. Lakini teknolojia ya kuchenjua madini hayo kwa sasa hivi ulimwengu mzima ni aghali na ni kidogo, itachukua miaka mingi mpaka tupate teknolojia hiyo hapa Tanzania. Ina maana kwamba, tukitaka kweli Mradi ule uweze kuchenjua *vanadium* na *titanium,* tungoje miaka mingine 50. Wananchi wale wanasema, jamani, tunazaliwa, tunakufa, tungoje mpaka watakapochenjua hicho chuma ni lini? Mheshimiwa Waziri, alipokuwa Ludewa aliwaambia wananchi wa Mundindi pale Liganga kwamba, utafiti huu uendelee, lakini tutaanza kuchimba chuma.

Mheshimiwa Spika, niliamini kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri atanipa mkakati wa kuanza kuchimba chuma kile. Sasa huku kwenye kitabu hili halizungumzwi kabisa, nimeshangaa sana kwa nini hilo liko hivi! Majumuisho yangu yanasema hivi, kama hatuwezi kupata mwekezaji mkubwa na kama hatuwezi kuanza kuchimba madini yale, basi Serikali na Waziri, waende Ludewa wakawaambie wananchi wale, alikosea kusema yale maneno kwamba, madini yale yataanza kuchimbwa. Mimi nitashindwa na

Mheshimiwa Waziri, aliwaona watu wale walivyokuwa wakali na walivyokuwa na ghadhabu.

Mheshimiwa Waziri, aende mwenyewe au Waziri Mkuu au Serikali, mkawaambie wale wananchi kwamba, mmeshindwa kutekeleza na kutimiza ahadi.

Mheshimiwa Spika, pili, wananchi wale wamengojea kuhodhiwa ardhi yao kwa kushikwa na Serikali kwamba, wasiitumie. Maadam Serikali haina nia ya kuendeleza madini yale, muwaruhusu wananchi wakaitumie ardhi yao kama wanavyotaka. Kwa sababu ufafanuzi huo nimeukosa kwenye kitabu hiki, ingawa naipenda sana nchi yangu, nakipenda Chama changu cha CCM, uzalendo utanishinda.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana nisiunge mkono hoja hii mpaka nipate ufafanuzi na nipewe maelezo kuhusu haya niliyoyazungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie kwenye hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kwimba, hakuna madini. Lakini ninafahamu niliposimama Mheshimiwa Waziri, anaweza kuwa anafikiria nitachangia wapi, sianzi huko. Nachangia kuhusu madini kwanza.

Mheshimiwa Spika, madini ni akiba ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Akiba kwa kawaida unaitumia wakati unapokuwa na shida, huitumii akiba wakati wowote, unapokuwa na shida ndipo unapoenda kuchukua sehemu ya akiba yako na kuitumia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasikiliza Waheshimiwa Wabunge wengi sana, hasa wale ambao wanatoka sehemu zenye madini. Nikaanza kufikiri labda ni vizuri tukaanza Kwimba kwamba, hatuna madini, maana hakuna hata mmoja ambaye ana raha. Lakini vilevile ukiangalia ni kana kwamba, tumeamua kuchimba madini yetu yote. Mimi nafikiri siyo busara sana.

Mheshimiwa Spika, huwezi kwenda benki ukafungua akaunti yako kwa ajili ya shughuli ya siku moja, siyo vyema. Unaenda benki kufunga akaunti kama tu ulikuwa umeweka fedha hizo kwa ajili ya shughuli hiyo. Mimi sijawahi kusikia mtu anaenda kufunga akaunti kwa shughuli ya harusi. Madini haya ni madini ambayo ukishayachimba, ukayatoa pale, hutayakuta tena pale, ni kama mtu ameenda kufunga akaunti benki. Kama unachimba madini halafu uyatumia vibaya, maana yake ni kwamba, yale madini yamepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia hasa faida tunayopata kutokana na madini tunaitumiaje? Ni vizuri tunajenga barabara, ni jambo njema, tukinunua madawa ni jambo jema, lakini vyote hivi ni vya kupita. Tunahudumia mambo ya leo si ya kesho. Utafika wakati madini haya hatutakuwa nayo na nchi hii inaweza kuja kuwa maskini zaidi kuliko tulivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, wazo langu, Serikali ijaribu kuangalia fedha hizi tunazozipata kutokana na madini, tuzielekeze wapi zaidi. Wazo langu mimi, madini haya kuwa endelevu yasije yakapotea. Tuyachimbe na tuyatumie lakini yasije yakapotea. Kwa namna gani? Wazo langu tuwekeze katika elimu, tuwekeze katika teknolojia, hiyo ndiyo itatuletea faida kubwa zaidi katika miaka ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo katika kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Richard M. Ndassa aliuliza swali, barabara ya Mwanza - Ilula tukaambiwa kuwa imetumia fedha nyingi sana baada ya miaka mitano, sita, barabara haipo. Mheshimiwa Waziri, hakutuambia dhahabu kiasi gani ambayo ilikuwa imetumika katika kujenga barabara hiyo. Madini yetu yanapotea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, fedha tunayoipata tuiweke fedha kiasi fulani kwa ajili ya elimu na fedha kiasi fulani kwa ajili ya utafiti. Hiyo ndiyo itakuwa almasi yetu ya baadaye, kitu hicho ndicho kitakachokuwa dhahabu yetu ya baadaye. Hivyo ndivyo watoto wetu na wajukuu wetu watakavyokuja kuweza kurithi dhahabu na madini mengine tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunafurahia labda tuombe kiama kije kesho, kama kiama hakiji kesho, watoto wetu watahitaji kupata faida ya madini yao na sisi tutakuwa tumeisha yatumia yote.

Mheshimiwa Spika, wazo lingine pamoja ni kuweka vipaumbele vya kutumia fedha tunazopata kutokana madini, tuanze kuchimba madini yetu kwa *blocks*. Tuanze na madini ya aina moja, labda dhahabu tu. Wawekezaji wanaotaka kuja kuchimba dhahabu, ndiyo tuwakaribishe madini mengine yasubiri. Kwa sababu nchi yetu hii, bado hatujafikia mahali pazuri pa kuweza kulinda mali yetu. Kila mmoja aliyesimama hapa, anasema dhahabu tunaibiwa, wengine wanasema *Tanzanite* tunaibiwa. Akisimama Mbunge wa Shinyanga Vijijini atasema, Almasi tunaibiwa. Hatuna uwezo, tukikaribisha watu wote watakuja kuiba na wataondoka.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kwamba, litakuwa wazo zuri, tukijiwekea vipaumbele kwamba sasa hivi tunaanza na kitu fulani, tukaweka nguvu zote kulinda kama ni dhahabu na hivi vitu haviozi, dhahabu haitaoza, almasi hataoza, bado inaweza kutumika baadaye.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu madini. Ni kuhusiana na watu wanaokuja kufanya tafiti za madini katika maeneo mbalimbali. Mimi ninachotaka kufahamu hasa watafiti wanaopewa vibali wana uhusiano gani na Halmashauri za Wilaya na wana uhusiano gani na wananchi wanakoenda kufanya utafiti?

Mheshimiwa Spika, ninayo mifano. Kuna kampuni moja inayoitwa *Free African Limited,* ilikuja Kwimba, ikapewa maeneo, akaenda Kata ya Mwaklyambiti, Kikubiji na Igongwa. Wilayani alifika salama, akatoa taarifa kwamba, amefika, baada ya kumaliza utafiti hakuaga, akaondoka kimya kimya. Nilijaribu kufuatilia, haijulikani alipata nini au

kama ameenda kujiandaa baadaye angerudi. Hatujui ni miaka miwili imepita! Vivyo hivyo alikuja mwingine anaitwa Fred na yeye akapewa maeneo ya kwenda kufanya utafiti, akafanya hivyo hivyo, akatembea katika sehemu mbalimbali, naye alipomaliza akaondoka kimya kimya. Wilaya haijui, wananchi hawajui na wala viongozi wao hawajui.

Mheshimiwa Spika, mtafiti mwingine yuko huko Wilaya ya Misungwi huko, kama miaka mitatu, minne. Hivi sasa bila shaka Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, ina taarifa. Lakini huwa anakuja mpaka Kwimba, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba haina taarifa. Mimi kama Mbunge, nimepita kule nikagundua kuwa, anapita pita kufyeka, wananchi wanajua amekubaliwa. Kwenda Wilayani, wakasema hawana taarifa naye. Tunafahamu kwamba, yupo Wilaya ya Misungwi. Sasa ninachotaka kufahamu, hawa watu wanapokuja kwenye Wilaya, wanakuja na maelekezo gani na hata hawawezi kutoa taarifa kwa Halmashauri za Wilaya, ndilo lilikuwa tatizo langu hilo? Kwa sababu ingefaa wakatoa taarifa, kama wamegundua basi watu waelezwe kwamba, hapa kuna matarajio ya kuja kufanya mradi Fulani, wakajiandaa, kama ni kuhama waanze kuhama na kujenga nyumba mahali pengine au kama ni kujiandaa kwa vyovyote, wajiandae.

Nashukuru sana kwa kengele hii ya kwanza, sasa nakwenda kwenye eneo la umeme. Kila mmoja hapa anafahamu uhusiano wa maendeleo ya nishati. Watu wa Kwimba hivyo hivyo, wanafahamu pamoja na kwamba, hawana madini lakini wanafahamu kwamba, nishati ni muhimu kwa maendeleo. Mimi kama Mbunge wao, tangu mwaka 1995 mpaka 1996 nilianza kufuatilia suala hili na huwa napata maelezo mazuri sana. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kabla hajateuliwa kuwa Naibu Waziri, maombi yangu ya umeme tayari yalikuwa katika Wizara hiyo. Kwa hiyo, naamini kwamba, anayajua.

Tumefuatilia, tumeongea naye akiwa Naibu Waziri mwenzangu, baadaye amekuwa Waziri nafuatilia. Ninapoongea naye ana kwa ana, naamini kabisa kwamba, anasema ukweli. Mimi namwamini sana na ninamheshimu sana, pamoja na kuwa ni mtani wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo nalipata ni kila ninapopata taarifa ambazo ni tofauti, mara ya kwanza ilikuwa mwaka nadhani 1999, niliambiwa kwamba, gharama ya kupeleka umeme katika maeneo ambayo nitakayoyataja ni shililngi 1.3 bilioni. Mimi nikafurahi kwamba, haiwezekani hii *amount* ikatajwa bila ya kufanyiwa utafiti. Mwaka 2005 nikapewa taarifa nyingine gharama ni shilingi bilioni 880 na kuwa huu Mradi utafanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza, bado haijaanza wala hatujafahamu kama Mradi huu upo au haupo? Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kila wakati ninapopata taarifa, huwa napeleka jimboni kwangu na moja ya sababu iliyonirudisha humu Bungeni ni kuwaambia kwamba, umeme utafika katika maeneo hayo nitakayoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema hivi sio kwa kujitungia, ni kwa sababu nilikuwa napewa taarifa hizo. Umeme ambao nauongelea ni umeme wa kijiji kimoja cha Hungumalwa ni kijiji kikubwa, wale ambao huwa mnasafiri kwenda Dar es Salaam

mnaweza kulinganisha na Kibaigwa kuna mnada mkubwa na ni *centre* ya watu wengi sana. Nimeomba umeme tangu mwaka 1996. Nimeomba umeme kutoka pale uende mpaka Shilima kwa sababu katika barabara hiyo utakuta kuna *ginneries* mbili. Kuna *ginnery* ya Mwalujo, Sangu na kuna *centres* nyingi tu katikati.

Kuna Shule za Sekondari saba njiani, kuna kituo cha afya, kuna *dispensary* na kuna wananchi. Mwaka 1999 wenye zile *ginneries* walikuwa tayari kuchangia angalau kuonesha ishara kwamba, watakuwa *consumers* wa umeme. Lakini majibu ya kuaminika bado hayajapatikana. Kwa sababu nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri ana kwa ana, alinijibu vizuri. Namwomba avumilie tu, leo arudie tena majibu aliyokuwa ananipatia kwamba, umeme utakwenda eneo hilo.

Nafahamu hapa katikati nilikuwa naumwa, inawezekana alikuwa ananipatia majibu mazuri kwamba, nisije nikapata *stroke* nyingine. Lakini napenda kumwondolea mashaka, asiwe na wasi wasi, siwezi kupata *stroke* nyingine hata akiniambia kwamba, umeme hautakwenda, lakini nitaelewa tu kwamba, haya yalikuwa ni matani yake huko nyuma. Lakini namwamini sana. *(Makofi)*

Namwondolea wasi wasi kwa sababu mtu akitokwa na woga unakuwa huru. Namwondolea ule woga wa kwamba, naweza kupata *stroke* ili awe huru, aweze kusema wazi kama Mradi upo au haupo?

Mwisho, ni masuala ya *biogas*. Napenda nitumie fursa hii, kuishukuru *UNDP* walitufadhili Mradi wa *Biogas* mwaka 2000/2001. Ulipokelewa vizuri sana na watu wa Kwimba hasa Tarafa za Mwamashimba na Nyamilama. Lakini kwa bahati mbaya sana, wale walioandaa ule Mradi nahisi kama walikosea. Matangi ya kuhifadhia gesi yalikuwa ya kudumu miaka miwili na nusu hii ndio *life span* yake. Baada ya miaka miwili, yakaanza kupasuka yote.

Tulipata *units* kama mia moja, sasa hivi hakuna hata moja ambayo ipo kwa sababu yamekwisha *expire* yote. Nilikuwa naomba Wizara hii, itusaidie katika nishati mbadala Wilayani Kwimba. Kwimba ikiwa ni eneo ambalo ni kame sana, halina miti, watuletee wataalamu waje kufanya *assessment* tu ya ule Mradi kama wanaweza kuufufua. Watu wa Kwimba wanaufahamu, wanachohitaji ni kupewa msaada tu wa kiufundi na fedha kidogo kwa ajili ya kuuendeleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwa mara nyingine tena ili niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, hoja ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanadamu kuwa na msimamo ni moja ya sifa adimu na kwa kweli adhimu vile vile kwa kiongozi. Lakini ni uungwana pia mwanadamu

kubadilika, ukikerwa nuna, ukifurahishwa ufurahi. *Wallah*! Waziri wa Nishati na Madini mimi amenifurahisha sana. Akiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo katika Serikali ya Awamu ya Tatu, aliutembelea Mradi wa *Mnazibay* mara mbili. Katika Serikali hii ya Awamu ya Nne yeye sasa ni Waziri kamili, safari ya juzi Jumamosi tarehe 15 Julai, 2006 pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni safari yake ya nne. Mwenzangu mmoja alisimama hapa akasema aah! Sawa Kusini, lakini Kusini Nyanda za Juu mbona mmekusahau?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu yeye mwenzangu ni Mbunge, simlaumu. Lakini mkiwa watoto wa baba mmoja, wewe umeshanunuliwa viatu, mwenzako akinunuliwa viatu usilalamike mbona mimi sijapata soksi, tupate kwanza viatu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme wenzetu Wabunge na wananchi wa maeneo mengine, wafahamu kuwa kupewa umeme watu wa Lindi na Mtwara, hatujapendelewa ni haki yetu. Tusimsikie mtu anasema hapa watu wa Lindi na Mtwara wanapendelewa *Mnazibay,* ni haki yetu kupata umeme kama Watanzania wengine wote. Tokea Uhuru korosho zetu na ufuta wetu, umekuwa ukiwamulikia Watanzania wenzetu umeme. Wakati umefika sasa na sisi kumulikiwa umeme kwa korosho zetu, ufuta wetu, pamoja na kahawa za wenzetu.

Nataka nimshukuru tena Mheshimiwa Waziri, kwa kutangaza jana kwamba, mwaka huu wa fedha, Vijiji vya Mchinga Moja na Mchinga Mbili navyo vimo katika kupata umeme. Kwa miaka 11 sasa nimekuwa nikiomba, kwa maandishi kama unavyofahamu, wakati ule nilikuwa siwezi kusema kama hivi na mwaka 2005 nikamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, nisingekuwa Naibu Waziri, leo ningemnyang'anya shilingi. Nashukuru amekumbuka, amefikiria sasa hivi na kuamua kusikia kilio chetu. Lakini nikumbushe tu tuliomba na umeme vile vile Ng'apa. Ninaamini kwa sababu sasa umeme mwingi unakuja wa *Mnazibay*, basi vijiji vilivyomo katika Tarafa tano za jimbo la Mchinga na vyenyewe vitafikiriwa kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu wakati ule umepita wa kudhania kwamba, vijijini hakuhitajiki umeme, eti kwa sababu hakuna utajiri wa kuweza kufidia gharama za umeme. Lazima tufahamu kwamba, umeme wenyewe peke yake ni chachu ya maendeleo ya kumtajirisha Mtanzania. Kwa hiyo, ukija umeme haya mengine yatakwenda, wenyewe tu tusilete habari ya yai na kuku kwamba, cha mwanzo kipi. Mimi nafikiri umeme ndio wa mwanzo, halafu maendeleo ya mwananchi yatafuata. Katika Tarafa zangu za Ng'apa, Milola, Nangaru, Mchinga na Mipingo, watu wanalima ufuta, korosho na mpunga kwa wingi. Umeme huu ukija, nina uhakika utakuwa ni kichocheo cha kuongeza shughuli hizo za kujizalishia mali maradufu zaidi.

Kwa hiyo, tungeomba basi huu umeme unaokwenda Mchinga, kwa sababu unapita katika Vijiji vya Mbanja, Mamburu, Kikwetu, Likong'o, Mto Mkavu na vyenyewe navyo wawekewe *transformer* walau moja kila baada ya vijiji viwili ili nao waweze kunufaika na umeme badala ya kuona unapita tu juu, ndiyo inafikia watu wengine hawaibi nyaya hizi kwa sababu ya kutafuta utajiri, ni kwa hasira, umeme unapita

hapo hapo unakwenda kuwamulikia wa mbali, nyie mnaangalia waya tu ndio unakuta wakati mwingine wanafanya vile kama namna ya kuonesha hasira yao.

Mheshimiwa Spika, hii Kampuni ya *ARTMUS* wakati inatafuta kuingia kwenye mkataba wa kufanya shughuli hii ya *Mnazibay,* tulikuwa tunapata habari nyingi sana. Habari za kitaalamu zilikuwa zinaonesha kwamba, *ARTMUS* ni watu wababaishaji, hawana uwezo wa kifedha wala utaalamu kuifanya kazi hii. Sisi kama Wabunge wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, tulilazimika kumfuata Mheshimiwa Waziri, kumwambia ukweli kwamba, tatizo la *ARTMUS* kuzungushwa zungushwa, sio uwezo wao wa fedha na utaalamu. Tatizo lililopo ni kwamba, kuna wataalamu hawawataki hawa kwa sababu zao binafsi. Tulionekana kama vile wazushi, waongo. Lakini tunashukuru, baadaye Mheshimiwa Waziri mwenyewe, baada ya kufuatilia na juzi Jumamosi baada ya Waziri Mkuu kufika, wameamini kwamba, *ARTMUS* ni Kampuni yenye *commitment,* yenye uwezo wa mtaji, lakini yenye uwezo wa kitaalamu. *Drilling* inayofanywa sasa katika kisima cha pili pale Msimbati, inatumia mitambo ya kisasa kabisa, ambayo haijawahi kuingizwa katika nchi hii.

Lakini hawa watu wanajali mazingira vile vile, pale walipokata mikoko ili kulaza mabomba kupita baharini, baada ya miezi minne wameahidi kuirudisha tena ile mikoko, maana bomba litakuwa limeshakaa. Wengine wanachimba madini, wanatuachia mashimo, hawa hata mikoko waliyokata wanaamua kuipanda upya, hawa ni watu wa kupongezwa na wala sio kulaumiwa. *(Makofi)*

Lakini kijijini Msimbati kwa Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, wamejenga na bweni kwa ajili ya Sekondari ya Wasichana. Wamemwahidi Waziri Mkuu juzi kwamba, watahakikisha asilimia 99 ya wafanyakazi wa Kampuni ile ni Watanzania. Wengine wanatuletea mpaka wapishi wa chapati kwenye mahoteli kutoka India, wale wanasema hapa hapa. Sasa mimi ningeomba jamani, mnyonge mnyongeni na haki yake mpeni, hawa tusiwavunje moyo, wanafanya kazi yao vizuri.

Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri, aniwie radhi sana. Umeme huu awamu ya kwanza wanasema utaingia Mtwara, ufike na Lindi. Ndiyo na hili Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Mtwara, mniwie radhi maana sisi tukivuka Mto Rufiji kuelekea Dar es Salaam, sisi wote ni Wamachinga au Wamakonde. Hawajui huyu wa Mtwara au Lindi. Sasa tusiwe kama samaki ndani ya dema, mmeshaingia mle, hatma yenu mnamsubiri mwanadamu aje, awafanyeni kitoweo mle mle mnaanza tena mimi kitapwi jamii ya chewa, wewe lazima nikule kwa sababu wewe pono, haifai. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu ya uzoefu, najua kuna udhaifu wa kujenga hoja kwa kutumia matukio yaliyopita. Lakini matukio haya yanapokuwa na tabia ya kujirudia rudia tukubali kwamba, uzoefu nao ni mwalimu bora. Kuna tabia ya Serikali kushindana kuididimiza Lindi na kuikuza Mtwara. Ndiyo maana nasema umeme huu ufike Lindi na nina ushahidi.

Mheshimiwa Spika, wala usipate tabu ya kusema lete ushahidi, nautoa hapa hapa. Moja, Mji wa Lindi peke yake una mashamba ya chumvi 43, Wilaya ya Kilwa 26, kunachimbwa vito Ruangwa, Nachingwea na Liwale, Ofisi ya Madini ya Kanda iko Mtwara. Juzi nilikuwa nasema wakati wa Wizara ya Miundombinu hapa kwamba, hata Ofisi ambayo iliwekwa pale ya mitambo tarehe 26 Aprili, 2006, iliandikwa barua kumhamisha huyo mtu Mtwara iwe ofisi yake. Nashukuru Waziri Mkuu, aliingilia na sasa Ofisi ile imebaki Lindi. Lakini mashindano haya hayaishii kwa Wizara hiyo tu. Juzi Waziri Mkuu hapa, ametoa shilingi bilioni moja kutoka Hazina kwa ajili ya pembejeo za zao la korosho. Shilingi bilioni moja iliyotolewa asilimia 70 ilipelekwa Mtwara, asilimia 30 ndiyo Lindi, Dar es Salaam, Tanga na Pwani, utani gani huu.

Sisi watu wa Lindi toka tunapata akili, tunajua watani zetu sisi Wayao, Wangoni, Wanyamwezi, Wasukuma na hawa akina Mheshimiwa George M. Lubeleje ndio watani zetu sisi. Huu utani wa Wizara ya Kilimo na watu wa Lindi, umeanzia wapi? (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni moja, asilimia 70 mnapeleka Mtwara. Wizara ya Elimu na Utamaduni waliihamisha *VETA* mwaka 1997 pale wakaipeleka Mtwara. Mimi Mheshimiwa Waziri wa Elimu, namfahamu vizuri, nilipokuwa Naibu Waziri wa Kazi ni mtetezi kweli yule mama wa wafanyakazi. Sasa na safari hii, naamini atakuwa mtetezi kwa watu wa Lindi vile vile. Chonde mama uliko huko, utakuwa unanisikia au salamu zitakufikia.

Mradi wa Songosongo gesi imekwenda Dar es Salaam, kipindi kirefu kweli mwaka huu ndio tunatarajia tena kwa upondo, hewehewe labda unaweza ukafika Kilwa Masoko. Umeme ufike Lindi Mheshimiwa Waziri, *Wallah* wewe kaka yangu bwana.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu hata ukaguzi Mtwara. Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, Mahakama Kuu Kanda Mtwara. Eeh! Wizara ya Maji, Mamlaka Bonde la Mto Ruvuma Ofisi Mtwara. Jamani hii Lindi ni mji.

Mheshimiwa Spika, nina wasi wasi kuna watu wanakwenda kuchukua ile KAMUSI ya Kiswahili Sanifu iliyotengenezwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili Dar es Salaam. Kule wameandika Lindi ni tundu la choo.

Mheshimiwa Spika, Lindi ninayoizungumza mimi ni Mji wa Lindi na Mkoa wa Lindi, wenye Wilaya za Nachingwea, Liwale, Ruangwa, Lindi na Kilwa. Kwa hiyo, tungeomba sasa kama hii ya madini wala huna hasara, ilete Lindi ndio kwenye watu wengi, kwenye shughuli hizo nyingi, lakini kila kitu Mtwara, Mtwara, Lindi tumekosa nini.

Watu wa Mtwara mtuunge mkono katika hili, sisi wote ni samaki tuko ndani ya dema, tunasubiri hatma yetu mwanadamu atuchukue akatupae macho tunaangalia, tukatwekatwe macho tunaangalia, tutiwe chunguni macho tunaangalia, tuliwe na kugeuzwa macho tunaangalia tu. Kwa hili tusitengane. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini namwomba kaka yangu, aufikishe umeme Lindi na Mchinga. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru mradi wa Chanika - Magamba uko kwenye *pipeline, scheduled at* 2009, ni ule wa kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kuwa *inflation* inachangia sana ku-*erode purchasing power* ya wananchi wa ngazi zote. *Contribution factors* ni chakula *(food basket)* na mafuta. Tulipoanza Bunge *inflation rate* ilikuwa asilimia 6.9 hivi sasa ni ni asilimia 7.7! Bado mfumuko huu utaendelea. *Measure* ya Wizara ya Fedha kufuta *VAT* kwenye mafuta, *impact* yake imekuwa *muted* na *excise duty*. Kwa vile mafuta yanachochea mfumuko wa bei, malalamiko yataendelea baina ya wananchi. *You might need to consult with Ministry of Finance to see how to nationalize the impact of VAT vis and vis excise duty* kwenye mafuta. Hongereni na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia tukiwa wazima na salama kwani yeye ndiye muweza wa kila kitu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii anatuahidi lini sisi wananchi wa Kisiwa cha Pemba tutapata huo umeme toka Tanga ambao amekuwa akiutaja mara kwa mara anapokuwa akijibu maswali hapa Bungeni.

Kwa kuwa sasa Wilaya nyingi zimeshapatiwa umeme, je, kwa nini Serikali haituonei huruma na sisi watu wa Kisiwa cha Pemba ikatupatia umeme kama wenzetu wa Unguja na tukaondokana na adha hii ya kutegemea umeme wa *generator* ambao hauna uhakika, mara unasikia hakuna mafuta, mara mashine imeharibika na matatizo mengine yanayojitokeza ya kiutawala.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme sio *luxury,* ila ni jambo la muhimu katika maisha ya binadamu bila ya kuwa na umeme kwa dunia ya leo hakuna maendeleo. Sasa sisi wa Kisiwa cha Pemba mnatuacha nyuma kimaendeleo . Hivyo basi, tunaiomba Serikali ya Muungano itupatie huo umeme toka Tanga badala ya kutoa ahadi ambazo hatuoni utekelezaji wake. Nasema hivi kwa sababu katika bajeti hii sioni kama kuna sehemu iliyoonyesha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa leo nimekusudia kuulizia jambo hili tu naomba jibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, sikupenda kueleza mengi kwa kuwa najua Wizara hii Wabunge wana hoja nyingi sana. Ahsante.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo ni kuhusu tatizo la kukatika kwa umeme na kutofuatiliwa kwa tatizo hilo katika maeneo ya Mikocheni. Umeme umekuwa ukikatika si sababu ya mgao bali hata umeme unaporudi baadhi ya nyumba zimekuwa zikilalamika kuendelea kukatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tatizo ni kwamba wafanyakazi wa *TANESCO,* Mikocheni hawajali kabisa malalamiko ya wananchi katika maeneo hayo. Katika ofisi yao kuna simu ambazo hazipokelewi, hivyo kufanya hata mteja mwenye tatizo katika nyumba yake kulazimika kwenda ofisini ili kuomba huduma. Hata hivyo, wafanyakazi hao wamekuwa na tabia ya kusema ahadi za uongo kwamba watafika sehemu husika kutengeneza lakini badala yake wanaweza kufika baada ya hata wiki moja

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara kuangalia upya Idara ya Huduma kwa jamii katika eneo hili, wananchi wamekuwa wakilalamikia Idara hiyo bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua wafanyakazi wa Idara hii hutakiwa kuwa na sifa gani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii kwa hotuba ya bajeti ambayo inaleta matumaini kwa umeme inayotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Naunga mkono hoja hii . Hata hivyo, ninayo maoni yafuatayo:-

Moja, umeme vijijini, Manyoni. Mji wa Manyoni ambako ni Makao Makuu ya Wilaya ulipatiwa umeme mwaka 2000. Tunashukuru sana Wizara hii kwa hatua hiii. Hata hivyo, mategemeo ya wananchi wa Manyoni yalikuwa kwamba sasa umeme huo ungeanza kusambazwa kufika vijijini hatua kwa hatua. Matokeo yake miaka sita imepita bila umeme kufikishwa hata katika kijiji kimoja Wilayani ukiacha Mji Mdogo wa Itigi.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Wizara chenye jedwali lenye vijiji vilivyopata umeme mwaka 2004/2005 unaonyesha kuwa Wilaya ya Manyoni hakuna hata kijiji kimoja kilichopata umeme, kwa nini? Ombi letu ni kwamba katika mpango wa *Rural Energy Fund* utakaoanza mwaka 2006/2007 baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Manyoni hasa Jimbo la Manyoni Mashariki viingizwe katika orodha ya kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu mipango ya nishati mbadala vijijini. Kwa kuwa itachukua muda mrefu sana kwa umeme wa *grid* kufikia vijiji vyote nchini, Wizara hii inashauriwa kuanzisha kitengo cha kusimamia nishati mbadala vijijini hasa umeme wa jua *(solar energy),* umeme wa gesi na umeme wa *biogas.* Kitengo hicho kisimamie elimu ya umma juu ya nishati mbadala pia vifaa na mitambo ya kuendesha

aina hizi za nishati vipatikane hapa nchini kwa bei nafuu ili viwe *affordable* kwa wananchi vijijini.

Tatu, kuhusu utoaji leseni kwa wachimbaji wadogo, hapa Tanzania wengi wamejiajiri katika sekta ya madini kama wachimbaji wadogo wadogo. Ilani ya Uchaguzi ya CCM inawatambua wachimbaji hawa, tunachoomba ni kuwepo kwa taratibu madhubuti za kuwatengea maeneo rasmi ya uchimbaji, kuwepo kwa elimu ya uchimbaji wa kisasa, kuwapa mikopo ya kununua zana na pia kuwapa leseni za kuchimba ili wasiendelee kuwa wachimbaji haramu.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wa machimbo Londoni katika Jimbo la langu la uchaguzi waliomba leseni za uchimbaji tangu mwaka 2004 lakini baadhi yao bado hawajapewa na wanalazimika kufanya uchimbaji haramu bila wao kupenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha na watendaji wote wema wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kutekeleza kazi kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Tandahimba tunawapongeza Wizara kwa mambo mawili. Mosi kuipatia Wilaya yetu ya Tandahimba umeme na pili, kwa kuwezesha mradi wa umeme wa gesi ya *Mnazi Bay,* Mtwara kufikia hatua ya kuanza maandalizi ya kuzalisha umeme. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa Wizara ya Nishati na Madini itasimamia vizuri zoezi la kuhakikisha maeneo yote tarajiwa kwa kupata umeme huo wa *Mnazi Bay* yanapata umeme kwa wakati ikiwemo Wilaya ya Tandahimba.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara ya Nishati na Madini ni kama ifuatavyo:-

Moja, ni vyema Taasisi zilizoko Vijijini, Wilayani Tandahimba zikapewa kipaumbele katika suala la umeme. Taasisi hizo ni Shule za Sekondari za Mnyawa, Mchichira, Maundo, Lyenje, Chaume, Luagala, Ngonja, Nachunyu, Namikupa, Mkundi, Kitama, Mkepeha, Mahuta, Dinduma na Mdimba. Pia Vituo vya Afya vya Namikupa, Luagala na Kituo cha Afya tarajiwa cha Mchichira.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa umeme ni chanzo cha maendeleo, hivyo ili kujenga maendeleo ya haraka nchini hatuna budi wananchi wa vijijini wakapewa nafasi kuitumia nishati kwa maendeleo. Tukumbuke kuwa wananchi wengi wanaishi vijijini.

Pili, pale ambapo umeme umepita karibu na vijiji visivyo na umeme, wananchi ambao hawajashushiwa umeme, basi wahamasishwe kuwekewa umeme kwa kulipia umeme kwa gharama za awamu. Mfano, katika maeneo ya Mchichira, kijiji cha

Nanhyanga kina umeme. Lakini wananchi wa Mchichira wapo tayari kugharamia kulipia. Mikorosho itakayokatwa kuruhusu *line* ya nguzo za umeme. Kama Serikali ikiwaletea umeme na wakaruhusu gharama zingine zikalipwa pole pole wapo tayari kabisa.

Tatu, Wizara iwaangalie wataalam wasiopita katika maeneo ya mradi. Wizara imepata shida na ngumu ya kufikia makubaliano na *Artumas Group* kwa sababu wataalam wa Wizara baadhi yao walitumia *remote control* kupata habari badala ya kuwafahamu mradi. Aidha, ni vyema Wizara ikaimarisha usimamizi kwa wataalam wake kwani baadhi yao wanalalamikiwa kujihusisha na ugonjwa au upendeleo wanapofanya maamuzi.

Nne, napenda kushauri kuwa ingawa nchi yetu haina matatizo makubwa ya maeneo, lakini bado kuna haja endapo inatokea mradi wa eneo fulani, basi Wabunge wawakilishi wa maeneo hayo wakajumuishwa kwenye Kamati za majadiliano hata kwa kuwa wasikilizaji tu *ex-official*. Hii itasaidia kuwabana wanakamati wazembe.

Tano, nashauri kuwa katika zoezi linaloendelea hivi sasa kwamba *Artumas group* kujadiliana na *TANESCO* na kuuziana umeme wa *Mnazi Bay,* Serikali ni lazima iwasimamie, vinginevyo mambo na muafaka wao hautaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi kuhusu Nishati na Madini. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Tatu, napenda kuchangia maeneo yafuatayo, moja, nishati kwa kuwa hivi karibuni Serikali ilitangaza kupunguza bei ya mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya taa. Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba bei ya mafuta inapungua na wale ambao hawajapunguza bei hiyo wamechukuliwa hatua gani baada ya Serikali kuondoa *VAT.* Kupanda kwa bei ya mafuta imesababisha kupanda kwa gharama ya nauli kwa vyombo vyote vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, gharama ya umeme ni kubwa sana, je, Serikali haioni kwamba kupunguza bei ya umeme kutasaidia sana kupata wateja wengi kuliko hali ilivyo sasa. Kwa kuwa umeme sio lazima uwe wa maji tu, je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi matumizi ya *solar power panel* hasa huko vijijini? Je, Serikali itakubaliana nami kwamba *solar power panel* inaweza kutumika kutoa huduma ya umeme kwenye Vituo vya Afya na Zahanati (majokofu ya kutunzia dawa za chanjo) kutumia mafuta ya taa gharama ni kubwa kuliko *solar power.*

Mheshimiwa Spika, je, ni lini vijiji vya Mima, Bumila, Idilo, Kisokwe, Berege, Iwondo, Igoji Kusini (Salaza) Lupeta, Mbori Godegode, Pwaga, Rudi, Chipogoro, Chunyu, Ipera, Chogola, Mbuga Tambi, Mlembule, Majani, Msagali, Mwenzele, watapatiwa umeme Wilayani Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi nzuri zinazofanywa na Wizara na taasisi zake katika kushughulikia masuala ya nishati na madini, tunatiwa moyo na taarifa kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa mafuta nchini. Suala hili sasa lishughulikiwe kwa kasi na nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati ya kutembelea nchi ya Bangladesh kati ya tarehe 03 na 07 Julai, 2006. Bangladesh wana *natural gas* kama sisi. Wamebadilisha magari yao hususan magari ya abiria na pikipiki za miguu mitatu kutumia gesi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linapunguza sana gharama na kuagiza mafuta kutoka nje na p ia matumizi ya gesi hayatoi moshi kama ilivyo kwa dizeli. Naishauri Serikali ianzishe mpango wa kuwezesha kutumiwa kwa gesi kwenye magari majimboni na kwenye viwanda vingi iwezekanavyo.

Suala la pili ni matumizi ya makaa ya mawe, mipango ya kutumia makaa ya mawe kuzalisha umeme ni mzuri na wa kupongezwa. Makaa ya mawe yanaweza kutumiwa kwenye viwanda vya ukubwa mbalimbali. Mipango ya kutumia makaa ya mawe kama chanzo cha nishati kwa viwanda ianze bila kuchelewa.

Makaa ya mawe pia yaandaliwe ili yaweze kutumika majumbani badala ya kuni na mkaa wa miti. Ili matumizi ya aina hii yawezekane, itabidi makaa ya mawe yaandae na pia yapatikane majiko kwa ajili hiyo. Lengo letu liwe kutumia vyanzo vya ndani vya nishati kwa kikamilifu na kujazia pengo litakalobaki kwa kuagiza mafuta kutoka nje.

Mwisho, mipango ya kuchimba chuma cha Liganga iharakishwe ili Taifa lifaidike na bei nzuri za chuma zilizoko duniani hivi sasa na wakati huo huo, kukidhi mahitaji ya chuma ya ndani.

Mheshimiwa Spika, naiunga hoja mkono.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Naibu Waziri, Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa kazi nzuri wanazofanya za Wizara hii, nawaweka mikononi mwa Mungu awape afya njema.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, ni kweli kabisa Ilani ya Uchaguzi ya CCM imetekelezwa kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wamefurahishwa kabisa katika hotuba hii kuhusu kuangaliwa upya mikataba ya madini. Mimi binafsi nakiri kuwa wawekezaji wamewekeza mitambo yao mingi Tanzania, lakini hata wao wamepata Almasi, Dhahabu

na *Tanzanite* nyingi hivyo hakuna yeyote atakayemnyoshea mwenzake kuwa yeye anapata hasara.

Mheshimiwa Spika, sasa inatosha wao kurudisha gharama zao, sasa walipe kodi zote wanazostahili kulipa, misamaha ifutwe yote.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana Waziri kwa kusimamia hatimaye migodi hii mikubwa wachangie sasa katika Halmashauri za Wilaya zote yalipo madini lakini Mheshimiwa Waziri sikusikia kama hata Halmashauri ya Wilaya ya Geita imo, nikumbushe vizuri kwa Geita waelezwe wapande na miti mingi ili walinde mazingira wasiache jangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba wachimba madini wadogo wadogo, Serikali iwawezeshe kwa kutoa nyenzo kama magalashi na mashine za bei nafuu kwa kutoa mikopo nafuu ambayo watamudu, nawaombea mkopo wanawake walioko Mgusu na Nyamgusu, Geita. Hali zao ni duni, wasaidiwe katika bajeti ya mwaka 2006/2007, ukiwatembelea hali zao ni mbaya nyenzo zao za kizamani haziendani na uboreshaji wa kuchimba madini kwa kulinda na afya zao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri asimamie bei ya mafuta, ametangaza bei ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa imepunguzwa lakini hawa watumiaji katika magari ya usafirishaji kama basi na teksi gharama bado ziko juu, wananchi wa hali ya chini wanashindwa kumudu hivi tume ya bei bado ipo? Mbona hawasaidii wananchi?

Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa kuwa Serikali ni moja yenye ari, nguvu na kasi mpya itusaidie wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Spika, leo naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie umeme Malya lini utapelekwa, nguzo zipo pale Ngudu zinanyeshewa mvua zinachakaa tu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri aagize zile nguzo zianze kuchimbia kama ni vikombe au sahani au *thermos* tunasubiri nguzo ziwe zimechimbiwa ili wakazi wa eneo la kata ya Lyome na Malya waone Serikali yao inawajali kuliko waone nguzo ziko chini zinanyeshewa mvua.

Mheshimiwa Spika, Malya ni kijiji kina Chuo cha Michezo cha Afrika naomba uone umuhimu huo sio kuwa nataka nimfagilie Mheshimiwa Richard Ndassa tu bali tunafuatilia ahadi tulizotoa katika uchaguzi mkuu mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, sina pingamizi na Bajeti hii apewe pesa zote atumie ili tutekeleze Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 -2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri imeniwezesha kutoa mchango wangu kwani Mheshimiwa Waziri ameiweka taarifa yake katika maeneo ya wazi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kutoa mchango wangu. Kwa kufahamu hili Wizara ni nuru ya kuifanya Tanzania yetu kupiga hatua ya maendeleo kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara hii ni nuru ya maendeleo ya Mtanzania ni wakati muafaka wa kuwahamasisha na kuwawezesha wananchi waweze kuzipata nishati ya uhakika na kwa bei nafuu. Pia pawepo na matumizi endelevu kwani kufanya hivyo ni kulipatia pato Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri nasikitika sana Wizara inakwenda kinyume na baadhi ya malengo yake. Wizara yetu hii mara nyingi inapoamka kufunga mikataba mara nyingi husahau wazawa. Wawekezaji pale panapokuwa na mkataba mara nyingi husahau wazawa na Watanzania ndio wanaoteseka na kuteswa sababu ni mkataba. Wachimba madini wadogo wadogo hupata kero kubwa. Watanzania bado wanateseka sana kupanda kwa vitu bei kiholela holela mara mafuta mara umeme.

Mheshimiwa Spika, tuiulize Serikali inayoongoza wananchi wa nchi hii miaka isiyopongua 43 ya utawala na leo nchi yetu ina asilimia 10 ya Watanzania wanaotumia nishati ya umeme. Hili linatokana na nini? Kwa mtazamo wangu kuna sababu zisizopungua mbili, kwanza Shirika la Umeme limeshindwa kuupeleka umeme nchi nzima na pili, ughali wa vifaa vya umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeiweka nchi katika njia panda. Ukweli wa mgao wa umeme nchi yetu haijaliweka, hii inatokana na lugha ya Wizara kwa wananchi wetu. Wizara inapozungumza Bwawa halina maji ya kutosha huku nchini kuna mvua za masika, hiki ni kitendawili na tungependa Wizara kitutegulie, vinginevyo wananchi wataleta dhana binafsi. Mwanadamu anahitaji kuishi kama raia huru katika nchi yake na sio kutawaliwa kiakili.

Mheshimiwa Spika, jambo la fedhaha katika Wizara hii ni kutangaza unafuu wa mafuta. Lugha hii ni juzi tu ambapo Serikali imeondoa kodi ya mafuta, Watanzania walipeleka kufurahia lakini la kushangaza hadi hii leo bei ya mafuta imepungua lakini imepungua kwa mfanyabiashara tu na sio kwa faida ya wananchi.

Watanzania sasa wameshajigomboa na wameshajitawala. Iko haja ya makusudi Watanzania wapewe nafasi katika nchi yao ili waitumie elimu yao walioipata ndani ya nchi yao. Hakuna sababu ya kujikomboa na halafu ukawa mtawaliwa hivyo Watanzania kila leo hatuna uwezo wa kufanya yetu mpaka tufanyiwe. Wakati umefika sasa kujua umuhimu wa elimu yetu ili tuweze kusimamia kila chetu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naitakia kila la kheri Wizara.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kwanza kumshukuru Waziri wa Madini, Naibu wake pamoja na wataalamu wao kwa

kuandaa bajeti nzuri kwa mwaka 2006/2007. Aidha, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuwa na mkakati wa kusambaza umeme vijijini kupitia programu ya *Rural Electrification* na *Rural Energy Fund* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba Wizara inieleze au iwaeleze wananchi wangu wa jimbo la Mbozi Mashariki ni lini hasa miradi ifuatayo itakamilika?

Mheshimiwa Spika, kwanza ni mradi wa Ruanda - Idiwili kupitia Iyula, pili ni Mahenje - Igunda hadi Shaji na tatu ni mradi wa Vwawa - Hasamba. Miradi hii ya umeme ilianza miaka mitatu iliyopita, miradi yote ilishachimbiwa nguzo na iligharimu takribani shilingi milioni 200 za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwape wananchi wa Mbozi maelezo ya kutosha yatakayowaridhisha kuhusu kutokamilika kwa miradi hiyo. Lakini cha muhimu zaidi tunataka tuelezwe ni lini sasa wananchi wa maeneo hayo watapatiwa umeme. Kuna sababu gani za msingi kuanzisha mradi ukakugharimu pesa nyingi kiasi hicho halafu ukauacha njiani?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwaeleze wananchi wa Jimbo la Mbozi Mashariki hasa kata za Isansa, Itaka, Halungu, Nyimbili, Msia na Nambinzo ambao ni wakulima wazuri sana wa kahawa na mazao mengine kama mahindi na ambao wana hamu kubwa sana ya kupata na kutumia umeme, ni lini hasa watapata umeme? Naomba niiarifu Wizara kwamba wananchi hao walishajiorodhesha na kupeleka maombi yao *TANESCO* lakini hakuna maelezo yoyote ambayo wamepewa. Ni vizuri Wizara ilione hilo iwasaidie wananchi hao ambao wapo tayari kutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara iwaeleze wananchi wa Mbozi kwamba wao wanafaidika na mimi kwa madini yanayochimbwa Mbozi kama yalivyoorodheshwa kwenye kitabu cha Taarifa ya Jumla Kuhusu Sekta za Nishati na Madini katika ukurasa wa 34. Naomba pia nikiri kwamba mimi kama Mbunge sijui hadi sasa faida ambazo tunapata kama Wilaya kutokana na madini hayo. Ni vizuri pia Waziri atakapokuwa anahitimisha bajeti yake basi atueleze wana Mbozi kwa kina sana jinsi ambavyo tumefaidika na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda na mimi niseme kwamba bado bei ya mafuta ya aina zote hasa petroli, dizeli na mafuta ya taa iko juu sana. Wananchi hawaoni kama kuna badiliko lolote kwenye nishati hiyo. Kwa mfano bei ya petroli imepunga kwa wastani wa shilingi 50 hadi 100, dizeli kwa kati ya shilingi 40 hadi 80 na mafuta ya taa yamepungua kwa wastani wa shilingi 100.

Mheshimiwa Spika, punguzo hili ni kama utani tu, inaonyesha kama vile Serikali hii ya awamu ya nne iliyodhamiria kuwakomboa wananchi wake! Tunaomba Serikali kupitia Wizara hii itoe kauli juu ya suala la mafuta, Serikali iseme na wananchi wajue ni kiasi gani hasa kilichopunguzwa, ni kiasi gani mwananchi wa kijijini atatumia kununua mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, nazidi kupongeza tena kwa kazi nzuri unayoifanya ni nzuri. Nimeshtushwa na tatizo la kutokuwa na kamishna wa madini, wananchi wanalalamika kuwa leseni ndogo zote za uchimbaji madini zimesimama zikisubiri kupatikana kwa kamishna. Hii ni pamoja na leseni za ununuzi wa madini na *transfer* ya *share* tatizo hili Serikali inalionaje nani atatoa vibari vya leseni hivyo. Hali hiyo ni kukwaza wananchi.

Mheshimiwa Spika, tafadhali Waziri mshauri mhusika ateue kamishna, huenda hajui kuwa ni tatizo, idara hii ni kubwa inahitaji kamishna aliyeteuliwa kisheria.

Tunaomba maelezo kuna tatizo gani wananchi wanasubiri maombi yao yaangaliwe na kupitishwa. Nasisitiza tena mshaurini Rais ateue Kamishna kama ndiye mhusika, nina imani watumishi wenye uwezo wapo.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri ya Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, maoni ya Kamati husika na maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu mwanzoni nchi yetu ilipatwa na tatizo la umeme *(Energy)* mgao wa umeme kutokana na upungufu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, suluhu ya umeme katika nchi yetu ni Mlima wa Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Ni muda mrefu sana Serikali katika Ilani yake imekuwa ikiahidi jambo hili lakini halitekelezwi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhoji utekelezaji wa mradi wa Liganga na Mchuchuma, Serikali inasemaje. Zipo faida nyingi za mradi huu wa Mchuchuma katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhoji, je, ni kwa nini katika bajeti ya mwaka 2006/2007 Mchuchuma na Liganga haipo. Baada ya majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya Mchuchuma nitakuwa tayari kwa niaba ya wapiga kura wangu wa mkoa wa Iringa kuunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri na nzito wanayoifanya. Napenda kuwasilisha kwenu maombi ya muda mrefu ya umeme Wilayani Kongwa na naomba sana kwa ombi hili nijibiwe angalau kimaandishi.

Mheshimiwa Spika, ombi la Umeme la *Narco Kongwa* - Hogoro - Matongoro - Mkoka (kilometa 35) mradi huu tumeahidiwa miaka mingi sana Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, alishatembelea na kuahidi, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwenye kampeni kaahidi, je, mipango ikoje?

Mheshimiwa Spika, ombi la Umeme Pandambili – Hemba hemba (kilometa 5 tu) na ombi la Umeme Mlali - Chamkoroma - Tubuge/Msata (kilometa 30).

Mheshimiwa Spika, suala la mikataba ya madini kupitiwa upya, tuelezwe kinaga ubaga hatua zilizofikiwa hadi sasa. Uganda wamegundua mafuta na wametangaza, sisi hapa kuna juhudi gani za kugundua mafuta? *Situation* ikoje ya ugunduzi wa mafuta? Siri siri za nini? Si tuambiane endapo kuna *prospects* zozote?

Mheshimiwa Spika, hatma ya *Net Group Solution* ni nini na kuna maandalizi gani ya menejimenti mpya baada ya hao *Net Group Solution* kuondoka?

Mheshimiwa Spika, *VAT* kwenye mafuta imeondolewa, bei ya mafuta haijapungua, kwa nini, je, mafuta yatapungua bei lini na kwa nini hasa hayajapungua bei? Naunga mkono hoja

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipata nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Waziri na Wizara hii pamoja na Naibu wake kwanza kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha hapa Bungeni.

Madini yanayochimbwa Tanzania yanafaidisha na kunufaisha makampuni ya uchimbaji wa madini (wawekezaji) kwani asilimia kubwa ya pato la rasilimali hii inakwenda kwenye nchi zao. Watanzania tumekuwa watazamaji tu tukishuhudia mali hizo zikihamishwa na sisi tumeendelea kuomba misaada kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, mikataba yote ya madini ni ya kitapeli na wenzetu wawekezaji wametuzidi kete sana, mikataba haikuwa wazi ina usiri mkubwa hata Mawaziri wa Wizara husika hawaelewi vizuri nini kiko ndani ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili madini yetu yaweze kusaidia uchumi wetu ni dhahiri kuna ulazima kwa mikataba hii yote kuangaliwa upya wawakilishi wa wananchi, Wabunge wa sehemu husika washirikishwe kuona mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi sehemu zenye machimbo ya madini ni maskini wa mwisho, hawana barabara, maji, umeme na huduma nyingine muhimu. Kuna sababu gani ya wao kushuhudia rasilimali zao zikivunwa kwa kasi na wao kubaki na mashimo makubwa na kuharibiwa mazingira yao wakati hawafaidiki chochote na madini hayo?

Naomba Waziri aeleze Bunge hili ni hatua gani za kihistoria zimechukuliwa kwa wawekezaji ambao walihusika makubaliano ya mikataba yao ya kutoa fedha kwa jamii inayozunguka machimbo hayo kwa muda wa miaka sita na baada ya kufuatiliwa sana wametoa shilingi milioni 200 hivi karibuni kama kifuta jasho kwa jamii mojawapo?

Pili, tunataka Waziri aeleze Bunge hili nini kuhusiana na kampeni hiyo na ninyi ambao kwa miaka mitano hawakutoa chochote kwa jamii hizo?

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kwamba haina wataalam wa kutosha na vifaa vya kuchimbia madinai yaliyoko ardhini, tangu tuanze kuchimba madini hayo kwa kutumia wawekezaji mpaka leo kuna utaratibu gani umeandaliwa uwezesha Taifa ili kuendesha shughuli hizi sisi wenyewe?

Mheshimiwa Spika, kuna wataalam wangapi wamepelekwa shule kupata utaalam wa kuweza kusimamia uendeshaji wa shughuli za madini hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda chombo gani cha kuweza kufuatilia *to monitor* wawekezaji mbalimbali kwenye ardhi ya Watanzania kuhakikisha kwamba wanafanya yale waliokubaliwa tu na sio vinginevyo?

Mheshimiwa Spika, wazungu wanatuzidi sana kwa uelewa na wanatumia udhaifu wetu kuchimba madini kwa siri kwenye maeneo ya wanayofanyia kazi zao nyingine bila sisi kutambua hilo. Ni muda muafaka kwa Serikali kufuatilia kwa karibu wawekezaji hawa kwenye sekta mbalimbali ili kunusuru rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, swala lingine ni kukosekana kwa umeme maeneo mengi hapa nchini ambazo ni *center* za biashara na hivyo kudumaza uchumi wa nchi kwa wafanyabiashara kukosa huduma ya umeme ili wazalishe kwa wingi na kwa gharama nafuu na kusaidia kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna urasimu mkubwa sana pale mwananchi anapoomba kupatiwa huduma ya umeme, *TANESCO* inaweza kuchukua muda wa mwaka mmoja hadi miwili kupatiwa huduma hii na hapo ni mpaka umtafute mtu yeyote anayehusika umweke sawa ndipo uwe na uhakika wa kupatiwa huduma hii. Mtu asiyekuwa na uwezo wa kutoa chochote hana uhakika wa kupata umeme wa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, rushwa *TANESCO* imekithiri Serikali iangalie kwa makini kwani kila mwananchi ana haki ya kupata huduma hii pale anapohitaji.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la watumishi wa *TANESCO* wanaopita kusoma mita wanaongeza *watt* zilizotumiwa kwa mwezi na hivyo wateja kuletewa bili kubwa tofauti na matumizi yake. Hili linaleta usumbufu kwa wateja/watumiaji ni kulazimika kwenye kwenye ofisi husika kulalamika ndipo apunguziwe baada ya kuangalia matumizi yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ifanye juhudi za awali kupeleka huduma ya umeme katika Wilaya ya Urambo, Kata ya Usinge na Tarafa ya Ulyankulu ambapo kuna uzalishaji mkubwa sana wa Tumbaku, Karanga na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii na nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara na wa mashirika yaliyo chini yake kwa hotuba nzuri na kwa mchango wao katika maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kupitia shirika la *TANESCO* kwa kueneza umeme katika nchi hii licha ya matatizo mengi yanayolikabili shirika la *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, Bara la Afrika ni Bara linalokosa mwanga kuliko Mabara mengine duniani *(The darkest continent in the world).*

Mheshimiwa Spika, maombi yangu ni Wizara ishawishi wasambazaji wa umeme Njombe katika Tarafa ya Lupembe wapitishe umeme wa gridi eneo la Idamba (Lupembe) wanapopeleka Kifanya ng'ambo ya mto Ruhudzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ieneze umeme wa gridi katika vijiji vya Kata ya Igongolo ambavyo ni Igongolo, Itipingi, Tagamenda, Kichiwa, (Ibiki), Ibumila na Ikando. Umeme wa gridi unapita juu ya kijiji cha Ikando kuelekea Lupembe. Vijiji hivi vina watu wengi na vimeshikana kama mnyororo. Tafadhali sana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* kupitia programu ya *ERT* (Ukurasa 12, Ibara 26) ieneze umeme katika vijiji vya Tarafa za Makambako na Lupembe na hasa katika vijiji vyenye miti mingi ya mbao *(pines)* na shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Mhaji na Igima vipatiwe umeme kwa vile nguzo zilipelekwa miaka nane iliyopita. Umeme unapita katika vijiji hivi na kuelekea mbele. Wizara (Serikali) ifute madeni ya zamani katika *TANESCO* na kuliwezesha lisimame katika miguu yake.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wa Wizara ya Nishati na Madini, nawapongeza kwa umahiri na umakini wao katika kuendesha Wizara na hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri akumbuke barua ya wananchi na wakulima wa Kilimanjaro kuunganishiwa umeme.

Naomba vile vile katika kuunganisha umeme katika maeneo mbalimbali, maeneo ya huduma za jamii muhimu kama shule, hospitali na vyuo vipewe umuhimu. Katika Wilaya ya Hanang maeneo mengi yameachwa nje na wakati umeme umepita karibu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya zetu zijue madini yapo maeneo gani ili waweze kushiriki ipasavyo. Ramani za madini zitawanywe ili wageni wasivamie maeneo wakati wananchi wa maeneo yale hawana taarifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati. Ahsante.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba sana niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara hii kwa hotuba nzuri sana. Nawapongeza sana.

Ushauri wangu ni kwamba hotuba hii ni nzuri sana, katika Jimbo la Korogwe Mjini ningependa kuwapongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa na ukweli usiopingika ni kwamba maeneo mengi katika nchi hii sasa yana umeme. Madini ya aina mbalimbali yanachimbwa tofauti na ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, umeme Korogwe Mjini upo, ahadi ya umeme ya muda mrefu ya kupatiwa umeme eneo la Mtaa au Kijiji cha Kwamata umeme upo tayari Kwamdolwa, hadi leo hii umeme haujafikishwa Kwameta tayari wananchi hao zaidi ya 50 wameshafanya *wiring* lakini hadi leo ni ahadi tu ya kuweka umeme.

Mheshimiwa Spika, ombi ni kwamba naomba nipatiwe umeme Kwameta. Kuhusu umeme kwenye shule za Sekondari Korogwe ninaomba sana kupatiwa umeme katika sekondari zifuatazo, *Old Korogwe Secondary School, Chief Kimweri Secondary School, Kilole Secondary School, Hale Secondary School* na kadhalika.

Sasa hivi tumekwenda kwenye elimu ya sayansi na teknolojia hasa kwa matumizi ya kompyuta, shule hizo zote zipo karibu sana na umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme kuzalishwa toka Mkonge yapo maneno ya kinadharia kwamba Katani itazalisha umeme. Kwa kuwa mkoa wa Tanga mashamba yapo mengi ya Mkonge, je, Wizara haioni mashamba hayo sasa yangeanza kuzalisha umeme badala ya kuzungumza maneno tu?

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu ni lini mradi huo utaanza, aidham niambiwe sasa kijiji cha Kwameta watapatiwa umeme?

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wizara hii na taasisi zake zote chini ya uongozi mahiri wa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wake.

Mheshimiwa Spika, napongeza na kushukuru kwa kuanza kwa ujenzi wa gridi ya msongo wa *KV 132* kutoka Makambako hadi Songea ambazo zitaanza katika kipindi cha mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika kipindi hiki cha kusubiri mradi huo wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanaomba kuzima na kukatika kwa umeme kama ilivyo hivi sasa ambapo hata siku tatu Mji wa Songea umekosa umeme.

Swali, tatizo ni nini iwapo Songea imepata umeme wa *generator?* Hali hii inasumbua sana manung'uniko makubwa. Miradi yao midogo midogo kupambana na

umaskini inakwama. Zaidi ya hao kunakuwa na matukio mengi ya mauaji katika kipindi ambapo umeme umekuwa ukikatwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu au wananchi wa Ruvuma waelezwe ya kuwa tatizo hilo halitajitokeza tena.

Mheshimiwa Spika, mwisho naitakia kila la kheri Wizara hii ili iweze kutekeleza vema mikakati yote iliyopangwa kwa mwaka 2006/2007.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Lawrence Masha kwa kuwajali wananchi wa Tanzania. Kwa namna ya pekee nawashukuru zaidi kwa kusikiliza kilio cha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, kwa bajeti hii hasa wale wa Mbinga kwa kuwaondolea kero ya ukosefu wa umeme. Bajeti ya shilingi bilioni mbili na nusu wameisikia, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kwa niaba ya wananchi wa Ruvuma nichukue nafasi hii kuishukuru Bodi ya *TANESCO,* Menejimenti ya *TANESCO* pamoja na wahandisi na wafanyakazi wote walioshiriki katika kufanya tathmini ya miradi ya umeme Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni faraja kubwa kwa wananchi wa Mbinga ambao wamekaa gizani kwa takribani umri wangu, karibia miaka 43 sasa tangu kuanzishwa kwa Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, niko safarini, lakini kwa jinsi wananchi wa Ruvuma wanavyoguswa na bajeti ya Wizara hii imebidi niichangie japo kwa maandishi, *Information (IT),* imeniwezesha kuchangia kwa maandishi *(E-mail)* na ndiyo maana tunaomba ofisi yako ituongezee ufahamu wa taaluma hii.

Mheshimiwa Spika, natambua wazi kuwa bajeti hii imetengwa kwa upendo mkubwa kwa wananchi wa Tanzania, hasa ikizingatiwa kuwa hali ya kipesa ya nchi yetu ni mbaya kutokana na njaa iliyotukabili pamoja na ukame uliokithiri katika vyanzo vyetu vya maji na kusababisha upungufu wa uzalishaji wa umeme katika mabwawa yetu ya Kihansi, Mtera na Kidatu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yetu kwa kutenga kiasi cha pesa ya tahadhari kwa ajili ya kununua umeme wa *Songas,* *IPTL* na Kiwira pamoja na kuongeza uzalishaji kwenye mitambo yetu ya dizeli.

Mheshimiwa Spika, asiyetambua umuhimu huo ni yule tu asiyependa kukiri ukweli wa madhara ya ukosefu wa umeme katika uchumi wa Taifa letu. Ukosefu wa umeme una madhara, mtakumbuka katika hospitali operesheni zitasimama, uzalishaji

wowote utasimama na wanaotegemea bidhaa hizo nao watasimama, mawasiliano ni tatizo na kadhalika.

Pia napenda kuwatahadharisha wale wanaodai kuwa *TANESCO* inauza umeme bei mbaya kulingana na  na nchi nyingine, watambue kuwa *TANESCO* haifuati kanuni ya *business is separate entity* kwa tajiri yake ambayo ni Serikali, inapeleka miradi hata pale ambapo hapana *profit* kwa wakati huo ili mradi kwa manufaa ya wananchi. Serikal inaangalia faida ya muda mrefu na madhara mtambuka. Tunawatia moyo ili muweze kuwakikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bajeti ya umeme iliyotengwa kwa ajili ya Mbinga ni ndogo ikilinganishwa na hali halisi ya matumizi yanayohitajika japokuwa ni vema kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mbinga umejengeka zaidi na una mzigo mkubwa nje ya kitovu cha Mbinga. Ili kuweza kukidhi wateja wa Mbinga kutahitajika angalau kiasi cha kilometa 20 za *11kV* au *33 kV* Mbinga Mjini ili kusambaza umeme na kuifanya *generator* kuwa katika mzigo wake *(full load).* Pia iko haja ya kuanza *extension* ya maeneo ya Litembo na Maguu kiasi cha wastani wa kilometa 10 za maeneo ya usambazaji ambako kuna matajiri wengi wa Kahawa wenye nyumba bora zilizokaa kwa mpangilio kama walivyojionea wahandisi wa umeme wa *TANESCO* wakati walipotembelea.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbinga wana uwezo wa kulipa *per capital income* yao inakadiriwa kuwa ni shilingi 167,000/= kwa mtu.

Mheshimiwa Spika, nazungumza katika furaha kuwa sasa Serikali imewageukia wananchi wa Mbinga, lakini basi tufanye kweli ili nao waote majibu katika kuongeza tija na uzalishaji kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kwa upande wa gridi ya Taifa. Tunashukuru kwa juhudi zilizofanyika mpaka sasa, lakini mwaka 2010 sio mbali, Ilani ya Chama cha Mapinduzi isisutwe,  kwa kuwa wawekezaji wanakataa kuwekeza Ruvuma kwa sababu ya ukosefu wa umeme. Tunazo raslimali nyingi zinaohitajika kusindikwa kama vile matunda, samaki, dagaa na madini. Bila umeme itakuwa ni ndoto kufikia malengo ya milenia *(MDG).*

Mheshimiwa Spika, sambamba na utafutaji wa wafadhili kwa ajili ya umeme wa gridi, kwa kuwa inasemekana kuwa tuna wafadhili ambao wapo tayari kwa ajili ya *33 kV line* toka Songea hadi Makambako, kwa nini wasitujengee kabisa hiyo *line* ya kutoka Songea hadi Namtumbo, kwa sasa tukaweka *step up transformer,* angalau waweze kupewa umeme toka Songea japo kwa mgao, angalau mara tatu kwa wiki kutegemeana na *peak* za *load* ya Songea kwa ajili ya shughuli maalum kwa kuanzia? Mimi nadhani inawezekana, kwani tumejifunza kutokana na mgao wa umeme unaondelea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua hayo naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuwekeza kwenye mitambo midogo au kutoa *support* kwa wazalishaji wa

umeme wadogo *(Mini hydro).* Kwa mfano pale Mbinga yupo Bwana Andoya ambaye ameanzisha mradi wake mdogo wa umeme kiasi cha *megawatt* moja *(1MW).* Umeme ule utasaidia katika kuwawezesha wananchi na pia kuunga mkono hujudi za wananchi wa Tanzania katika teknolojia ya umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naomba sasa nitamke kuwa naunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii inayoniwezesha kuchangia katika hotuba hii.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kuandaa hotuba hii. Naunga mkono hoja hii ili kuiwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake na mipango yake kama Waziri alivyojielekeza katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niitumie fursa hii kuchangia katika maeneo kadhaa yanayohusiana na hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, umeme kama nishati ni muhimu sana kwa maendeleo kama ilivyo muhimu kwa wananchi wote, umeme ni muhimu kwa maendeleo ya watu wa Kwimba, tena naomba nifahamishwe juu ya maendeleo ya kupeleka umeme katika Kijiji cha Hungumalwa, Mwalujo, Sangu hadi kijiji cha Shilima mpakani mwa Kwimba na Shinyanga vijijini. Mara mbili nimepewa gharama ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mara ya kwanza mwaka 2002 niliarifiwa mradi huo ungegharimu shilingi za Kitanzania bilioni 1.32, mwaka 2004/2005 niliarifiwa gharama na ingakuwa shilingi za Kitanzania milioni 800 na ungekuwa wa awamu mbili zenye mgawanyo wa takriban shilingi za Kitanzania milioni 400 kwa kila awamu.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hotuba yake atoe taarifa kama Wizara katika mipango yake ni kweli mradi huu umo/upo, upembuzi uliofikia kwenye gharama hizo ulifanywa lini? Unatarajiwa kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Spika, nimefarijika na taarifa kuwa fedha za kuanzisha mfuko wa nishati vijijini zimetengwa kwenye bajeti hii na kuwa utekelezaji wa majukumu wa mfuko huo utaanza mara baada ya mtendaji mkuu na wakala na wasaidizi wake kuajiriwa. Je, mradi huu utegemewe kutekelezwa na mfuko huu?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona mpango wa kuyapatia umeme wa gridi maeneo hayo niliyoyataja maeneo yanayohusika yana gineri mbili, vijiji *(Centres)* vikubwa kama saba hivi, kituo cha afya kimoja, zahanati saba, shule za sekondari nane unasuasua, niliomba kupatiwa *generator* kwa kijiji cha Hungumalwa. Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini hivi sasa ndiye Waziri wa Nishati na Madini, alitushauri kuwa na subira na gharama ya *generator* ingekuwa juu mno kwa wananchi hivyo

nawashauri wananchi kuwa na subira. Naomba kufahamu kama umeme wa gridi bado ni mgumu kupatikana je, leo anasemaje? Wananchi wanaendelea kuwa na subira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *biogas* kama nishati mbadala, naomba nitumie fursa hii kwanza kabisa kuishukuru *UNDP* kwa kuifadhili Wilaya ya Kwimba mradi wa *biogas,* ilikuwa mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, tunasikitisha kuwa ni kwa bahati mbaya sana mradi huo haukuendelea. Kulikuwa na upungufu wa kiufundi katika mradi huo, matanki ya kuhifadhia/kukusanyia gesi yalikuwa yakidumu miaka miwili na nusu tu na kweli baada ya muda huo yaliza kupasuka pasuka ikawa mwisho wa mradi.

Mheshimiwa Spika, ombi, tafadhali naomba kama Wizara iko makini katika Ibara ya 37 ya hotuba yake itutumia wataalam wa kuja kufuatilia mradi huo uliokuwa wa *units 100* kwa nia ya kuangalia uwezekano wa kuufufua mradi huo. Wananchi wa Kwimba wanafahamu umuhimu na uzuri wa *biogas,* wanachohitaji ni kusaidiwa kuufufua mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, naomba nihitimishe mchango wangu kwa kuomba melekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ili anifahamishe nafasi ya Halmashauri za Wilaya na wananchi wake katika mchakato wa utafiti kwenda kufanya utafiti katika eneo fulani Halmashauri ya Wilaya ina nafasi gani. Namaliza hivyo kuwa ipo mifano Kwimba inayoashiria kuwa Halmashauri ya Wilaya na wanawake hawana nafasi katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano, *Free African Mining Ltd* walikuja Kwimba wakaenda katika Kata za Mantare, Bungulwa Ngula, wamefika huko wakafanya kazi zao kimya kimya, wakaondoka bila kutoa taarifa yoyote Wilayani wala kwa viongozi wengine wa maeneo hayo. Haijulikani kwa Halmashauri ya Wilaya wala kwa wananchi kama kulipatikana chochote na kuwa wameondoka ili kwenda kujiandaa kuja kuanza kazi ya uchimbaji kama waligundua kitu.

Kuna kampuni nyingine kwa jina la *Fred* ilifika Kwimba mwaka 2001. Ilikuwa imepata kibali mwaka 1999, walipofika Kwimba walienda katika Kata za Mwakilyambiti, Kikubiji na Igongwa. Wamefika huko wakafanya kazi zao, nao kama wa kwanza wakaondoka kimya kimya. Wilaya iko gizani na wananchi wake wana nafasi gani katika mchakato wa utafiti wa madini?

Mheshimiwa Spika, kampuni moja iliyopo katika Kata ya Shihalo, Wilayani Misungwi, pamoja na kufanya shughuli zake huko tunazo taarifa za kuaminika kuwa wanaingia Wilayani Kwimba katika Kata za Fukalo na Bupamwa yote yanafanyika bila ufahamu wa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba .

Mheshimiwa Spika, naomba nisaidiwe nini nafasi ya Halmashauri ya Wilaya na wananchi katika mchakato huo?Naumba mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa mbele ya Bunge. Hotuba ni fupi lakini imesheheni mambo mengi muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua mwekezaji anayefanya utafiti wa madini ya *Nickel* katika eneo la Kabanga (Ngara) ni muda mrefu yuko katika eneo hilo, kagundua nini? Kama bado ni lini tutaona matokeo? Wananchi wa Ngara tunayo hamu sana kujua kinachoendelea. Je, Serikali imejihakikishiaje kama huyu mwekezaji siyo mjanja? Ningeomba utoe maelezo kuhusu kinachoendelea. Naomba kujua ni lini mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya Rusumo kwa kushirikiana na nchi jirani utaanza? Mradi huu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri binafsi na Naibu wake, Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa umahiri wenu na ufasaha sio tu katika utendaji lakini pia uandaaji wa hotuba yao.

Pili, kuhusu bwala la Mtera, sina hakika kama Wizara inaliona tatizo halisi. Tatizo la bwawa hili ni *siltage and sedimentation* tangu lilipotengenezwa hakukuwa na *dredging system* na matokeo yake ni kwamba ujazo *(volume)* wa maji umepungua. Hata mvua ikinyesha mwaka mzima mfululizo bado halitajaa. Suala linalojitokeza ni je, Serikali ina mpango gani kusafisha bwawa hilo? Vinginevyo bwawa hili litakufa na sipendi kuwaza matokeo yake.

Mheshimiwa Spika, tatu, jimbo la Kalenga linaelekea kuwa na dhahabu sehemu mbalimbali na kwa kweli uchimbaji unaendelea japo kwa kiwango hafifu kwa sababu yake ni kwamba hatuna mwelekeo wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itumie wataalam Wilaya ya Iringa wachunguze na kutusaidia ili uchimbaji wetu uwe wa manufaa kwetu na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusiana na usambazaji wa umeme vijijini, naomba Wizara ifikirie kupeleka umeme angalau katika vijiji vikubwa vya Kiponzelo, Kata ya Maboga, Igula, Kata ya Magulilwa na Kiwere, Kata ya Kalenga, naomba vijiji hivi viingizwe katika ratiba yako angalau kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji katika Wizara ya Nishati na Madini kwa maandalizi mazuri ya hotuba na hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango ili kuboresha utendaji mzuri wa Wizara hii. Moja, vyanzo vya umeme katika nchi yetu viko Kaskazini ya nchi tu kwa muda mrefu sasa. Sehemu nyingine nyingine zina hazina kama hiyo lakini inakuwa tabu sana kuviendeleza. Naomba sasa tuangalie sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Wizara kwangu ya tarehe 23 Machi, 2006 Wizara ilisema itaendeleza Mradi wa Nakatuta. Katika ukurasa wa 11 wa Taarifa ya Wizara, mradi huu haupo. Ni nini kinaendelea juu ya mradi huo?

Pili, katika taarifa ya Wizara pameorodheshwa vijiji vilivyopatiwa umeme mpaka 2006. Ukiangalia vijiji hivi vingi ni juu ya Reli ya Kati ukiondoa tu Iringa, kijiji kimoja, Lindi kijiji kimoja, Mbeya vijiji viwili na Mtwara kijiji kimoja. Inaelekea mipango yetu si mizuri. Wakati Wilaya za kale kama Mbinga yenye uzalishaji wa kutosha haina umeme mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mkoa wa Ruvuma uingizwe kwenye *ERP*. Utaona Lindi ipo na Mtwara ipo, lakini Ruvuma jirani ya mikoa hiyo imerukwa. Kiutendaji ni vyema yote ikawa katika programu moja.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwapongeze wafuatao, vijana wa Kata ya Mikaranga wanaosaga nafaka kwa kutumia mitambo inayotumia nguvu ya maji. Pamoja nao ni *Caritas* - Mbinga, Ndugu Mbunda (Andoya) anayejitahidi kutengeneza mradi utakaozalisha umeme wa *Megawatt 1.2* katika Mto Mtandazi. Naomba Serikali imsaidie na pongezi nyingi sana kwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Naibu Waziri Mheshimiwa Lawrence K. Masha, kwa ushirikiano mzuri sana wa kuhakikisha umeme unapatikana Makao Makuu ya Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni lile lile la kuhakikisha kwamba Kata za jirani kama Ramira, Matai, Kigonzera, Myangayagi, Litumbo, Mbuji, Maguni, Utiri, Kilimani, Mabanagamao, Mpaji na Nyoni. Nawapongeza pia *TANESCO* kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, naomba Wizara ishughulikie maombi ya leseni kwa wachimbaji wadogo wadogo wa maeneo ya Masugwi, Ngembambili, Kitai na Makoro. Lakini, pia naomba maeneo hayo yatengwe *(exclusively)* kwa wachimbaji wadogo wadogo tu. Jambo hili limechukua muda mrefu, naomba sasa liishe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashukuru sana kwa ushirikiano wa Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Naibu Waziri, Mheshimiwa Lawrence K. Masha. Natarajia safari ya Naibu Waziri itakuwa ni pamoja na kuweka jiwe la msingi katika Kiwanja cha *TANESCO,* Mbinga.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Naibu wake pamoja na watalaam wa Wizara kwa kazi nzuri na muhimu wanayofanya ya kuendeleza nishati na madini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itekeleze ahadi yake ya kusambaza umeme katika Jimbo la Nkenge kupitia mradi unaofadhiliwa na *SIDA*. Maeneo ambayo yanasubiri utekelezaji wa mradi huo ni pamoja na Gera - Ishozi - Ishunju, Bunazi hadi Mutukula, Minziro, Kitobo hadi Ruzinga na Kyaka hadi Kilimilile.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mutukula ni muhimu sana kupatiwa umeme kwa sababu ni mlango wa kuingia Tanzania unapotokea Uganda na ni mlango wa Tanzania kuingia Afrika Mashariki. Aidha, ikumbukwe wazi mradi mkubwa wa kutoa umeme Uganda kuja Tanzania una kipengele kinachoeleza umuhimu wa kutoa kipaumbele kusambaza umeme maeneo yote ambayo njia kuu ya umeme kutoka Uganda kuja Tanzania inapita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme kutoka Uganda unapita Mutukula lakini hadi sasa wakazi wa Mutukula mpakani mwa Tanzania na Uganda hawajapata umeme. Umeme ukifika Mutukula utasaidia sana kuongeza kasi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba *TANESCO* wasaidie kukipatia umeme Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera. Chuo hicho ni muhimu sana katika harakati za kupambana na umaskini vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kwa asilimia mia moja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHALULA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia kwa kuzungumza, naomba niseme yafuatayo, wapo wachimbaji wadogo waliokwisha sajili Chama cha Ushirika kwa jina la Wachimba Madini Katente walioko Ushirombo Bukombe.

Mheshimiwa Spika, chama hiki kinadai kupatiwa *PML* ya viwanja vinne ambavyo muda mrefu wanazungushwa na Ofisi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tayari *documents* zote nimezikabidhi kwa Katibu wa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Naomba chama hiki kipatiwe *PML* zao.

Mheshimiwa Spika, kama kuna sababu za kufanya wasipatiwe *PML*, naomba nipatiwe taarifa za kukwama na jinsi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, chama hiki tayari kimeshawasilisha maombi ya mkopo kati ya shilingi 60,000,000/= na shilingi 100,000,000/= ili tuboreshe maeneo yao ya kufanyia kazi hata kuwezesha wachimbaji waliovamia kwenye misitu warejee kwa uhuru na amani.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie majina na wamiliki wa leseni 145 zilizopo Bukombe kama nilivyojibiwa kwenye swali langu katika kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, wanaofanya utafiti katika Hifadhi ya Kigosi/ Myowosi muwe nao kwa karibu sana kwani niliwahi kuwatembelea tukiwa na Mheshimiwa *DC* Paul Chiwile, Ndugu Chales Nzella, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Ndugu Bulali, Kaimu Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Ndugu Sahari, *OSC* wa Ushirombo, walituambia dhahabu imo nyingi. Kwa nini Serikali isifungue mgodi eneo hili? Ni nini kinakwamisha? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifanye utaratibu, ofisi ya madini ifunguliwe Wilayani Bukombe kwani kila kitu kipo. Nini kinazuia?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba katika kitabu cha taarifa ya jumla kuhusu sekta ya nishati na madini ukurasa wa 38, sehemu madini yanakopatikana nchini, vijiji vifuatavyo vitambulike ni vya Bukombe wala si vya Kahama ambavyo ni Nhungwiza, Ushirombo (Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe) na Kanegele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini aliyoitoa leo hapa Bungeni Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha kwa ufasaha na umahiri mkubwa. Sikutegemea vinginevyo toka kwake, kwani namfahamu siku nyingi tukiwa wote Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo tulikuwa Wahadhiri. Baada ya hapo tulifanya kazi Serikalini katika Serikali ya Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Amesaidia kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha na ufundi kama unavyotegemea toka kwa Mwanasheria maarufu.

Mheshimiwa Spika, kabla siajaendelea na kwa ajili ya rekodi, naunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utakuwa mfupi na unajikita zaidi kwenye suala la umeme katika Jimbo la Rungwe Mashariki. Utakuiwa mfupi kwa sababu haupishani na ule niliotoa kwenye Mkutano wa Ishirini, Kikao cha Ishirini na Tano kama ulivyoandikwa kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard)* ya tarehe 12 Julai, 2005.

Mheshimiwa Spika, niruhusu ninukuu taarifa hiyo iliyo katika ukurasa wa 121 wa taarifa hiyo rasmi. Nanukuu: " Hata hivyo, kuna maeneo machache ambayo tayari yako katika mipango ya *TANESCO* lakini imechukua muda mrefu kuitekeleza. Dalili za utekelezaji zipo kwani katika maeneo nitakayo yataja nguzo zimesimikwa na katika maeneo mengine hata nyaya zimeletwa ama zimefungwa au zipo zipo tu. Hii imechukua zaidi ya miaka mitatu. Inaleta vishwawishi vya hujuma kama vile wizi wa nyaya. Maeneo haya ni Ntaba mpaka Ipinda, njia hii ni kiungo mbadala cha umeme kati ya Wilaya ya Rungwe na Kyela. Nguzo ziliwekwa miaka mitatu iliyopita na nusu ya urefu wa laini hiyo ya *KV33* imewekwa nyaya. Kila tunapouliza, mara nyaya hazitoshi,

zikipatikana, gari bovu. Gari likipatikana, fedha za kuwalipa mafundi hakuna, ili mradi maelezo mzunguko. Tunaomba *TANESCO* ikamilishe ujenzi wa laini hii.

Mheshimiwa Spika, Kandete - Luteba, tayari nguzo zipo na wananchi walihusika kutoa nguvu kazi katika kusimika nguzo hizo. Tunaomba *TANESCO* wakamilishe ujenzi wa mradi huu wa muda mrefu, Kandete - Mpombo (Mwakaleli - Mpombo) nguzo zilisimikwa miaka minne iliyopita, Isange - Mbigili, nguzo zilisimikwa miaka minne iliyopita. Hapa kuna mteja wa kudumu, *Mobitel* wana mnara Mbigili. *TANESCO* wangefanya haraka kupeleka umeme Mbigili ili kumpata mteja huyo mbali na wananchi na taasisi nyngine. Kandete - Matamba (Mwakaleli - Matamba) napo nguzo tayari zimesimikwa." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, imekuwa rahisi kwangu kutoa mchango kwa kunukuu *Hansard* ya Hoja ya Waziri wa Nishati na Madini mwaka 2005, kwa sababu mpaka sasa hakuna kilichofanyika! Nimerudia mchango huo kwa sababu kilichobadilika ni miaka. Badala ya nguzo kuwa zimewekwa (na nyaya sehemu nyingine) ni miaka mitatu iliyopita sasa ni miaka minne iliyopita. Pale mwaka jana niliposema miaka minne iliyopita, sasa ni miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, nguzo zimeanza kuanguka na nyaya zinaibwa. Haitoi picha nzuri ya Serikali na *TANESCO* mbele ya wananchi ambao walikubali maeneo yao yachukuliwe bila fidia.

Mheshimiwa Spika, bila shaka jibu la haraka litakuwa mfuko wa umeme vijijini, sawa. Lakini hii ni miradi ya siku nyingi na kwa kuwa umbali wa miradi hii midogo ni kilometa saba kwa mradi, inawezekana ikatekelezwa kwa gharama ambazo si kubwa.

Mheshimiwa Spika, naamini mchango wangu wa hoja kama hii mwakani *Inshallah* utakuwa tofauti.

Kwa kumalizia, nampongeza Bwana Arthur Mwakapugi, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Ni mzoefu wa siku nyingi katika Serikali, ni mchumi aliyebobea. Sekta ya Nishati na Madini ni msingi imara wa uchumi. Ninaamini atachangia kuifanya sekta hii iwe chachu ya maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki natoa mwaliko kwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri kutembelea Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na nakushukuru.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Ni jambo la kusikitisha kwamba kwa miaka 45 sasa baada ya Uhuru, lakini bado ni asilimia 10 tu ya wananchi wana umeme.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha pia kuona tunapata umeme wa mgao hata wakati wa masika. Je, kuna tatizo gani huko Mtera? Ni kwa nini Serikali inashindwa ku-*recycle* maji yanaachwa yanaelekea baharini?

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba umeme wa maji ndiyo rahisi kuliko vyanzo vingine kama gesi, makaa ya mawe, *Uranium* na mafuta.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi yoyote iliyobinafsisha Shirika la Taifa la Mafuta. Hii ni kwa sababu nyingi ikiwemo ya usalama na kudhibiti bei. Tanzania iliamua kuacha mafuta kuwa soko huria na hivyo tunashuhudia ongezeko kubwa la vituo vya mafuta. Tujiulize ni kwa nini vituo vingi hivi vinafunguliwa kama havina faida kubwa?

Mheshimiwa Spika, kuna kila sababu ya *TPDC* kuwa na mamlaka ya kuleta mafuta na ndiyo iyauzie makampuni mengine. Ni kwa sababu hii bei ya mafuta inayumba yumba kila leo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mkataba, inasikitisha kuona mikataba haishirikishi wananchi na hata Wabunge kuipitia na kuiridhia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za kuboresha maisha ya Mtanzania, wananchi wanasumbuliwa sana katika uwekwaji wa umeme. Mfano, inamchukua mtu zaidi ya mwaka kufungiwa LUKU.

Mheshimiwa Spika, suala la Mererani linatia mashaka na wasi wasi kwani Tanzania inaelekea imewathamini wakezaji wa nje zaidi ya wenyeji. Machimbo yamekuwa yakinyang'anywa toka kwa wazawa na kwenda kwa wazungu. Je, ni kwa nini Serikali inafanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, *Tanzanite* ni madini yanayopatikana Tanzania pekee, lakini cha ajabu yanauzwa kwa wingi Kenya na ilifikia wakati ikaonekana wazi kuwa madini haya yanapatikana Kenya.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Serikali na Wizara husika kuitangaza vyema *Tanzanite.*

Mheshimiwa Spika, ni jambo lililo wazi kwamba wananchi wameuwawa, wamedhalilishwa na Serikali imeshindwa kuwatetea.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wenyewe hawana sheria inayowabana ili waweze kuendeleza sehemu wanazochimba madini. Mfano huduma zimekuwa ni za hiari. Sasa kama ni hiari ina maana wanaweza wasifanye chochote. Ni matumaini yangu kuwa wawekezaji watapewa masharti ili waweze kutoa huduma za jamii kama vile shule, hospitali na soko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *Net Group Solution,* tumesikitishwa na taarifa ya hasara iliyopatikana ya shilingi bilioni 400 kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 400 ni fedha nyingi sana, zingesaidia sana katika maendeleo ya nchi. Pamoja na umaskini wetu, fedha hizo zingeboresha maisha yetu . Cha ajabu wafanyakazi wa *Net Group Solution* wamekuwa wakilipwa fedha nyingi na ndio maana tunapata hasara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba nimalizie kwa kusema kuwa umeme ni maendeleo na ndio sababu nchi zote zilizoendelea hazina umeme wa mgawo, hivyo hii ni changamoto kwetu tuwe na umeme kwani umeme ni muhimu mno kwa maendeleo ya nchi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo, kwa kuwa viwanda vingi ikiwemo kampuni ya *Cement* ya Wazo, Kampuni ya Bia Tanzania, Kampuni ya *Aluminium Africa* inayotengeneza mabati, vimeunganishwa kwenye mtandao wa gesi ya *Songas* na kwa kuwa kuna taarifa kuwa Kampuni ya *Cement* ya Wazo tangu ilipounganishwa na gesi hiyo hadi Juni, 2006 imeweza kuokoa shilingi bilioni 18 tofauti na kama wangetumia *Industrial Diesel*. Sasa je, Watanzania wananufaika vipi na gesi hiyo? Serikali ina mpango gani kuhakikisha manufaa ya gesi hiyo yanajitokeza katika kushuka kwa bei ya bidhaa kama bati, bia na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utafiti wa mafuta katika *Economic Zone* yetu hasa katika maeneo ya Pwani ya Zanzibar na Pemba na kwnye *Deep Sea* ulifanyika miaka ya 1960 na tangu wakati huo hakuna kazi inayoendelea, ni sababu gani za msingi zinazofanya uchimbaji wa mafuta hayo usiendelee wakati hata sasa mafuta hayo yanaelekea kububujika tu juu ya ardhi, jambo linaloashiria wingi wa mafuta? Je, ni chombo ganai hasa kitaifa kina jukumu la kushughulikia maendeleo ya mafuta? Je, kama ni *TPDC,* kama jina lake linavyosema, sheria yetu inasema nini na inawezesha kufanya kazi Zanzibar kwa kiasi gani? Iwapo kuna utata tunafanya nini kuondoa utata huo mara moja ili tusiendelee kuchelewa katika shughuli ya utafiti wa mafuta katika pande zote za Muungano?

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumepata Gesi ya Songosongo na tumeanza kuitumia. Pia tuna mpango wa muda mrefu wa wa kuisambaza gesi hiyo maeneo mengi kwa matumizi ya umeme viwandani moja kwa moja na hata kama nishati ya kuendeshea magari. Tuna taarifa kuwa gesi hiyo inaweza kutumika kwa miaka kati ya 25 na 50 tu, je, tuna mpango gani wa kutafuta gesi zaidi ili baada ya *investment* kubwa tuliyofanya hadi sasa tusirudi tena nyuma? Ningependa wakati wa majibu kupata maelezo ya kina kuhusu mpango wa muda mfupi, kati na mrefu wa kutafuta gesi zaidi. Tumetenga fedha kiasi gani kwa ajili uya utafiti kuanzia mwaka 2006/2007 na iko kwenye kasma gani?

Kama Taifa tunafanya nini kuimarisha chombo chetu cha *TPDC* katika kukiwezesha kusimamia, kuratibu na hata kuratibu shughuli za utafutaji mafuta katika nchi yetu? *TPDC* ina wataalam wangapi na wa sifa zipi na tunawawezesha vipi kulinda maslahi ya Taifa katika eneo hili nyeti sana kwa Taifa siyo kiuchumi tu bali hata kiusalama?

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kama ifuatavyo, machimbo ya madini ya bati yaliyoko Karagwe sehemu ya Kyerwa, mnamo miaka ya 1960 hadi 1970 eneo la Kyerwa lilikuwa likitoa madini ya bati maarufu kama *TIN*. Mradi huo ulisaidia na kuchangia sana pato la Taifa letu kwa kiasi kikubwa sana.

Vile vile mradi huo ulichangia kwa kiasi kikubwa kutoa ajira kwa wananchi wa Tanzania hususan wananchi wanaopakana na machimbo hayo yaani wananchi wa Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu ni kwa nini mradi huo ulifungwa na Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha machimbo hayo yanafufuliwa na ni lini machimbo hayo yataanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, kwa ufahamu wangu mdogo ni kwamba Wilaya ya Karagwe inayo madini mbali mbali ambayo bado hayajachimbwa. Kwa kuwa mimi si mataalam wa madini, ningeomba sana Serikali kwa faida ya wananchi wa Karagwe na Taifa kwa ujumla, inifahamishe ni madini yapi yanapatikana Wilayani Karagwe na yapo sehemu zipi na kama yapo, naomba Serikali itujulishe ni lini yataanza kuchimbwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei kubwa ya *petrol* na kutokana na kupanda kwa bei ya *petrol* nchini, kumesababisha nauli za magari kupanda pamoja na gharama za usafirishaji. Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe ni Wilaya ya mpakani na pembezoni hivyo kufanya bei ya *petrol* kupanda zaidi kuliko sehemu nyingine nchini, hali ambayo imechangia kudidimiza uchumi wa wananchi wa Karagwe, je, Serikali ina mkakati gani wa kuipa upendeleo Wilaya ya Karagwe katika kupunguza beiza mafuta ya *petrol* na *diesel?*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ya Kilombero ndiyo yenye migodi miwili ya kufua umeme kwa kutumia maji yaani mgodi wa Kidatu na Kihansi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ina tarafa tano za Kidatu, Mang'ula, Ifakara, Mngeta na Mlimba. Kati ya tarafa hizo nne zina umeme. Tarafa ya Mngeta pekee haina umeme. Pamoja na kwamba niliuza swali kuhusu tarafa hii ya Mngeta na kupewa majibu mazuri na Naibu Waziri, nilipenda nitoe mapendekezo yafuatayo kwa unyenyevu mkubwa kwenye Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tarafa ya Mngeta kama walivyo wenzao wa Wilaya yangu ni walinzi wa *pilons* za gridi ya Taifa kutoka Kihansi. Wanajihisi kwamba Serikali yao imewaonea kwa vile ni tarafa pekee ambayo haina umeme.

Mheshimiwa Spika, maombi na mapendekezo, tunaomba Wizara ifikirie kuwapatia wananchi wa tarafa ya Mngeta umeme katika vijijini vya Udagaji, Chita Chita

JKT, Ikule, Mkangawalo,  Mchambe, Njage, Mbingu na Mafu, ili nao waone ni sawa na wenzao na pia tuweze kuchochea uchumi wa eneo hilo kwa kuibua viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji, hapa napendekeza njia mojawapo katika hizi ninazozitaja hapa, kwanza ni kutoa umeme kutoka Bwawa la  Mto Mngeta, kwa kuongeza *turbines* nyingine tatu ili jumla ziwe tano ambazo kwa pamoja zitakuwa na uwezo wa kuzalisha *megawatt* moja  (kila *turbine* ina uwezo wa kufua *kilowatt*  200). Umeme huo utasambazwa katika tarafa nzima ya Mngeta au vijiji kadhaa kufuatana na ushauri wa watalaam.

Pili kutoa umeme kwa kujengwa kutoka Kihansi kwenda Mji wa Mlimba. *Line* hiyo mpya itajengwa kutoka Mdogi wa Kihansi kupitia vijiji vya Udagaji, Chita kijijini, Merera, Chita JKT, Ikule, Mkangawalo Mchombe, Njage, Mbingu na Mofu ambavyo ni vijiji vya tarafa na Mofu.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa Wizara itaona jinsi gani wananchi wa tarafa hii wanavyojisikia wanapoona tarafa nyingi nne zina umeme na wao hawana. Naomba kwa heshima na taadhima Wizara iwasaidie wananchi hao ambao wana matumaini makubwa na Serikali yao ya Awamu ya Nne, ili umeme uwe chachu ya kutekeleza MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wao natanguliza shukrani zao za dhati katika Wizara yako. Umeme kutoka Mji wa Ifakara ufike katika Gereza la Idete umbali wa kilometa 20, ambako kuna shughuli nyingi za kilimo.

**MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu wachimbaji wadogo. Mkoa wa Kigoma unaaminika kuwa na maeneo mengi yenye madini hasa dhahabu. Wachimbaji wadogo ni wengi wanajishughulisha lakini utalaam na zana zinazotumika ni duni na sio salama. Hata hivyo wachimbaji wadogo wanachimba kwa kubahatisha tu, je, kuna utaratibu wa kuwapa elimu au taarifa/*geological maps* ili ziwaongoze wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, madini ya aina mbalimbali ambayo mengine siyo *traditional* yanapatikana wapi na soko lake liko wapi? Kuna haja wachimbaji kuelimishwa juu ya madini ya aina zote yanayopatikana Tanzania. Aidha, katika Wilaya ya Kibondo, kuna maeneo mengi yenye madini ya chaki ambayo matumizi yake ni makubwa kama vile katika kusafirisha ngozi, kutengeneza *Pluster of Paris (PAO)* ya hospitali, kutengeneza chaki za shuleni na kadhalika, je, Wizara inaweza kusaidia wachimbaji utaalamu wa kuchimba madini hayo na kutoa taarifa za soko la madini hayo? Baadhi ya sehemu zenye madini ya chaki yako katika hifadhi ya Moyowozi. Je, haiwezekani Wizara za Nishati na Madini na Wizara ya Maliasili na Utalii kuangalia uwezekano wa kusogeza mipaka (kidogo) ya hifadhi kuwaruhusu wachimbaji wadogo kuchimba chaki hiyo kuliko kuiacha ardhini? Wananchi pia wangejipatia ajira.

**MHE. DANIEL N. NZANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nzuri na kubwa za Wizara ya Nishati na Madini sasa kuunganisha Mkoa wa Kigoma na gridi ya Taifa, bado nasukumwa na hoja ya *project* ya *Mini hydro* pale Kasulu.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo ya tangu mwaka 1998 kati ya *Kaeco Cooperative, SIDA (Donors), TANESCO* na Wizara yako, bado nahisi ni vizuri wananchi sasa wafahamu hatima ya *project* hii. Je, kweli *SIDA* bado wana nia ya *funding*. Je, *mini-hydro plant* hii haiwezi kuwa sehemu ya mkakati wa umeme vijijini? Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na jedwali sioni mradi wowote wa umeme vijijini kwa Mkoa wa Kigoma. Bado sisi Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tunashukuru sana Wizara yako kwa juhudi za kuunganisha Kigoma na gridi ya Taifa, *good job.*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa umeme Mbinga. Kwanza nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kuchaguliwa kuiongoza Wizara hii nyeti. Kwa kipindi hiki kifupi cha miezi sita tu mmeonyesha uwezo na uwajibikaji wa hali ya juu katika kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Spika, pili kwa niaba ya wananchi wote wa Wilaya ya Mbinga, naomba nilete shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Waziri, Rais na Waziri Mkuu, kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha kupatiwa huduma ya umeme katika Mji wa Mbinga. Mbinga ni Wilaya yenye *stability* ya mazao na madini ambayo yamejenga sana nchi yetu. Tatizo letu lilikuwa ni umeme ili tuzalishe kwa teknolojia mpya ambayo bila umeme huwezi kufanikiwa.

Mwisho naomba ufanywe utafiti ili umeme huu ufikishwe vijiji vyote vya mwambao kama *Mbamba Bay,* Liuli, Luodo na Lituhi ili nasi tuweze kufanana na wenzetu wa Malawi ambao tunapakana nao. Kule mwambao wa Malawi kila kijiji kina umeme na maendeleo ni makubwa. Hongera sana Waziri wetu.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watalaam wao wote waliohusika katika kufanikisha hotuba hii nzuri na fupi.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii nitachangia kwa mtazamo ufuatao, kwanza masuala ya dunia, pili masuala ya sekta ya nishati na mwisho masuala ya sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 15 ya hotuba tumeelezewa mafanikio yaliyopatikana kutokana na sekta ya nishati kwa mwaka 2005/2006. Tumeelezwa pia matatizo yaliyoikumba sekta hii. Lakini cha kusikitisha hotuba haikugusia matatizo yaliyoikumba sekta ya madini. Tungependa kuelezwa je, mbali na mafanikio

yaliyopatikana ni matatizo yapi yaliyoikumba sekta hii ya madini katika mwaka huo huo wa 2005/2006?

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 17 ya hotuba ya Waziri amezungumzia umeme ulizalishwa kwa mwaka 2005 ulifikia *Gigawatt hours 3,6205* ikilinganishwa na *Gigawatt hours 2,126.4* zilizozalishwa mwaka 2004 sawa na nyongeza la asilimia 58.7.

Mheshimiwa Spika, aya ya 18 ya hotuba imeongelea utekelezaji wa sekta ya nishati katika mwaka 2006/2007. Nilitarajia kwa kufuata Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilipaswa utekelezaji uanze kwenye sekta ya madini, malengo na namna ya utekelezaji yameelezewa katika aya ya 42 iliyopo katika Ilani ya Uchaguzi kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya nishati. Naipongeza Serikali katika jitihada za kutafuta nishati mbadala lakini ningeshauri Serikali ijielekeze zaidi kwenye maeneo ambayo ni makame zaidi ili kudhibiti ukataji ovyo wa miti kwa ajili ya kuni.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Mkoa wa Mara ni makame sana hivyo naomba Serikali itoe kipaumbele kwa nishati mbadala katika Mkoa huu, vile vile huongoza kwa mfumo dume, akinamama tu ndiyo hufanya kazi za ukataji wa kuni ambapo hulazimika kwenda maeneo ya mbali ili kuzipata kuni hizo.

Hotuba pia imeelezea nishati mbadala ya vyanzo mbalimbali kama kasi ya upepo na tayari utafiti unapanga kufanywa kwenye maeneo ya Kilimanjaro (Mwanga), Iringa (Njombe), Singida (Kitimo) na Tanga (Korogwe). Ukiachia mbali Wilaya ya Tarime katika Mkoa wa Mara, maeneo yaliyobaki yote ni nyika na tambarare. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni vigezo vipi alivyovitumia katika kuchagua Mikoa hiyo na kuiweka katika utafiti?

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza vyanzo mbadala hotuba imeongelea utafiti wa joto ardhi, napenda pia kuishauri Wizara iangalie maeneo mengine ya nchi mfano kule kwetu Musoma katika Tarafa ya Ngoremi kuna eneo linaloitwa maji moto ambako kuna *hot water springs*. Nashauri Serikali iliingize eneo ili katika utafiti huo wa joto ardhini.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya wafugaji yapewe kipaumbele katika utafiti mzima wa *bio-mass* ambayo itaweza kutumika kama nishati mbadala kwa kupikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa umeme. Naipongeza Wizara kwa mipango ya muda mfupi na wa kati wa kuongeza uzalishwaji wa umeme lakini Waziri hajatueleza ni ipi mipango ya muda mrefu. Ilani yetu imezungumzwa mipango ya uzalishwaji wa umeme katika Mto Rusumo (Kagera), *Stiglers Gorge* na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Mheshimiwa Waziri ametaja makaa ya mawe ya Mchuchuma kwa kifupi sana. Je, ni nini kimemzuia kuongelea mpango huo kwa mapana zaidi na hiyo mipango mingine iliyotajwa katika Ilani iko vipi? Tunaomba tuelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya umeme, hotuba imetuonyesha baadhi ya mipango ya uzalishaji umeme kuwa imeanza. Cha kushangaza mpaka hivi sasa matarajio ya Watanzania kuhusu kupungua kwa bei ya umeme yamekwisha kumekuwepo makala za magazeti mbalimbali zinazoelezea ongezeko la bei ya umeme kwa siku za usoni kwa kutegemea *long run marginal cost.* Sasa Wizara inaweza kutueleza ni kwa nini bei zipande wakati imeandaa mipango kabambe katika uzalishaji wa umeme?

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya madini, naipongeza Wizara kwa kusaidia wachimbaji wadogo wadogo. Naishauri Serikali iwaangalie akinamama kwa kuwapa mikopo na vifaa vya uchimbaji ili nao waweze kuchimba madini na kujipatia riziki. Pia watengewe maeneo maalum ili wasinyanyaswe na kina baba ambao hudhani kazi hii huwafaa wao tu.

Kuhusu ukaguzi wa migodi, lipo shirika lifanyalo ukaguzi wa uzalishaji wa dhahabu *(Alex Stewart Government Business Cooperation)* ambao hulipwa 2/3 ya mrabaha. Kiasi kinachotozwa na Serikali kwa mrabaha wa dhahabu ni 3%. Sasa bado tunatoa kiasi hicho cha 2/3 ya asilimia ya mrabaha na kupewa hiyo kampuni. Je, Serikali haioni nchi yetu inapata hasara? Na je, katika Serikali hii mpya yenye ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya imejiandaa vipi ili kuhakikisha pesa za nchi hazipotei?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupitiwa upya mikataba ya madini. Waziri hakueleza katika hotuba hadi sasa ni matatizo gani yamegundulika katika mikataba hiyo. Je, Waziri anaweza kutueleza ni matatizo gani yaliyogundulika na ni nini maamuzi ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia tena kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watalaam wote na ninasema naunga mkono hoja, ila nitaomba ushuari nilioutoa Serikali iuzingatie na pia atupe maelezo kwa maeneo yote niliyohoji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa jinsi na alivyoshughulikia matatizo ya umeme kipindi hiki kwani wananchi wanafahamu siku yao ya mgao. Utaratibu huu umepunguza malalamiko na upendeleo. Nampongeza pia Naibu Waziri kwa ufundi wa kujibu maswali Bungeni. Majibu yanakuwa mafupi na yanayolenga swali. Baada ya pongezi hizi naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Waziri naomba anipe ufafanuzi kuhusu sheria tuliyotunga hapa Bungeni kuwa Serikali itachangia asilimia 25 ya gharama za kuweka umeme vijijini pale ambapo watu binafsi/mashirika wanapotafuta vyanzo vya umeme na kusambaza huko vijijini. Mpaka sasa watu wangapi wamepata mchango huo wa Serikali katika kusaidia uanzishaji na usambazaji wa umeme vijijini?

Mheshimiwa Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Waziri kwamba katika Jimbo la Njombe Kusini zipo taasisi ambazo sasa hivi zinaendelea na utafutaji wa vyanzo vya umeme wa maji na wangefurahi sana kama mchango huo wa Serikali ungepatikana mradi ambao Mheshimiwa Waziri anafahamu ni ule ambao Kanisa Katoliki Jimbo la

Njombe wameanzisha katika Mto Ruhuji na wananchi wameshiriki kuchimba mitaro ya kupitisha maji. Mradi huo ukikamilika una uwezo wa kutoa umeme hadi megawati saba. Tumeanzisha kilimo cha chai kwa wananchi. Umeme huo unatakiwa kuwezesha umwagiliaji wa mashamba ya chai katika eneo hilo.

Sasa naomba Waziri atuthibitishie kuwa tukileta maombi yetu ya mchango huo wa asilimia 25 ya gharama za umeme huo atatusaidia? Serikali ikifanikiwa kutoa mchango huo basi Jimbo langu latika miaka kumi ijayo litang'ara sana na uchumi wetu utakuwa na umaskini uliopo sasa utaondoka kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono na kuwatakia afya njema Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wa Wizara hii.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Naomba nichangie mjadala wa Waziri wa Nishati na Madini kuhusu usambazaji wa umeme. Lakini huo umeme haujasambaa vijijini. Tunaomba *TANESCO* iwezeshwe ili isambaze umeme katika miji midogo ya Kabanga, Rulenge mpaka Murusagamba, hii itasaidia kuleta maendeleo katika jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, *Kabanga Nickel* imeanza kutafuta madini kwa muda mrefu lakini mpaka sasa wanafanya utafiti. Huu utafiti lazima uishe na uzalishaji uanze. Ningependa kuuliza huu utafiti utaisha lini? Mheshimiwa Waziri naomba jibu kwa swali hili.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba nzuri sana iliyowasilishwa kwa umahiri mkubwa. Nimpongeze pia Naibu Waziri Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi na watalaam wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2005, Wizara ya Nishati na Madini iliahidi kupeleka umeme katika maeneo ya Kituri, Kirerenge, Mbambua, Kiti cha Mungu, Njia Panda, Kiwanja, Handeni, Vuchama Ndambwe na Mgagao katika Wilaya ya Mwanga.

Napenda kuishukuru Wizara ya Nishati na Madini kwa kufikisha umeme katika vijiji vya Kituri, Kisangiro, Mbambua, njia Panda na Kiti cha Mungu. Hata hivyo wakati umeme ukifika Njia Panda, Kiti cha Mungu na maeneo mengi, gharama za kuunganisha umeme ilikuwa imepanda kutoka shilingi 105,000/= mpaka kufikia shilingi 203,000/=.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilituahidi kuwa wananchi wanaweza kulipa gharama hizi kwa awamu. Lakini *TANESCO* haikutekeleza ahadi hii ya Serikali iliyotolewa Bungeni. Tunaomba sasa ahadi hii itekelezwe ili wananchi wengi wafaidike na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, katika kijiji cha Mgagao na Kijiji cha Kiverenge, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aliwaahidi wananchi umeme kufika vijijini hapo kabla ya mwezi Desemba, 2002, baadaye mwaka 2004 *TANESCO* ikapitisha nyaya za umeme juu ya vijiji vya Mgagao na Kiverenge, lakini hadi leo umeme haujasambazwa kwenye vijiji hivyo. Kwa niaba ya wananchi wa Mwanga, naomba mradi huu sasa ukamilishwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo utaona bado ahadi ya Serikali ya kufikisha umeme kiwanja na Handeni katika eneo la Nyumba ya Mungu bado haijatekelezwa. Kwa kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme kwenye eneo hili kwa kujibu swali Bungeni, wakati umefika kwa Serikali kutekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuanzisha wakala wa umeme vijijini na mfuko wa umeme vijijini, sisi wananchi wa Mwanga tulipata matumizi makubwa ya kafikisha umeme katika vijiji vya Vuchama Ndambwe, Songoa na Mringeni katika maeneo ya milimani na Ngulu, Kwakoa Toloha, Kigonigoni, Butu, Kambi ya Simba, Jipe na eneo lote la Kivisini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wakala hizi kuanza pole pole tunaomba Wizara itusaidie kupeleka umeme kwenye shule za sekondari Kamwala na Kilobeni kutoka kijiji cha karibu cha Kirongaya. Aidha, Serikali itusaidie kupeleka umeme katika shule za sekondari Kwangu na Kigonigoni katika Tarafa ya Jipe- Ndea.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa uchumi wa Wilaya ya Mwanga, kunategemea kukua kwa sekta ya kilimo katika tarafa ya Jipe - Ndea. Eneo hilo, ndiko lilipo Ziwa Jipe. Baada ya ziwa kupata maji, uvuvi umeongezeka na wananchi wengi wamehamia kutoka eneo la Nyumba ya Mungu. Maeneo haya ya kiuchumi yatapata msukumo wa kipekee kama yatapata umeme kupitia wakala huu.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi na wananchi wote wa Mwanga tunaitakia Wizara hii mafanikio makubwa na baraka za Mwenyezi Mungu.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini na kuwapongeza sana kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara. Ombi langu napenda nikumbushe ombi la wananchi wenzangu wa Kata ya Manchali iliyoko kwenye njia ya umeme utokao Dodoma kwenda Mpwapwa.

Ombi hili ni la muda mrefu na bahati nzuri *TANESCO* ilikwishaiwekea bajeti kazi ya kuteremsha umeme katika vijiji vya Manchali na Chalinze kijijini vilivyoko kwenye Kata hiyo. Wananchi wa vijiji hivi bado wanasubiri ahadi ya Serikali ya kuwapatia umeme na wengi walikwisha weka *wiring* kwenye nyumba zao kwa tegemeo la kuletewa umeme.

Naomba Mheshimiwa Waziri kwa vile ulikuwa umekwishatoa msukumo juu ya suala hili, naomba ulikamilishe kwa kulitekeleza kupitia Bajeti hii ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji hivyo leo wamekuja kusikiliza hotuba ya Wizara kwa mategemeo kuwa watapata habari njema za kupatiwa umeme na mimi Mbunge wao naomba niwasilishe rasmi mchango wangu kwa niaba yao. Natanguliza shukrani na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika kuboresha Wizara hii hasa katika kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hii ni Wizara nyeti sana ambayo naweza kusema ndiyo kichocheo cha maendeleo, maana kuna nishati ambayo iko katika *petrol, diesel, kerosine* na kadhalika ambavyo husaidia kusukuma mitambo mbalimbali katika uzalishaji na hata kuleta mwanga.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme nayo tunaona inapatikana katika maji, makaa ya mawe, petroli na hata gesi. Lakini tujiulize Serikali mpaka sasa ina mikakati gani ya makusudi kuhakikisha nishati hizi zinapatikana katika nchi yetu bila tatizo? Je, ina malengo ya muda mrefu kuhakikisha umeme utafika Tanzania nzima?

Tatizo ninaloliona ni kwamba itachukua muda mrefu nchi nzima kupata umeme wa uhakika kwani hata maeneo yaliyo na umeme, umeme unakuwa anasa na sio nishati muhimu. Mkoa wa Dar es Salaam na Kigoma Mjini, mgao ni jambo la kawaida sana, kwa nini Serikali haina utaratibu wa kufanyia *service* mitambo yake na kuondoa iliyochakaa? Matokeo yake tatizo linakuwa sugu ndio Serikali inaanza kuhaha kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nashauri hatua ziwe zinachukuliwa mapema hii itakuwa kinga.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la nishati ya umeme na Serikali isisubiri tu mwekezaji au wawekezaji katika sekta hii. Nchi yetu ni tajiri tukiamua tunaweza bila wazungu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika sekta ya madini, nchi hii ni tajiri sana, madini ya aina mbalimbali yametapakaa na yanavumbuliwa kila siku na la kufurahisha ni kwamba Tanzania pekee ndio ina madini ya *Tanzanite,* hayapatikani popote duniani. Je, madini hayo ya *Tanzanite* yameongezeka kiasi gani katika Pato letu la Taifa? Maana ni madini ya kujivunia duniani kote.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Kamishna wa Madini Tanzania inakaimiwa, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini Kamishna wa Madini atapatikana? Ni sababu zipi zinazofanya nafasi hiyo ikaimiwe kwa muda wote huo?

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona maeneo yaliyo na madini yalivyo duni, nenda Geita leoni aibu, nenda Bulyankulu na maeneo mengine hawana huduma bora za jamii, umeme, barabara, maji safi na salama sekondari za kutosha na huduma za

afya ni tatizo. Hapo ndio inabidi mikataba iangaliwe upya, mikataba hiyo haina maana kama haijali maisha ya wananchi wanaoishi maeneo yenye madini.

Mheshimiwa Spika, mrabaha unaotokana na madini pia ni vichekesho, haiwezekani mali yetu ichukuliwe kwa asilimia 97 halafu Tanzania tubaki na asilimia tatu. Kama wawekezaji wana teknolojia na vifaa sisi tuna mali.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa Serikali ikiamua mrabaha utaongezwa, tuige mfano wa Botswana, pato linalotokana na madini, linasomesha watu wao na sisi tuanze kusomesha wataalam wa kutosha ili baadae tusiwe na haja na wawekezaji wa aina hiyo kwani ni wanyonyaji. Tusilale, tutalala hadi lini? Mali inaondolewa. Ni jambo la kawaida kusikia ndege zinabeba mali kutoka migodini kwa kisingizio kwamba wanaenda kufanya utafiti nchini Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo ninapoendelea kusisitiza uzalendo, hebu viongozi tuangalie maisha ya Watanzania baada yetu sisi watakuta nini? Uzalendo unahitajika katika kuangalia maslahi ya nchi yetu, viongozi tuepuke unafiki na ubinafsi bila hivyo nchi hii haitaendelea.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida kwa nchi hii kuweka kabatini ripoti mbalimbali zinazotolewa baada ya kuundwa na uchunguzi kufanyika. Namwomba Mheshimiwa Waziri atuelezee hatma ya ripoti ya ndugu Mboma na Mang'enya, kama haina tija tujue ili hatua zingine zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 26 anasema nanukuu; "Ili kujiridhisha zaidi kiutendaji, Wizara imeunda Kamati ya Wataalam kupitia na kuchambua taarifa za Mkaguzi ili kubaini upungufu uliopo kwenye udhibiti na usimamizi wa uzalishaji na usafirishaji wa madini ya dhahabu hapa nchini. Kamati itatoa mapendekezo yatakayofanyiwa kazi ili kuboresha usimamizi na udhibiti wa madini ya dhahabu," mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Waziri hakutoa kipindi maalum au muda wa kufanyika kwa zoezi hilo. Tafadhali katika majibu ya hoja atupe *periodization* yake.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara katika kuangalia upya mikataba hiyo, iangalie mahusiano kati ya wafanyakazi wa migodini na mabosi wao (wawekezaji) wananchi wafanyakazi wananyanyasika, hawana haki na baadhi yao wamehama, taarifa nyingi zimekuwa zikieleza hivyo katika vyombo mbalimbali vya habari ingawa si vizuri ku-*rely information* za *press* lakini lisemwalo lipo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwe makini katika kuingia mikataba mingine mipya ili kuepuka matatizo yaliyopo sasa, bora tupate mapya kuliko kurudia yale yale.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na natarajia majibu ya maswali niliyouliza na nina imani mchango wangu utaboresha kazi ya Wizara hii.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, naomba usambazaji wa umeme ufike katika Kata ya Kizumbi (Bugayambelele na Nhelegani), Kata ya Ngokolo (kuongeza mtandao), Kata ya Kambarage (kuongeza mtandao) na Kata ya Ibadakuli hususan uwanja wa ndege Shinyanga/Ibadakuli katika Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari zote zifikishiwe umeme ili zifikie viwango vya sekondari katika Manispaa ya Shinyanga.

Kuhusu madini, nashauri ili madini yaweze kuinua Pato la Taifa na maisha bora ya wananchi, sera, sheria na miongozo mingine itambue miliki ya Serikali (hivyo kuwa na hisa katika migodi mikubwa) lakini pia miliki ya ardhi ya wananchi. Katika eneo husika itambuliwe kwa mujibu wa *Land Act 1999* na *Village Land Act 1999* na hivyo nao kustahili kuwa na hisa katika migodi mikubwa, badala ya kutegemea huruma ya wawekezaji au viwango vya malipo visivyozingatia kuwa Mwenyezi Mungu aliwaumba na kuwapa madini/utajiri chini ya ardhi yao. Hii inatumika katika nchi zenye mafuta. Madini ni utajiri wa watu wanaoishi juu ya ardhi hiyo kwanza, hivyo watajirike nao.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii na vile vile kwa moyo wa dhati naipongeza hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, sitapenda kueleza mambo mengi isipokuwa ni kuishauri Serikali kuhusu umeme Gairo, tunaishukuru Serikali kupitia Wizara yake ya Nishati na Madini kwa kuupatia Mji Mdogo wa Gairo umeme lakini pamoja na hayo kuja kwa umeme Gairo kumefanikisha kijiji kimoja tu cha Gairo ukilinganisha mahitaji ya lazima ya umeme katika jimbo la Gairo. Umeme unawanufaisha watu wachache sana.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ushauri kwa vile Serikali imepata gharama kubwa ya kutoa umeme Dodoma hadi Gairo ambapo ni kilometa 132 na umeme huu umepita katika vijiji vichache sana ambavyo ni Buigiri, Kinangali, Chalinze, Mbande, *Narco Kongwa,* Mtanana, Kibaigwa, Pandambili na mwisho Gairo yenyewe. Ukiangalia utakuta umeme kuelekea Gairo una vijiji vikubwa viwili tu ambavyo ni Kibaigwa na Gairo, kama Serikali imeamua kuwasaidia wananchi wake wa vijijini pamoja na Shirika lenyewe kufanya kazi ya faida halioni ni hasara kuweka umeme vijiji vichache namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini na kufanya kazi kwa faida. Sasa ipeleke umeme katika Kata ya Chakwale ambapo ni kilometa 11 tu ambapo umeme huo utapitia Kata ya Kibodya kutoka Gairo na ipeleke umeme kata ya Msingisi ambapo ni kilometa tano tu kutoka Gairo haitakuwa na maana yoyote kama umeme huo katika jiimbo la Gairo utakuwa katika kijiji kimoja, naihakikishia Wizara husika kwamba mahitaji ya umeme katika Kata nilizozitaja ni muhimu sana na yanahitajika sana na wapo wanaouhitaji na vijiji vyenye wakulima wenye uwezo na wakazi wasiopungua 35,000 na Kata ambazo zinahitaji matumizi ya umeme kwa ajili ya pampu za maji mashine nyingi za kusaga na matumizi mengine mengi.

Kwa maoni haya, natumaini Serikali sasa itapeleka umeme katika kata nilizozitaja kutokea Gairo. Kwa kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara ya Nishati na Madini chini ya Mheshimiwa Waziri na watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Mchuchuma Project,* naomba Serikali isimamie Wizara ya Nishati na Madini ili Mchuchuma ianze kazi kwanza na umeme upatikane na mkaa wa mawe uweze kupatikana. Hakuna sababu kwa hili, utafiti na gharama za Serikali zilitumika na wataalam kutoa maelezo ya kina. Naomba Serikali na Wizara yake itupe maelezo lini inaanza mradi na Serikali kwani nini mpaka leo bado tuko nyuma.

Mheshimiwa Spika, Mererani kwa *Tanzanite* naomba wachimbaji wadogo wadogo wapewe kipaumbele na wapewe vibali na *plot* na wawezeshwe kifedha. Sio wawekezaji wakubwa tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa Liganga. Liganga pia utafiti ulifanyika kwa gharama za Serikali na wataalam wetu kutoa matokeo mazuri kuwa chuma kingi kipo Liganga na madini mengine tani kwa tani na kuahidiwa wananchi wa Liganga watapata ajira na pia watafaidika kwa mengi utakapoanza mradi huo na kuvunwa chuma na hayo madini mengine. Je, Serikali na Wizara ya Nishati na Madini sasa haioni wakati muafaka kuweza kuanza *project* na kwenda na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne. Naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hotuba ya Waziri iliyoonyesha kazi nyingi ziliyofanyika. Ni kweli maeneo mengi yamepata umeme na mipango inaendelea kwa baadhi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi wa umeme vijijini ndio ukombozi wa nishati vijijini ni lini mradi huu utaanza na itaanza kwa Kanda au kwa utaratibu upi mpaka uenenee nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, napata shida kuelewa ukweli wa umeme wa Longido - Namanga kwani tangu mwaka 1995 mpaka leo bado ni ahadi tu. Naomba maelezo ili wananchi wa Wilaya ya Longido wajue ni lini watapata umeme. Naomba sasa ikumbukwe kwamba Longido ni Wilaya, wanastahili kupata umeme. Namanga ni mji unaokuwa haraka sana pamoja na kukuwa, umeme upande wa Kenya umeme umefika sasa ni aibu kama kwetu haujafika huku wenzetu wakiwa na umeme.

Kuhusu madini, napenda kuelezea mgodi ambao uko Longido. Mgodi wa *Ruby Mine* ni mgodi wa zamani sana, ni mgodi maarufu kwa kuzalisha aina nzuri sana. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mgodi huu unazalisha kila mara, ni utaratibu gani Serikali inatumia kujua uzalishaji wa mgodi huo ili wajue namna ya kudai *royalty.* Ni muda mrefu sana wakieleza kwamba bado wako kwenye marekebisho huku wanaendelea kutoa madini na kupeleka kuuza.

Kwa kuwa mgodi huu uko kijijini na wanapopata madini hakuna taarifa sahihi ambayo Serikali itajua kwamba madini inapatikana, je, Serikali itatumia utaratibu gani wa kupata fedha kwenye mgodi huo huku wenye mgodi wanaficha uvunaji. Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na madini mengi na kwa aina tofauti, je, kuna uwezekano wa kufanya utafiti kwenye maeneo mengine kwenye jimbo la Longido wawekezaji waweze kwenda huko kuchimba madini zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la umeme limekuwa kero kwa wananchi wa Longido/Namanga wakati ukitoa majumuisho naomba ueleze upatikanaji wa umeme ili wajue utaratibu wake. Ahsante sana.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu kwa hotuba hii ni kama ifuatavyo, umeme wa maji *(Hydropower Electricity)* Serikali iendelee kuweka mikakati ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji.

Mheshimiwa Spika, zipo sehemu katika nchi yetu zenye mito mikubwa ya uhakika, mfano ni Mto Lumakalya, ambao chanzo chake ni Wilayani Makete, Mto huu unapeleka maji katika Ziwa Nyasa. Mto huu wakati wote umejaa, kutokana na ukweli kwamba Wilayani Makete mvua zinanyesha kwa muda wa miezi saba mfululizo yaani kuanzia Novemba hadi mwezi Mei.

Mheshimiwa Spika, tafiti zilizofanywa huko nyuma zinaonyesha kwamba mto huu una uwezo wa kutoa umeme zaidi ya *MW 222,* kiwango ambacho ni kikubwa kuliko vyanzo vya Mtera *MW 80,* Kidatu *MW 220,* Kihansi *MW 60* na kadhalika. Kuwepo kwa uzalishaji wa umeme katika mto huu wa Lumakalya, kungesaidia kupunguza tatizo la umeme kwa kuwezesha mikoa ya Kusini kufaidika na umeme huu ambapo mikoa mingine ingetumia vyanzo vingine vya umeme.

Mheshimiwa Spika, taratibu na sheria/mikataba ya uchimbaji madini zipitiwe upya. Mapendekezo yangu, sehemu hii yanazingatia sana hali halisi inayoendelea sehemu nyingi ambazo uchimbaji wa madini unaendelea ambapo mambo yafuatayo yanajitokeza:-

(a) Uharibifu wa mazingira, Makete kuna madini yajulikanayo kwa jina *Platnum*. Wachimbaji wa kutoka *South Africa* wanapitisha vifaa vikubwa kwenye barabara na madaraja waliyoyajenga wananchi ambazo hazina uwezo wa kustahimili vifaa hivyo. Uchimbaji huu wa madini haya umeacha mashimo mengi katika kijiji changu cha Ujuni, kitu ambacho ni uharibifu wa mazingira mkubwa na hatari kwa wananchi.

(b) Mapato yanayotokana na madini haya wananchi hawafaidiki. Madini yanahamishwa bila wananchi kupata chochote kwenye mali iliyotoka kwenye ardhi yao.

(c) Serikali/Wizara haishirikishi Halmashauri pamoja na wananchi kuhusu hawa wachimbaji. Wachimbaji wanaingia Wilayani bila taarifa yoyote kwa Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Wilaya, wananchi na kadhalika ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuwashirikisha viongozi hawa wa Wilaya ili wajue kinachokuwa kimetazamiwa na Serikali kuu. Mapendekezo yangu, napendekeza Serikali isitishe uchimbaji wa madini hadi hapo taratibu na mapitio ya mikataba yatakapokamilika, maana mali nyingi ya wananchi inaibiwa wakati huu ambapo taratibu hazijakamilika.

Kuhusu usambazaji wa umeme kijijini, Serikali kupitia Wizara hii, iweke mikakati ya wizi inayoonyesha utaratibu wa kusambaza umeme katika nchi. Utaratibu wa sasa sio mzuri, kwani haujulikani na hauzingatii vipaumbele vya Taifa kama vile uchumi na matatizo ya Wilaya. Mfano, Wilaya ya Makete ina matatizo makubwa ya UKIMWI, pamoja na hazina ya uchumi mkubwa wa mbao, matunda, utalii na kadhalika ambapo tulitegemea kwamba ingepewa kipaumbele cha kusambaziwa umeme katika kata na vijiji vyake, kwani hatua hiyo ingewezesha wawekezaji kuvutiwa na hivyo kuwekeza katika Wilaya hii na kukuza uchumi wa wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii.

**MHE. KHADIJA S. A. AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kufika hapa Bungeni hali nikiwa mzima. Baada ya shukrani zangu hizo sasa naomba niende kwenye mchango wangu katika Wizara hii.

Kwa kuanza naenda katika suala la umeme. Nchi yetu haina sababu ya kuwa kiza kama vile ni nchi isiyo na wenyewe, Wizara ya Nishati na Madini inaiweka nchi katika kiza bila kujali hasara ya Serikali na wananchi kwa jumla. Hadi leo Watanzania tuliozungukwa na madini yanayoweza kutupatia umeme lakini mpaka leo tunahubiri nabwawa hayana maji. Kuna sababu gani tusitumie umeme tunaoweza kuupata katika mkaa wa mawe?

Mheshimiwa Spika, upo uhakika nchi yetu kuweza kupata umeme kwa kupitia mkaa wa mawe nchi nzima na tukaweza kuuza kwa jirani zetu, kama vile Kenya na Uganda. Kwa nini Wizara haiendi na wakati miaka 43 sasa tangu tujitawale.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie suala la madini. Nchi yetu ina maeneo ambayo yana madini. Tuiulize Wizara ya Nishati na Madini, inajua mwananchi wa nchi hii anaweza kuishi kwa raha kupitia uchumi wetu wa madini. Ni kipi kinachomzuia? Wageni ndio wanatajirika katika nchi yetu, hadi leo wapo Watanzania ambao hawajapata kuiona madini katika nchi yao. Lakini mgeni aliyepata mkataba na Serikali ndiye anayejua na ndiye anayefaidika, Wizara kwa maksudi inasimama haki kwa mgeni na kuwaacha wananchi wanateseka kwa umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya madini iangalie namna gani tutatumia madini yetu ili tuwakwamue wananchi katika umaskini ambao si wa lazima. Ahsante sana na nashukuru.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri inayotoa matumaini kwa wananchi wa Tanzania. Umeme ndiyo nyenzo kuu ya kuleta maendeleo ya maisha ya watu, biashara na viwanda kwa haraka. Ameahidi kuwa Utete, Makao Makuu ya Rufiji itapata umeme wa mradi wa Songosongo. Kwa hili wapigakura wangu hasa wa pale Utete, Nyamwage, Mohoro, Kibiti na Ikwiriri wanashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, maombi, kijiji cha Mkongo kilometa 8 kutoka Utete ni *junction* kubwa ya barabara itokayo Utete- Mkongo- Kibiti - Dar es Salaam. Pia ni *junction* kubwa ya barabra itokayo Ikwiriri - Mkongo - Kilimani - Mloka *(Selous Game Reserve)*. Aidha, kuna *Mkongo Secondary School*. Naomba kijiji cha Mkongo kipatiwe umeme wa mradi huu.

Kwa vile kijiji cha Kilimani kuna *ginnery* ya kusindikia Pamba, kufufua kwa *ginnery* hii kunasinzia sana kwa ukosefu wa nishati hii umeme. Ili kuleta maendeleo ya kilimo cha pamba Rufiji, tunaomba nishati ya umeme ya kuendeshea *ginnery* ya pamba pale Kiliman. Umeme wa *generator* ni ghali sana.

Mheshimiwa Spika, katika njia mbalimbali ya kufua umeme ni pamoja na nishati ya mionzi ya jua. *Rural Electrification* itakuwa rahisi sana kwa nishati ya jua.

Naiomba Serikali iondoe kodi ya vifaa vya kufua umeme wa jua, ikiwezekana Serikali itoe ruzuku kwa vifaa hivyo ili gharama za kusimika mitambo hiyo iwe chini na iwawezeshe wananchi kutumia aina hii ya umeme na kufanikisha *Rural Electrification.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa kuandika katika hotuba hii ya nishati na madini. Kwanza napongeza kwa hotuba nzuri ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, je, mpango wa kuwepo kiwanda cha mbolea Kilwa - Masoko miaka 20 iliyopita kulikuwepo na mpango huo. Je, Serikali ina mpango gani kiwanda hicho cha mbolea kwa kuwa mbolea inahitajika sana kwa nchi nzima na nchi mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa migodi mbalimbali nchini imeanza kutoa ruzuku kwa Halmashauri zao, je, Serikali ina mpango gani kwa Wilaya ya Kilwa kupata ruzuku kutokana na *gas* asilia iliyoko Songosongo kwa kuwa Wilaya ya Kilwa iko nyuma kimaendeleo, naomba Kilwa kupewa ruzuku hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kunusuru mazingira yetu kwa kutumia *gas* asili, naomba Serikali iwe na mpango kupata mwekezaji kwa kupata kiwanda cha *gas* ya nyumbani. Naomba kiwanda kiwepo Kilwa ili wananchi wa Kilwa kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TPDC,* mimi binafsi nawapongeza sana shirika hili linafanya vizuri sana kwanza kabisa kuhusu *data* za Songosongo zilifichwa na kampuni za *AGIP,* lakini *TPDC* ilifichuliwa *data* na leo kupata *gas* ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hiki ni chombo muhimu kwa Taifa lazima kiwepo na kupewa haki zote. Naomba wapewe uwezo wa kutafiti zaidi na kuzindua sehemu nyingi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hotuba kwa asilimia mia moja. Nashukuru.

**MHE. BRG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, suala la nishati ni *strategic,* ni lazima iwepo kwa maendeleo ya watu na wa nchi *Stigler's Gorge Project* sikusikia ikitajwa katika mipango yetu ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, bado wananchi wa Jimbo la Mlalo wanasubiri kukamilishwa kwa mradi wa kutandaza umeme katika maeneo yaliyobaki ya Rangwi, Sunga, Mtae, Shume, Manolo, Mnazi, Lunguza na Mng'aro.

**MHE. JAMES P. MSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja lakini ninayo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mikataba ya madini iliyopo kipo kipengele kinachotaka wenye migodi kulipa dola za Kimarekani zisizopungua 200,000. Halmashauri hazikuweza kudai pesa hizi kwani hazikutimiza sharti la kuwa na sheria ndogo ili kudai pesa hizo kitu ambacho ni makosa ya Wizara yako kwani Halmashauri hazikuambiwa na mikataba hiyo ni siri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza yeye na Naibu wake kwa kufanya mazungumzo na hao wenye migodi na kwamba pesa hiyo imeanza kulipwa. Naomba nielezwe basi kama watalipa malimbikizo ya nyuma, na hii *GGM* walilipa pesa hizo Geita?

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Kharumwa, Wilayani Geita kupitiwa na umeme wa gridi ya Taifa kutoka Ibadakuli hadi *KMCL.* Awali kulikuwa na ahadi ya kushusha umeme Kharumwa na wapo wateja zaidi ya 100 ambao sasa wanatumia umeme wa *generator* moja.

Sasa hivi kuna mradi wa kupeleka umeme huo tena kutoka *KMCL* kwenda kijiji cha Nyamtukuza *(sound smith)* ili kupampu maji yaendayo Kahama na Shinyanga.

Umeme huo tena unapita pale Kharumwa imeingizwa na kuwekwa kwenye mchoro wa alama. Naomba maelezo yako kuhusu ombi la wananchi hawa kupatiwa.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa mita za umeme Geita, ikumbukwe kuwa Geita umeme ni bado miaka takribani minne tangu upatikane, watu wengi sasa wanaunganishiwa umeme, Mji wa Geita unakuwa haraka na uko gizani na wapo wawekezaji wana mikopo kwenye mabenki, mita zinakwamisha, tunaomba mita za umeme.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na safu nzima ya utendaji kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuleta hotuba nzuri mbele ya Bunge lako Tukufu. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Rungwe Magharibi lina kata 19 na vijiji 118 lakini umeme unapatikana mjini na katika vijiji 12 tu. Wananchi wanashangaa wanaposikia takwimu kwamba umeme unawaka kwa zaidi ya asilimia 50 ya vijiji. Kama Jimboni kwangu ni chini ya asilimia 25 vilivyo na umeme hii, ina maana Wilaya nyingine ni zaidi ya 80% ndipo upate wastani huo.

Mheshimiwa Spika, kata zilizo mashariki mwa mji wa Tukuyu hazina mlingoti hata mmoja wa umeme. Umeme ufika kijiji cha Mbambo kilichoko Jimbo la Mashariki. Baada ya kupiga kelele, upembuzi ulifanyika toka Mbambo hadi kijiji cha Busisya kilometa nane. Baada ya hapo mafundi hawajaonekana tena. Ombi la wananchi ni kuunganisha umeme toka Mbambo hadi mjini Tukuyu umbali wa kilometa 25.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa makaa ya mawe ya Kiwira una *potential* ya kutoa *MW 100* za umeme kutokana na makaa ya mawe yanayochimbwa pale. Wananchi wanaoingia mgodini na kuhatarisha maisha yao wanatoka vijiji vya jirani vikiwemo Ilima, Katundulu, Lubanda na Lutete. Umeme unaozalishwa unaingizwa katika gridi ya Taifa lakini ni kijiji cha Ilima peke yake ndicho chenye umeme. Vingine vinaona nyaya zinazopita kwa juu, umeme wanaozalisha unakwenda kupeleka maendeleo mahali pengine. Naomba Wizara iyaone mapungufu hayo na kuwapatia umeme wananchi wa vijiji nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita niliuliza swali kuhusu gharama za kupeleka umeme katika shule za sekondari za mporoto na Kinyala na vijiji vya Syukula na Nkunga. Nilipewa gharama lakini wananchi wanauliza hizo pesa bado Serikali haijapata? Mbona sehemu nyingine nchini kila eneo tunasikia wanapelekewa umeme? Naomba Wizara iwakumbuke Watanzania hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza juhudi za Wizara kuamua umeme wa gridi kufika Ruvuma na hasa kuunganishwa kwa kupitia Makambako.

Mheshimiwa Spika, uko mpango wa umeme vijijini, mji wa Peramiho uko kwa mujibu ya sheria ya *Local Government.* Ni lini umeme utapelekwa Peramiho kutoka cha Lilambo kilometa chache kufika Peramiho. Naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, Makao Mkuu Mkoa wa Manyara, Babati unapata umeme wa gridi kupitia kituo cha Babati chenye uwezo wa *megawatt* 32 kwa sasa mkoa wa Manyara unatumia *megawatt 5.6 MW* tu kufikia Agosti, 2005 na wateja 5,872 tu. Hii ina maana kuwa umeme haujasambazwa kwa kiwango cha kutosha kwa wakazi wenye uwezo na vijiji visivyo kando kando ya gridi ya Taifa.

Ombi langu kubwa kwa kipindi hiki ni kuvipatia umeme vijiji vya Managha, Himiti, Bonga na Haraa. Vyote vina uwezo wa kutumia umeme kwa shughuli za huduma na kiuchumi na vyote vipo kando kando ya njia ya gridi iendayo Kondoa kutoka Babati na vyote vipo kilometa chache kilometa 15 kutoka umeme wa gridi ulipoishia kijiji cha Singa kutosha Babati Mjini.

Mheshimiwa Spika, ni vema pia umeme ukasambazwa kwa mitaa yote ya Babati. Natanguliza shukrani zangu kwa ushirikiano wa Waziri wa Nishati na Madini kwa muda wote.

Naunga mkono hoja ya Waziri kwa asilimia mia moja na kutamkia yeye Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. Kila la kheri na karibu Babati Mjini.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda niitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza bajeti kwani ina mwelekeo wa kutoa huduma kwa Watanzania na kuinua pato la Taifa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri Mheshimwia Lawrence Masha, Katibu Mkuu na watendaji walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

(a) Kuna ucheleweshaji mkubwa wa kuwekewa umeme kwa wateja baada ya kutimiza masharti (malipo).

(b) Kuna tatizo la usomaji wa mita kwa wale ambao hawajawekewa LUKU ukilinganisha na matumizi yaliyotumika kati ya nyumba na yumba.

(c) Vijiji vinavyopitiwa na nguzo za umeme vipewe kipaumbele kupatiwa umeme hususan vyenye idadi kubwa ya watu.

(d) Wawekezaji wa uchimbaji madini wakubwa na wadogo watambuliwe na uongozi wa maeneo husika. Vile vile wawekezaji wawe wanalipa gharama za uharibifu

wa mazingira na kulipa asilimia ya mapato na mapato yao yadhibitiwe na Serikali ili haki itendeke kwa wananchi.

(e) Pawepo na soko maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo kuliko kutegemea walanguzi kwani wananunua kwa bei ndogo ukilinganisha na thamani ya mali iliyouzwa.

(f) Kwa kuwa sasa kuna wazalendo wanaochimba madini kwa vikundi, Serikali au asasi mbalimbali mfano, *TASAF* iwawezeshe wana vikundi hawa hususan akinamama wapatiwe vifaa vya kisasa na vyenye ubora unaokubalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu naunga mkono hoja hii na nawatakia utekelezaji wenye ufanisi ikiwa ni pamoja na kuangalia mikataba ya wawekezaji upya.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii muhimu. Aidha, nawapongeza watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa jitihada za kuboresha huduma za Wizara kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza katika maeneo machache yafuatayo:-

Kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa maendeleo mazuri ya mradi wa mgodi wa makaa ya mawe Kiwira, kama ilivyoelezwa katika aya ya 21 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Napenda kutumia nafasi hii kuikumbusha Wizara kwamba mgodi huu sehemu yake kubwa iko katika Wilaya ya Ileje. Kwa hiyo, ni matarajio yangu pamoja na wananchi wa Ileje kwamba Wizara itakumbuka kutushirikisha kwa ukaribu zaidi, kwa hali na mali, katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuzingatia hoja ya kwanza naomba uongozi wa Mgodi wa Kiwira uendelee kutoa mchango wake kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kwa mujibu wa sheria. Endapo kuna malimbikizo ya malipo kwa kipindi cha nyuma, naomba malipo yafanyike bila mivutano yoyote.

Tatu, napenda kutumia nafasi hii kukumbushia ombi letu kwa Meneja wa Mgodi wa Kiwira, kutoa huduma ya umeme katika Kijiji cha Kapeta. Barua yetu Kumb. Na. HW1/D. 30/67/123 ya tarehe 28 Aprili, 2006 yahusika.

Nne, namuomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie malalamiko ya baadhi ya wafanyakazi wa Mgodi wa Kiwira kuhusu malipo ya mafao yao. Barua ya wafanyakazi hao Kumb. Na. TAMICO/SMS/VOl. 3/01 ya tarehe 02 Julai, 2006 kwa Mheshimiwa Waziri yahusika. Inaelekea tatizo hili ni la muda mrefu na linajirudia rudia. Ni vema likashughulikiwa na kulimaliza mapema ili Wabunge na maeneo hayo tusiendelee kugonganishwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa kuwasilisha vizuri. Nimekwisha changia kwa maandishi nalazimika kuandika dokezo hili kwako baada ya kusoma kijitabu kuhusu sekta za nishati na madini ukurasa huo huo imeonyeshwa kwamba *Songwe Kiwira Coal Mine,* iko Kyela. Hakuna Makaa ya Mawe yanayoonyeshwa kwenye eneo la Ileje. Je, taarifa hiyo ni sahihi?

Mheshimiwa Spika, naomba Wilaya ya Ileje tutendewe haki. Tumemezwa sana huko nyuma siyo vizuri hali hiyo ikiendelea. Naomba kuunga hoja mkono.

Mwisho, nawapongeza kwa kazi nzuri mliyoanza nayo. Nawatakieni mafanikio mema na naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilwa, nilitaka kumuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atueleze hatma ya Kiwanda cha Mbolea ambacho kiliahidiwa kujengwa Kilwa Masoko ambako hadi leo hii eneo lililotengwa bado lipo.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini kitajengwa na ni kitu gani kilisababisha ifike hadi leo hii bila ya kujengwa?

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, afanye juhudi za makusudi ili Kiwanda cha Mbolea kijengwe Kilwa kama ilivyokusudiwa hapo awali, ili na vijana wa Kilwa na wananchi waweze kupata ajira kutokana na raslimali zao wenyewe kama ilivyo katika Mikoa mingine wanufaikavyo na raslimali zao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa juhudi kubwa wazifanyazo katika kuuweka sawa Mradi wa Gesi ya *Mnazibay,* Mtwara.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaunga mkono hoja yako uliyotoa Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja kwa kuanzia na shukrani ya kupatiwa umeme katika vijiji vya Kibiti, Mchukwi na Bungu katika mwaka huu wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huu kuna kasoro iliyojitokeza inayohusiana na kutolipwa mafao yao waathirika waliopitiwa na barabara/laini ya umeme. Hali hii imesababisha wananchi wa vijiji vya Mkupuka, Kitembo na Kibiti, kuilalamika Serikali kwamba haiwatendei haki.

Mheshimiwa Spika, wapimaji waliokwenda kupima na kuthamini *(evaluation)* ni chanzo kikubwa cha wananchi hao kutolipwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwenye majumuisho ya Mheshimiwa Waziri kujibiwa kuhusu ulipwaji wa mafao yao wananchi hawa wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu uhusiano baina ya Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Maji kwa ujumla nyie ni pacha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara ya Maji itaweka pampu katika visima vilivyo katika vijiji vya Kibiti, Mtawanya, Bungu na Kimbunga. Kwa kuwa visima hivi vyote vipo kati ya mita 300 hadi kilometa 2, naishauri Wizara ipeleke nguzo za umeme hadi huko kwenye vyanzo vya maji ambako kutafungiwa pampu vyanzo hivi vyote vya maji vipo ndani ya vijiji ambavyo umeme utapita katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana iwapo utanikubalia ombi langu hili kwa ajili ya manufaa na maendeleo ya wananchi wa maeneo hayo. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia mia moja.

Pili, naomba kukumbusha ahadi ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2004/2005 ya kumalizia mradi wa umeme wa Kijiji cha Kivukoni ambacho tayari nguzo zimeshasimikwa lakini hakuna waya wala vikombe kuanganisha nguzo zile. Aidha, tatizo lingine hakuna *transformer.* Wakati wa Kampeni ya mwaka 2005 ahadi ya Mheshimiwa Rais na yangu ni kuwa mradi huu utakamilika mwaka huu wa 2006. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kazi hii ikamilike pamoja na *transformer* ya Kijiji cha Igumbiro ambacho kiko kati ya Kijiji cha Milola na Mji Mdogo wa Lupiro ambavyo vyote vina umeme. Tafadhali tuondoe *anomaly* hii.

Tatu, nakumbusha mradi wa umeme wa Tarafa za Malinyi na Mtimbira, mradi ambao ulianza kutafutiwa (upembuzi yakinifu) tangu mwaka 1998. Mradi huu ulipata msukumo kwa ahadi ya Rais Jakaya Kikwete wakati wa kampeni kuwa kipindi hiki kitashuhudia kazi hii itakamilika. Suala hili tumeshalizungumza kati yetu na Mheshimiwa Waziri na Mbunge Mheshimiwa Dr. Ngasongwa. Najua kazi hii umeshaagiza *TANESCO* waitekeleze.

Naomba sasa uwasukume hapa Bungeni kwa kuuchukua umeme kutoka Kihansi *(66 KV)* kwenda Malinyi, Mji Mdogo wa Makao Makuu ya Jimbo langu. Hatimaye umeme huu ufike Miji Midogo ya Mtimbira, Itete na Lupiro hadi Mahenge na kuachana na ule *33KV.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, katika kipindi kisichopungua miaka 40 cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kiasi cha asilimia 10% tu ya Watanzania wanatumia nishati ya umeme. Hii inatokana na bei ya juu ya nishati hiyo kiasi ya kuwafanya wananchi washindwe kuitumia. Naiomba Serikali ipunguze 20% ya *VAT* katika gharama za umeme wa majumbani ili wananchi waweze kunufaika na nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, pia nishati ya mafuta ya taa, petroli na dizeli nazo ziangaliwe na kusimamiwa vizuri ili kuwe na uwiano wa bei ya nishati hizo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Bei za nishati za mafuta ni kubwa sana katika nchi yetu ukilinganisha na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina vyanzo vingi vya nishati lakini hakuna mipango mizuri ya kutumia vyanzo hivyo kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingine vya nishati kama vile *biogas,* mabaki ya mkonge, miwa na kadhalika vinafaa vitiliwe maanani katika sekta binafsi za wazalendo ili viongezee nguvu katika gridi ya Taifa na kuweza kuwapunguzia gharama za umeme wananchi walioko vijijini hasa katika maeneo ambayo nishati hizi zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kuna madini mengi kama vile almasi, dhahabu, chuma, makaa ya mawe, *Tanzanite* na kadhalika. Je, madini hayo na mengineyo ambayo sikuyataja yanasaidia vipi kukuza uchumi wa nchi yetu na hivyo kuweza kuboresha maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu bila upendeleo wa aina yoyote. Ahsante sana.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii, baada ya kuipongeza hotuba iliyosomwa na Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo ambazo zinakwenda sambamba na jitihada ambazo zinafanywa na Wizara, naomba yafuatayo yafanywe kwa kutuma wataalam Wilayani Kibondo kuangalia maeneo yenye madini ili baada ya kuthibitishwa hatua za haraka zifanywe kwa kuweza kuwapa ajira vijana na kuweza kuinua hali ya maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayohusika ni yafuatayo:-

(i) Mlima wa Kumwambu uliopo Kibondo Vijijini na mlima huo unayo chokaa nyingi mno ambayo wananchi wamekuwa wakichimba na kuuza. Kwa kuwa Mlima huo unayo chokaa nyingi napendekeza ithibitishwe na Serikali kwa kuhusisha Wizara yenye dhamana ili eneo hilo ama mlima huo ufahamike rasmi kuwa na madini hayo na Shughuli za uchimbaji zianze mara moja. Chokaa inayotoka hapo inatumiwa na wananchi kujenga nyumba.

(ii) Mto wa Kumwanga Kata ya Murungu, Mto huo unayo chumvi nyingi ambayo wananchi wanaivuna kienyeji. Naomba wataalamu waende kuthibitisha hilo na kisha kuhalalisha uchimbaji wa chumvi hivyo kwa kuinua kipato cha mwanakibondo .

(iii) Machimbo ya Mwironge - Buyungu, eneo hili linayo madini ambayo wananchi wanayachimba kienyeji. Kwenye eneo hili pia pafanyiwe utafiti ni kina. Machimbo hayo yatambuliwe na kupewa usimamizi wa Serikali.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kugundulika kwa gesi asilia na kuanzishwa kwa sera zilizowezesha mradi wa matumizi ya gesi asilia kutoka Songosongo kutumika viwandani, mnamo mwezi Julai 2004, viwanda kadhaa tayari vimeshaunganishwa katika mradi huo yaani vime-*convent* kutumia gesi asilia (katika *boilers etc).* badala ya mafuta *(heavy fuel oil)* ambayo yanaagizwa kwa gharama kubwa kutoka nchi za nje. Baadhi ya viwanda hivyo ni kama *Kioo Limited, TBL, Aluminium Africa (ALAF), Wazo, NIDA Textile* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia gesi asilia, viwanda hivi vimeweza kupunguza gharama za uendeshaji. Kwa mfano, *Wazo Hill* peke yake kuanzia Julai, 2004 hadi Juni, 2006 kimeweza ku-*save* shilingi bilioni 18.57. Bila ya shaka na viwanda vyote ambavyo vimejiunga na mradi huu navyo vina-*save* pia.

Mheshimiwa Spika, ingawa Serikali huwa inapata *royalty* na kodi kiasi fulani, bado wananchi wa Tanzania hawajaweza kunufaika na maliasili hii ya gesi asilia. Ni kwa nini viwanda hivi havijapunguza bei za bidhaa zao, baada ya wao kupunguza gharama za uendeshaji, ili mwananchi mmoja mmoja nao wakanufaika na maliasili hii ya gesi asilia na kusaidia katika mpango wa MKUKUTA.

Nashauri Serikali ihakikishe kwamba wananchi wananufaika na maliasili yao ya gesi asilia na sio wawekezaji (wenye viwanda) peke yao.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa *TPDC* na *Pan African Energy* (wawekezaji kutoka Canada) wanaendesha utafiti juu ya miradi ya gesi asilia kutumika majumbani na kwenye magari na inawezekana matokeo ya utafiti huo yakapatikana hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, ili Watanzania wanufaike, nashauri Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuiwezesha *TPDC* ipasavyo ili katika mradi huo *TPDC* wawe ndio *lead seller* na sio *Pan African Energy* au wawekezaji wengine. Nashauri Serikali iwekeze zaidi katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Hata kama tayari gesi asilia imeshaonekana na tayari inatumika, ikumbukwe kwamba gesi asilia nayo huisha, hivyo utafiti zaidi ni muhimu sana. Wenzetu wa Uganda na Kenya wamekazana katika shughuli za utafiti na wanawekeza kweli kweli.

Mheshimiwa Waziri angetueleza ni kiasi gani kimetengwa kwa shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia pekee sio maendeleo kwa ujumla. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, hongera kwa bajeti nzuri ambayo ina mwelekeo kwa ujumla. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na wahusika wote katika Wizara ya Nishati na Madini. Ukweli mwelekeo ni mzuri na ni vyema sisi Wabunge tukawapa muda wa kutekeleza Mpango wenu nzuri.

Nashukuru kwa juhudi ambazo Wizara inafanya kufanikisha kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Chato, naomba ahadi ya Wizara kukamilisha kupelekwa umeme katika mji mdogo wa Muganza ukamilike, nguzo zimekaa karibu mwaka mzima.

Aidha, ombi la kupeleka umeme katika mji wa Buzilayombo, Busanga na Buseresele likafanyiwa kazi. Ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia moa moja.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotolewa kwa Wilaya zilizo na madini Wilaya ya Chato isisahaulike. Wizara inafahamu kuwa Chato ni Wilaya kama ilivyo Wilaya ya Biharamulo. Si vyema kuendelea kupata hisani toka Wilaya mama kila fedha zinapopatikana mfano zinapopatikana toka kwa migodi yetu. Mfano, Tulamaka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono na ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi na wote katika Wizara ya Nishati na Madini. Hongereni na Mungu awajalie katika kazi hii muhimu katika uchumi wa nchi yetu.

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujua Serikali ina mkakati gani kuhusu wachimbaji wadogo wadogo wa machimbo ya Mererani, Geita kwa sababu wanapata matatizo makubwa sana hasa kama Mererani wana matatizo makubwa sana kuhusu huyo Mwekezaji.

Kuhusu umeme wa Mtera, wakulima wanaoharibu vyanzo vya maji, Serikali ina mkakati gani ili kuweza kukidhi vyanzo vya maji? Naomba kujua hayo niliyoyaandika kwenye maswali yangu ya maandishi pamoja na sehemu nyingine ambazo wakulima wanaharibu vyanzo vya hivyo kuwa na kesi tunazozisikia huko Mererani ni kweli au ni uwongo wa watu?

Kuhusu kuleta umeme Mkoa wa Kagera, sehemu moja ya Rusumo Mto Ruvu Kagera: Je, Serikali haioni kuwa ni vizuri kutengeneza umeme kuliko kuchukua umeme Uganda?

Je, huko Uganda wakiamua kutukatia umeme hatuoni kuwa ni shida kubwa sana? Hatuna sehemu kubwa za mito mikubwa ya kuweza kukidhi mahitaji yetu, pamoja na kwamba Mto wa Kagera huwa haukauki?

Mheshimiwa Spika, hata kama Bajeti hii haiwezekani, naomba Mheshimiwa Waziri aweke kwenye mipango yake ya mwaka ujao. Nitashukuru kamao maombi yangu yatafanyiwa kazi.

Naomba kuwasilisha.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja katika Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, tunayo Madini ya kutosha mpaka Madini mengine tunayaitwa jila la nchi yaani *Tanzanite*. Hii ni ishara tosha kuwa Tanzania ambayo siyoi maskini.

Lakini la kushangaza, Watanzania hawa ni maskini vya kutosha, yaani umasikini umekithiri kwa Watanzania na nchi hii ina Madini ya kutosha kama dhahabu, almasi, bati, chuma*, uranium, phosphate*, makaa ya mawe, vito, *nickel*, chokaa, jasi, jaribosi, chumvi, mfinyanzi na gesi. Madini haya hayajatumiwa kukuza uchumi wetu na kuboresha maisha ya Watanzania. Je, ni lini basi Madini haya yatawasaidia Watanzania? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na sera ya makusudi ya kuwapiga vita wachimbaji wadogo wadogo wa Madini, badala ya kuwasaidia kuboresha shughuli zao. Kutokana na sera hii wachimbaji wadogowadogo wanakuwa na taabu sana.

Naishauri Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kuwa utajiri mkubwa wa Madini ya nchi yetu unatumika kikamilifu kuinua hali ya uchumi wa nchi yetu na hivyo kuboresha hali ya maisha ya watu wetu na kufanya maisha ya Watanzania kuboreka. Pia, ushauri wangu ni kwamba Serikali iziunde Sera mpya ya Uwekezaji katika Sekta ya Madini, Sera mpya ya Madini izinduliwe kwa lengo mahsusi la kulinda maslahi ya wananchi na wachimbaji wadogo wadogo.

Pia, mapato ya Serikali toka kwenye Madini yanayouzwa yaongezwe ili kuweza kukuza haja ya Watanzania. Serikali iweke utaratibu wa kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo taarifa muhimu zinazohusu bei toka masoko ya ulimwengu kila mwanzoni mwa Juma, kila kwenye eneo la machimbo kutakuwa na Mnada wa madini mbalimbali yanayopatikana hapo. Wafanyabiashara watakaotaka kushiriki kwenye Mnada huo watatakiwa kukata leseni halali zinazowahusu kununua Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja hii. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa hotoba yake fasaha.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la *Net Group Solution* na Mkataba wa Serikali. Matarajio ya Serikali kutokana na uendeshaji wa *TANESCO* hayakufikiwa kwa kuridhisha kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ilijulishe Bunge lako Tukufu *cost/benefit analysis* ya Mkataba ulioingiwa kati ya *TANESCO* na *Net Group Solution,* yaani mapato na matumizi, pia faida na hasara zinazotokana na *Net Group Solution* kuiendesha *TANESCO* kwa kipindi chote cha Mkataba uliopo tangu ulipoanza.

Mheshimiwa Spika, mapato na matumizi (faida na hasara) kwa kipindi cha Mkataba wa *Net Group Solution* zilinganishwe kwa kipindi hicho hicho kilichotangulia wakati *TANESCO* ilikuwa ikiendeshwa katika nafasi za Menejimenti kuwapisha *Net Group Solution.*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu utakuwa na manufaa ya kujifunza kwa undani maeneo yenye matatizo ya kweli katika masuala yamtaji, mipango, vipaumbele vya miradi, matumizi ya fedha kwa ajili ya utawala na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa *comparative cost/benefit analysis* kwa mfumo nilioeleza hapo juu, utasaidia Serikali kuchukua tahadhari katika siku zijazo patakapojitosheleza hali inayofanana na ile iliyoikumba *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkataba wa *Net Group Solution* utakwisha mwezi Desemba, 2006, baada ya kushindwa na kwa kuwa Viongozi wa Menejimenti ya Wazalengo iliyowapisha *Net Group Solution* wana uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 20 katika uongozi wa *TANESCO* na hawakuwa na makosa yoyote walipoagizwa na Serikali waachie ngazi, Je, Serikali haiwezi kufikiria kuwatumia kwa utalaam walionao katika miradi au shughuli nyingine za *TANESCO*?

Mheshimiwa Spika, swali hili naliuliza kwa sababu viongozi walioachia ngazi wako Mitaani wasota kwa muda mrefu kujitafutia ajira za kujiajiri. Wachache sana wamepata ajira.

Mheshimiwa Spika, tatizo nililonalo mimi na wenzangu wengi ni kuwa wataalam hawa wenye sifa adimu waliosomeshwa vizuri kwa kodi za wananchi na wapo hawana kazi, papo hapo, kuna miradi mingi ya umeme inayoongezeka nchini kujikwamua katika upungufu wa umeme, wanapaswa waendelee kutoa mchango wao wa ajira kulitumikia Taifa hili lililowasomesha.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifikirie kuwapa ajira watumishi hao ambao kwa mwono wa watu wengi, wana hisia kuwa waliondolewa madarakani isivyostahili.

Mheshimiwa Spika, suala la kupatikana nishati mbadala kwa matumizi ya mkaa wa kuni, lini umuhimu wa pekee nchini hasa Vijijini wanakoishi asilimia 80 ya Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, kwanza naiomba Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu matumizi ya mkaa na kuni nchini kwa kupikia ni sawa sawa na *Megawatts* ngapi?

Mheshimiwa Spika, hivi hakuna uwezekano wa Serikali kutafuta mtandao wa wafadhili wakereketwa na suala la hifadhi ya mazingira wakaweza kuikopesha nchi yetu ili kutafuta kuleta na kusambaza teknolojia rahisi ya kutengeneza majiko madogo madogo kwa wingi yanayotumia mionzi ya jua?

Ni maoni yangu kuwa hasara ya kurekebisha mambo yote yanayoharibiwa kwa uharibifu wa mazingira ni kubwa sana ikilinganishwa na gharama za kutengeneza na kusambaza majiko madogo maalum kwa kupikia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ijitose kufanya utafiti huu ili kujinusuru na adha kubwa inayotokana na uharibifu wa mazingira kutokana na matumizi ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za mpito za hifadhi ya nishati inayotokana na mkaa na kuni, naishauri Serikali kwa kupitia Wizara za Nishati na Madini, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, zipange utaratibu utakaotumika katika kila Kata kuyatambua na kuyatenga maeneo maalum yatakayokuwa *source* ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, wachoma mkaa, wakata kuni na wauzaji wote wa mkaa na kuni wa jumla na rejareja mkaa wasajiliwe na wapewe sharti la kujiunga katika *SACCOS* za nishati ya mkaa/kuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua wana-*SACCOS* ya nishati waundiwe kanuni zitakazowalazimu kutunza maeneo yaliyotengwa kwa mkaa/kuni na taratibu zote za kukata na kupanda miche ya miti ya mkaa. Siku ya kupanda miti au tarehe ya kupanda miti iwe tofauti kwa kila Wilaya au Mkoa kufuatana na wakati mzuri wa msimu wa mvua. Wakati huo mbegu au miche ya miti husika iwe imeenezwa katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya haya, kanuni zielekeze kuwa upandaji miti uwe endelevu kwa kipindi chote cha msimu wa mvua. Kwa njia hii, itakuwa rahisi kudhibiti suala zima la ukataji, utunzaji na upandaji miti na wana-*SACCOS* hawa ndio wawe na jukumu la msingi la kusimamia na kuendesha biashara ya mkaa na kuni ambayo ndiyo miradi yao. Napendekeza kuwa Serikali ianzishe utaratibu niliouleza hapo juu kwa *pilot scheme,* hususan katika maeneo ambayo ni vyanzo vya maji na pia katika Kata za pembezoni katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa Jimbo la Mikumi, napendekeza Kata ya Ndunda Kata ya Uleling'ombe na Kijiji cha Munisagara ambacho kijiografia kiko peke yake kama Kisiwa na ni vigumu kukifikia kwa sababu kimezungukwa na milima mirefu, kila upande.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati kunipa majibu ya mambo niliyoyaeleza. Kwa kumalizia, namwomba Waziri wa Nishati na Madini aangalie uwezekano wa kuviunganishia umeme katika Vijiji vifuatavyo katika Jimbo la Mikumi: Kivungu, Zombo, Ulaya na Kisanga.

Mheshimiwa Spika, Kijiji Kivungu kipo mita 500 kutoka kiwanda cha Katani hapo, ambapo tayari kuna umeme. Tatizo ni kuwa *Transformer* iliyopo ni ndogo, kwa maelezo ya *TANESCO* Kilosa.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vingine nilivyovitaja vina umuhimu wa pekee. Zombo na Ulaya vyote viko katika barabara itokayo Kilosa kuelekea Mikumi. Zombo ni kama kilometa nane kutoka Kijiji cha Masauze ambapo tayari umeme umefika. Ulaya iko kilometa 12 kutoka Zombo.

Zombo na Ulaya viko katika barabara ya Kilosa – Mikumi, ambayo imo katika Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2005 kuwekwa lami kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007. Umuhimu wa umeme katika Vijiji nilivyovitaja ni kukuza uchumi wa wananchi kwa mazao yanayolimwa kama pamba, ufuta, mahindi, miwa, maharage na mpunga.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kisanga kiko kilometa 30 katika *junction* ya barabara ya kutoka Mikumi – Kilosa iliyopo kilometa 14 toka Mikumi kuelekea Magharibi. Mazao yaliyotajwa hapo juu, yanalimwa Kisanga pia. Kisanga kuna Shule yenye sifa za pekee iitwayo *Msolwa Secondary School.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kuniwezesha kuchangia hoja hii. Naunga mkono hoja hii kwa kila hali.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia tena kwa maandishi kwa mara ya pili baada ya kusoma hotuba na Mipango ya Wizara ya Nishati na Madini na kuielewa.

Mheshimiwa Spika, katika kuusikiliza utaratibu wa kawasaidia wananchi wa maeneo mengine, utaratibu wa kuwafikishia wananchi huduma hiyo, unafika hata Vijijini. Matumaini waliyopewa wananchi wa Kigoma sio ya kuwapatia matumaini ya kupata umeme hivi karibuni. Hata kwa utaratibu uliopo, mpango ni wa kufikisha umeme Makao Makuu ya Mkoa tu.

Mheshimiwa Spika, huoni kwamba Serikali kwa makusudi mazima imewatenga wananchi wa Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya zake za Kasulu na Kibondo? Nilidhani wananchi wa Kasulu na Kibondo nao wangechukuliwa kama Watanzania kwa kupewa angalau jenereta wakati utaratibu wa kitaifa wa kufikisha umeme kwenye Wilaya hizo ukiandaliwa.

Mheshimiwa Spika, inawasikitisha wananchi wa Kigoma kuwa Wizara imeandaa kufikisha umeme katika Vijiji vya Mikoa mingine wakati Wilaya za Kasulu na Kibondo hazijawahi kuona mwanga unaoitwa umeme.

Mhesimiwa Spika, naomba haki itendeke kwa kila Mtanzania.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimechangia kwa maneno, lakini dakika 15 hazitoshi. Ningeomba kusisitiza jambo ambalo nimelichangia kwa maneno jana hapa

Bungeni. Tanzania sio maskini kwa sababu tunao utajiri wa rasilimali ambazo nchi nyingine nyingi duniani hazina.

Mheshimiwa Spika, naongea kwa uchungu sana, nikiona Tanzania tumeshafikia mahala tumekata tamaa na kuacha madini yetu yawe yanachimbwa kwa kiwango kikubwa na Wawekezaji. Ninaomba sana Serikali ya Awamu ya Nne ianze sasa kupanga *long term plans*, miaka 10, 15 kuanza kujitayarisha kiteknolojia na vifaa vya kisasa vya kuchimbia madini ili baada ya muda huo tuweze kuchimba madini. Serikali sasa ifike mahali iache kabisa kutumia *vocabulary* ya hatuwezi na tubadilike mara moja na kutumia *vocabulary* ya tutaweza. Nitaomba Waziri atakapotoa majumuisho atoe *comments* kuhusu hili ili na Watanzania waone kwamba Serikali ina mpango wa kuwakomboa kutoka kwenye umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa la nchi, sasa nirudi kwa wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki. Naipongeza sana Serikali kwa kuweza kunipatia umeme kwa japo asilimia 60 kwa Kata zangu nne za Tambarere.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu kubwa ni Kata zangu za Milimani. Jiografia ya Milimani katika usambazaji wa umeme, nilishamwandikia barua Naibu Waziri ili afanye ziara, aone ni jinsi gani Serikali itawasaidia wananchi wangu wa milimani. Kuhusu miradi ya umeme ambayo Serikali iliidhinisha, ifanyike tangu mwaka 2005/2006 na imeachiwa njiani. Naisihi Serikai wakati wanatoa majumuisho, wawajibu wananchi ni lini wataikamilisha miradi hii – Mradi wa Kadando, Mradi wa Kizerui, Mradi wa Mtii na Mradi wa Parane, Myamba, Mpinji, Ivuga, Sambweni mpaka Bwambo.

Mheshimiwa Spika, kuna Kata zangu za Milimani ambazo ziko kwenye giza totoro na hawa ndio ikifika saa 11.00 jioni tu, basi ni kulala na Mheshimiwa Waziri sikumsikia akiongea lolote kuhusu Kata hizi. Mfano Kata ya Vunta, Kirangare. Ningeomba Mheshimiwa Waziri aongee kuhusu Kata hizi mbili na pia kuhusu ziara ya Naibu Waziri kwenye Kata za Milimani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nimpongeza Mheshimiwa Msabaha, Mbunge, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri Lawrence Kego Masha, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wake wote kwa maandalizi na hadi kuiwasilisha Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha mwaka 2006/2007 Wizara pia izingatie yafuatayo:-

(1) Madini kama raslimali muhimu na inayopatikana aridhini, ni muhimu sasa sheria za umiliki na namna ya kuyapata lazima iwe bayana ili kuondoa manung'uniko miongoni mwa mwananchi ambao mara nyingi wameona kama wanadhulumiwa hasa pale panapokuja maelezo juu ya kuwepo Mwekezaji kwa ajili ya kutafiti na kisha kufanyia kazi eneo lenye raslimali hiyo na hivyo

wahusika ama wamiliki (kienyeji) wa eneo hilo kuelezwa kwamba hawana haki isipokuwa ni Serikali ndiyo yenye mamlaka juu ya matumizi ya mali zote zilizomo chini ya ardhi.

(2) Taratibu za mwekezaji mmoja kupewa zaidi ya eneo moja kwa ajili ya utafiti, nao haufai kabisa unaashiria kuwepo na harufu ya rushwa. Kama ilivyo kwa Kampuni ya *Barrick Gold Co-oporation Limited* kwa kumiliki migodi ya Bulyahulu- Kahama, Nyabigena na Nyabirana – Tarime na Biharamulo, kwa nini iwe Barrick sehemu hizo zote? Hakuna Wawekezaji wengine?

Mheshimiwa Spika, umeme ni nishati muhimu hasa kwa kipindi cha sasa cha kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya nishati hii. Utaratibu wa namna ya uzambazaji umeme huu una urasimu mkubwa sana hasa kwa wananchi wenye hali ya chuki kimapato (wale waishio Vijijini). Zipo dalili nyingi za rushwa hadi kuupata umeme.

Wananchi wa Vijijini hasa wakulima wapewe fursa ya kukopa na baadae wafanye malipo taratibu.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa mafuta utiliwe mkazo katika kuepuka mafuta yenye mchanganyiko wa kemikali kama vile mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya taa na kadhalika, kwani maji yameleta madhara wakati wa matumizi. Naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo: Kwa kweli Tanzania ina madini mengi ikiwemo dhahabu, almasi, bati, chuma, *uranium, phosphate,* vito, makaa ya mawe, *nickel*, chokaa, jasi, jaribosi, chumvi, mfinyanzi na gesi. Madini haya hayatumiwi kukuza uchumi wa nchi na kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Kama nchi ingetumia vyema madini yaliyopo, kwa hakika hali ya umaskini kwa kiasi fulani ingepungua sana.

Serikali imesahau kushughulikia baadhi ya maeneo ya madini, mathalani, madini ya chumvi na mfinyanzi. Haya ni madini ambayo yanapatikana nchini kwa wingi kabisa ambayo hayana tatizo la masoko. Wakati chumvi ina soko kubwa katika nchi jirani ambazo hazina vyanzo vingi vya madini hayo, halikadhalika mfinyanzi ni madini yenye soko kubwa katika viwanda vya petroli na sehemu mbalimbali za ulimwengu.

Kuhusu petroli, tuna hazina kubwa sana ya petroli katika maeneo ya Bahari yetu ya Hindi. Petroli ni nishati inayotumika ulimwengu mzima. Upembuzi yakinifu ungefanywa na nchi ingefanikiwa kupata nishati hii, ingeondokana na umaskini uliokithiri kwa kiasi kikubwa sana.

Mheheshimiwa Spika, yapo madini ya chuma na makaa ya mawe. Serikali ingechimba chuma na makaa ya mawe na kuweza kuanzisha viwanda vya chuma cha pua. Kuna soko kubwa la makaa ya mawe, chuma na chuma cha pua hasa katika nchi ya Jamhuri ya Watu wa China. Naomba kuwasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa kisasa, uchumi endelevu. Hakuna mwekezaji yeyote awe wa ndani au wa nje atakayekuja kuwekeza ikiwa upatikanaji wa umeme sio wa uhakika. Kwa hiyo, Wizara kutokana na matatizo yaliyoikumba nchi yetu mwaka 2006 na mwaka 2005, athari zake kiuchumi zimeonekana wazi, hivyo Wizara haina budi ikajiandaa kikamilifu kwa Bajeti hii ili mapungufu hayo yasijitokeze tena.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu sasa nianze kuchungia.

Kuhusu Shirika la Maendeleo la Petroli *(TPDC).* Hili ni Shirika muhimu sana Tanzania kama vile *NDC* kwa sababu ndiyo chombo pekee hapa nchini chenye mamlaka ya kufanya utafiti wa mafuta ya gesi. Naipongeza Serikali kwa kutatua tatizo kubwa la Ofisi pale *TPDC* baada ya malumbano marefu kupatiwa sehemu ya jengo la Mafuta *House* kwa ajili ya kutunza nyaraka muhimu za Kampuni za Miamba *(Siemic Data).*

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na malalamiko mengi sana kuhusiana na suala la mafuta na gesi hasa upande wa Zanzibar. Hii inatokana na mambo mengi, lakini kwa upande wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na suala hili, sisi tunajiuliza suala moja tu ambalo naamini Mheshimiwa Mbunge wa Chama Tawala nao wanajiuliza au wanapaswa kujiuliza pia kwamba *TPDC* ilianzishwa kwa *Government Notice No*. 140 ya tarehe 30 Mei, 1969 *Act No. 17* ya mwaka 1969 ya Mashirika ya Umma. Maana yake ni kwamba *TPDC* ni Shirika la umma na sio Shirika la Muungano. Lakini pia *TPDC* linafanya kazi chini ya Wizara ya Nishati na Madini ambayo nayo sio ya Muungano. Lakini katika ibara ya 4(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nyongeza ya kwanza mafuta na gesi vimetajwa kuwa ni vya Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa itakuaje vitu vya Muungano vishughulikiwe na Shirika na Wizara zisizokuwa za Muungano? Sio ukiukwaji mkubwa na wa makusudi wa Muungano kwa vyombo ambavyo sio vya Muungano. Hili ni moja kati ya kero za Muungano na vyombo husika, lazima kutatua kero hii.

Mheshimiwa Spika, sheria ya uchimbaji wa mafuta, *The petroleum exploration and production Act,* inatamka kwamba itafanya kazi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Lakini kuna tetesi kuwa iliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, lakini haikuridhiwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Kama hili ni kweli, hali hii itakuaje?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika *Zanzibar Laws Decree 1951*, pamoja na *regulation* ya mwaka 1952 kuhusu *mining (mineral)* ambayo ndiyo iliyotumika tarehe 16 Desemba, 1953, *British Resident for Zanzibar* kwa wakati ule Visiwa vya Unguja na Pemba, *Decree* hiyo hadi hii leo haijafutwa na pia imetamka waziwazi kwamba mafuta yakipatikana ni mali ya Zanzibar. Je, huu sio mgongano mwingine mkubwa wa kikatiba?

Mheshimiwa Spika, swali la uwakilishwaji wa Zanzibar, hivi sasa Serikali ya Zanzibar ina uwakilishi dhaifu katika Serikali ya Muungano. Huwezi kusema kuna u-*member* wa Bodi wanaowakilisha maslahi ya Zanzibar. Mjumbe wa Bodi anaweza

akawa ni mtu yeyote. Je, katika *TPDC* na katika Wizara ya Nishati na Madini vyombo vyenye mamlaka ya mafuta na gesi vinawawakilishi gani kutoka Zanzibar, ambao unaweza kukubali kama mdau au kukataa kwa maslahi ya Zanzibar na kwa mujibu wa sheria ya nchi. Zanzibar inafaidika vipi? Huwezi kusema kuwa Zanzibar inafaidika na umeme wa gesi kutoka Ubungo, ambao huingizwa katika *grid* ya Taifa na baadaye kupelekwa Zanzibar.

Kwa taarifa, Zanzibar inanunua umeme huo kama ambavyo Mombasa itaweza kununua au Mji mwingine wowote wa nchi ya jirani. Faida halisi ya gesi itapatikana ikiwa zitajengwa *pipelines* hadi unguja na Pemba ambako vitajengwa vinu vinavyoweza kutumia gesi kule tena, kwa gharama za Mfuko huo huo wa gesi. Hii itahakikisha upatikanaji endelevu wa umeme Visiwani na kuacha kuitegemea *submarine cable* iliyopo sasa ambayo tayari imezeeka. Nashukuru sana.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao kushika wadhifa huo na pia kwa kuwasilisha vizuri hatoba yao ambayo ni fupi, lakini imekidhi.

Baada ya shukrani hizo napenda nichangie hotuba kwa kutaka kujua kwamba ni lini Serikali itaongeza jitihada zake za kuweza kuwakwamua wanawake kwa kuwapatia nishati mbadala ambayo itasaidia kupunguza ukataji miti hovyo na kuwapunguzia mzigo wa kuhangaika kutafuta kuni au kuchoma mkaa?

Mheshimiwa Spika, tatizo hili huchukua muda mrefu katika shughuli za kila siku za mwanamke na hivyo kupelekea kuchoka na hata umahiri wa uzalishaji mali huwa hafifu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 90ya kutumia nishati ya kuni na mkaa kwa nchi ya Tanzania na hata nchi jirani za Zambia, Malawi na kadhalika. Kwa kweli hili ni tatizo ambalo madhara yake kwa nchi yetu ni makubwa sana.

Hivyo, ni vyema Serikali inihabarishe ni lini ufumbuzi wa kupata nishati mbadala utapatikana ambao utakuwa ukombozi kwa mwanamke na nchi kwa ujumla.

Tumeshuhudia matatizo ya ukame, mmonyoko wa ardhi na hata mafuriko. Kama vile haitoshi, tunahitaji kuwasaidia wanawake wa Vijijini na hata wa Mijini ambao nao pia wanakabiliwa na tatizo.

Mwisho, naomba Wizara husika ipeleke umeme kwenye Vijiji vya Wilaya za Mkoa wa Pwani ambako kuna baadhi ya maeneo wanaishia kuona nguzo na waya za umeme zilizopitishwa kwenye maeneo yao. Naomba nipatiwe majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa wananchi wa Kijiji cha Singa hawajafungiwa *transformer* kama Mheshimiwa Waziri wa Madini alivyoahidi ya kwamba Meneja wa Mkoa wa Singida angetekeleza kazi hiyo. Naomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali langu kuhusu umeme wa kwenda Ilumda, Iambi, Nduguti Mkalama na Ibaga, pamoja na Vijiji vya Mwanga, Mwangeza, Kidarata na kadhalika alisema kwamba maeneo hayo yatapata umeme kupitia Mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Naomba maelezo kupitia Bunge hili wakati ukihitimisha, maelezo yako ili wananchi wa Iramba Mashariki wasikie na kukaa mkao wa kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Nkungi Hospitali wakiwepo wafanyakazi na raia wengine wengi wamelipia gharama za kuwekewa umeme ndani ya nyumba zao, lakini mpaka sasa mwaka wa pili, kazi hiyo haijatekelezwa na hata bila maelezo. Naomba Maelezo.

Sio lengo langu kushika Shilingi au kusimama, lakini nisipopata majibu itabidi niyadai kwa kusimama wakati Bunge likikaa kama Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wengine wote.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba nzuri na ninaiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa kazi nzuri zinazofanywa na Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa ufuatiliaji wa karibu kwa Shirika la *TANESCO* ambao umewezesha Wilaya ya Mbarali kupata umeme mapema sana.

Mheshimiwa Spika, bado kazi ya kusambaza umeme inaendelea taratibu sana kwa sababu ya ukosefu wa vifaa mbalimbali vinavyohitajika kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, tangu Wilaya ya Mbarali kupandishwa kuwa Wilaya, *TANESCO* hakuna vifaa kama usafiri wa Meneja wa *TANESCO* Wilaya, wala nyenzo za kumwezesha kufanya kazi kama vile *billing* zote anatumia maandishi ya mkono. Naomba msaada wa ufuatiliaji.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Watendaji wengine kwa kazi ya kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri ya kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ni miaka isiyopungua arobaini tangu uanzishwe Muungano wetu, lakini hadi sasa ni asilimia kumi tu ya wananchi wa Tanzania wanaotumia umeme majumbani mwao. Hii ni kutokana na bei kubwa ambayo wananchi wanashindwa kuimudu. Umeme unachangia kwa kiasi kikubwa ajira na pato kwa wananchi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye bidii ili umeme uenee nchi nzima na bei yake iwe nafuu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina madini mengi kama vile dhahabu, almasi, chuma magadi, makaa ya mawe na kadhalika. Je, ni kwa namna gani madini haya yanachangia uchumi wa nchi yetu pamoja na kuweza kuboresha maisha ya wananchi wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, naomba mikataba isimamiwe vizuri ili iweze kuwa na manufaa kwa wananchi wa nchi hii na isiwe kwa manufaa ya wageni na sisi tukabakia na unyonge wetu. Kwa mfano, kule Mererani wananchi wanadhalilishwa na Wazungu na mishahara wanayolipwa wananchi ni midogo sana ukilinganisha na Wazungu. Je, Serikali haioni huu ni uonevu? Naiomba Serikali ifanye iwezavyo ili Watanzania waweze kufaidika na mikataba mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali imepunguza kodi ya mafuta ya taa, petroli pamoja na dizeli, lakini bado bei ya mafuta haijapungua. Naiomba Serikali ifuatilie suala hili ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa hatua inazozichukua kuhusiana na wachimbaji wa madini, wabaneni walipe kodi. Pamoja na hayo, napenda kueleweshwa yafuatayo:-

Moja, hatima ya Watumishi wa MEREMETA walioko *Tembo Mine* wanaishi bila mishahara na wana matatizo mengi na makubwa. Nilikwishamwona Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi akasema pesa za watu hao zinashukulikiwa, lakini mpaka leo hakuna kinachotekelezeka.

Nilikwishamwona Gavana wa Benki, naye akasema pesa zao zipo. Cha kushangaza hadi leo hakuna pesa zilizopelekwa. Watumishi hawana mishahara!

Naomba maelezo kuhusu mafao yao. Kwa nini Gavana wa Benki na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi walinidanganya? Ushahidi upo! Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kuimarisha Ikama yake ya Watumishi. Watumishi hawatoshi, pamoja na kutotosha waongezewe utalaamu wa kuhakikisha kazi za madini. Tusitegemee wageni kuja kufanya ukaguzi, ni gharama sana. Gharama hizi zingesomesha wataalam wetu wa kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migodi, sheria irekebishwe ili Watumishi kutoka nje waje ambao utalaamu wao haupo hapa. Watumishi wasitoke nje, kwa mafno, Nyamongo, Walinzi ni Wa-Nepal. Hivi Wa-Nepals ni Walinzi wazuri kuliko Wakunya? Tafadhali hili lirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni nafasi ya Kamishna. Nafasi ya Kamishna itajazwa lini? Ni tatizo kubwa. Wataalam mnaopendekeza wawili au mmoja nafasi izibwe.

Mheshimiwa Spika, naomba umeme katika maeneo ya machimbo, eneo la Nyakagire, Nyarugusu, Rwamgasa na Katoro. Umeme uendao Bukombe tafadhali upitie maeneo hayo kufanya biashara ya umeme. Umeme utaimarisha uchimbaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kigezo gani kilitumika kila mgodi kulipa Dola 200,000 wakati migodi yote hailingani? Wanasheria hawakuwa makini! Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri. Vilevile, nimpongeze Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Wizara nzima kwa maandalizi mazuri yenye mwelekeo wa kuongeza huduma ya umeme Mjini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa makusudio yake ya dhati ya kukabiliana na tatizo la umeme kwa Ari, Nguvu na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda sasa nianze kuchangia katika Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nchi bila ya nishati kwa ujumla wake haiwezi kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Maendeleo katika nchi yanaonekana kutokana na uchumi wake unavyokua na uchumi haiwezi kupanda bila viwanda, teknolojia endelevu na zana/mtambo kutumika kikamilifu. Kwa hiyo, nishati ni nyenzo muhimu sana katika kupunguza umaskini kwa wananchi wa nchi husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, mfupi naomba mchango wangu niuelekeze zaidi kwenye vyanzo vya nishati aina mbili:-

- Nishati ya umeme inayotokana na upepo; na
- Nishati ya gesi na umeme inayotokana na mabaki ya zao la mkonge

Mheshimiwa Spika, Nishati ya umeme inayotokana na upepo inaweza kuwa ni njia mbadala katika uzalishaji wa umeme badala ya kutegemea nishati ya maji. Tunayo maeneo mengi hapa nchini ambayo kasi ya upepo zaidi ya *8m/Sec* inaweza kuendesha

*turbine* za kuzalisha umeme. *Turbine* moja ya hali ya chini inaweza kuzalisha *MW2* au zaidi kutegemea hali ya upepo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme kwa njia ya upepo hauharibu mazingira wala hauhitaji mafuta *(Diesel au Petrol).*

Mheshimiwa Spika, umefika wakati muafaka Serikali ifanye utafiti wa hali juu na haraka ili matokeo yake yapate kujulikana.

Mheshimiwa Spika, nishati ya gesi na umeme inayotokana na mabaki ya zao la Mkonge *(biogas)* ni nishati inayoweza kuzalisha umeme kutokana na gesi inayozalishwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la kusaidia mazoa (*C.F.C*), Shirika la Umoja wa Mataifa la kuendeleza Viwanda *(UNIDO)* vikishirikiana na Serikali pamoja na *Katani Limited* katika shamba la mkonge la Hale, zimeonekana dalili njema za kuweza kupata kutokana na zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo mazuri ya utafiti huo, leo hii unajengwa mtambo wa uzalishaji nishati ya *biogas* huko Hale. Mashamba ya Mkonge yaliyopo sasa yanaweza yakatoa mabaki yenye uwezo wa kuzalisha *MW 50.*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa *MW 50* sio haba, kwani hiki ni kiwango kikubwa kuliko kile kinachopatikana hapo Hale *(MW21)* kutokana na maji au *Mnazi Bay MW 15* kutokana na gesi ya *Mnazi Bay.*

Mheshimiwa Spika, zao la mkonge linaongezeka kila mwaka, hivyo uzalishaji wa nishati ya umeme kwa kutumia mabaki ya zao la mkonge utazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, tukitumia vizuri teknolojia hii, bila shaka Serikali itakuwa imepunguza tatizo la nishati ya umeme kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya nchi yetu na hata kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nusu ya Wilaya ya Lushoto, yaani Tarafa za Umba, Mlola na Mgashi ziko gizani kwa kutokuwa na umeme na hivyo kuathiri uchumi na maendeleo ya wakazi wa maeneo hayo. Naomba Waziri atoe tamko wakati wa majumuisho ni lini Tarafa za Mlola, Umba na Mgwashi zitafikishiwa huduma ya umeme. Naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza wewe Waziri na Naibu Waziri kwa kuchaguliwa kuiongoza Wizara hii nyeti. Kwa kipindi hiki kifupi cha miezi sita tu mmeonyesha uwezo wa uwajibikaji wa hali ya juu katika kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli.

Pili, kwa niaba ya wananchi wote wa Wilaya ya Mbinga, Warumba namletea shukrani za pekee Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha kupatiwa huduma ya kuenea umeme katika Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Spika, Mbinga ni Wilaya yenye *stability* ya mazao na madini ambayo yamejengwa sana katika nchi yetu. Tatizo letu lilikuwa ni umeme ili tuzalishe kwa tecknolojia mpya ambayo bila umeme huwezi kufanikiwa.

Mwisho, naomba ufanywe utafiti ili umeme huu ufikishwe Vijiji vyote vya mwambao kama *Mbambabay*, Lindi, Lundo na Lituli ili nasi tuweze kufanana na wenzetu wa Malawi ambao tunapakana nao. Kule mwambao wa Malawi kila Kijiji kina umeme na maendeleo ni makubwa. Nampa hongera sana Waziri wetu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mnayoifanya na pia naunga mkono hoja yako. Mheshimiwa Waziri mpaka sasa wananchi wa Kijiji cha Singa hawajafungiwa *transformer* kama ulivyoahidi ya kwamba Meneja wa Mkoa Singida angetekeleza kazi hiyo. Naomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali langu kuhusu umeme wa kwenda Ulunda, Iambi, Nduguti, Mkalama na Ibaga, pamoja na Vijiji vya Mwanga Mwangeza Kidaratu na kadhalika, alisema kwamba maeneo hayo yatapata umeme kupitia mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Naomba maelezo kupitia Bunge hili wakati ukihitimisha maelezo yako ili wananchi wa Iramba Mashariki wasikie na kukaa mkao wa kupata umeme. Wananchi wa Nkungi Hospitali wakiwepo wafanyakazi na raia wengine wengi wamelipia gharama za kuwekewa umeme ndani ya nyumba zao lakini mpaka sasa mwaka wa pili kazi hiyo haijatekelezwa na hata bila maelezo. Naomba maelezo.

Siyo lengo langu kushika shilingi au kusimama lakini nisipopata majibu itabidi niyadai kwa kusimamia wakati Bunge limekaa kama Kamati. Nakutakia kazi njema wewe, Naibu Waziri na Watendaji wengine wote.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Manaibu wake.

Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia machache katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Nchi yetu hii ya Tanzania ni tajiri na sisi wenyewe Watanzania ndio tunaoifanya nchi hii kuwa ya kimaskini.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza sana, mali nyingi Mwenyezi Mungu alijaalia kuziweka hapa Tanzania na Watanzania wenyewe ndio wanaozitoa mali hizo na kuwapa wageni kwa thamani ndogo tu kwa Watanzania, wakati nchi hii inadidimia kwa

umaskini hali ya kuwa mali nyingi tunayo, lakini mali hiyo inatumika kwa kuwaondoshea umaskini watu wasiokuwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania hatuna pesa, lakini tunayo mali, tutumie mali zetu kwa kuitajirisha nchi yetu na watu wake. Ni jambo la kushangaza sana, itakuwaje wageni ndio wawe wamilikishaji wakubwa wa migodi ya madini?

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunasema tuondoe umaskini, hivyo mali ambazo zingetusaidia kuondoa huo umaskini, badala yake tunaachia wageni wachukue mali hiyo, je, huo umaskini utaondokaje.

Mheshimiwa Spika, Watanzania kila tukisoma, kwa nini tunakuwa wepesi wa kuzitoa mali zetu? Umefika wakati sasa tujirekebishe, tuwe na uchungu wa mali zetu mali za Tanzania zisitumike kwa kuzijenga na kuziondolea umaskini nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii baada ya kuipongeza Hotuba iliyosomwa na Waziri mwenye dhamana. Baada ya pongezi hizo ambazo zinakwenda sambamba na jitihada ambazo zinafanywa na Wizara, ninaomba yafuatayo yafanywe kwa kutumia watalaam Wilayani Kibondo, kuangalia maeneo yenye madini ili baada ya kuthibishwa hatua za haraka zifanywe kwa kuweza kuwapa ajira vijana na kuweza kuinua hali ya maisha ya Wananchi. Maeneo yanayohusika ni yafuatayo:-

(i) Mlima wa Kumwombu uliopo Kibondo Mjini huo unayo chokaa nyingi mno ambayo wananchi wamekuwa wakiichimba na kuuza. Kwa kuwa mlima huo unayo chokaa nyingi, napendekeza ithibitishwe na Serikali kwa kuhusisha Wizara yenye dhamana ili eneo hilo ama mlima huo ufahamike rasmi kuwa na madini hayo na shughuli za uchimbaji zianze mara moja. Chokaa inayotoka hapo inatumiwa na wananchi kujengea nyumba.

(ii) Mto wa Kumwanga Kata ya Muvungu unayo chumvi nyingi ambayo wananchi wanaivuna kienyeji. Ninaomba watalaam waende kuthibitisha hilo na kisha kuhalalisha uchimbaji wa chumvi hiyo kwa kuinua kipato cha mwanakibondo.

(iii) Machimbo ya Mwironge – Buyungu, eneo hili linayo madini ambayo wananchi wanayachimba kienyeji. Kwenye eneo hilo pia pafanyiwe utafiti wa kina ili machimbo hayo yatambuliwe na kupewa usimamizi wa Serikali.

**MHE. ABASS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri ya Bajeti na kazi nzuri mnayofanya toka kuteuliwa kushika nafasi hiyo. Nakupongeza pia Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

(a) Temeke kuna tatizo kubwa la muda wa kukata umeme na kuurudisha.

*(b)* *TANESCO* ifikirie kuweka Luku nyumba zote za Temeke na Dar es Salaam yote kwa ujumla itasaidia kuondoa malalamiko ya *bill* kubwa na *TANESCO* watapata faida kubwa.

(c) Kuna Luku nyingi za wizi zinauzwa Dar es Salaam. *TANESCO* ijitahidi kutafuta mashine zinazotengeneza hizo Luku.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoandaa na kuiwasilisha hotuba ya Wizara hii kwa Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, umeme ambayo ndiyo nishati kuu kwa matumizi ya mitambo viwandani unazalishwa kwa kiwango kidogo, kwa ufanisi mdogo na bei yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji umeme nchini Tanzania kwa asilimia 90 unategemea maji ya mvua. Hili lisingekuwa ni tatizo sana kama hifadhi ya maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme ingekuwa ya uhakika. Kwa bahati mbaya uhakika huo haupo. *TANESCO* pia huzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya diseli na hivi karibuni gesi ya Songosongo.

Mheshimiwa Spika, mitambo inayotumia diseli ya *IPTL* ambayo ilijengwa mwanzoni mwa miaka ya tisini kwa ajili ya kuzalisha umeme wa kuiuzia *TANESCO*, sio tu haijasaidia kuondoa tatizo la umeme, lakini pia imekuwa ni mzigo mkubwa kwa watumiaji. *TANESCO* inailipa Kampuni ya *IPTL* mabilioni ya fedha kila mwezi na kuhamishia gharama hizo kwa wateja wake. Ilitarajiwa kuwa tatizo la umeme lingepungua sana baada ya *TANESCO* kuanza kutumia gesi ya Songosongo.Bado matatizo yamebaki pale pale kama sio kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuifukuza Menejimenti ya Wazalendo ya *TANESCO* na kuiajiri *Net Group Solution* katika mazingira yaliyojaa utata, kukatika ovyo kwa umeme kumekuwa ni jambo la kawaida. Nadhani sababu kubwa ni uchakavu wa mitambo ya *TANESCO*. Kwa nini uchakavu huo haupatiwi dawa ikizingatiwa kuwa *TANESCO* inauza umeme wake kwa bei za juu ikilinganishwa na nchi za jirani na kwa muda mrefu Shirika hilo lilinufaika kwa ruzuku iliyokuwa inatoka kwenye Mfuko wa Nishati?

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanachangia Dola nyingi kwa manunuzi ya bidhaa ya petroli. Sehemu kubwa ya fedha hii inaingia kwenye Mfuko wa Nishati na fedha inakwenda kwenye *TANESCO*. Kwa nini isiweze kuimarisha miundombinu yake?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atumie uwezo wake wote ili kuboresha Sekta hii kwani inachangia kiasi kikubwa uzalishaji na kuliongezea Pato la Taifa letu na kupunguza umaskini. Ahsante.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitamke kuwa naunga mkono hoja na kuitakia Wizara utekelezaji wenye fanaka ili Wizara ya Nishati na Madini ifanikiwe kuwahudumia Watanzania.

Baada ya kueleza hayo ya utangulizi, napenda sasa nizungumzie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Serikali imeona haja ya kuufanya Mkoa wa Kigoma nao uingie kwenye *grid* ya Taifa kwa kupata umeme toka Tabora. Hali hii itawezesha maeneo ya Nguruka, Uvinza, Kazuramvimba, Kalenge, Mpela, Simba ambavyo ni Vijiji katika Jimbo la Kigoma Kusini kupata maendeleo ya haraka.

Hata hivyo, nashauri ufanywe utaratibu wa kuzalisha umeme toka Mto Malagarasi. Umeme huo ukizalishwa Malagarasi katika Mkoa wa Kigoma itakuwa rahisi kufikisha umeme kwa watu wengi kuliko Vijiji vya Mkoa wa Kigoma. Naamini itakuwa rahisi pia kuwezesha Makao Makuu ya Wilaya nyingine mbili kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Kaperafuru, Kata ya Igalula, hususan eneo la kati ya Vijiji vya Rukoma na Lubalisi, ipo Kampuni inayotafiti madini. Hili eneo lipo jimbo la Kigoma Kusini, Kusini mwa Jimbo la Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Kampuni inayofanya utafiti wa madini katika eneo hili, imekuwa pale kwa takribani miaka kumi.

Mpaka sasa hakuna matokeo yanayoeleweka na ambayo yataweza kuelezeka mbele ya safari tangu jamii inayozunguka au Tanzania kwa ujumla. Wizara inatoa kauli gani kwa Kampuni hii inayofanya utafiti?

Nitashukuru katika majumuisho Serikali iwaondoe Watanzania hofu ya kuwa mali inachukuliwa kwa siri kwa kisingizio cha kusafirisha udongo wa Sampuli, kwani wananchi wana imani kuwa kinachopelekwa nje sio sampuli bali ni uchimbaji wa siri unaohamisha madini.

Naomba Wizara itoe kauli kwa hili.

Namalizia kwa kuwatakia kila la kheri kiutekelezaji. Ahsante.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliokwishachangia kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo wa kuleta matumaini katika sekta hii.

Naishukuru Serikali kwa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Chunya, hatimaye kusambazwa hadi Miji midogo ya Makongolosi Mkwajuni. Kwa

kuwa Serikali tayari ilikwishachimba nguzo Mbala, Kanga hadi Galula: Je, ni lini umeme utaunganishwa kwenye njia hiyo ili wananchi wa Vijiji hivyo nao waendelee kufaidika na huduma hiyo?

Hivi sasa nchi nzima iko katika harakati za kujenga majengo ya Shule za Sekondari. Nashauri Wizara iamue kupeleka umeme kwenye maeneo hayo ya Shule ili wanafunzi wapate fursa ya kuendelea kujisomea hata wakati wa usiku. Shule hizo hasa zilizoko kwenye njia za umeme kama vile Shule ya Sekondari ya Maweni Mkwajuni.

Katika Makao Makuu ya Jimbo la Songwe, tatizo na kero kubwa ni ukosefu wa huduma ya maji. Tatizo hili linatokana na nguvu ya umeme ambayo haitoshelezi kusukuma mashine ya kusukuma maji. Sababu ni kwamba *transformer* iliyoko haina uwezo wa kueneza umeme kwenye mashine hiyo. Wilaya Chunya, dhahabu imeenea karibuni kila eneo. Lakini leseni za uchimbaji ni kidogo sana ukilinganisha na zile za utafutaji kumbukumbu, ziko Ofisi ya Madini Chunya. Nashauri badala ya kuongezewa muda wa *renewa*l wa zaidi ya miaka kumi, uwe chini ya miaka kumi.

Ukurasa wa 27, muhtasari wa Taarifa ya Jumla katika Sekta ya Nishati na Madini, naomba niwajulishe kuwa Makaa ya Mawe *(Coal*) pia yanapatikana sehemu ya Mngamba-Jimbo la Songwe ambako Kampuni binafsi ya *AMCO* inaendelea kuyafanyia utafiti zaidi juu ya matumizi yake.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, nishati inayotegemewa karibu na asilimia zaidi ya 80 ni nishati ya kuni na mkaa. Kutegemea nishati hiyo, kwa asilimia hiyo, ni dhahiri mazingira yetu yataathirika na kwa kweli yameshaathirika. Ili wananchi waondokane na hali hiyo, inabidi nishati mbadala ambayo ni mkaa wa mawe baada ya kusanifiwa ili mkaa huo uweze kutumika kwa kupikia na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, pia ipo haja ya Wizara kuandaa mkakati maalum kwa kushirikiana na Wizara husika wananchi waweze kutumia gesi katika kupikia. Kwa mpango endelevu na wenye gharama nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ieleweke na hali yetu inayotukabili ya kupatikana kwa umeme kwa njia ya maji, lakini bado ipo haja mazingira yatunzwe ili vyanzo vya maji viendelee kutupatia maji kwani hizo njia za kutupatia umeme kwa leo zinaonekana endelevu. Kwa mfano gesi na makaa ya mawe iko siku nishati hiyo itamalizika.

Kwa hiyo, bado vyanzo vya maji vikitunzwa vizuri, umeme utaendelea kupatikana kutokana na maji. Kwa hiyo, Wizara hii ina ulazima ishirikiane na Taasisi husika ili mazingira yatunzwe. Wizara igharamie pia katika kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini inalalamikiwa sana kuwa haina faida kubwa kwa Serikali na wananchi na kwamba, ipo haja ya makusudi sheria na mikataba ya madini iangaliwe upya ili kuleta uwiano ulio sawa baina ya wawekezaji na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa kuwa nchi yetu iko katika soko huru, lakini ipo haja ya makusudi Serikali ijiingize sio kufanya biashara, bali kuratibu shughuli zote za mafuta ili wananchi waweze kufaidi punguzo la kodi ya mafuta ambalo Serikali imetangaza.

Pia, Serikali ikiratibu shughuli za mafuta itapunguza upandaji wa bei ambazo hazina ulazima isipokuwa ni utashi wa wafanyabiashara binafsi ya kutaka kujiongezea faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kukomboka katika suala la nishati na madini, ni lazima na kwa makusudi Taasisi zinazohusiana na Sekta hii ziwezeshwe kikamilifu kufanya kazi zake. Mfano *STAMICO, TPDC* na Chuo cha Madini.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pale Dar es salaam tunayo *storage* kubwa ya mafuta *(Tipper)* ambayo Serikali yetu inayo hisa kubwa. Naomba kuishauri Serikali iweke utaratibu wa kutumia *storage* hiyo kupokelea mafuta yote yanayoinga nchini, halafu wenye mafuta wachukue tokea hapo *(Tipper)* kwenda kwenye *storage* binafsi.

Mheshimiwa Spika, faida za utaratibu huo wa *storage* utasaidia kuwa na akiba ya kutosha ya mafuta katika nchi yetu. Pili, itakuwa nirahisi Serikali kuweza kudhibiti ukwepaji kodi wa mafuta kwani kitendo cha mafuta yote kuingia pale ni rahisi sana Serikali kufahamu kiasi kilichoingizwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kukiwa na mafuta ya kutosha nchini, ni rahisi kuzuia bei zisipande mara kwa mara kwani kwa kuwa na *stock* kubwa, *competition* ya kupunguza bei ili wauze itakuwa kubwa na hivyo kusababisha bei kupungua. Ahsante.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, hoja hii ni nzuri na imeandaliwa vizuri sana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua yafuatayo: *TANESCO* imepima tayari *line* ya umeme kutoka Iringa Mjini hadi Ismani kupitia Vijiji vya Igingilanyi, Kisinga, Mkungugu, Ndolela, Ismani Tarafani, Kihorogota hadi Nyang'oro.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate ratiba ya ujenzi wa umeme kwenda Ismani. Tarafa hii iliahidiwa tangu miaka ya 1970 wakati Serikali inahamasisha mradi wa Mtera. Naomba tu nipate ratiba ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, *Ruaha National Park* ni Mbuga ya pili kwa ukubwa nchini. Naomba nipate taarifa ya mpango wa Serikali kupeleka umeme *Ruaha National Park* kupitia Vijiji vya Nyamahana, Mlowa, Mapogoro, Idodi, Tungamalenga hadi *Ruaha National Park.*

Mheshimiwa Spika, naomba majibu yangu kwa maandishi. Ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge na hatimaye kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara nyeti ya Nishati na Madini. Nampongea Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara chini ya kuongozi wa Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya Bajeti iliyoandaliwa kitaalam na yenye matumaini kwa Watanzania katika kuinua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kutoa ombi kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu maeneo yafuatayo: Kkatika Jimbo la Rorya, *geological survey* imeonyesha kuwa kuna aina mbali mbali za madini. Hii imetokana na sampuli za miamba zilizokusanywa na wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, madini na vito vilivyopatikana ni pamoja na *Rubies,Tourmaline, Sapphire* na kadhalika. Pamoja na vito hivyo, *geological survey* pia imebainisha kuwa kuna kuna mkanda wa dhahabu chini ya ardhi ambayo watafiti wa madini wameipa jina la *Utegi Gold Belt.* Kutokana na utafiti huo, Kampuni ya *Barrick Gold* inayomiliki *North Mara Gold Mine* ilianzza kufanya uchimbaji wa awali katika ukanda wa Utegi eneo la *DET*, Tarafa ya Luo-Imbo Kata ya Nyathorogo Jimbo la Rorya. Wananchi wa Jimbo la Rorya wameomba Wizara itoe wataalam, nyenzo na iunde mkakati wa kuanza kuwasaidia wachimbaji wadogo wa maeneo ambayo yamepatikana vito nilivyotaja pamoja na uchimbaji wa dhahabu, hatimaye kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje. Ninaomba msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Rorya, aina ya Gesi ya Helium inapatikana kwa kiwango kikubwa. Mazungumzo ya awali kuhusu namna ya kuzalisha gesi hii yalifanyika mwaka 1992/1993. Kulikuwepo na wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza, lakini majadiliano hayakufanyika kwa kuwa eneo hilo barabara ilikuwa haifiki. Kwa sasa barabara imetengenezwa. Wananchi wa Tarafa ya Girango Kata ya Goribe, Kijiji cha Nyamusi ambako Gesi ya Helium inabubujika, wanaomba Wizara itume timu ya wataalam wakiongozwa na *STAMICO* ili matumizi ya gesi hii yaweze kutoa mchango wa kuibua uchumi wa wananchi wa Jimbo la Rorya na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hauwezeshi kumpa haki ya kuchangia inayotakikana Mbunge yeyote. Kwa hiyo, nitatoa tu matangazo. Hapo ndiyo tumefika mwisho wa uchangiaji, Waheshimiwa Wabunge kwa hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Saa 11.00 nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini, ambaye atajibu hoja kwa dakika 20. Baada ya hapo, nitamwita Mheshimiwa mtoa hoja Waziri mwenyewe wa Nishati na Madini, ataongea kwa dakika 40, ajibu hoja zilizotolewa. Saa 12.01 tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Sasa ninayo yafuatayo ya kufafanua, bahati mbaya si wengi, wengine wametoka na hivi, lakini nataka tuelewane utaratibu.

Kwanza, maana ya Kamati ya Matumizi ni kupata maelezo, hayo ndiyo maneno, kupata maelezo au ufafanuzi. Sio kudai mradi mpya au kung'ang'ania lisilokuwemo kwenye bajeti sasa liwekwe, hayo hayamo ni ufafanuzi na maelezo.

Kwa maana hiyo, nakuombeni sana, leo tuna muda wa kutosha Waheshimiwa Wabunge, nendeni kwenye vifungu mtaona kitabu cha pili na hata cha nne na hususan cha nne.

Waheshimiwa Wabunge, ukitazama kwa makini, ukatumia muda wako huu wa saa chache hizi, utaona mahali ambapo kwa uhalali kabisa, bila mgongano wowote na Spika, utafika mahali kwenye kifungu utaliuliza swali lako kuhusu ufafanuzi na litafafanuliwa.

Lingine hapa kwenye Kamati ya Matumizi, hatukamati mishahara ya maafisa, hawatuhusu hawa. Hili Bunge uwajibikaji wa Serikali ndani ya Bunge, unahusu Waziri tu.

Kwa hiyo, ukitazama kitabu cha pili ni kile kifungu cha kwanza tu ambacho ndio humo mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Sasa unapotaka kuuliza ufafanuzi kwa suala la Sera, hapo ndipo unaweza kusema juu ya mshahara wa Waziri.

Baada ya hapo tukiingia, kwenye Mkurugenzi wa Madini, Mkurugenzi wa Nishati, Kamishna sijui wa kitu gain, hairuhusiwi na haina maana yoyote, unapoteza muda kusimama na kudai kwa jazba kwamba, sasa na wewe unataka kuondoa shilingi. Hatuondoi shilingi kwa Idara, tunaondoa kwenye mshahara wa Waziri.

Nikumbushe jambo moja, mara nyingine huwa mnaniona nakuwa kidogo mkali, lakini kanuni ziko wazi kabisa. Kanuni ya 49(5): "Iwapo wakati wa majadiliano Bungeni Spika atasimama, Mbunge yeyote aliyekuwa anazungumza wakati huo, ataketi na kukaa kimya."

Sasa inatokea mimi nasimama ili nitoe mwongozo, mtu anajisikia vizuri kuendelea tu. Hilo siwezi kuliruhusu, kwa sababu ni kuathiri kanuni. Pale nikikemea kwamba, ukae chini ndio natimiza kanuni. Kwa hiyo, hilo ningependa tuelewane kwa sababu vinginevyo, kazi ya Spika ni kama *empire* ama refa katika michezo. Uamuzi wake analitazama suala kwa mazingira yake na kutoa uamuzi pale pale.

Mara nyingine anakosea, mara nyingine anapatia, lakini ndio uamuzi. Sasa usisubiri kuna adhabu nyingi sana zinafuatia hapo, kasomeni kanuni, mtu anayedhani haya ni mzaha, kama utang'ang'ania basi ziko adhabu na adhabu zinakwenda hatma yake naweza kupendekeza kwenye Kamati mtu akafukuzwa katika uwakilishi huu tulionao. Yote haya yamo humu. Kwa hiyo, si mambo madogo.

Baada ya kusema hayo, naomba tu kuwakumbusha kuhusu mpangilio, wengine wanasahau wananiuliza mara kwa mara. Jumatano na Alhamisi, yaani kesho na kesho kutwa, tarehe 19 Julai, 2006 na 20 Julai, 2006 ni zamu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Halafu sasa zinafuata siku moja moja tu zile Wizara kwa mtiririko ufuatao, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, siku ya Ijumaa, Jumatatu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo tarehe 24 Julai, 2006, Jumanne tarehe 25 Julai, 2006 ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumatano tarehe 26 Julai, 2006 ni Wizara ya Usalama wa Raia na Alhamisi tarehe 27 Julai, 2006 ni Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mtiririko ili mjiandae. Wengine wanaanza kukosa nafasi, kwa sababu ukichangia mapema Wizara nyingi, basi utakosa nafasi kwenye Wizara ambayo pengine ulikusudia, kwa maana ya jimbo au uwakilishi wako ndio ulikusudia hiyo ndiyo nzuri kuisemea.

Sasa tunatazama kwenye rekodi, kama umekwishaongea mara nne, tunampa nafasi yule ambaye hajachangia. Kwa tahadhari hiyo basi, sasa naomba nitangaze kwamba, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza kabla ya kusitisha shuguli za Bunge pale saa 6.55, sasa tutaingia hatua ya kusikiliza majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini amepewa dakika ishirini na Mheshimiwa Waziri kama Mtoa Hoja amepewa dakika 40. Kwa hiyo, sasa namwita Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ikiwa mara yangu wa kwanza kuchangia hoja katika Bunge lako Tukufu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kwa kuwa Rais wa Tanzania wa Awamu ya Nne na pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumwezesha Mheshimiwa Rais kuniona na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mohammed Ali Shein kwa kuchaguliwa tena kwa mara ya pili kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngayai Lowassa, kwa kuchaguliwa tena kwa kura nyingi kwa kuwa Mbunge wa Monduli na hatimaye kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyotuongoza na kutuelekeza wakati wa utekelezaji wa majukumu yanayotukabili kwa kutumikia Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha kwa jinsi anavyoniongoza na anavyonielekeza katika utendaji kazi kwenye Wizara yetu ikizingatiwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kushika wadhifa nilionao.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu Athur Mwakapugi pamoja na Watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano wa karibu wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika, Mawaziri, Manaibu Waziri pamoja na Wabunge wenzangu wote wa Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi wa Tanzania kwa kupitia Majimbo yenu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wote kwa ushirikiano wa karibu mnaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu Bungeni na nje ya Bunge. Nielekeze shukrani zangu za pekee kwa wananchi wa Nyamagana ambao wameniwezesha kuingia katika Bunge lako Tukufu. Napenda kuwaeleza kuwa, niko nao, pamoja na kwamba namwomba Mungu anipe nguvu ili niwatumikie vyema.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumaliza salamu zangu za pongezi kwa kumshukuru mke wangu Stella kwa kunipa nguvu na kuniwezesha kuwatumikia wananchi wa Nyamagana pamoja na Taifa langu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ningependa kusema wazi kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na idadi kubwa ya Wabunge ambao wamechangia hoja hii. Nitajitahidi kujibu hoja moja moja kama ilivyoletwa. Kwa wale ambao tutashindwa kuwajibu, nitaomba wasubiri na watapokea majibu yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya ametoa hoja kwamba Serikali ione umuhimu wa kuendeleza nishati mbadala kama vile makaa ya mawe na gesi ya kupikia, mionzi ya jua, upepo na kadhalika. Hili linafanyiwa kazi na wadau mbalimbali. Majaribio ya matofali ya makaa ya mawe na utumiaji wa *LPG* kupikia unaendelea. Matumizi ya umeme nuru yanaendelezwa, utafiti wa upepo kuzalisha umeme unaendelea katika maeneo kadhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Missanga, ametoa hoja kwamba mradi wa *ERT* itachangia na kuleta ajira na kuhifadhi mazingira. Ni kweli mradi wa *ERT* utakapoanza, unatarajiwa kuchangia katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii na Mheshimiwa Job Ndugai, walichangia hoja kwamba, *Net Group Solution* wamekuja kuzoa na kubeba fedha na kwamba, baada ya kuondoka *TANESCO* iwezeshwe, wameuliza hatima ya *Net Group Solution* ni nini? Je, kuna maandalizi gani ya *management* mpya baada ya *Net Group* kuondoka na Serikali iwezeshe *TANESCO* ili iweze kuwekeza na kutatua matatizo Vijijini na Vijiji viwe na mita za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *Net Group Solution* ulikuwa na madhumuni ya kuimarisha *TANESCO* kifedha na kazi ilifanyika vizuri isipokuwa katika kipindi cha pili, Sekta ya Imeme ilikumbwa na matatizo mengi yasiyohusiana na na Mkataba wa *Net Group Solution*. Serikali imeliangalia Shirika upya na inaandaa mpango wa kuboresha *TANESCO* kifedha katika kipindi cha mwaka 2006/2007. *Net Group Solution* wataondoka *TANESCO* baada ya Mkataba wao kwisha tarehe 31 Desemba, 2006. Maandalizi ya kuandaa watalaam wazaleando kushika nafasi zao yameanza na yanaendelea. Hadi sasa nafasi ya Meneja Mkuu, Uzalishaji Umeme tayari imeshikwa na mzalendo.

Aidha, wataalam wazalendo wengine watatu wameteuliwa kushika nafasi za Naibu Meneja Wakuu, maeneo ya usafirishaji, usambazaji na huduma kama mpango mahsusi katika kuimarisha *Menegement* mpya. Serikali itaendelea kuwawezesha *TANESCO* kama kwenye Bajeti hii imetoa hela nyingi kuwawezesha kujenga miundombinu na kusambaza umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, ametoa hoja ya umeme kupelekwa Katoro, Rwangasi na Nyarugusu. Serikali itaangalia uwezekano wa kufikisha umeme katika maeneo yaliyotajwa. *TANESCO* itatuma Wataalam kuangalia njia ipi itafaa kupeleka umeme katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jackson Makwetta, ametoa hoja kwamba kuna hofu ya dunia kuhusu kwisha kwa vyanzo vya nishati visivyo yadidifu na mabadiliko ya hali ya hewa. Ipo haja ya kuendeleza vyanzo endelevu vya nishati kama vile maporomoko ya maji, upepo, mionzi ya jua, mabaki ya mimea na mbao. Amesema, tuache ku-*maintain status coal*. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendeleza vyanzo yadidifu vya matumizi bora ya nishati ikiwa ni pamoja na kuweka taratibu za kuendeleza *bio-fuel* na utumiaji wa mabaki ya mimea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ametoa hoja kuhusu *transformer* kuwekwa kwenye Sekondari ya Mkuyu na ameuliza, lini *TANESCO* itaanza mradi wa kupeleka umeme Songe. *TANESCO* itafuatiliwa kuweka *transformer* shuleni na mara fedha zitakapotolewa na Serikali *TANESCO* itaanza kazi ya kupeleka umeme Songe.

Mheshimiwa Spika, Eustace Katagira, ametoa hoja kwamba umeme upelekwe katika Vijiji vya Nkwenda, Kagete, Mlongo na kadhalika na hasa kwenye Shule za Sekondari, pia ameuliza kwamba, kwanini Kata zifuatazo hazimo katika Mpango wa Umeme Vijijini? Yaani Kamki na Kamora. Serikali pia itumie vyanzo vyake vya uzalishaji umeme na kuondokana na *IPP's*. *TANESCO* itatuma wataalam ili kutathmini upelekaji wa umeme katika Vijiji hivyo, yaani Nkweda, Kagete na Mrongo.

Aidha, mradi huo utajumuishwa kwenye awamu ya pili ya mradi wa *ERT*. Utekelezaji wa mpango wa *ERT* una awamu tano. Katika jedwali hili limeionyesha awamu ya kwanza tu. Hivyo, katika awamu nyingine, miradi hiyo mingine ile ya Kamki na Kamora ndiyo itajumuishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaangalia uwezekano wa kuimarisha *TANESCO* kuendesha shughuli za kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ili Taifa lisitegemee wageni tu. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kuboresha Mikataba iliyopo ili izingatie kikamilifu maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ameuliza, ni lini mradi wa Kagando, Kizerui, Mtii na Parani utakamilika? Pia amesema, kabla ya mradi mwingine kuanza, iliyotajwa hapo juu iwe imekamilika. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Malecela kwamba *TANESCO* itakamilisha kazi katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa William Ngeleja, ameuliza utekelezaji wa Mradi wa *ERT* umefikia wapi na ameuliza mradi kama utatekelezwa ameomba kwamba umeme upelekwe Nyamililo, Chifunfu, Katunguru, Kamanga na kwenye vinu vya kuchambulia pamba. Maandalizi ya kupanua upeo wa Mradi wa *ERT* kuongeza Vijiji vingi zaidi vinaendelea na awamu ya kwanza itaanza mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Sengerema ambalo ndio Jimbo la Mheshimiwa Ngeleja, Vijiji ambavyo vitapata umeme katika awamu ya kwanza ni Nyamililo, Nyampelela, Katunguru, Chamabanda, Nyamatongo, Karumo, Kamanga, Nyamahona, Chifunfu na Kijiweni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Kwaangw', ametoa hoja kwamba masahihisho ya Vijiji kwenye Jimbo lake vifanyike na umeme upelekwe Bonga Garapo, Halala na Nangari. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge umepokelewa na utafanyiwa kazi. Serikali kwa kutumia *TANESCO* ina njia mbalimbali ya kutekeleza Miradi ya Umeme Vijijini ukuwemo mradi wa *ERT*, Vijiji ambavyo havitakuwa kwenye mpango wa *ERT* vitaangaliwa jinsi ya kupatiwa umeme katika miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ametoa hoja kwamba kwa kuwa mradi wa umeme Vijijini *(ERT)*, ndiyo mkombozi wa nishati Vijijini, ni lini mradi huo utaanza? Hilo jibu tumeshatoa kwamba, utaanza katika kipindi cha mwaka 2006/2007.

Pia, ameuliza: Je, Mradi wa Umeme Vijijini utaanza katika Kanda gani au utaratibu gani utafuatwa ili uenee nchi nzima? Mradi wa *ERT* una sehemu mbili, Vijijini na Mijini.

Kwa kuanzia, miradi iliyoko kwenye Kanda ya Mashariki na Kaskazini, itatekelezwa kwanza. Ameuliza pia kwamba, tangu mwaka 1995, umeme Longido, Namanga bado ni ahadi, anaomba maelezo ili wananchi wa Wilaya ya Longido wajue ni lini watapata umeme. Ameomba tupeleke umeme Namanga kwa

kuwa upande wa Kenya una umeme. Serikali inatafuta fedha za kutekeleza mradi wa kupeleka umeme Longido na Namanga, fedha zikipatikana Mheshimiwa Mbunge ataarifiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma Said Omar, aliuliza kwamba, nchi yetu ina aina nyingi za madini. Je, madini haya yanasaidia vipi kukuza uchumi wa nchi yetu na hivyo kuweza kuboresha maisha ya Watanzania? Madini inachangia asilimia 3.5 ya *GDP* ya nchi. Mauzo ya nje ni zaidi ya asilimia 50.0. Inachangia katika kuboresha miundombinu na huduma za jamii katika maeneo ya machimbo na kadhalika. Pamoja na faida hizo, Serikali imeunda Kamati ya Kupitia Mikataba ya Madini ili kuweza kufaidika zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Binilith Mahenge, ametoa hoja kwamba Serikali itoe maelezo kuhusu uharibifu wa mazingira uliofanywa na Makampuni ya Utafiti wa Madini ya *platinum* kutoka Afrika Kusini katika Kijiji cha Ujuni. Pili, amesema wananchi hawafaidiki na mapato yanayopatikana na madini na tatu, Serikali haizishirikishi Mamlaka za Wilaya na wananchi wakati wawekezaji wakubwa wanapopewa leseni za utafutaji madini katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna Makampuni mawili ya utafutaji madini yaitwayo *Warthog Resources Limited* na *Tausi Minerals Company Limited,* Wizara italifuatalia kwa karibu eneo husika kubaini uharibidu uliofanywa na hatimaye kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanafaidika na mapato yanayotokana na madini kama nilivyoeleza awali na Sheria ya Madini inamtaka kwamba, mwenye leseni kubwa za utafiti wa madini kupata kibali cha maandishi kutoka mamlaka zinazohusika ikiwa ni pamoja na Vijiji mara wanapotaka kuanza kazi. Aidha, mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ya kusitisha uchimbaji wa madini, siyo muafaka kwa kipindi hiki kwa sababu Taifa linaweza kupata hasara.

Mheshiimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Kijiko ametoa hoja kwamba Wizara imepeleka watalaam Wilayani Kibondo ili kuangalia maeneo yenye madini, ili baada ya kuthibitika, hatua za haraka zichukuliwe kwa kuweza kuwapatia vijana ajira. Wizara yangu itafungua Ofisi ya Madini katika Manispaa ya Kigoma mwaka huu wa fedha 2006/2007 ambayo pia itahudumia Wilaya ya Kibondo, hivyo kuondoa matatizo yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa James Musalika ameuliza kwamba, katika Mikataba ya Madini, kipo kipengele kinachotaka wenye migodi kulipa Dola 200,000 kwa Halmashauri za Wilaya. Pesa hizo hazikulipwa kwa Halmashauri na Halmashauri hazikudai kwa kutokujua, kutokana na juhudi za Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Pesa hizo zimeanza kulipwa. Je, Halmshauri zitalipwa malimbikizo ya nyuma?

Mheshimiwa Spika, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mikataba ambayo tunaongelea hapa haikuwa na kipengele kilichotaka migodi ilipe Dola 200,000 kwa mwezi, kipengele ambacho baadhi ya Mikataba ilikuwa, malipo ya migodi kwa Halmashauri isizidi Dola 200,000. Kama tulivyoeleza awali, sasa hivi Mikataba inapitiwa na katika kupitia Mikataba, tunaangalia namna ya kuwezesha migodi kupata malimbikizo kama itawezekana. Lakini ifahamike kwamba hii yote itatokana na majadiliano ambayo yanaendelea na Makampuni ya migodi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gideon Cheyo ametoa hoja kwamba, mgodi wa makaa ya mawe ya Kiwira sehemu kubwa ipo Wilayani Ileje, hivyo Wilaya ya Ileje ishirikishwe kikamilifu katika utekelezaji wa mradi na kutoa mchango wake kwa Halmashauri ya Wilaya. Pia, malalamiko ya baadhi ya wafanyakazi wa Kiwira kuhusu mafao yao, tumepokea hoja. Serikali haina kipingamizi kwa Halmashauri kushirikiana na mgodi. Aidha, mgodi huu ulikuwa unamilikiwa na Serikali kabla ya kubinafsishwa, hivyo madai ya nyuma kwa kipindi hiki tunaomba Mheshimiwa Gideon Cheyo aje Wizarani tuyaangalie kama yatakuwepo. Serikali inatambua tatizo la wafanyakazi na inalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chiza ameuliza kwamba wachimbaji wadogo wanachimba madini kwa kubahatisha: Je, kuna utaratibu wa kuwapa elimu au taarifa, yaani *geological maps*? Pia ameuliza madini mbalimbali ambayo sio *traditional* yanapatikana wapi na soko lake liko wapi? Vilevile, ameuliza kwamba, Wizara inaweza kusaidia utaalam wa kuchimba madini ya chaki kwa wachimbaji wadogo na kutoa taarifa za Soko la Madini hayo? Mwisho, je, kuna uwezekano wa kusogeza mipaka ya

hifadhi ya Mayowosi ili kuruhusu wachimbaji wa madini ya chaki kufanya shughuli zao katika eneo hilo ili wananchi wajipatie ajira?

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikiwapatia huduma za ugani wachimbaji wadogo ili waweze kuchimba kwa ufanisi, zaidi taarifa yaani *geological maps* zinapatikana kwa malipo katika Kituo cha *GST* Dodoma. Baadhi ya maeneo katika Wilaya za Tanzania Bara yenye madini, zimo katika kitabu chenye taarifa ya jumla ya Sekta iliyoambatanishwa na hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Aidha, kuna *mineral currents maps* na vijarida vyake ambavyo vinapatikana *GST*. Ningependa tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kati ya kipindi cha mwaka 2006/2007, Shirika la *STAMICO* kwa ukaribu sana na wachimbaji wadogo wadogo na tungewaomba kwamba wavute subira ili tuangalie namna ya kuweza kushirikiana nao ili wapate taarifa watakayokuwa wanaihitaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gosbert Blandes, ametoa hoja kwamba mradi wa Kyerwa *tin* ambao ilishamiri katika miaka ya 1960, hadi 1970, umefungwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha machimbo haya yanafunguliwa? Pia, ametoa hoja kwamba inaaminika kwamba Wilaya ya Karagwe ina madini mengi: Je, madini gani yaliyopo Wilayani Karagwe na yapo katika maeneo gani?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafungua machimbo hayo ya bati kwa wachimbaji wadogo na leseni mbalimbali za uchimbaji na utafiti zimeshatolewa. Madini ya *Beryl*, *cassiterite*, *tungsten* na *wolfrimite* ni baadhi madini yanayopatikana Karagwe. Maelezo zaidi yanapatikana katika kitabu na vijarada vinavyopatikana *GST* Dodoma. *Mineral occurance map* ina taarifa kuhusu madini mengine yanayopatikana Karagwe na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Stephen Galinoma ametoa hoja kwamba uchimbaji wa dhahabu kwa kiwango kidogo kwenye Jimbo la Kalenga na anaomba wataalam kuchunguza. Tunamshukuru Mheshimiwa Galinoma kwa taarifa hii na tunamhakikishia kwamba wataalam watatumwa ili kuchunguza hii taarifa.

Mheshimiwa Spika, Job Ndugai ametoa hoja kwamba, ameomba kufahamishwa hatua zilizofikiwa katika upitiaji wa mikataba ya madini. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Ndugai kwamba, tumeshaanza kuzungumza na Wawekezaji kwa kupitia Tanzania *Chamber of Minerals* na hivi sasa tunavyoongea, Serikali iko katika majadiliano na baadhi ya Makampuni ili kuweza kurekebisha Mikataba ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Esther Nyawazwa ameomba kufahamishwa kupitia upya Mikataba ya Madini imefikia wapi na tumeshalijibu swali hilo na ameomba kufahamishwa mchango wa Halmashauri zenye madini hazijahusisha Wilaya ya Geita na Wawekezaji wa Geita ameomba kwamba wapande miti wasiache jangwa. Ni kweli kwamba migodi ambayo inachimbwa Geita haijalipa ile Dola 200,000, bado tuko katika majadiliano nao na tunaamini kabisa watalipa kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa wote kwa michango yao mizuri ambayo ni changamoto kwa Wizara yangu. Wapo waliochangia kwa kusema na wapo walichangia kwa maandishi. Naomba kuwatambua.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kusema ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dr. Christant Mzindakaya, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Omary Kwaangw', Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Abubakar Bakary, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Dora Mushi, Raynald Mrope, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa John Lwanji,

Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na mwisho Mheshimiwa Lawrence Masha - Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walichangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Diodorus Kamala, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Christopher Chiza. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa John Komba, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy na Mheshimiwa Abdallah Kigoda. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Mwajuma Khamis, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye nimemsahau ama kwa yule aliyechangia kwa kuongea au kwa maandishi, kwanza nimwombe radhi, pili naomba anikumbushe ile niweze kumtambua.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maeneo makuu yafuatayo, ambayo nadhani Wabunge wengi wamechangia na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye namshukuru sana kwa mchango wake hapa ni kwamba haitawezekana kutambua mchango wa kila Mheshimiwa Mbunge kwa kuzungumza hapa, lakini napenda niwahakikishie Wabunge kwamba michango yenu tunaithamini sana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, ni changamoto kubwa katika kuboresha utendaji wa Wizara ya Nishati na Madini, tutaifanyia kazi na tutahakikisha kwamba kabla Bunge hili halijaisha, basi Waheshimiwa Wabunge wawe wamepata nakala za majibu kwa maandishi katika kila maeneo ambayo wameelezea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwanza nitambue mchango mkubwa wa Kamati ya Biashara na uwekezaji, chini ya uongozi madhubuti na maarufu wa ndugu yangu Mheshimiwa William Shellukindo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli maoni ya Kamati hii ambayo ninaanza nayo, imekuwa kama vile yana mkusanyiko wa mambo mengi, lakini kama nilivyosema awali hata Waheshimiwa Wabunge wengine wamechangia.

Lakini kabla sijaja kwenye jambo moja moja, napenda nitoe utangulizi kwamba, katika miaka mingi iliyopita, Bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Nishati na Madini, ni Bajeti ambayo Serikali imetoa fedha nyingi sana kwenye Sekta ya Nishati na ndio maana Serikali imeweza kutangaza hapa kupeleka umeme katika maeneo ambayo kwa miaka mingi Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamikia kwamba hakuna umeme.

Tumeweza kupeleka umeme Kigoma, tumeanza kupeleka Mkoa wa Ruvuma, tutaweza kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya saba kwenye Vijiji vingi ambavyo vingine amevitaja Mheshimiwa Naibu Waziri na vingine tutawaarifu Waheshimiwa Wabunge kupitia mradi maalum wa *ERT*.

Haya yote yamewezekana kutokana na Serikali kutoa fedha nyingi sana kwenye Sekta ya Nishati na mimi nadhani kwa kasi hii ambayo Serikali yetu imeanza nayo, ni matumaini yangu kabisa kwamba tutakapofika miaka michache ijayo, suala la umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote itakuwa ni historia. Kukosa umeme itakuwa ni historia, suala la kukosa umeme kwenye Mikoa kama Kigoma na Ruvuma na maeneo mengine itakuwa pia ni historia. Kama nilivyosema mwanzo, suala la umeme wa Kusini, kwa kupitia mradi wa *Mnazi Bay* ambao tayari Serikali imeshauidhinisha ukosefu wa umeme kule itakuwa pia ni historia.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge waungane nami katika kuipongeza Serikali katika hatua yake kubwa kabisa hii iliyochukua, lakini sio kwa upande wa nishati tu, pia katika upande wa madini.

Serikali imechukua hatua madhubuti, baada ya uzoefu wa miaka kumi ya uwekezaji katika Sekta ya Madini, baada ya kusikiliza maoni na malalamiko mbalimbali na baada ya kuteua Tume mbalimbali na kufanya kazi ikiwemo Tume au Kamati ya Dr. Johnas Kipokola, Serikali chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, imeamua kwamba sasa ni wakati wa kupitia upya Mikataba hii ya Madini ili tuweze kunufaika na rasilimali. Kama nilivyosema jana wakati nawasilisha hotuba yangu hapa, suala ni kwamba sisi hatuna teknolojia na hatuna mtaji, lakini tuna madini. Wenzetu wana teknolojia na wana mtaji, lakini hawana madini. Lazima tukutane katikati, wao wanufaike kwa mitaji yao, lakini na Tanzania pia inufaike kwa rasilimali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, napenda nipitie maoni ya Kamati ya Biashara na Uwekezaji, na napenda niseme kwa kuanza kabisa kwamba Kamati hii, Wizara yangu na mimi mwenyewe binafsi tunaithamini sana, tunafanya kazi kwa karibu sana na mimi ni imani yangu kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa karibu sana. Kamati hii ina Wajumbe na Wabunge mashuhuri na maarufu sana na wenye uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo yametajwa katika Kamati hii, moja, ni *IPTL*.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwa ufupi kama ifuatavyo: Serikali imedhamiria kuchukua hatua mbili muhimu. Kwanza, kuhakikisha kwamba badala ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta, mitambo hii sasa izalishe kwa kutumia gesi na hii italeta unafuu kwa *TANESCO* kulipia fedha kidogo ambazo zinaitwa *Energy Charge* au malipo ya nishati hii bila ya kupata mzigo mkubwa inayoupata hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini, hatua nyingine ya pili ambayo ni muhimu zaidi, Serikali imeamua kwamba mitambo hii lazima tuinunue. Imeunda Kamati madhubuti na Kamati hii inaongozwa na Gavana wa Benki Kuu, Dr. Balali. Sasa, mimi nadhani ni hatua muhimu na sasa hivi wako katika hatua muhimu ya kuhakikisha kwamba masuala haya yote yanazingatiwa. Mambo mawili, kwenye upande wa mfumo wa urekebishaji, shughuli inaendelea na katika Bajeti ya mwaka huu wa 2006/2007, Serikali imetenga fedha na pia kwenye upande wa kununua pia Serikali imeanza hatua hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge na pia limezungumzwa kwenye maoni ya Kamati, ni suala la kutumia gesi asilia kwenye matumizi ya majumbani. Mimi nakubaliana kabisa na Kamati hii na maoni yake kwamba sasa wakati umefika na ndio mkakati wa Serikali.

Maonyesho mnayoyaona hapa ya *TPDC* Bungeni, ni matokeo ya ziara ya watumishi wa *TPDC*. Baadhi ya Wabunge walikuwemo katika ziara ile na watumishi wengine wa Umma na wananchi wengine ambao waliteuliwa kwenda China kwa ajili ya kutazama mfumo mzima wa utumiaji wa gesi asilia. Timu hii iliongozwa na mwananchi, raia wetu maarufu sana hapa nchini ambaye amewahi kuwa Mkuu wa

Majeshi, Generali Mstaafu Robert Mboma, ambaye ninaamini labda pengine yupo kwenye *Gallery*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliporudi wameweza kutufahamisha, siyo tu kwamba mpango wa kutumia gesi majumbani ni mpango ambao unawezekana sana, lakini ni kwamba tayari wameweza kupata na wawekezaji ambao sasa hivi tunavyozungumza, wako nchini kwa ajili ya kufanya tathmini ya namna ya kuweza kutumia gesi asilia kwa majumbani na kwa mambo mengine kama ambavyo imeonyeshwa kwenye maonyesho.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limetajwa katika maoni ya Kamati, ni suala zima la utafutaji wa mafuta kwa upande wa Zanzibar. Mimi nataka niseme kwa uchache tu, kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi, wameweka utaratibu wa kulizungumzia hili suala na sio jambo ambalo ni la ajabu. Hata katika familia, hata marafiki, hata Kampuni, mnaweza kukubaliana wote hatima ya jambo fulani, lakini mnaweza mkatofautiana namna ya kufikia ile hatima. Ni jambo la kawaida sana. Panapokuwa na suala kama la rasilimali kama mafuta au gesi na chochote, lazima watu muweze kukaa mjadiliane mwone namna gani mnaweza mkagawana, mnaweza mkatumia kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, lazima niseme kwamba sisi siyo peke yetu, duniani kote mahali ambapo kuna gesi, kuna mafuta, kuna madini, kuna rasilimali nyingine, masuala haya ya kukaa baina ya Majimbo na Majimbo, baina ya Majimbo na Serikali Kuu, baina ya Serikali na Serikali, ni masuala ya kawaida na ndivyo ambavyo sisi hapa tunafanya na nadhani tutafika wakati ambapo suala hili litakuwa limetatuliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la bei ya mafuta. Tumesikia sana kilio cha wananchi, kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu bei ya mafuta na imejionyesha hata katika maoni ya Kamati. Serikali iliondoa *VAT* kwa makusudi kabisa ili mtumiaji wa mafuta wa mwisho aweze kunufaika. Lakini, matokeo yake hayakuwa hivyo, kwa sababu wauzaji wa mafuta wameamua kutokufikisha kwa mtumiaji wa mwisho faida ile ambayo Serikali imetoa na wanasema ni kwa sababu ya Serikali kuweka kodi nyingine ambayo inaitwa *Exercise Duty*.

Mheshimiwa Spika, lakini nchi nyingine za Afrika Mashariki pia zina utaratibu wa aina hiyo. Ninachosema ni kwamba, Serikali imeona tatizo hili na palitarajiwa kama nilivyosema mwanzo pawe na unafuu kati ya Sh.50/= hadi Sh.80/= kwa kila lita kwenye bei ya reja reja. Unafuu huu haumfikii mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali imeamua yafutayo: Kwanza, inayataka Makampuni makubwa ya mafuta kuhakikisha kwamba wauzaji wa reja reja wanafikisha unafuu huu kwa mtumiaji wa mwisho.

Napenda niseme hili bila ya kigugumizi chochote kwamba, tutayachukulia hatua Makampuni yale ambayo yanashika nembo zao, hawafikishi unafuu huu kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Makampuni hapa imekuwa ni kawaida, kwamba, Serikali inapotoa punguzo la kodi au ushuru katika sekta fulani, lakini mwananchi wa kawaida hanufaiki na hatua hiyo. Sasa hatuwezi kukubali suala hili likaendelea kama lilivyo. Nimeshazungumza na baadhi ya Makampuni makubwa ikiwemo *BP*. *BP* kwa mfano wamenihakikishia kwamba wao wanafuatilia kwa wateja wao wa reja reja. Lakini napenda nitoe wito kwa Makampuni yote ya mafuta kwamba Serikali haitakaa kimya na utaratibu huu na tabia hiyo wanayoifanya. Lazima mwananchi wa mwisho aweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Serikali imeamua kuiruhusu *TPDC* kuingia katika uagizaji mafuta, kuleta mafuta kwa wingi nchini. Lazima pawe na ushindani na changamoto katika ushindani wa biashara ya mafuta na njia pekee ya kuleta changamoto hii ni kuleta Shirika la Serikali kama *TPDC* ambalo zamani lilikuwa linafanya kazi hii kwa ufundi kabisa, nayo iingie katika kuleta mafuta. Tatu, Serikali imeamua kupitia *TPDC*, kuanzisha *Strategic Oil Reserve,* yaani kuanzisha akiba ya mafuta nchini ili kuhakikisha kwamba pale panapotokea matatizo, basi nchi yetu iwe haina matatizo ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo limezungumzwa, ni suala la Mchuchuma. Napenda niseme kwa ufupi tu kama ambavyo nimesema wakati nimetembelea Ludewa kwamba, kulingana na Ilani

yetu ya Uchaguzi, wakati wa kutekeleza Mradi wa Mchuchuma ni sasa. Tafsiri ya sasa ni baina ya mwaka 2005 mpaka 2010.

Kama kuna mtu yeyote ana wasiwasi na hili au ana mashaka na hili, nasema akae chonjo angojee Serikali itakavyofanya. Lakini, tuna dhamira thabiti ya kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa na suala hili ni mtambuka, kwa hiyo, ni Wizara nyingi ambazo zinahusika na hivi karibuni Serikali itakaa na itatoa mwelekeo wa namna gani ya kushughulika na suala hili? Lakini, nawaomba wananchi wa Ludewa na Watanzania kwa ujumla na Waheshimiwa Wabunge waamini kwamba tuna nia thabiti na mipango thabiti ya kushughulikia suala zima hili la Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie suala la Mererani ambalo pia limetajwa na Kamati na pia Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka na pia Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara, pia amelizungumza na Waheshimiwa Wabunge wengine humu wamelizungumza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, nilitembelea mwezi Mei eneo hili baada ya maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mku. Tumekwenda, nikashirikiana na Mkuu wa Mkoa, tukafanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba Mererani panatulia, kuhakikisha kwamba uchimbaji wa *Tanzanite* Mererani unakwenda kwa utaratibu. Bado ipo kazi ya kuendelea kuifanya, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba matatizo ya Mererani ambayo yamekuwepo wakati hadi wakati na yamepitiwa na Kamati au Tume ambazo zimewahi kuteuliwa na Wizara.

Mapendekezo ya Tume zile Serikali imeyatumia katika kuhakikisha kwamba inaifanya Mererani kuwa eneo maalum au *Controlled Area* na kuweka taratibu nyingine za uchimbaji wa madini pale Mererani. Lakini, sio hivyo tu, wakati nimetembelea Mererani, palikuwa na maombi maalum na nilitoa ahadi ya kutenga eneo maalum kwa ajili ya wananchi waliokuwa wanachimba katika eneo ambalo linaitwa Machekecho ambalo tuliona ni hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, tayari nimeshaidhinisha eneo la kutengwa pale Mererani kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka anaweza kurudi Mererani kifua mbele na kesho tarehe 19 Julai, 2006 tunaweza tukampa uthibitisho wa ndani kabisa wa maeneo ambayo yametengwa. Kama kawaida, Kamati ambayo itashughulikia pale itakayokuwa chini ya Uongozi wa *DC*, itakaa itawagawia ndugu zetu wale ambao wanahitaji kupata maeneo ya kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Kamati ya Biashara na Uwekezaji, imezungumzia suala hili la Mererani, imezungumzia pia suala la *EPZ*, tunaunga mkono mia kwa mia maoni ya Kamati na ndiyo msimamo wa Serikali vile vile. Suala la kwamba sasa pasiingie mchimbaji mwingine mkubwa, tunakubaliana kabisa na Kamati, maana ndio msimamo wa Serikali huo. Kwanza pale Mererani hakuna nafasi kubwa sasa ya kuja mwekezaji mwingine mkubwa. Kwa hiyo, maeneo yaliyobaki pale Mererani yatabaki kwa ajili ya wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda niseme kwamba hizi ripoti za Tume mbalimbali ambazo zimefanyia kazi suala la Mererani ikiwemo hii ya mwisho ambayo iliongozwa na Jenerali Mboma, nitakukabidhi, ninayo hapa, lakini pia tutahakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wanapata nakala wiki hii hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lingine ambalo limetajwa na Kamati la la umuhimu wa kuwa na *Master Plan* ya umeme nchini, Waheshimiwa Wabunge mkitizama vitabu vya Bajeti mwaka huu wa 2006/2007, kipo kipengele cha Shilingi milioni 250, nadhani cha kuhakikisha kwamba kazi hii inafanyika. Ni jambo ambalo tumelipanga kulifanya. Lakini nataka niseme tu kwamba *Power System Master Plan*, siyo Msahafu, kwa sababu hii ni dira na panapotokea hali ambayo siyo ya kawaida, Serikali inachukua hatua wakati mwingine kuharakisha miradi hata ile ambayo pengine katika *Power Sytem Master Plan* imewekwa miaka ya mbele na ndivyo ambavyo tumefanya hivi sasa. Ndivyo ambavyo tumefanya kuhusu mradi wa Kinyerezi, ndivyo ambavyo tutafanya kuhusu mradi wa Mchuchuma.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba mlielewe hili suala kwamba *Power System Master Plan* itapitiwa upya ili iweze kuhakikisha kwamba inarasimisha haya ambayo tumeyaandaa sasa, lakini pia na kutoa mwono wa mbali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine limezungumzwa, lakini sasa hili halikuzungumzwa na Kamati, lilizungumzwa na Waziri Kivuli, ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa. Mimi nilikuwa na mategemeo makubwa sana kwamba Ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa labda atanipa mambo ambayo ni tofauti na Serikali ya CCM iliyoyayapanga, lakini katika yote aliyoyazungumza, naona yote alikuwa anapitia yale ambayo tayari CCM na Serikali yake inayafanya. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa kuelewa umuhimu huo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, amezungumzia habari ya mikataba, amezungumzia habari ya wachimbaji wadogo, amezungumzia habari ya bei ya mafuta, vyanzo vingi vya nishati, mambo ya Mchuchuma, haya ni mambo yote ambayo Serikali inayafanya katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Kwa hiyo, ndiyo maana namshukuru kwa yeye kutambua kwamba kwa kweli hatukuingia madarakani kwa kubahatisha, hatukupata asilimia 80 na zaidi kwa kubahatisha, hapa. Tumeingia madarakani kwa sababu wananchi wa nchi hii wamekiamini Chama chao na Serikali yao na ndiyo maana tunaweza tukatekeleza hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo ameyataja, ambalo nataka niligusie moja ni hili suala la *Net Group*. Anasema kwamba, *Net Group* inabadili *Power System Master Plan* na kadhalika. Nataka niseme hivi, mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba *Net Group* haina uwezo na wala haitakuwa na uwezo wa kubadili *Power System Master Plan*. Haina uwezo wa kubadili maamuzi ya Serikali. Uongozi wa Shirika lile unaweza ukatoa ushauri, lakini hawana uwezo wa kubadili chochote. Yanayofanywa yanafanywa kwa mujibu wa maamuzi thabiti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya hili, pia napenda nigusie suala moja ambalo amelizungumzia juu ya matamshi yangu kwamba nikizungumzia masuala ya utekelezaji wa miradi kama vile Mchuchuma na kadhalika na kwamba mambo haya nimesema wakati ni sasa. Nadhani nimeshatoa tafsiri ya maana ya wakati ni sasa. Wale ambao wamekuwa wakifuatilia ziara zangu, kila niliposema wakati ni sasa, nimetafsiri hivi hivi kwa maana kwamba ndivyo Ilani inavyotuambia mwaka 2005 na 2010 na hatutawaachia kwamba sisi tufike 2010 kabla hatujaanza utekelezaji wa miradi hii ili tuwape nafasi ya kuja kuisuta CCM na Serikali yake. Tutaitekeleza hii miradi na watakapofika mwaka 2010, watakuwa hawana hoja ya kuweza kuisuta. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja pia imezungumzwa na ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kuhusu bei ya mafuta, suala la *IPTL* na kadhalika. Nadhani nimetoa ufafanuzi juu masuala haya. Lakini, nitazungumzia suala moja: Mvua zinayesha, kwa nini kuna mgawo? Sasa, mimi namfahamu ndugu yangu, kaka yangu huyu, ni mwerevu sana, msomi mzuri, ninaamini anaelewa kwamba mvua zinaweza zikanyesha Kibaha, lakini zisinyeshe Mtera na kwenye *catchment area* yake. Kwa hiyo, mimi nadhani niishie hapo tu, kwamba ndugu yangu huyu anaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amezungumzia pia masuala ya ucheleweshwaji wa mradi wa Mchuchuma, akataja suala la *Seamens* na kadhalika. Nataka niseme kwamba, ni kweli hapo nyuma *Seamens* walijitokeza wakaja Wizarani, kwanza Baraza la Mawaziri lilifanya uamuzi, wakaja Wizarani, wakawa wanawasiliana na Wizara wakati hadi wakati kuhusu uwezekano wa kutafuta wateja zaidi, tukawaruhusu na kadhalika. Lakini, pakapita muda, *Seamens* wakawa hawaonekani.

Mheshimiwa Spika, sasa, nchi haiwezi ikamgonjea mtu aliyeingia Mkataba wa Makusudio *(Agreement of Intent)* mpaka atakapotaka yeye na ndiyo maana tukaamua kwamba ni vizuri tukaribishe na wengine wanaotaka kushughulikia mradi wa Mchuchuma. Sasa, *Seamens* wao wanayo nafasi kama walivyokuwa na nafasi watu wengine. Lakini wakati ukifika wataingia katika mchakato ambao mtu yeyote ataingia katika njia za uwazi za kuhakikisha kwamba anapatikana mwekezaji. Lakini, tusingeweza kukaa kusubiri *Seamens*.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezunguzwa ni suala ambalo amelizungumza ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Amezungumzia suala la kwa nini Serikali inatoa ruzuku kwa *IPTL*, Shilingi bilioni 18? Ninataka niseme kwamba, Serikali inatoa ruzuku kwa *TANESCO* ili kuweza kununua umeme *IPTL* na suala la *IPTL* kama nilivyosema, tumeshalizungumza. Kila mtu anakubali kwamba *IPTL* ni mzigo kwa Taifa. Hili jambo tunakubaliana sote kwamba ni mzigo na ndiyo maana Serikali imechukua hatua ambazo nimezisema hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tukumbuke, kwamba wakati mwingine mkiwa katika shida mnaweza mkajikuta mmeingia katika mazingira ambayo hamkuyataka na nadhani ndiyo *IPTL* ilivyokuwa. Sasa hivi inatusaidia kwa maana ya kwamba inatoa *Mega Watt 100* katika kipindi kigumu sana cha mgawo wa umeme. Lakini ni mazingira haya haya ndiyo yaliyosababisha tukaingia, tukafanya maamuzi ya haraka haraka miaka hiyo iliyopita, mpaka ikapatikana *IPTL*. Serikali imetambua kwamba *IPTL* ni mzigo na ndiyo maana inachukua njia hizo ambazo nimezizungumza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia pia suala la *TANSORT.* Niseme tu kwamba mapato ya *TANSORT* yanapelekwa Hazina na ndiyo maana sasa hivi *TANSORT* wanatengewa Bajeti kutoka nyumbani na kuna mambo mengi ambayo Kamati iliyokwenda London ilishauri, yametekelezwa na kama nilivyosema awali, jambo kubwa la msingi ni kwamba sasa Serikali imeamua kuirejesha nyumbani *TANSORT*, hiki kituo cha kuchambua Almasi kilichopo London ili tuwe na udhibiti nacho, ili tuwe na uhakika kwamba wanaweza wakafanya kazi kama inavyopasa na tuondoe gharama za kukiweka London. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, dada yangu na shemeji yangu, napenda niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imesikia na mimi nimesikia. Namwomba baada ya Bunge hili tufuatane kwenda Kilindi. Ninaamini kaka yangu Mzee William H. Shellukindo ataafiki hili kwamba tufuatane twende Kilindi tukashughulikie matatizo ya Umma, matatizo ya watu. Yale aliyoyasema kwa uchungu mkubwa nayaelewa na wale ndugu zetu waliokuja toka Kilindi tunawaambia kwamba warejee nyumbani na wawe imani kubwa na Serikali yao, kwamba utafika wakati tutakwenda, tutashughulikia yale matatizo kule kule Kilindi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, napenda kuongeza kwa Mheshimiwa Anna K. Malecela, aliyekuwa amezungumzia maeneo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri pia ameyagusia. Niseme tu kwa ufupi kwamba, kwanza mimi nakubaliana naye kifalsafa, maana amezungumzia masuala ya kuchimba sisi wenyewe madini. Kama hiyo itawezekana, ni jambo ambalo mimi sina ugomvi nalo kifalsafa.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka hasa, nizungumzie suala la miradi hii ambayo ameizungumzia na Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza. Miradi ambayo haijakamilika, niseme kwake yeye na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana miradi ya umeme ambayo haijakamilika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba katika mpango wa umeme Vijijini *(ERT),* tuanze kwanza na maeneo ambayo miradi yake imeanza na imesimama ili tuhakikishe kwamba tunaikamilisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, amezungumzia habari ya matatizo ya umeme wa Zambia. Ninakubaliana naye mia kwa kwa mia. Nimekuwa nikipokea taarifa hizi za matatizo ya umeme wa Zambia na tumewasiliana na Waziri mwenzangu wa Zambia, kutakuwa na Mkutano hivi karibuni Zambia kuhusu masuala ya umeme unaounganisha Zambia, Tanzania na Kenya na tumekubaliana kwamba wakati ule tuzungumzie na suala hili. Lakini pia Serikali itatizama njia nyingine za kuhakikisha kwamba tunaondokana na tatizo hili la umeme ambao sio wa uhakika, wa kukatikakatika sana, unaowatia katika majaribu ndugu zetu wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitambue mchango wa Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary. Ameniambia nirekebishe kauli yangu juu ya matumizi na faida wanayopata ndugu zetu wa Zanzibar kwenye gesi ya Songosongo. Mimi nataka niseme, kila swali linapoulizwa, kuna *angle* ambayo pengine unataka kuishughulikia. Wakati najibu swali hili, sehemu ambayo nilikuwa nataka niishughulikie, ni suala la ongezeko la uzalishaji *(Generation)* wa umeme. Ndiyo maana nikasema kwamba kwa kuwa Songosongo

ndio inachangia sana katika uzalishaji wa umeme na bila kuwa na umeme wa kutosha, Zanzibar haiwezi kuwa na umeme, kwa sababu umeme wake unatoka huku. Kwa maana hiyo, Zanzibar inanufaika na umeme ule. Sasa, natambua kwamba kuna masuala ya mapato. Suala la mapato ni suala lingine. Suala la mapato sikutaka kulishughulikia kwa sababu mbili. Moja, kuna Kamati ya Mheshimiwa William H. Shellukindo, Tume ya Muungano inayoshughulikia masuala haya, namna gani ya kuja kugawana. Nisingetaka kuingia katika eneo ambalo kazi yake haijakamilika na Serikali haijatoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, hata katika utaratibu huu niliousema wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi, pia wanashugulikia baadhi ya masuala haya. Kwa hiyo, wakati nazungumza, mimi nafahamu kabisa kwamba suala la mapato lina njia zake nyingine. Lakini, nilikuwa nazungumzia suala la *generation* ya umeme na namna gani *generation* hii basi inanufaisha Zanzibar. Sikuwa na maana ya kwenda kwenye maeneo mengine kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, amezungumza kwa uchungu sana juu ya miradi midogo midogo ya umeme na mimi namkubalia ni muhimu. Amezungumzia pia suala la umuhimu wa bomba la mafuta, namkubalia pia kwamba ni muhimu na hivi karibuni, leo kwa kweli ilikuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu asimamie Kikao cha Uwekezaji wa Kitaifa, Kamati ya Uwekezaji Kitaifa, lakini kutokana na kazi nyingi hatukuweza kukutana. Lakini ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu ataitisha Mkutano hivi karibuni na suala hili litazungumziwa.

Lakini, nataka niseme kwa ujumla kwamba msukumo wa Serikali mwaka huu umekuwa katika kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kigoma unafikishiwa umeme wa Gridi ya Taifa. Kazi ya kufikisha umeme wa Gridi ya Taifa inaanza. Ndiyo ulikuwa msukumo wenyewe. Katika kufanya kazi hiyo, maana yake pia na Wilaya zake pia zitapata umeme wa Gridi ya Taifa. Sasa, nafahamu umuhimu wa hii miradi midogo midogo *(Mini Hydros)*, hasa ndiyo suala lenyewe lilikuwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchango wa Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, amezungumzia suala la zebaki kwenye mito na kadhalika mpaka inatiririka kwenye Ziwa Victoria. Mimi ningemshauri ndugu yangu Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe kwamba, sisi tunajua kwamba kuna udhibiti wa kutosha katika masuala haya, lakini wakati mwingine ni vizuri tukatahadhari kidogo. Tunaweza tukatoa hofu kwa Jumuiya ya Kimataifa, tukahatarisha uchumi wetu. Lakini, kama ambavyo nimewahi kumjibu Mheshimiwa Mbunge siku moja hapa Bungeni, kwamba upo utaratibu mimi nafahamu, lakini pia nilikubali kwamba tutafuatilia kwa karibu ili tuhakikishe kwamba kama kuna wasiwasi wowote, pengine kwa kutokujua tu kama kuna utaratibu, basi pia tuuondoe. Kwa hiyo, tutafuatilia, lakini nataka niwahakikishie kila mtu anayehusika na suala hili kwamba Serikali ina utaratibu wa kutosha wa kuhakikisha kwamba hakuna athari kubwa kama hizo zinazoweza kuingia na kuathiri binadamu na viumbe wengine. Lakini kama nilivyosema, tutafuatilia pia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige amezungumzia na Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia masuala ya maeneo yao kuwa yote yanageuzwa kuwa mgodi. Hili ni tatizo na mimi nimeliona. Juzi Ijumaa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alituruhusu mimi, Waziri wa Maji na Waziri Mheshimiwa Stephen M. Wasira wa Mazingira Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya kwenda Buhemba. Sasa, Buhemba, baadhi ya matatizo tuliyoyaona ambayo Mheshimiwa Nimrod E. Mkono amekuwa akizungumzia ni kama haya.

Kwa hiyo, ninapenda niwaahidi, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo ya migodi kwamba, tutapita kwenye maeneo hayo ambayo yataonekana yana matatizo ili tuweze kwa pamoja na viongozi wa kule kutatua matatizo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kusema, kwa kweli haiwezekani tukajikuta kwamba wanageuza Wilaya nzima kuwa migodi kwa tafsiri kwamba kila mahali mwananchi anapotaka kugusa, hana mahali pa kugusa. Tutatazama utaratibu uliotumika na tuone namna gani tunaweza tukafanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Dr. Raphael B. Mwalyosi na mradi wa Mchuchuma, nadhani nimeshaongelea suala hili na kama nilivyosema ni suala ambalo linahusisha pia Wizara nyingine. Tunamsubiri Mheshimiwa Waziri wa Viwanda atakapokuja, basi suala hili litapata msukumo wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, naomba nitambue mchango wa Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, ndugu yangu, aliyoyasema yalikuwa ni ya uchungu sana. Ameyasema kwa unyenyekevu sana, kwa heshima kubwa kwangu. Mimi ni mtu mzima, nimemsikia, nimemwelewa. Namuahidi kwamba mimi na yeye tutafanya kazi bega kwa bega kwenye suala hili ili tuweze kutatua maeneo yake ambayo kama alivyosema, kwa kweli yamekuwa yakimsumbua kwa muda na kuna wakati hapa kama mwenyewe alivyosema alipata matatizo ambayo wote tunayajua na wakati mwingine alikuwa anadhani pengine tulikuwa tunamfahamisha labda kwa kutaka kutokumtia hofu. Hiyo inawezekana, lakini hasa kwa sababu na sisi pia tulikuwa tunatoa taarifa kwake.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunazipata hizi taarifa kutoka kwa Watendaji kwa matumaini kwamba fedha zingekuwepo. Sasa, kwa bahati mbaya kutokana na hali hii ya ukame wa miaka mitatu mfululizo, uwezo wa Shirika la Ugavi wa Umeme nchini, *TANESCO* na uwezo wa Serikali umekuwa ukielekezwa katika suala zima la uzalishaji wa umeme. Lakini, namwomba kama ambavyo amevuta subira kwa wakati wote, basi aendelee kuvuta subira. Lakini mimi namuahidi nitafanya naye kazi bega kwa bega ili tuhakikishe kwamba maeneo yake yanashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine alilitaja Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi ambalo wakati namtaja nililisahau, ni kuhusu Madinga, Kampuni ya Madini Madinga na amelizungumza kwa uchungu sana na amelizungumza kwa kuonyesha kwamba nchi yetu inaweza ikapata aibu na mimi nakubaliana naye. Namuahidi Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi na namwomba kwa kweli, kesho saa saba tukimaliza Bunge, tukutane, tupange kwenda kwenye eneo hili ambalo amelizungumzia ili tuifanye kazi ya kuhakikisha kwamba kama kuna matatizo yoyote ambayo yanaweza kushughulikiwa pale na mengine tuje tuyashughulikie wakati tukirudi. Lakini napenda nimuahidi kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimalizie kwa kuwatambua baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia. Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Anna K. Malecela kwa maandishi na Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwingine ambaye alichangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Nuru Awadhi Bafadhili na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirejee kwa kusema kwamba isingekuwa rahisi kumjibu kila Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli naomba radhi kwa hilo, lakini nawaahidi kwamba tutawajibu kwa maandishi mambo yote yale ambayo yamezungumzwa ama kwa kuongea hapa Bungeni au kwa maandishi yaliyoletwa kwenye Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza kwa makini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General* ... .... .... .... .... Sh. 1,921,866,200/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya awali. Niko kwenye *Vote* 58, *program* ya 10, *sub-vote* ya 1001, kifungu cha 250100 - mshahara wa rafiki yangu sana. Lakini asiwe na wasiwasi sina haja ya kuzuia Bajeti. Katika mchango wangu wa mdomo na hata wa maandishi na pia kwenye mchango wa Kambi yetu, tuli-*raise* mambo kadhaa ambayo Mheshimiwa Waziri au kwa kutokuwa na muda hakuyajibu au ameyajibu, lakini hakuingia kwa undani kwa sababu pia ya muda au vile vile ameweka siasa kidogo kwa sababu amesema ni Sera ya CCM. Sasa yoyote itakavyokuwa, mimi ningependa anipe maelezo ya kina kuhusu suala la Meremeta. Meremeta tunaihoji kwa sababu maalum. Tunahoji kutaka kujua taarifa kuhusu Meremeta kama tulivyouliza na kama ilivyo kwenye *paper* yetu, kwa sababu kwa muda mrefu Meremeta ni Kampuni iliyokuwa chini ya Jeshi letu la Wananchi. Taarifa tuliyonayo ni kwamba sasa ni Kampuni iliyosajiliwa tofauti na ilivyokuwa awali. Meremeta ni Kampuni ya wananchi, mali ya Watanzania, Kampuni iliyokuwa imekusudia kusaidia wachimbaji wadogo wadogo, Kampuni iliyokuwa inatakiwa isaidie shirika letu la Nyumbu. Maswali yote tuliyouliza, hakuna hata moja lililojibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa ambayo siyo sahihi kwamba, hata sasa ina-*operate off-show*. Sasa ni mambo ambayo Bunge hili linapaswa kujua. Watanzania tunapaswa kujua, ndiyo maana tulitaka taarifa ya kina kuhusu hilo. Kwa hiyo, yale yote tuliyohoji kuhusu Meremeta, ningependa Mheshimiwa Waziri, kwa ruhusa yako atujibu na hiyo ni pamoja na Kampuni ya *Mwananchi Gold Mines,* ambapo Serikali yetu kupitia *BOT* ina asilimia 20. Sisi tulitaka kujua hizi Kampuni kwanza ni za nani na kwenye Meremeta kama imeandikishwa sasa kama Kampuni: Je, sisi kama Serikali, tuna asilimia ngapi na *dividend* yetu ni ngapi na ina-*operate* mahali gani?

Kwa hiyo, haya ni maswali ya msingi ya kuyajibu. Mheshimiwa Waziri atambue kwamba tunapohoji haya tuna nia kwamba wabaki kwenye utawala mwaka 2010 kama alivyosema, lakini mwananchi daima anufaike kwa kuuliza kwetu. Ndiyo maana ya mfumo wa Vyama Vingi. Sisi tunauliza, mwananchi ananufaika, ukifanikiwa kutekeleza, utatawala. Lakini pia kwa makosa yako haya haya ambayo unayafumbufumba, tunaweza tukakuondoa mwaka 2010. Naomba majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali yanayohitaji ufafanuzi ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kama ifuatavyo: Meremeta kama alivyosema yeye mwenyewe, imekuwa ni Kampuni yetu. Ilianzishwa na moja ya sababu zake ni kusaidia wachimbaji wadogo wadogo. Ilipata matatizo kama ambavyo Kampuni nyingine yoyote inaweza ikapata matatizo. Sekta ya Madini ni Sekta ngumu, watu wanaweza wakaingia wakapata matatizo ya kutokupata faida na ndivyo ilivyokuwa. Baada ya hapo, Kampuni hii pia iliingia katika uchimbaji wa mgodi wa Buhemba, wakati wanashughulika. Lakini pia hawakufanya vizuri na kwa sababu hiyo, Kampuni hii sasa haijishughulishi na shughuli hizo na ndiyo ufafanuzi ambao naweza nikautoa na kwamba kwa upande wa shughuli za mgodi wa Buhemba, mgodi huo ni wa Serikali.

Kuhusu *Mwananchi Gold Mine,* hii ni Kampuni ambayo imeanzishwa na watu mbalimbali, ni kama vile *Public Private Partnership* kwa lengo la kutekeleza azma ya sera ya Serikali inayotokana na Chama cha Mapinduzi na siyo siasa. Kama ni siasa, ndiyo ukweli kwamba tufanye kazi ya kuongeza thamani ya madini yetu nchini kabla hayajasafirishwa nje. Sasa mnapokuwa na sera nzuri kama ambavyo ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Serikali kazi yake ni kushawishi Makampuni ya watu binafsi au Taasisi nyingine kuweza kuingia katika Sekta hii na ndivyo ambavyo imefanyika na kama ambavyo nimesema, kuna baadhi ya Taasisi zinahusika. Lakini kwa ufupi ni kwamba, ni mfano wa ushirikiano baina ya Sekta Binafsi kwa maana ya watu mbalimbali wa hapa nchini na pia na Taasisi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, naona hujaridhika.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na ninaweza kwenda baadaye kwenye kifungu cha 81 (2) (c) lakini kwa sasa niishie kwenye 81 (2) (b) kinachotakiwa ni maelezo zaidi. Suala mahsusi hapa ni: Je, Meremeta sasa hivi *status* yake ikoje? Kwamba, sisi tuliokuwa tumewekeza kwa kodi yetu , sasa hivi tuna nini kule kwamba: Je, ni Kampuni au ni *cooperation* ilivyokuwa na sasa je, iko nchini au iko *off-show* kama inavyosemekana na kama iko kule, fedha zetu zinalindwaje?

Waziri amemalizia kwa kusema uamuzi huo ni wa Serikali. Nataka kwa kifungu cha 63 (2) cha Katiba ya Jamhuri, Bunge lina wajibu gani basi kama hata kujua suala hilo linabakia kuwa siri ya Serikali? Kama ni siri ya Serikali, Bajeti inapoletwa hapa, ni kitu gani kinaletwa hapa na Wabunge hawa sisi tutakiwe kupitisha wakati unabaki kuwa ni uamuzi wa Serikali.? Mgawanyo wa madaraka uko wapi? Hili ndilo tunalosema na ndiyo sababu Mheshimiwa Waziri hakulijibu. Suala la pili, *Mwananchi Gold Mines* ni ya nani? Sisi tunajua tu kwamba tuna asilimia 20, hii asilimia 80 ni mali ya nani? Kama ni ya kwetu, ile sehemu ya kwetu sisi je, kama *management* yake tunaingiaje? Ndiyo maana tukataka kujua Bodi ya Wadhamini ni akina nani? Ni nini kinafichwa kwenye vitu hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Mitaani kuna maneno kwamba kuna sisi wakubwa tuko ndani, ndiyo maneno haya labda yanaogopwa kusemwa na nimetumia neno huko Mitaani. Sasa maneno ya Mitaani yataondoka tu iwapo Serikali itakuwa tayari kutimiza wajibu wake wa kutoa taarifa kwa Bunge kwa ibara ya 63 (2) yaani Bunge lenye kusimamia lijulishwe taarifa hii na Serikali haiwezi kusema daima kwamba hili ni jukumu lake. Tunajua jukumu lake, hakuna asiyejua. Tunajua kazi ya Serikali ni kutawala, hakuna asiyejua. Lakini kazi ya Bunge pia ni kusimamia. Sasa kama ni kusimamia, Wabunge hawa wote lazima tujue ili tuthibitishe kwamba tunapotoka hapa, posho zote tunazopata hapa ziwe zimefanya kazi kwa kusimamia mali ya wananchi ambao wana haki ya kujua kupitia kwetu yetu. Hawana njia nyingine ya kujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, usihangaike sana na Katiba, Katiba nailinda mimi hapa. Majibu lazima yatapatikana tu, sasa wewe unarukia kama vile hutajibiwa. Umeuliza masuala mahsusi upate majibu. Sasa unarukia Katiba na hivi kama Katiba inavunjwa, hakuna kitu cha namna hiyo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba Serikali haina inachoficha kwa maana ya kuwadhulumu wananchi au kufanya chochote. Nadhani ni vizuri pia tusiwapotoshe watu kama vile kuna jambo ambalo linafichwa, hapana. Isipokuwa na yeye Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba, mambo mengine haya baadhi ya ufafanuzi anaouhitaji unaweza ukahitaji muda wa kupata takwimu za kuzitoa na kuzieleza na kadhalika. Zinapokosekana, haina maana kwamba Serikali inaficha jambo hakuna inachoficha. *(Makofi)*

Sasa kwa ufupi, nataka niseme yafuatayo: Kwanza Meremeta amesema imeanzishwa *off-show,* hata mwanzo ndiyo ilivyokuwa na sasa iko katika *process* ya *winding up.* Kwa hiyo, kinachoendelea sasa ni katika mtiririko huo. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, suala la mwananchi, kama nilivyosema mwanzo, labda tukitumia maneno ya Kiingereza ni *(institution investor)* kama Kampuni kwa maana kama nilivyosema mwanzo ni mfano wa *public private partnership* katika kuhakikisha kwamba panakuwa na uongezaji wa thamani ya madini yetu. Kampuni ya aina hii inahitaji utalaam mkubwa na kwa ajili hiyo, watu wa Italia wana hisa kama asilimia 15 na mwananchi *trust* ambao ni Watanzania wana asilimia 45 ya hisa na kadhalika.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, hakuna kinachofichwa. Narudia tena, hakuna kinachofichwa. Kama Mheshimiwa Dr. Slaa atataka taarifa zaidi ambazo zinahitaji takwimu, tunaweza tukampatia baadaye. Lakini hakuna kinachofichwa.

**MWENYEKITI:** Sasa hadi hatua hiyo, kwa maana tu ya kujibu, majibu umepata. Ngoja nisimame. Majibu Mheshimiwa Dr. Slaa umekwishayapata. Yale ya takwimu yasitusumbue sana kwa sababu bado tupo hapa hadi tarehe 15 Agosti. Kwa hiyo, badala ya kuiweka Kamati mpaka ujibiwe kwa vitu ambavyo Serikali imeonyesha utayari wa kuleta takwimu zote kuhusu mwananchi. Nadhani ungeachia kifungu ili tuendelee na wengine watoe maoni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niko kwenye *vote 58 program* Na.10 *sub-vote* 1001, kifungu cha 250100 - Mshahara wa Waziri. Katika hotuba ya Mheshimiwa Mbunge wa Kambi ya Upinzani, kuna mambo ambayo tulitaka kuyajua na mojawapo ni la Kampuni ya

*Tanzanite One* ambayo imejisajili katika *stock market* ya *London*. Kambi ya Upinzani ilitaka kujua ni kwa nini haikujisajili katika soko letu la hisa hapa ili na Wanzania nao waweze kununua hisa hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwenye maelezo anayotaka kufahamu Mheshimiwa Grace Kiwelu kama ifuatavyo: Kampuni ya *Tanzanite One* iliomba kusajiliwa hapa nchini. Lakini kama unavyofahamu, kila nchi na Taasisi zake zina taratibu, waliotaka wasajiliwe ili wauze hisa zina taratibu zake.

Kwa mujibu wa *capital market, authority* yetu ilionekana wakati ule kwamba Kampuni hii ilikuwa bado haijafikia uwezo wa kujisajili bila ya kuwepo na tishio kwamba inaweza ikapata hasara. Nadhani pengine inatokana na uzoefu kwamba hatuna uzoefu kwenye uandikishaji wa Makampuni yanayoshughulika na madini. Sasa uoga huo na kutokutumizwa kwa masharti yaliyowekwa, aina hiyo ndiyo imefanya hiyo Kampuni ikajisajili nje. Lakini mimi naamini kwamba hapo baadaye inawezekana kabisa Kampuni hii na Kampuni nyingine zikajiandikisha hapa nchini.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nilitaka kushika kidogo hela ya Mheshimiwa Waziri kwenye kifungu cha *vote* 58 *program* Na.10 *sub-vote* 1001 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli nilitaka ufafanuzi tu kuhusiana na migodi ya Ludewa, amenipa ufafanuzi mzuri kwamba jinsi alivyowaahidi wananchi wa Ludewa alipokwenda kule kwamba miradi ile miwili itaanza kushughulikiwa katika kipindi hiki na kuanzia leo mpaka 2010 amenieleza hilo nimeridhika na wao huko waliko wameridhika. Lakini kabla sijaachia senti zilizobaki, nilitaka ufafanuzi katika vitu viwili vidogo.

Moja, niliuliza kitendo cha kuunda Kamati kushughulikia rasilimali za Ludewa bila kuwahusisha wananchi wa Ludewa, nilitaka ufafanuzi kwamba, kwa nini wananchi hatuhusishwi na hata mwakilishi wao hahusishwi?

La pili, kwa vile kulikuwa na Mikataba kati ya *NDC* na Vijiji vile kuhusu ardhi ile na mikataba ilikwisha mwaka 2003 na wananchi hawa hawajalipwa fidia na masuala ya fidia yanachukua muda mrefu: Je, Waziri anasemaje kuhusu suala zima la fidia kama tutaingia tena mkataba au tutaanza sasa kushughulikia fidia za wananchi kwenye maeneo yale? Naomba kupata maelezo katika hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe ufafanuzi ndugu yangu Profesa Mwalyosi kama ifuatavyo: Nadhani Kamati anayozungumzia, inawezekana ni Kamati ambayo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ameiunda ambayo inachukua watalaam kutoka Wizara mbalimbali. Kama ni hiyo, mimi sioni tatizo kumwomba MheshimiwaWaziri mwenzangu uwe *observer* uone kinachoendelea maana siyo tatizo, kwa sababu hakuna kinachofichwa.

Mimi nadhani nia ya Mheshimiwa Mbunge ni njema kwamba anataka aelewe kinachoendelea kwa ajili ya kuwafahamisha wananchi wa Ludewa. Tulishafanya hivyo kwa mradi wa *Mnazi Bay* wakati wa majadiliano kulikuwa na wasiwasi mkubwa na mimi nilimteua Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kuwa *observers*. Kwa maana hiyo, mimi nadhani hakuna ubaya, utatusaidia pia katika kupeleka taarifa kwenye Jimbo na Wilaya yake ya Ludewa.

Kuhusu fidia, nadhani Mheshimiwa Mwalyosi tuonane tu kuanzia kesho ili tushughulikie hilo. Fidia ni muhimu, wananchi wetu wanapokuwa wamechukuliwa mali zao, fidia ni muhimu na ndiyo sera ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Susan Lyim*o.*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Wakati nikichangia kwa maandishi na vile vile kwenye Kambi ya Upinzani tulikuwa tumetoa hoja kuhusu *IPTL*, nashukuru Mheshimiwa Waziri ameijibu, lakini bado tulikuwa tunahoji, kwa sababu Waziri amekiri kwamba Serikali imeona *IPTL* ni mzigo, sasa nilikuwa naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri: Ni lini

Serikali imelitambua hilo na ni lini Serikali itatoa tamko rasmi la kuinunua *IPTL* ili kupunguza gharama za umeme kwa wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuiona *IPTL* kama mzigo ilionekana zamani tu karibu miaka kumi iliyopita na ndiyo maana Serikali ilichukua hatua ya kwenda kwenye Mahakama ya Kimataifa, inayohusika na usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji. Lakini la pili, kuhusu tamko tumekuwa tukisema mara nyingi tu kwamba *IPTL* ni tatizo. Kama mashine ni nzuri sana, lakini ule mfumo wake ndiyo mbaya kwa maana ya kuwa na *capacity charge* kubwa na *energy charge* kubwa na ndio maana mtazamo wa Serikali katika suala hili ni kubadilisha mfumo wa uzalishaji umeme na pia kuinunua.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunikumbuka. Programu Na. 10, *sub-vote* 1001, kifungu kidogo cha 250100 - Mshahara wa Waziri. Wakati nikizungumza kwa mdomo, nilitoa mapendekezo mengi, sitaki kuyasema yote, nataka niseme tu mawili yafuatayo: La kwanza, tangu migodi hii ya dhahabu imeanza, Serikali hajaiweka udhibiti wa kutosha katika kuhakikisha usalama na uhalali wa kile kinachosafirishwa na kile kinachoripotiwa.

Makampuni haya yote ya madini yanafunga mizigo yenyewe, yanasafirisha yenyewe. Makampuni hayo tangu yameanza kuchimba, wanapofunga mzigo wakiwa peke yao, hakuna mwakilishi wa Serikali pale kuhakikisha kilichofungwa ni kiasi gani na hata wakati wa kusafirisha wanasafirisha wakiwa peke yao wakati wa kupokea ndiyo inakuwa *agency* ya Serikali ambayo imekodiwa ambayo nilisema jana ni Kampuni ya Wazungu.

Mimi nilitoa maoni kwamba, kwa nini isiwepo Kampuni ya Serikali kama *TRA* kuhakikisha kwamba, kuanzia ufungaji, upakiaji, usafirishaji na mapokezi kule yanakopelekwa ili kudhibiti kile kilichopokelewa ni kiasi gani na hata mauzo ni kiasi gani? *(Makofi)*

Nikapendekeza kwamba *TRA* inaweza ikafanya hii kazi kuliko kuazima mtu wa nje ambaye anaweza akaelewana nao kwa sababu wote ni wafanyabiashara. Kinachotokea sasa hivi, tunategemea kupata *return* kutoka kwa wachimbaji hawa, wamesafirisha hivi, wameuza hivi, kwa bei hii ndiyo tunachukua *royalty* au kodi yote ambayo tunaipata. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hili kama Serikali inakubali iweze kuweka *TRA* kwa ajili ya kusimamia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri kwa juhudi zao baada ya kuingia Awamu ya Nne kuona kwamba, sehemu ambazo wanachimba dhahabu waweze kulipwa Dola laki mbili. Nawapongeza sana kwa juhudi hizo. Wananchi wa sehemu hizo wanasema, kweli Serikali ina masikio mengi kama chandarua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nzega ni sehemu ambayo ina migodi ya dhahabu, ndio wa kwanza kuanza. Nzega imekuwa ni sehemu ya majaribio, hata kwa migodi mingine. Nimesema jana kwamba Nzega imerudi nyuma kibiashara kutokana na wachimbaji hawa kununua hata bidhaa nyingine kutoka nchi za nje hata nyanya. Sasa wachimbaji hawa, Nzega wamekuwa wana kigugumizi kikubwa sana kwa kulipa kodi, wengine wote wamelipa kodi isipokuwa hawa wa Nzega.

Sasa jana nilizungumza nikasema, kwa nini hawa wa Nzega wasichukuliwe hatua kuhakikisha kwamba wamelipa na wamelipa *areas* na hizo *areas* kwa sababu wamekuwa na kigugumizi cha ubishi, basi walipe na *interest* ili hizo fedha zirudi kwa wananchi kwa ajili ya kuleta maendeleo. Sasa sikupata maelezo mazuri ya Wizara. Nilikuwa napenda nipate majibu ya usahihi juu ya haya mambo mawili.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi anaoutaka Mheshimiwa Selelii, kama ifuatavyo: Kwanza, kuhusu mapendekezo yake, napenda nimhakikishie kwamba mapendekezo mengi aliyoyatoa kama nilivyosema wakati najibu maswali wakati nachangia ni kwamba tumeyahifadhi tutayafanyia kazi kiujumla kwanza. Lakini pili hili la ufungaji wa madini kwanza sheria ya madini hairuhusu kwamba mchimba madini ajifungie tu mwenyewe asafirishe tu pasiwe na uthibiti wa aina yoyote.

Kwa hiyo, kumekuwa kunatokea nini? Siku zote pamekuwa na Maafisa *at least* wawili, mmoja wa *TRA* na mmoja Afisa Madini kushuhudia kwamba shughuli inayofanywa ndiyo ilivyo kama ambavyo imefungwa na *TRA* wanaweka siri. Lakini basi, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge yeye anasema kwamba haifanyiki hivyo, mimi nitashukuru akitupa mfano ili tuweze kufuatilia, maana hii ni nchi yetu wote, kama yeye ana uhakika kwamba pamoja na taratibu nzuri zilizopo, lakini kazi hii haifanyiki. Atupe mfano na mimi nitachukua hatua mara moja. Hilo la kwanza.

Lakini la pili ni kwamba, Serikali imekwenda mpaka kuhakikisha inachukua Kampuni ya Ukaguzi kuhakikisha kwamba hatuibiwi na Kampuni hii imekuwa ikifanya kazi ya kujaribu kuthibitisha uzalishaji na mambo mengine yanayohusu migodi.

La tatu, kuhusu Kampuni ya Nzega, mimi nakubaliana nayo kwamba, wale watu wa Nzega, Kampuni ile ya Madini haikutoa ushirikiano mzuri wakati tunajadiliana nao kama wakati nahutubia Bunge jana, nilisema kwamba, kabla ya majadiliano haya yaliyoanza sasa tulikuwa na majadiliano *talks before talks* katika kipindi hicho, hawakuonyesha ushirikiano mkubwa lakini na sisi tulihakikisha kwamba Kampuni ile inaweka *commitment* ya kulipa na wameahidi wataanza kulipa kuanzia mwezi Septemba, kwa Wilaya ya Nzega wao pengine wanaweza wakapata zaidi ya Dola laki mbili kwa sababu katika mkataba ule ile, *formula* inayotumika kwao ni tofauti na Wilaya nyingine.

Sasa na hili tunashughulika pia na Mheshimiwa Waziri mwenzangu Pinda wa TAMISEMI kutazama kama hizo *areas* za nyuma ni vipi na tuweze kushughulika nao ili ziweze kulipwa. Sasa napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii inafanya kazi kwenye suala hili na ndiyo maana tangu mwanzo nimesema kwamba tutahakikisha kwamba kile kilicho chetu, basi tukipata. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu nami nimwulize Mheshimiwa Waziri, kifungu 58 *program* 10 *sub-vote* 1001 kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri. Kwanza, nianze na kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuahidi kwamba atapeleka watu wa *TANESCO* waende Nyarugusu, Lwamgasa na Bukoli kuangalia ni jinsi gani waweke umeme.

Pamoja na shukurani hizo, napenda anifahamishe Mheshimiwa Waziri, wakati wa kuchangia nilieleza kilio cha wananchi wa Lwamgasa, Katolo na Nyarugusi, eneo hili ni eneo karibu Kata tatu zimechukuliwa na Kampuni ya *East Africa Mine* ambayo sasa inaitwa *I am Gold* na kulikuwa na wachimbaji wadogo na wakulima.

Sasa kuna migogoro mikubwa, wanagongana sana. Sasa wakawa wameomba kwamba maeneo ambayo haitafanyiwa kazi kwa kuwa imekaa muda mrefu, basi wapewe wao waendelee na kufanya shughuli ya uchimbaji au wengine kuendeleza shughuli zao, lakini kwa sababu kuna mahali pengine, inaonekana migongano mikubwa sana. Kila siku ni kesi na *DC* anaingilia huko, lakini uamuzi bado haujapatikana.

Lingine limezungumzwa, lakini ni tofauti kidogo. Watumishi wa Meremeta wamekaa sasa hivi, ni kama ina-*wind-up* lakini wamekaa karibu miaka miwili hawalipwi, wanaishi kwa shida sana. Nilianza kumwona Kamishna aliyekuwepo akaniambia, sasa hivi nimepelekwa Jeshini, nikaenda kumwona Katibu Mkuu - Wizara ya Ulinzi.

Katibu Mkuu alinipa muda, nikarudi tena, akaniambia fedha zao karibu zinatafutwa, lakini ikaonekana kuna ugumu. Nikamwandikia Gavana, akanijibu kwa kinoti akaniambia fedha zao zimepatikana. Sasa hivi ni karibu mwezi wa sita hawa watu hawajalipwa na inaonekana maisha yao ni magumu sana, sijui hatima yao itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililolizungumzia ni kuhusu Dola. Bahati nzuri amejibu, lakini nilikuwa napenda wakati anafuatilia suala la Dola 200, sisi mgodi wa Geita nadhani haujalipwa na katika ukurasa wa 24 haikuweza kuelezwa. Hazijalipwa hizo Dola 200, tatizo ni nini? Kwa sababu wapo na utaratibu huo umefuatwa, sasa ni kiburi au ni nini? Naomba tueleweshwe.

La pili, nilikuwa nimezungumzia juu ya *human resources* nikauliza ya kwamba, ni vyema kwa sababu kuna leseni nyingi hazijasainiwa na Kamishna kwa sababu ya kukosa Kamishna. Ningeomba liimarishwe hili, lakini nikashauri kwamba baadhi ya watumishi ambao kwenye migodi tunadhani wanaweza waka-*replace* mara moja kama nilivyokwenda Nyamongo tukakuta walinzi na tunajua Wakurya ni walinzi wazuri sana. Basi, waondoke waende wakafanye kazi. Ni hayo tu Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Nikumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, utamaduni wa Kamati hii siyo tena kurudia yote mtu uliyosema. Unalenga kwenye jambo mahsusi, lakini ukikumbushia kwenye mambo manne, matano inakuwa tena tunarejea kwenye mjadala wa ile hoja ambayo siyo kazi ya Kamati hii. Nadhani baada ya Mheshimiwa Rwilomba, atakayefuata kama atakuwa na mambo matano sijui mangapi, basi nasikitika itabidi nimzuie kwa sababu ni kinyume cha utaratibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe ufafanuzi Mheshimiwa Rwilomba, kama ifuatavyo:-

Haya maeneo ambayo ameyataja wakati anahutubia, nimkumbushe juu ya safari aliyonipeleka yeye Kobote, Lwangasa, Katoro, Nyarugusu na kadhalika. Nadhani ni maeneo ambayo amesema kwamba watu wanataka maeneo ya kufanyia kazi. Kuna utaratibu hata wale wanaoshika maeneo ya kuyaachia wakati hadi wakati. Ni eneo ambalo pengine halisimamiwi vizuri sana. Mimi nataka nimwahidi kwamba, nitashirikiana naye tuone namna gani watu wa maeneo haya wanaweza kwa kutumia utaratibu huu wa kisheria wanaweza wakapata haya maeneo ya kufanyia kazi. Hilo la kwanza.

La pili kuhusu fidia ya watu wa MEREMETA, nimewaahidi tu kwamba, hili suala Serikali inalishughulikia hivi sasa. Atakumbuka Mheshimiwa Rwilomba kwamba hata Mgodi wa Geita, miaka michache iliyopita palikuwa na matatizo, mgodi ulitoa fidia lakini fidia zile zikachapwa na baadaye Serikali ikaamua kuondoa kero ikatoa fedha kwa ajili ya wananchi wale. Kwa hiyo, kama nilivyosema awali, suala la fidia Serikali inalitazama kwa umakini sana. Kwa hiyo, tutalishughulikia.

Kuhusu mgodi wa Geita, anauliza kwamba ni kiburi au ni nini. Jibu ni kwamba wana kiburi, lakini tutawashughulikia. Ndiyo! Tumewaambia hivyo na nadhani wataelewa. Suala la Kamishna linashughulikiwa, naamini baada ya muda sio mrefu sana tutapata Kamishna. Suala la wafanyakazi wa migodi wazalendo, ni moja ya mambo ambayo hata katika majadiliano haya tunataka tuhakikishe kwamba kila mgodi una utaratibu wa kuhakikisha kwamba *quoter* ya wananchi wanaofanya kazi pale inaongezeka na katika maeneo ambayo yanahitaji utaalam, lazima tuhakikishe kwamba Watanzania wanapata nafasi ya kufanya kazi kwenye migodi iliyoko katika nchi yao.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Ni kuhusu suala la hawa watumishi wa MEREMETA. Ni kwamba, wao hawalipwi mishahara, wamekaa tu pale. Lakini nilipomwona Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Gavana wa Benki, walisema kwamba fedha zao zipo. Nafikiri suala ni kuwapelekea fedha zao.

Nakubaliana na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Katika hilo, basi wahimizwe wapelekewe, kwa sababu wanaendelea kupata taabu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kutumia *Vote 58,* Programu ya 10, na *Sub-Vote 1001* na kifungu kidogo kabisa cha 250100. Nilikuwa napenda kufahamishwa mambo mawili kama nilivyochangia kwa maandishi. Kwanza ningependa kufahamu, lakini pia wananchi wafahamu kuhusu Kampuni ya *Kabanga Knikel* iliyokaa katika *site ile* kwa muda mrefu sana, wakitafuta madini hayo ya *Knikel,* je, ni lini watafanya kazi tuone madini yanachimbwa ili wananchi nao waweze kufaidi kwa namna moja au nyingine?

Lakini la pili, nilikuwa naomba kufahamu ni lini Serikali itashughulikia uzalishaji wa umeme kwa kutumia maporomoko ya Rusumo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo mawili tu nilikuwa napenda kufahamu.

**MWENYEKITI:** Wewe ulichangia kwenye maandishi. Maana yake hatua hii jamani ni kuomba ufafanuzi. Sio kuanza hoja mpya. Ulichangia?

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Nilichangia!

**MWENYEKITI:** Ahaa! Ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Batenga, kama ifuatavyo:-

Kampuni ya Kabanga hapa katikati kidogo imekuwa ikipata wabia tofauti na nadhani kwa sababu unapoingia mbia, panakuwa na majadiliano, inachukua muda na hiyo pia imechukua pia sehemu ya muda ya kuchelewesha kazi ya *exploration* ambayo walikuwa wanaendelea nayo. Kulikuwa na Kampuni ambayo imeingia sasa hivi *Falcon Bridge* ya Canada, halafu na pia ya Bariki ya Canada, lakini naambiwa inawezekana pia kuna mbia mwingine anataka aingie.

Tunafuatilia kwa karibu. Wote tuna maslahi na uanzishwaji wa kuchimba madini haya ya *nickel* haraka na wao wenyewe nimekwisha kuwa na majadiliano nao kama mara mbili na viongozi wa juu wa Kampuni hii wamekuwa wakipanga mipango yao vizuri. Nadhani tutakapokuwa tayari, basi tutatoa taarifa. Lakini kwa sasa siwezi kusema kwamba wanaweza kuanza kuchimba kesho au keshokutwa.

Kuhusu maporomoko ya mto Rusumo, nchi zetu tatu za Burundi, Rwanda na Tanzania, tumeshafikia makubaliano na sasa hivi tunatafuta fedha za kuhakikisha kwamba umeme kupitia maporomoko ya Mto Rusumo ambayo ni *MW 60* unazalishwa. Sisi tunautazama mradi huu kuwa ni muhimu kwa sababu ya kuimarisha hata kama tunapeleka umeme kwa *grid,* lakini ukiwa na umeme unaotokea kule, kunakuwa na *stabilizing effect* kwenye *grid,* yaani inaimarisha *grid* kwa upande ule kule. Kwa hiyo, ni mradi ambao tunaufuatilia kwa karibu.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 10 *Administration, sub-vote 1001 – Administration and General* kifungu kidogo cha 250100. Ni suala la kuweka kumbukumbu sawa. Nilipokuwa nachangia, niliomba kwamba kwenye kitabu cha taarifa ya jumla kuhusu Sekta ya Nishati na Madini kwamba, Vijiji vilivyoandikwa havipo kwenye Jimbo langu. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba tayari wamekwisharekebisha.

Lakini wakati sasa Mheshimiwa Waziri anajibu hoja, kwa bahati mbaya nadhani ametamka Kijiji cha Galapo kwamba mimi nimesema ninakiombea umeme. Kijiji kile nilikitolea mfano tu, kama Kijiji kilichofanikiwa vizuri sana baada ya kupata umeme. Nilisema kwamba, Kijiji ambacho kipo karibu na Galapo, sasa kwenye *Hansard* nina hakika itaonekana kwamba nimeomba na Galapo ipatiwe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu rekodi iwekwe vizuri kwamba siyo kijiji cha Galapo. Kwa vijiji vingine ambavyo amevitaja, ufafanuzi zaidi nina hakika nitaupata kwenye majibu ya Wizara kwenye swali langu la tarehe 14 mwezi wa nane, 2006. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tutalisubiri hilo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niko programu ya 10 *Sub-Vote 1001, 250100,* nilisikia majibu ya Waziri kuhusu umeme katika Mji wa Namanga. Lakini nilipenda kujua kwa sababu mimi tangu niingie Bunge hili mwaka 1995, umeme Namanga ilikuwa ni ahadi tangu wakati ule nadhani Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mkapa alipoingia madarakani mara ya kwanza aliahidi umeme Namanga. Hivi umeme Namanga haina muda? Ni ahadi tu kila wakati? *(Kicheko)*

Hiyo ni moja, inakuwa tu toka wakati huo napata majibu yale yale na mwaka 2005 nilikataa kuunga mkono Bajeti hii na nilisema iandikwe kabisa kwamba Mbunge wa Loliondo amekataa. Imekuwa ni ahadi toka mwaka 1995 hadi sasa. Napenda kuuliza, hivi kwa nini mnaweka katika ahadi, kama haupo utaratibu wa kupeleka umeme Longido?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliandika kwenye mchango wangu, tuna mgodi ulioko Longido*,* *ruby* nzuri kabisa Afrika inatoka Longido, Tanzania. Lakini Serikali inaona huo mgodi ni kama haupo, wameusahau kabisa na kila mwaka wanavuna, Serikali haitambui, wenyewe hawafahamu hata wako katika Halmashauri ipi, hawajui hata Kijiji wanachokaa, hakuna uhusiano na Halmashauri, hakuna uhusiano wa Vijiji, ni wavunaji tu kila wakati. Hivyo, nataka kuuliza, huo mgodi ni kwamba Serikali haitambui wala haitaki, *royalty* kutokana na *ruby* au *ruby* siyo madini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuuliza kwa sababu hawakujibu kwenye hoja. Nilisubiri sana nisikie, lakini hawakujibu. Sasa nataka majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naona umeziweka vizuri tu karatasi zako. Kwa nini Namanga haina umeme mpaka sasa na ni ahadi ya miaka 10 na kuna Kijiji kinavunwa *ruby* pale na watu, Wizara haina udhibiti wowote? Nilikuwa nakusaidia tu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunisaidia kunikumbushia maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe ufafanuzi ndugu yangu Mheshimiwa Lekule Laizer kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, kwa muda mrefu amekuwa akizungumzia umeme wa Namanga. Ni kweli kabisa! Tatizo ni kwamba, tunapotoa ahadi, sio kwamba tunatoa kwa maana ya kuongopa, hapana. Tunatoa kwa matarajio kwamba mipango ipo ya kupata fedha. Lakini wakati mwingine fedha hizo zinakuwa hazipatikani. Isipokuwa mimi naamini kwamba kila wakati tunampa majibu ya aina hii, pengine itakuwa ni mara ya mwisho. Kwa hiyo, namwomba pamoja na kusubiri sana kwa muda mrefu, namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Lekule Laizer anikubalie kwamba nitalifuatilia suala hili kwa makini tufikie mwisho wapate umeme.

Kuhusu taarifa ambazo amezitoa za mgodi huu wa *Ruby* na kama mambo ndivyo anavyoyasema kwa sababu kwa taarifa zetu sisi kuna Ofisi ya *Zone* ya Madini Arusha na wao wana kazi ya kuhakikisha kwamba watu wanachimba madini kwa mujibu wa sheria na taratibu na kadhalika. Lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametoa taarifa hizi na kauli ya Mbunge, ni kauli ya watu, basi inawezekana kwamba haya yapo. Kwa hiyo, namshukuru kwa taarifa hizi na nitazifanyia kazi mara moja. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu Mheshimiwa Waziri, afanye mambo mawili, aende Namanga kufuta kauli kwamba hatutapata umeme mwaka huu, au aende kueleza kwamba umeme utapatikana mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kawaida, Kamati...., Mheshimiwa Waziri, unalo la kusema kweli?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo la kusema. Namwomba Mheshimiwa Lekule Laizer asishikilie kwamba niende nikafute kauli kwa sababu Serikali imekuwa ikifanya kazi ya kupata fedha kwa ajili ya mradi wa umeme Namanga. Ninavyojua ni kwamba fedha hizo zitatokana na *BADEA* na sisi sasa tunafuatilia toka Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, upo mpango madhubuti ndiyo nimempa kauli ile kwamba mara hii itakuwa ni mara ya mwisho, siyo kwamba nilikuwa nazungumza porojo.

**MWENYEKITI:** Tunaomba Wizara mjitahidi jamani, Namanga tunapakana na Kenya. Upande huu ukiingia kiza, upande wa pili umeme upo, kidogo nayo haipendezi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*
*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1002 – *Finance and Acounts* ... Sh. 530,108,800/=
Kifungu cha 1003 – *Policy Planning*... ... ... Sh. 208,459,000/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2001 – *Minerals* ... ... ... ... Sh. 2,431,906,100/=

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba ufafanuzi katika suala ambalo wakati nilikuwa nachangia niligusia kwamba wananchi...

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ni programu ya *20 Minerals Exploitation Sub-Vote 2001*, kifungu kidogo cha *261000 - Utilities.* Kwa bahati nzuri, Waziri ametoa maelezo kwamba Serikali ina lengo la kuwapa maeneo wachimbaji wenyeji waweze kuendelea na shughuli zao.

Lakini kwa upande wa Tarime, eneo la Nyamongo kuna hitilafu iliyofanyika. Aidha, kwa makusudi au kwa bahati mbaya, mwaka 1996 kwa kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 1975 ambayo inatambua kuwapo kwa wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo na inasema kwamba maeneo ya wachimbaji wakubwa yatakuwa ni maeneo ya wachimbaji wakubwa na maeneo ya wachimbaji wadogo yatakuwa ni maeneo ya wachimbaji wadogo, lakini kwa mwaka huo wa 1996 wachimbaji wadogo, walipewa na Serikali eneo ambalo walikuwa wanaendelea kulichimba, lakini sasa baada ya miezi mitatu hilo eneo likatolewa kwa Kampuni ya kigeni.

Kwa hiyo, tangu mwaka 1996, hao wachimbaji na watafiti zaidi ya laki mbili na familia zao, maeneo yao yameshikwa mpaka sasa wanasubiri kupewa uamuzi wa Serikali utakuwaje. Vile vile, kuna maeneo ambayo watu walipewa leseni kufuatana na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 nao pia hawajaruhusiwa kuyaendeleza. Naomba majibu na ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani haya maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Wangwe, ambayo anataka ufafanuzi, mimi ningemwomba ndugu yangu Mheshimiwa Wangwe, kwa sababu jambo ni mahsusi kabisa, anipatie ili tuweze kushughulikia kwa sababu ni jambo ambalo ni tatizo ambalo liko kwake yeye analielewa vizuri zaidi kwa jinsi alivyolieleza. Kwa sababu, wote tunawashughulikia na tunawahudumia wananchi kwa sababu ni tatizo ambalo analisema, anasema lipo, basi mimi niko tayari kupokea taarifa hiyo na tuishughulikie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani ni uamuzi mzuri huo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Niko kwenye *Vote* hiyo hiyo ya 58, programu ya 20, *Sub-Vote 2001*, Kifungu kidogo cha 250100. Katika kuchangia hoja hii, nilimwomba Mheshimiwa Waziri atueleze hapa Bungeni kwamba ni hatua gani zimechukuliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya, samahani, naomba ukae. Hapa ni mshahara, sasa wewe unatafuta ufafanuzi. Kwa sababu hapa sio mshahara wa Mheshimiwa Waziri sasa. Tumeingia kwenye hizi Idara. Ni mshahara wa Mkurugenzi, sijui anaitwaje, au Kamishna. Haturuhusiwi Wabunge kuwajibisha Serikali kupitia Watendaji, tunapitia kwa Waziri. Sasa kama bado una hoja itafute labda kwenye Kitabu cha Nne kama ipo kama mradi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2002 – *Madini Institute* ... Sh. 842,204,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2003 – *Research and Laboratory Services...* ... ... ... Sh. 999,539,300/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dogo tu. Wakati wa kuchangia kwa maandishi, nilikuwa nimeandika kuhusu utafiti wa gesi katika nchi yetu na namna ya kuboresha utafiti huo.

**MWENYEKITI:** Taja kifungu kwanza.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Kifungu cha 58*, Sub-Vote 2003* na ninatumia kifungu kidogo zaidi cha 310400 ambacho kinazungumzia *Acquisition of Technical Equipment and Tools.* Katika eneo hili, bahati nzuri wewe mwenyewe ulitutangazia twende tukaangalie maonyesho ya *TPDC* pale nje.

Tuliokuwa watundu wa kwenda kuchunguza, tumepata taarifa nyingi sana. Moja ya taarifa tuliyogundua pale ni kwamba gesi yetu hiyo inaweza kwisha kati ya miaka 25 na ikizidi sana inaweza kwenda hadi 50. Lakini watu wetu wataalam tuliowafundisha zaidi ya 40 wana uwezo wa kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kwenye kifungu hiki cha *Research and Laboratory Services* nimepitia kitabu cha nne, vile vile pamoja na kuona mafungu makubwa sana katika kitabu cha nne, lakini hakuna kifungu chochote kinachoelekea kwenda kwenye utafiti.

Sasa najiuliza tumekwishaweka mitambo mikubwa sana, sasa tuna-*convert system* zetu hata kwenye viwanda: Je, kama hatutawekeza kwenye utafiti, tutafika wakati gesi imekwisha na hatujafanya utafiti, tutafanye? Nilitaka Waziri anihakikishie kama hata sio mwaka huu, ni lini tunaanza kuwekeza kwenye utafiti ili tuwe na uhakika kwamba gesi hii ambayo ni nafuu iweze kuwa na manufaa na ya kuendelea katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Hilo ni halali kabisa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza alilolisema Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ni jambo la muhimu ambalo Serikali inalitekeleza, kwamba katika maeneo haya yenye gesi pale Songo Songo na pia *Mnazi Bay* na maeneo mengine, kuna utafiti unaoendelea wa kuhakikisha kwamba tunapata *gas reserves* nyingine.

Hata wale Waheshimiwa Wabunge ambao walikwenda na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi *Mnazi Bay* watathibitisha kwamba wameona visima vingine vinavyochimbwa. Kwa hiyo, suala analolisema, ni muhimu, zuri, tunalifahamu na Serikali ndiyo inalishughulikia na inafanya hivyo pia kupitia kwa Wawekezaji.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2004 – *Transport – London* ... Sh. 1,235,485,600/=

Kifungu cha 3001– *Energy and Petroleium*...Sh. 24,487,608,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General* ... ... ... ... ... ... Sh. 441,000,000/=

Kifungu cha 1003 – *Policy Planning* ... ... ... Sh. 200,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2001 – *Minerals* ... ... ... ... ... Sh. 5,260,000,000/=

**MHE. MOHAMED H. MNYAA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 58, sub-vote 2001* Kifungu Kidogo *1114 – Mineral Sector Development Project.*

Katika maelezo yangu au katika mchango wangu nilizungumzia hii *percentage* ya madini kwamba, yanatuingizia kiasi gani nchini? Yaani katika pato la nchi nzima, Sekta ya Madini inatuingizia asilimia ngapi?

Nikajaribu kuonyesha kwamba tukitazama Bajeti ya Wizara hii, mkusanyo wa maduhuli yote yanayohusiana na madini halafu ukichukulia Bajeti ya Wizara ya Fedha, makusanyo ya ndani yataingiza kama trilioni mbili, bilioni 995 ki-*percentage* inakuja asilimia 1.33. Katika Hotuba ya Bajeti inazungumzia mchango wa madini ni asilimia 3.5.

Nilitaka kujua hii asilimia 3.5 tunaipata vipi wakati makisio yetu katika Bajeti yetu yako namna hiyo? Au ikiwa ndiyo tunafikia hivi, lakini baadaye yanatokezea mapato ya madini yanakuwa makubwa sana, ndiyo inafikia asilimia hiyo. Mheshimiwa Waziri anijibu.

Halafu hapo hapo kuna hii Kampuni ya *Alex Stewart* ambayo ipo kwa hayo madini. Kuna *percentage* kubwa sana ambayo inachukua hapo hapo. Je, wakishachukua *Alex Stewart ,* sisi tunabaki na *percentage* ngapi, naomba ufafanuzi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mnyaa nimpe ufafanuzi kwamba *percentage* ya 3.5 mimi nadhani sisi kwa mahesabu yetu ndiyo ilivyo. Lakini tuko tayari kukaa naye baadaye tuelimishane juu ya hii asilimia 3.5 inavyopatikana. *(Makofi)*

Kuhusu *Alex Tour,* hawa wanachukua, *royalty* ni asilimia tatu, hawa wanachukua asilimia 1.9. Lakini nataka niseme kwamba, Serikali imeshaamua kwamba pamoja na kazi nzuri inayofanywa, lakini kiwango hiki cha tozo ni kikubwa na kwamba hatuwezi kuendelea nacho mkataba utakapokwisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shellukindo, nilikuona.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwamba bado hujasahau.

**MWENYEKITI:** Watu wako wapo hapa? Wale pale.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Ndiyo wapo. Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilisema sitaunga mkono hoja mpaka nipate majibu ya mambo matatu. La kwanza, niliomba kwamba hawa ndugu zangu waliofika pale juu waondoke na jibu madhubuti na walisema hawaondoki mpaka waondoke na jibu.

Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri na kwamba, tutaambana mara baada ya Bajeti. Nimwombe tu kwamba asiweke siku moja kwa sababu eneo lenyewe ni nyeti na ni kubwa. Kwa hiyo, aje amejiandaa angalau kwa siku tatu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani na watu wangu wataondoka na jibu ambalo kwa kweli ni zuri, nadhani kule kutakuwa ni furaha na chereko na itaongoza imani yao kwa Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake.

Lakini niseme mawili kwamba, nakusudia kuunga mkono hoja hatimaye, lakini bado kidogo. Nina mambo mawili pia. Niliomba tupate Afisa Madini katika Wilaya ya Kilindi. Miaka minne sasa, bado tunamtumia Afisa Madini wa Handeni. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko.

La mwisho ambalo niliomba, ni kwamba, tumekuwa tukiwaambia watu waombe maeneo ya kuchimba madini. Tuna maombi 796 ambayo watu wamelipa Sh.135,000/= kila mmoja na fedha hizo zimepelekwa Hazina. Sasa kwa miaka mitatu wanasubiri tuweze kuwapimia viwanja waanze kuchimba ili tusionekane matapeli na tucheze ngoma ya Awamu ya Nne. Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu hilo ili tuweze kujua kama fedha zitatoka tuweze kupima. Baada ya hapo ndio nitatoa tamko. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hilo la pili na la tatu mimi sina la kusema, lakini lile la kwanza la kukaa siku tatu, Spika, anaongeza, napenda niwaongezee siku ya nne ili mlimalize kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa maeneo mawili ya Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kwamba yote haya amepata. Afisa Madini, atateuliwa mara moja, aende kwenye Wilaya hii ya Kilindi. Kuna uchimbaji mdogo mdogo mwingi sana kule na ni muhimu tu kuwasogeza huduma kwa wananchi pale pale kwenye Makao Makuu ya Wilaya na haya maombi tutayashughulikia 796, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba haiwezekani watu wamekaa tangu miaka mitatu iliyopita, wameshalipa na hawajashughulikiwa.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tamka rasmi kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3001- *Energy and Petroleum ... ... ... ...* Shs.426,643,995,000/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vote 58 *sub-vote* 3001, kifungu kidogo cha 3108 na kifungu kidogo cha 3198. Naanza na kifungu kidogo cha 3108.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hoja ya Waziri, nilikuwa nimeonyesha kitabu ambacho kiliwasilishwa kwenye Kamati ya Biashara na Uwekezaji, kwa ajili ya ruzuku ya inayopelekwa *IPTL* ya bilioni 18 na vilevile bilioni tatu ambazo ni kwa ajili ya ruzuku kwa kupanda bei ya mafuta. Katika Kitabu hiki cha Maendeleo, vifungu hivyo viwili vimetenganishwa na hapa imeandikwa *credit to TANESCO.* Sasa nilitaka ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kwamba katika kile kitabu ambacho kimeanzishwa kwa Kamati ambacho kitatumiwa na Wizara ya baadae kinaelezea ni ruzuku. Hapa inaonekana kwamba hiyo *credit* ya kwanza inakwenda *IPTL*, kwenye hii ya sasa inakwenda *TANESCO,* lakini vilevile nikitaka kufahamu kwamba *IPTL* ni Kampuni Binafsi, kwamba: Je, Serikali inatoa ruzuku kwa *IPTL*?

Pili, ni kwamba: Je, hii mitambo ya *IPTL* ambayo ni mali ya *IPTL* yenyewe na kwamba Serikali hivi sasa ime-*invest* pesa nyingi: Je, kuna hatua gani zinazochukuliwa katika ununuzi wa *IPTL?* Hii fedha ambayo Serikali inawekeza kwa *IPTL* imeingiaje mkataba na *IPTL*? Kwa sababu *TANESCO* inapewa fedha inaingiza *IPTL* kuitengeneza *IPTL*, lakini *ownership* ya *IPTL* sio ya *TANESCO* wala sio ya Serikali ni ya *private company.* Hii *investment* inayofanywa kwa *IPTL,* fedha ni za nani?

Pili, Serikali inatoa ruzuku kwa *IPTL* kwa kupitia *TANESCO,* kwanini inaipa *private company* ruzuku, lakini katika kitabu hiki imeandikwa *credit?* Kwa hiyo, nasema, kuna utata wa hata hizo *information* zenyewe. Kwa kifungu cha 3198 nayo vilevile *IPTL* inapewa bilioni hizo 18.458 kama suala langu lile la pili kwamba je, *IPTL* ni chombo cha Serikali? Huku mwanzo *TANESCO*, hapa *IPTL:* Je, *IPTL* ni Taasisi ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa lile la kwanza nadhani *subsidy* tuliyonayo ya *operating cost,* tumeipitisha kwenye kitabu cha pili kwenye ukurasa wa 208, haya ni maendeleo. Sijui Mheshimiwa Waziri umeliona vizuri hilo! Kwenye kitabu cha pili ndio kuna *transfers and subsidy* chini ya 280, 700 ya bilioni 21. Nilidhani *operating expenses* inalipwa kutoka kwenye fedha za matumizi ya kawaida. Hiki kilichopo hapa hakiwezi kuwa ndio *subsidy* kwa *TANESCO* kwa maana hiyo.

Ila la pili unalosema 3198 ni halali, la kwanza sio, kwa sababu hiyo tumekwishapitisha. Ya pili ni 3198, ambayo ni *convention to gas* ambayo ni *development expenditure,* hiyo ndio ameuliza.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe ufafanuzi Mheshimiwa Hamad Rashid kwamba, suala la *convention,* nimelieleza hapa umuhimu wake kwa ajili ya kupunguza gharama za umeme tunaonunua. Ndivyo ilivyokuwa katika mkataba ule kwamba itakapofikia hatua za kubadilisha mfumo wa uzalishaji, gharama hizo ziingizwe au zichukuliwe na sisi. Mambo mengi ambayo tunaweza tukayasema juu ya *IPTL* mengi kama nilivyosema awali ni kwamba *IPTL* tuna matatizo nao mengi. Lakini hili la *convention* ndio limo katika kwenye mkataba kwa maana ya kuhakikisha sisi ndio tunaogharamia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad, hebu 3108 unaiona kabisa ni *Forex* kutoka Sweden, sasa wewe unataka kung'ang'ania kwamba hizo hizo, ndio unajenga hoja kuhusu ruzuku kwa *IPTL,* sivyo! Sasa sielewi unachotaka kusimama, kama unasimama kwenye 3108 hiyo ndio *ruling* yangu na ni mwisho. Sasa kama unataka kusimama kwenye 3198 bado una hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:**Asante. Ndio aliyoitolea maelezo, ndio maana nikasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawekeza kwa *IPTL. IPTL is a private company,* hizi fedha inazowekeza Serikali kwa *IPTL* maana yake ni kwamba, huu mradi bado ni *ownership* ya *IPTL*. Tunauliza hizi fedha je, ni sehemu ya kununua *IPTL* au nini, sijapata maelezo bado.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa ufafanuzi Mheshimiwa Hamad Rashid kwa mba, *convention* ni muhimu hata kama kesho tunanunua ule mradi wa *IPTL*, kama nilivyosema awali, ni mkakati wa Serikali kununua. Kwa hiyo, lazima tufanye kubadilisha sasa mitambo ile ili tutakapomaliza mchakato wa kununua ule mtambo, tuwe tumeshakamilisha kazi hiyo. Lakini suala la kusema kwamba ni Kampuni Binafsi na kwamba Serikali inatoa ruzuku kwa Kampuni Binafsi, mimi nataka nilisemee hivi, nadhani suala hapa ni faida gani inapatikana kutokana na umeme ule unaotoka pale.

Kwenye mradi wa *Mnazi Bay,* Serikali pia imetangaza kwamba itatoa unafuu ili kuwawezesha wananchi wa maeneo yale kununua umeme sawasawa na Mikoa mingine na hii ni Kampuni Binafsi. Kwa hiyo, inategemea malengo ya Serikali yenyewe na matumizi ya ule umeme nao ni nini. Suala hapa ni huduma kwa wananchi na Serikali inatoa hivyo kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata umeme wenye bei nafuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bado nadhani swali la Mheshimiwa Hamad, lina uhalali wa kiasi fulani kwa maana tu kwamba, hii mnayowekeza katika kujaliana sasa kuinunua *IPTL*, haya yanayowekezwa sasa yatakuwa ni sehemu ya mjadala au siyo? Vinginevyo haiwezi kuwa na maana! Haingii akilini. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES W. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fungu hilo la 58, kifungu kidogo cha 3001, vifungu vidogo 31, 37, 31, 76, 31 na 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tulipounganisha gesi, bei zimepanda badala ya kushuka. Kwa hiyo, tulipounganisha Ubungo kuzalisha umeme, bei zimepanda, tumeunganisha kiwanda cha *cement*, bei za *cement* ya Dar es Salaam zikapanda, ukilinganisha na Tanga, na Mbeya, tumeunganisha na bia, bei ya bia ikabaki pale pale. Hivi tunafaidikaje na gesi hii?

Halafu la pili, hii gesi ni ya nani na pesa zinazopatikana kutokana na kuiuza, zinaingia wapi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa ufafanuzi Mheshimiwa Keenja kwamba, kwanza, nakubaliana naye kwa mtazamo ule wa ujumla, kwamba wakati mwingine wananchi wanakuwa hawapati unafuu ambao Serikali inatoa kwa Kampuni za biashara na ndio maana wakati naelezea juu ya kutolewa kwa *VAT* kwenye biashara ya mafuta nilikemea suala la wafanyabiashara kutokufikisha faida hiyo au punguzo hilo kwa wananchi wa kawaida.

Sasa kwenye upande wa gesi, tunapaswa kufaidika na unafuu unaosemekana kupatikana unaotokana na watu kujiunganisha na gesi kwa sababu kwa upande wao lazima gharama zao za uzalishaji zinapaswa kupungua. Kuna tofauti baina ya kutumia gesi na kutumia mafuta mengine. Nikuchukua mfano huu wa *IPTL* kwamba *energy charge* itakayolipwa kwa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi, itakuwa ni asilimia 50, pungufu kuliko ambavyo tunavyolipa hivi sasa. Kwa hiyo, ndio faida zake. Lakini napenda nitoe wito kwamba kwenye Makampuni haya au Kampuni za biashara zinapaswa kufikisha faida ile mwisho kwa mwananchi au kwa mtumiaji wa mwisho.

**MHE. CHARLES W. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo tu. Niliuliza kwamba, hii gesi anayeuza ni Serikali ama ni nani? Pesa zinazotokana na mauzo zinaingia wapi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi ya *TPDC*, wakishirikiana na Kampuni ya *Pan African Energy* na maduhuli yanaingia Serikalini. Kile kiwango ambacho kinabidi kiende Serikalini, kuna *formula* ambayo inatumika katika kugawa mapato kwenda kwenye Serikali.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nizungumzie katika *vote* 58, *sub-vote* 3001 katika kifungu kidogo 3(1) 7(6). Wakati nilipokuwa nachangia hasa kuhusu suala la gesi, Mheshimiwa Waziri alijibu majibu ambayo nakubaliana nayo na alisema kwamba suala la makusanyo ya fedha hizi anaziachia Kamati mbili ambazo zimechaguliwa au zimeundwa, moja ikiwa ni ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi.

Sasa swali langu liko hapa, kwamba, kwa sababu makusanyo haya yameanzia kipindi cha nyuma kuanzia mwaka 2004 tokea gesi ilipoanza kuuzwa na kwa sababu ya utaratibu wa Kamati zetu, inaweza ikachukua miaka minne, mitano au zaidi: Sasa je, malimbikizo au mauzo haya ya gesi, fedha ambazo zitapatikana, ule mgao wa Zanzibar utagawiwa *respectively* kuanzia mwaka 2004?

**MWENYEKITI:** Nadhani itakuwa ni sehemu ya majadiliano, wazo lako ni nzuri tu linaingia kama agenda kama kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo nadhani ni vizuri tu tunaendelea.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya swali langu ameuliza Mheshimiwa Keenja, lakini ninakwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu hicho cha 3001 na 98, 3198, tunapeleka Shilingi bilioni 18, ni hela zetu ni nyingi kweli kweli! Lengo kama Waziri alivyosema ni kupunguza makali kwa mwananchi mwishoni. Kwa bahati nzuri takwimu zilizoko pale nje, *TPDC* zinaonyesha kwamba kwa muda tuliounganisha Makampuni yetu, Kampuni moja tu imekwishapata faida ya Shilingi bilioni 18 tofauti kama ingelitumia mafuta ya kawaida au umeme wa kawaida *TANESCO*. Sasa Je, *reflection* hiyo katika bei zetu inakuwaje? Majibu kwa Mheshimiwa Keenja hayakunitosheleza, kwa sababu kusema unatoa tamko wakati wewe hapa ni *shareholder,* unaweka pesa yako, wala sio suala lile la kusema kwamba biashara ni huria kwa hiyo *market demand.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapaleka hela tukitegemea 50 *percent* ya bei itakuwa chini. Sasa kwenye bati haikupungua, kwenye *cement* haikushuka, kwenye umeme wenyewe ambao wananchi wanautumia pamoja na kwamba tumeongeza Songosongo pale Ubungo nayo haikushuka. Serikali inatupa mkakati gani wa kuhakikisha kwamba bei ya vitu hivi ambavyo kwa kweli ndiyo mkombozi kwa mwananchi, nyumba zitahitajika kujengwa na wananchi waondokane na umaskini na wataondokana na raslimali hii nzuri, Serikali inatuhakikishia mkakati gani wa kwamba bei hizi zinapungua kwa kuwa tumewekeza hela nyingi kiasi hiki?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwamba, kwanza, kwa upande wa *IPTL* ni sehemu ya makubaliano kwamba patakapo kuwa na matumizi ya gesi katika kuzalisha umeme, mahesabu ambayo yamefanyika yatapunguza gharama ambazo *TANESCO* inanunua umeme kutoka *IPTL* kwa asilimia 50. Sasa *TANESCO* ndiyo baadaye inauza umeme huu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida ungesema pia na *TANESCO* iuze umeme huu rahisi kwa wananchi. Lakini *TANESCO* katika kuuza umeme kwa wananchi inatilia maanani mfumo wa nchi nzima.

Kuna maeneo hapa nchini ambayo yanazalisha umeme kwa bei ya juu sana. Kwa mfano haya maeneo yote yanayotumia mashine za *diesel*. Uzalishaji wa umeme karibuni senti 30 hadi 40 za Kimarekeni *Kilowatt per hour*. Sasa haya yanafidiwa na maeneo mengine ambayo yanazalisha umeme kwa njia za maji na njia nyingine kama za gesi.

Kwa hiyo, hatimaye suala la *TANESCO* kuweza kupunguza bei kwa mtumiaji wa mwisho haliwezi tu kutegemea ile *conversion* ya *megawatt* 100 inayopata kutoka *IPTL*, inategemea masuala mapana zaidi katika suala zima la uzalishaji wa umeme nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, hoja ya msingi ya kwa ujumla kwa Serikali kutafakari namna gani katika mapana na marefu, hizi nafuu ambazo zinapatikana kwa viwanda vyetu na biashara zetu, namna gani kumnufaisha mwananchi wa kawaida na kwa sababu hiyo, hili ni suala ambalo linakubalika kufanyiwa kazi.

**MHE. DR. WILBROD W. SLAA:** Mheshimwa Mwenyekiti, ninakubaliana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwamba, Serikali inakubali kulifanyia kazi. Lakini ningependa kuweka rekodi sawa. Sasa hivi kwa muda wa karibu mwaka mmoja, tumeunganisha Makampuni karibu kumi, *direct* kutoka kwenye *line* ya Songosongo kwenda kwenye Kampuni hawatumii tena umeme wa *TANESCO*. Kwa maana hiyo, tayari tumekwisha kuwa pungufu. Sasa ni kitu gani kinazuia kwa mfano *Aluminium Africa* ambayo imeunganishwa, bei ya bati isishuke, kwani ni kitu gani kinazuia?

*Breweries* ambayo tayari nayo imeunganishwa, wana *switch* tu wakati mwingine ukitaka wa *TANESCO* wanaweka ile *switch,* wanatumia ya *TANESCO*, lakini waki-*switch* wanatumia ya Songosongo, sasa hiyo imeshaonekana kwenye takwimu kuwa mnapata faida. Kwanini Serikali isitoe tamko la moja kwa moja? Wale wanaotumia Songosongo kwa kuwa wamepata punguzo hilo, basi na wao *automatically* wapunguze kwa kiasi hicho na Serikali iende kufuatilia?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ndugu yangu ameelewa niliyoyaeleza mwanzo, kwamba, swali alilolisema, ni suala ambalo lina msingi, lina mantiki, lakini sio suala ambalo mtu unaweza ukakurupuka nalo ukatolea tamko hapa. Ni lazima likafanyiwe kazi ipasavyo. Sasa mimi nadhani, haya ni majibu ambayo ningemwomba Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na yeye mtu mzima mwerevu, ayakubali haya, kwamba, atupe nafasi Serikali katika ujumla wake ifanyie kazi na yeye tutamshukuru kama tutapata mchango wake na Waheshimiwa Wabunge wengine watushauri wanafikiri iweje, lakini ni suala ambalo linahitaji kufanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Kwa jinsi Spika alivyokuelewa na kwa hiyo, ameielewa Serikali kwamba linakwenda kufanyiwa kazi. Kwa maana hiyo, ama matokeo yake tutayapata kabla ya Mkutano ujao, hapana! Kazi kubwa, lakini mjue wananchi wanahoji hili. Sasa nadhani ni vizuri angalau tupate taarifa ya utendaji katika Mkutano ujao. Itasaidia kutuliza nchi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii tena. *Vote* ya 58, *sub-vote 3001,* kifungu cha 3118 - *Environmental of Kihansi Project*. Katika hotuba yangu nilihoji matumizi ya pesa hizi kwa nia njema tu ya kumsaidia kaka yangu Mheshimiwa Waziri kwa kuwa watu wengi wanahoji *TANESCO* inatumia pesa nyingi sana na kule Kihansi

kunafunguliwa maji wanapewa vyura, ambapo yanapoteza maji yale wakati yangeweza kuzalisha *Megawatt* 15 nusu ya matumizi ya Kisiwa cha Zanzibar.

Vyura wale ni viumbe hai ambao wako hapa Tanzania tu, tunajua, tunapenda, tunataka tuwe nao lakini matumizi ya fedha za viumbe hao zimekuwa ni kubwa mno. Juzi tulijibiwa na Mheshimiwa Waziri anayehusika na Mazingira, Mheshimiwa Prof. Mwandosya, kwamba Dola milioni 75,000 zinalipwa na Tanzania kila mwaka kwa kuwahifadhi vyura walioko Marekani hao sijui 400 waliopelekwa na asilimia 61 inalipiwa na Serikali ya Marekani. Sasa sisi tunapoteza maji hayo ya *Megawatt* 15 katika ukame huu kwa kuwapa viumbe hao na wakati huo huo katika Bajeti hii wamepangiwa milioni 250 kwa viumbe hawa na wakati huo huo hatujaambiwa vyura hao kama ni suala la utalii wanaingiza kiasi gani? Kama ni suala la kitowewo wanaingiza kiasi gani? Sasa tutaendelea kwa muda gani vyura hawa kutu-*cost* kama hivi? Naomba ufafanuzi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika kutoa ufafanuzi wa hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo: Kile kifungu kinahusu *Environmental Management of the Kahansi Project*, hakihusu moja kwa moja na vyura, vyura ni sehemu mojawapo ya kutunza na kuendeleza Baionuwai ya mradi wa Kihansi. Labda kwa ufafunuzi tu niseme kwamba maji yalipoacha kupita kwenye ile *gorge* ili yaende chini yakazalishe umeme, basi sehemu kubwa ya msitu wa Kihansi ilikosa maji, sasa katika makubaliano ilikuwa kiasi fulani kiachiwe ili kiende angalau ule msitu wa baionowai ikiwa ni pamoja na vyura, basi iweze ikaendelea kwa uasilia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndio ufanunuzi ninaoweza kutoa na wala haihusu moja kwa moja tu na vyura wa Kihansi, lakini niseme hata vyura vya Kihansi ni muhimu kwa sababu katika mikataba ya kimataifa ambayo sisi tumeingia hasa mkataba wa bainowai tunawajibika kutunza viumbe ambavyo kwa kawaida vingepotea. Kwa nini tuvitunze? Ni kwa sababu hatufahamu, tunachukua tahadhari kwamba inawezekana kabisa katika viumbe hivyo, labda baadaye katika utafiti tunaweza hata tukaja kupata hata dawa ambayo inaweza ikatibu maradhi ambayo hatuyajui. *(Makofi)*

Halafu hapo hapo, kwa maana ya mradi huu, niseme na nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Kamati itakwenda kule Kihansi ili iweze kupanda ule mlima na waone ule msitu. Ni msitu ambao mbali na hawa vyura, kuna miti, kuna maua, kuna vipepeo vya aina yake duniani. Kwa hiyo, mradi wote huu kwa kweli ni muhimu sana, si kwa Tanzania, lakini kwa dunia.

**MWENYEKITI:** Jambo moja inaweza kufanya Serikali ni kumchukua Mheshimiwa Mnyaa, naye atembelee Kihansi. Mnajua mambo haya, Kihansi mtu anaweza kuwa anafikiria vingine kabisa! Mheshimiwa Mnyaa utakwenda Kihansi basi. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niko kwenye *vote* hiyo hiyo ya 58, *sub-vote 3001.* Nina maswali mawili yanayohusu vifungu vidogo 2(1) na kile cha 3112, suala la Umeme Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kurejea maneno niliyoyasema wakati nikichangia mada hii kwa maandishi kwa kuwa yatapoteza muda. Naomba niende moja kwa moja kwenye maswali. Kifungu hicho ningependa kufahamu ni lini Mji wa Peramiho, ambao upo karibu sana na eneo ambalo *TANESCO* imeishia katika kuweka umeme utapatiwa umeme?

Je, katika fedha iliyotengwa katika kifungu hiki, itahusisha na Mji huo wa Peramiho ambao ni muhimu sana kwa nchi nzima ya Tanzania na Mkoa mzima wa Ruvuma? Wengi wanafahamu umuhimu huo. Lakini katika kifungu kidogo cha 3121, napenda sana kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu sasa wa kuunganisha Mkoa wa Ruvuma kwenye gridi wa Taifa, ule mpango wa Songea, Makambo, naipongeza Serikali.

Ningependa tu kufahamu kama mpango huu wa Makambako, Songea utahusisha pia Vijiji vyote vilivyoko katika Kata ya Wino, Kata ya Madaba Mahanji, Kata ya Ngubiro na Kata ya Tanga.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu au kumpa ufafanuzi Mheshimiwa Mhagama kama ifuatavyo: Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mhagama kwamba Mji wa Peramiho ni Mji muhimu na Serikali imepanga kwamba katika mwaka huu wa 2006/2007 kazi ya kujenga na kufikisha umeme Peramiho itafanyika. *(Makofi)*

La pili, hizi Kata mbalimbali ambazo amezitaja, nadhani itabidi tuonane baadaye, labda kesho, kwa sababu inahitaji kukutana na *TANESCO* na kupitia maeneo, ile ramani ambayo mradi huu utapita.

Lakini kwa ujumla, nafahamu kwamba wakati mradi huu unajengwa kwenda Songea, kuna maeneo mbalimbali ambayo njiani yatapata umeme, lakini kwa uthibitisho, kwa sababu ametaja majina mahsusi, basi nadhani ingekuwa vizuri tuonane na Mheshimiwa Jenista Mhagama halafu tunaweza tukampa ufafanuzi huo. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi, lakini nazungumzia *vote number 58 sub-vote 3001 - Energy and Petroleum* kifungu kidogo cha *3125 ERT.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kujua, nilipochangia kwa maandishi nilitaja miradi mitatu ya umeme ambayo ipo Wilayani Mbozi. Natambua kabisa Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu alisema kwamba watazingatia miradi yote ya nyuma ambayo ilikwishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nimekuwa napata msukumo sana kwa wananchi pale nilipofanya Mikutano, wanasema tunaomba tuulizie Serikali inatuambia nini kuhusu miradi hii ambayo imeanza tangu mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo zimechimbiwa na nina hakika Serikali imetumia pesa, lakini hakuna kinachoendelea. Naomba niitaje miradi hii. Mradi wa kwanza ni Rwanda - Uralidiwili, wa pili ni Mahenje – Igunda hadi Kijiji kinaitwa Shaje na mradi wa tatu ni Vwawa Asamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi walishaonyesha hamu sana ya kutaka kutumia umeme baada ya kuona nguzo zile zimetundikwa, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea.

Sasa, inawezekana kabisa wamesikia hiyo *general statement* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini ninaomba Mheshimiwa Waziri aisemee sasa miradi *hii in particular* kwamba Serikali inawaambia nini wananchi wa Mbozi?

Lakini kwa sababu pia tunapata umeme ambao unatoka Zambia ambao kama wenzangu walivyosema, umeme tunaoupata hauko *reliable* kwa sababu unakatikakatika sana, hili tulikuwa tunamwomba Mheshimiwa Waziri atambue kwamba, Wilaya ya Mbozi pia tunapata umeme kutoka Zambia.

Kwa hiyo, wanapofanya mipango ya kukutana na Viongozi wa Zambia, basi kama kuna aina yoyote ya kuhusisha, basi watuhusishe na sisi Wabunge wa Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza, napenda nirejee kauli yangu ya ujumla ambayo nimeisema mwanzo kwamba miradi ambayo imeanza na ikasimama ni dhahiri kwamba ni hasara na busara inatupa kwamba lazima tuikamilishe hiyo kwanza na kama nilivyosema awali kuwa kwa kupitia huu mpango wa *ERT* tutaifanyia kazi hiyo. *(Makofi)*

Lakini la pili, kuwa mahsusi kwa Mheshimiwa Godfrey Zambi, napenda kumfahamisha kwamba kwa mujibu wa majadiliano tuliyokuwanayo na *TANESCO,* hii miradi ambayo ameitaja inatarajiwa kukalishwa katika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Fereji amejitoa. Majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa hoja za Mheshimiwa Keenja yamemtosheleza. Kwa hiyo sasa tunaendelea na Mheshimiwa Mudhihir.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ubinadamu kwamba ukiwa umetarajia jambo kwa muda mrefu halafu ukapewa ahadi kwamba sasa mambo ni mazuri, basi badala ya kutua moyo, basi moyo unakuwa na wahka.

Jana Mheshimiwa Waziri alitamka kwamba Mchinga safari hii msiwe na wasiwasi, umeme umepatikana. Sasa mimi nimeangalia katika kibatu chake cha hotuba ya Bajeti sikuona Mchinga.

**MWENYEKITI:** Ungetaja Kifungu Mheshimiwa.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fungu 58, fungu dogo 3001, kifungu cha 3112 - Umeme Vijijini.

Sasa kwa sababu kwenye hotuba hakutaja Mchinga wala humu hamna, nilikuwa nauliza, fedha hizi za kupeleka umeme Mchinga zitatoka hapa kwenye kifungu cha 3112 au kuna sehemu nyingine? Nafikiri nimeeleweka.

**MWENYEKITI:** Iko wazi kabisa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Mudhihir kwamba Mchinga *A* na *B* imo katika mpango wa umeme mwaka huu na imo katika fungu la umeme Vijijini na katika vitabu vya ufafanuzi ambavyo vipo Wizarani kwetu ipo hiyo pia. Nadhani kwa kumthibitishia hiyo zaidi, basi tuonane halafu nitaweza kumweleza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge zima imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makisio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2006/2007yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01:42 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 19 Julai, 2006 Saa 03:00 Asubuhi)*